# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Thethathini na Moja – Tarehe 25 Julai, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI :** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na ratiba yetu ya leo, nina tangazo dogo fupi. Nimepokea taarifa kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utangazaji Tanzania (TUT).

Waheshimiwa Wabunge, tunaombwa kuarifiwa kwamba kwa siku hii ya leo, kipindi cha saa 2:00 mpaka saa 3:50, TVT hawatakuwa hewani, hawataweza kutangaza kipindi chetu cha Maswali na Majibu. Hii inatokana na Shughuli Maalum inayofanyika leo Dar es Salaam.

Tunafahamu kwamba, leo ni Siku ya Mashujaa na ni Shughuli ya Kitaifa iko kule. Kwa hiyo, vyombo vingine vitaendelea lakini TVT tutaungana nao baada ya muda huo niliousema, kama shughuli ile ya Kitaifa itakuwa imeshakamilika kule Dar es Salaam.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-
**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa fedha 2007/2008.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 282

### Makao Makuu ya Chunya

**MHE. GUIDO GOROGOLIO SIGONDA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1972 Serikali iliamua kuhamishia Makao Makuu ya Chunya toka Chunya Mjini, kwenda Mji Mdogo wa Mkwajuni, ambako ndiko Makao Makuu ya Jimbo la Songwe yalipo; na kwa kuwa miundombinu yote inayohitajika kuwepo kwenye Makao Makuu ya Wilaya kama Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Kituo cha Polisi, Soko, Hospitali Teule ya Wilaya, Benki, Magereza, Posta, Nyumba ya Mkuu wa Wilaya, Nyumba ya Mkurugenzi wa Wilaya na ya *OCD* na *DSO* ilijengwa sehemu hiyo; na kwa kuwa, uamuzi huo wa Serikali haukutekelezwa:-

(a) Je, ni sababu zipo silisitisha uamuzi huo licha ya kwamba, miundombinu yote imekamilishwa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, ni jambo la aibu na fedheha kutotekeleza uamuzi huo baada ya kutumia gharama kubwa ya fedha ambayo ingetumika kwa shughuli nyingine za Maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Guido G. Sigonda, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, mwaka 1972 Serikali iliamua kuhamishia Makao Makuu ya Chunya toka Chunya kwenda Mji Mdogo wa Mkwajuni, ambako ndiko Makao Makuu ya Jimbo la Songwe yalipo kwa sasa. Pia ni kweli kuwa baadhi ya miundombinu inayohitajika kuwepo kwenye Makao Makuu ya Wilaya kama Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Kituo cha Polisi, Soko, Hospitali Teule ya Wilaya, Benki, Magereza, Posta na nyumba za kuishi viongozi na baadhi ya watumishi mbalimbali, kwa wakati huo zilikuwepo. Hata hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Tawala za Mkoa a Serikali za Mitaa, ilisitisha uamuzi huo kwa barua Kumb. Na. *RALGD-C/D/60/42/2* ya tarehe 29 Aprili, 1991.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kuu za kusitishwa kwa uamuzi huo ni kwamba, kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya wakati huo kwamba, Mkwajuni siyo katikati ya Wilaya ya Chunya kwa jiografia wala kwa mawasiliano hivyo, Makao Makuu kuwa Mkwajuni kusingeleta unafuu kimawasiliano, kwani ni pembeni mwa Wilaya. Aidha, kiuchumi Wilaya ya Chunya imegawanyika katika kanda tatu; yaani Ukanda wa Kilimo cha Tumbaku katika Tarafa ya Kipembawe, Ukanda wa Pamba katika Tarafa ya Songwe na Ukanda wa Mazao mchanganyiko katika Tarafa ya Kiwanja na Kwimba.

Hivyo, uamuzi wa kuhamisha Makao Makuu ya Wilaya ya Chunya, ungelenga kuwakaribia zaidi wakulima wa pamba bila kufikiria Maendeleo ya Ukanda wa Tumbaku, ambao unahudumiwa kwa urahisi zaidi kupitia Makongorosi na Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sababu nilizozitaja hapo juu, Serikali ilizingatia pia maoni yaliyotolewa na wadau mbalimbai, wakiwemo watalaamu na wananchi hivyo, ikaonekana kuwa, kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya Makwajuni, kungeongeza gharama kwa Serikali kutokana na kujenga maiundombinu mipya Mkwajuni na kutelekeza miundombinu iliyokuwa tayari imejengwa Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, uamuzi huo siyo jambo la aibu wala fedheha, bali ni uamuzi wa busara, uliozingatia mahitaji ya wakati ule na ni maoni ya ushauri wa wadau mbalimbali.

**MHE. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa vigezo vyote vipo na hasa miundombinu. Je, Serikali haioni kwamba pengine uongozi huo ungeheshimika angalau kwa kuipa hadhi ule mji uwe na Halmshauri kamili?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr.Guido G. Sigonda, kama ifuatavyo: Ni kweli kwamba, miundombinu ipo na ninadhani suala la Halmahauri ni masuala ambayo tumepata maombi mengi sana na taratibu zake tumekuwa tukizieleza hapa. Kwa hiyo, kama kuna haja hiyo ya kuwa na Halmashauri, jambo hili lifuate utaratibu wa kawaida na Serikali itajaribu kadri ambavyo itaonekana inafaa.

Na. 283

**Barabara ya Lami – Mji wa Kahama**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa Kampeni za Uchaguzi mwaka 2005, Mheshimiwa Rais aliwaahidi Wananchi wa Kahama kwamba, Mji wa Kahama utapatiwa walau Barabara moja ya lami, kwani aliona kuwa Mji huo unastahili kuwa na Barabara ya aina hiyo; na kwa kuwa Wananchi wa Kahama walishiriki vizuri katika kukiwezesha Chama cha Mapinduzi kupata ushindi wa kishindo. Je, ni lini Serikali imepanga kuitekeleza ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James D. Lembeli, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua juhudi mbalimbali kuhakikisha kuwa, Miundombinuya Barabara nchini inaboreshwa. Kuhusu uhitaji wa Barabara ya lami Kahama, Serikali inatambua ahadi mbalimbali zinazotolewa na Viongozi wake Wakuu, akiwemo Mheshimiwa Rais. Kama nilivyojibu swali la Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mbunge wa Ubungo tarehe 18 Julai, 2007 katika Mkutano huu, Serikali kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008, imetenga fedha kwa Manispaa atano za Sumbawanga, Songea, Musoma, Mtwara na Kigoma. Halmashauri nilizozitaja zimetengewa shilingi milioni 300 kila moja, kwa ajili ya kilometa 1.5 za lami. Serikali itaendelea kutenga Bajeti kwa ajili ya miji mbalimbali ikiwemo Kahama, kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais aliahidi ahadi nyingi wakati wa kampeni na kwa kuwa najua kabisa hizi ahadi zitatekelezwa. Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa wa kupanga muda na mkakati wa kutekeleza hizi ahadi alizoahidi Rais likiwepo Daraja la Mto Sibiti?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, kama ifuatavyo: Ni kweli kwamba, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi na katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuna ahadi nyingi ambazo zitatekelezwa katika kipindi hiki cha miaka mitano. Nafurahi kusikia kwamba, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, anaamini kama tunavyoamini sote kwamba, ahadi zote zitatekelezwa.

Sasa kuhusu utaratibu wa kupanga, ndiyo maana kuna Bajeti ya kila mwaka, kila mwaka tunapanga mipango ya kuonyesha mwaka huu tunatekeleza nini na ndani ya miaka mitano tutekeleze yote hayo ambayo yaliahidiwa likiwemo na Daraja la Sibiti.

Na. 284

**Matengenezo Makubwa ya Vyuo vya Serikali**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka 2006/2007, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya matengenezo makubwa ya Vyuo vyake Dar es Salaam na Tabora; na kwa kuwa mpaka sasa, takribani robo tatu ya mwaka wa fedha husika umekwisha. Je, utekelezaji wa matengenezo ya Chuo cha Watumishi wa Umma Tabora umefikia wapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kukikarabati Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Tawi la Tabora, ulianza mwaka wa fedha 2005/2006, ambapo kampuni ya *Co-Architecture* ilifanya upembuzi yakinifu wa ukarabati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Serikali ilitenga jumla ya shilingi 600,000,000 kwa ajili ya ukaratabati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uwezo wa Serikali, kazi ya kukikarabati Chuo cha Utumisni wa Umma Tanzania, Tawi la Tabora, utafanyika kwa awamu. Awamu ya kwanza ya ukarabati ilianza tarehe 18 Juni, 2007, ambapo Kampuni ya B.H. Ladwa, inakarabati majengo matatu ya chuo; ambayo ni Jengo la Hosteli la Shaban Robert, Jengo la *Block A* la madarasa na Jengo la Utawala, kwa gharama ya shilingi 606,394,860.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa kila mwaka ili kuhakikisha kwamba, majengo yote ya chuo yanafanyiwa ukarabati. Mwaka huu wa fedha 2007/2008, Serikali imetenga shilingi milioni 450 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati huo.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri.

La kwanza, chuo hiki kinafundisha watumishi wa Serikali katika karne ya *TEKNOHAMA,* kwa maana vitendea kazi siku hizi ni kompyuta na utaalamu wa *ICT* ndiyo wenyewe. Kwa hiyo, nauliza katika ujumla wa ukarabati wa Chuo hiki. Je, Serikali inafikiria kuongeza vitendea kazi kama kompyuta hapo chuoni, tena mpya siyo za kutoka Magogoni kwenda Tabora kama wanavyofanya sasa hivi?

La pili, maktaba ya Chuo hicho ni ndogo, hivi sasa kuna wanafunzi takriban 600, *sitting capacity* ya makbata ya Chuo ni karibu watu 30 kwa wakati mmoja. Je, Serikali inalionaje hilo kwa upande wa maktaba vilevile kwamba ipanuke kufuatana na ukubwa na mahitaji ya chuo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya yongeza ya Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni malengo yetu kukikarabati Chuo cha Utumishi wa Umma, Tawi la Tabora na kukipanua, kwa sababu sasa hivi kozi zote zile za kuanzia, tunazihamishia Tabora na mimi mwenyewe nilikitembelea Chuo hicho na nilikwenda hata kwenye hiyo *library* ya kompyuta anayoizungumzia, kwa kweli vitendea kazi ni vibovu, tumeviona.

Mwaka huu tunamalizia maabara ya kompyuta katika Tawi la Dar es Salaam na baada ya hapo, tutakikarabati awamu kwa awamu kuhakikisha kunakuwa na vitenda kazi vya kutosha na majengo ya kutosha ikiwemo kompyuta na maktaba ambayo ameizungumzia na sio kuhamisha kompyuta za Dar es Salaam kupeleka Tabora.

Na. 285

**Serikali Kusaidia Ujenzi wa Shule Kisarawe**

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO** aliuliza:-

Kwa kuwa Wananchi wa Kata za Msanga, Mzenga, Cholesamvula na Msimbu wakishirikiana na Halmashauri ya Wilaya, wanaitikia wito wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kujenga angalau shule moja ya Sekondari katika kila Kata ya Kata hizo lakini shule hizo hazijakamilika kwa sababu nyumba za walimu, madarasa na majengo ya utawala, hayajatosheleza wala kukamilika na baadhi ya majengo hayo yaliyoanzishwa yamekwama kutokana na ukosefu wa fedha za kumalizia:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu kusaidia Wananchi wa Kata hizo ili majengo hayo yakamilike na wanafunzi wasome bila bugudha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiunga mkono juhudi za wananchi katika ujenzi wa shule za sekondari nchini. Kwa mwaka 2006/2007, Serikali iliupatia Mkoa wa Pwani jumla ya shilingi 1,327,000,000 ikiwa ni ruzuku ya ujenzi wa nyumba 106, vyumba vya madarasa na nyumba 65 za walimu. Uongozi wa Mkoa uligawa ruzuku hiyo na kuipatia Wilaya ya Kisarawe jumla ya shilingi 202,000,000 shilingi 112,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 16 na shilingi 90,000,000 nyumba kumi za walimu. Serikali itaendelea kuunga mkono wananchi wanaojenga shule za sekondari, kadri ya upatikanaji wa fedha. Aidha, Halmashauri na wananchi, wanashauriwa kukamilisha majengo yaliyopo kabla ya kuanza mapya.

**MHE. ATHUMAN S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Je, yuko tayari kutembelea Mkoa wa Pwani hasa Wilaya ya Kisarawe, aone majengo ambayo yamekamilikia na aweze kuona ni namna gani Serikali inaweza ikasaidia kwa ziada? La pili, kwa kuwa Wilayani Kisarawe zipo Kata tano sasa hivi ambazo hazijapata hata shule moja ya sekondari na wananchi wako tayari kuungana na Serikali kutimiza ile azma ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya kuwa na shule ya sekondari katika kila Kata. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufanya haraka kupeleka msaada katika Kata za Mafizi, Mzenga, Marui, Kurui na Vikumbulu ili nako waweze angalau kupata shule moja ya sekondari?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Athuman S. Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Awali ya yote, naupokea kwa dhati kabisa mwaliko wake, nitafanya ziara mara moja nitakapomaliza Bunge hili ili twende tukaone hali halisi ilivyo Kisarawe.

Swali la pili, kuhusu Kata tano ambazo hazijapata shule za sekondari, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Maunzo ya Ufundi, naomba kumwagiza Afisa Elimu wa Mkoa kwa kushirikiana na Afisa Elimu wa Wilaya na Mratibu wa Elimu ya Sekondari, wafanye haraka kwenda kufanya upembuzi na kuona ni kwa nini hawakuweza kujenga shule hizi katika awamu iliyopita. Kwa maana hiyo basi, kwa kuwa kuna mgao mwingine wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 800, wahakikishe kwamba, Wilaya hizo ama Kata hizo ambazo hazijapata, zinapata madarasa hayo mwaka huu. *(Makofi)*

Na. 286

**Uhaba wa Shule Mikoa ya Kusini**

**MHE. FATMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Kwa kuwa inaonesha wazi kuwa Mikoa ya Kusini ikiwemo Lindi ina shule chache za msingi na sekondari, hali inayosababisha wananchi wa maeneo hayo, kukosa elimu kutokana na mfumo wa elimu wa kikoloni uliorithiwa, pamoja na mfumo ulioanzishwa katika miaka ya 60, kwa kuzifanya shule zote za sekondari nchini kuwa za kitaifa, hali inayowezesha Mikoa iliyokuwa na nguvu na uwezo kiuchumi, kupata fursa ya kuwapeleka watoto hao kusoma popote Tanzania na wasio na uwezo kubakia kutosoma hata kama shule ipo katika Mkoa wake, kwa kuwa zinakuwa zimejazwa na watoto wenye uwezo:-

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kuisaidia Mikoa hiyo kwa makusudi, ukiachia fedha za MMEM na MMES kwa kutenga fedha za ziada kwa ajili yao, ukizingatia kuwa wananchi wenyewe sasa wameshaonyesha nia ya kujenga shule hizo kwa kujitolea?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kuna baadhi ya Mikoa yenye shule za msingi na sekondari chache, ikiwemo Mikoa ya Kusini. Serikali imechukua hatua za makusudi, kwa kuipatia fedha za ruzuku ya Maendeleo zaidi Mikoa ambayo iko nyuma kielimu, kuliko Mikoa mingine ukiwemo Mkoa wa Lindi. Kwa mfano, mwaka 2006/2007, ruzuku ya shilingi 1,064,500,000 ilipelekwa Mkoa wa Lindi, kwa ajili ya kuchangia ujenzi katika shule za msingi. Aidha, kwa kuzingatia uchache wa shule za sekondari zilizokuwepo, ruzuku ya shilingi 1,175,000,000 ilitolewa kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa shule za sekondari. Ruzuku hiyo imechangia nguvu za wananchi, ambapo Mkoa umeweza kujenga shule mpya za sekondari zipatazo 41 mwaka huu. Ongezeko la shule hizo, limewezesha Mkoa kuchukua asilimia 100 ya wanafunzi waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2006. Hili ni jambo la kuwapongeza Wananchi wa Mkoa wa Lindi. Ukiachia fedha MMEM na MMES katika mgawanyo wa Maendeleo kwa Mikoa, Mkoa wa Lindi umeongezewa mgao kutoka shilingi 892,000,000 mwaka 2006/2007 hadi shilingi 15,269,000 mwaka 2007/2008. Aidha, ipo miradi 29 ya elimu inayosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF).* Kwa kutumia fursa hizo, Mkoa una wajibu wa kuweka vipaumbele vyake, ikiwa ni pamoja na miradi ya elimu. Serikali itaendelea na juhudi za kuitazama Mikoa iliyo nyuma kielimu ili kuleta usawa katika upatikanaji wa nafasi za elimu nchini.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwneyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Elimu na ninamshukuru kwa msukumo wake alioufanya tangu apate nafasi hiyo, kwa sababu alipokuja alizikuta shule 20 tu na sasa zipo shule za sekondari 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule za Sekondari 90 ambazo msukumo wake ameupinga ni shule 45 tu mpaka sasa ambazo ni za viwango. Sasa hivi langu si swali, nina ombi kwamba, hizi shule 45 nyingine ambazo zimebaki basi ziendelee kuwa katika mazingira ya shule, mazingira ya shule kuna maeneo matano, eneo la kwanza ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, kama ni ombi nafikiri limeshafika na utaendelea kuwasiliana na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa masuala mengine ya ziada.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na asante sana.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa, hakuna ubishi kwamba, toka mwaka 1961 tulipopata Uhuru, hakuna shule iliyojengwa na Serikali ukitoa zile za kurithi; na kwa kuwa mkoa mzima ni *Lindi Secondary School* peke yake ndiyo yenye madarasa ya *A-Level*. Je, siyo wakati muafaka sasa, pamoja na jitihada zote za Serikali, kuusaidia Mkoa wa Lindi kuongeza madarasa ya *form five* na *Six* walau kwa shule tatu au nne kwa mwaka huu wa fedha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Awali ya yote, napenda kuwapongeza Wabunge hasa wa Mkoa wa Lindi, kwa namna ya kipekee wanavyofuatilia Maendeleo ya elimu. Pili, naomba kumwahidi Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, kwamba mipango hii ya Maendeleo sasa imeteremshwa katika Halmashauri kwa mpango wa *D by D.* Katika kiasi cha pesa kitakacholetwa maamuzi wapeleke wapi na kipaumbele ni nini, ni yao wenyewe, sisi Wizara tutapeleka fedha pale. Kwa hiyo, nawaomba tu wakae katika Halmashauri yao, wapange ni shule zipi wanazotaka kuziboresha ili fedha hiyo iweze kufanya kazi hiyo kama watakavyokusudia na sisi tutakubaliana nao.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Pia nashukuru kwa mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, kwa mkakati mkubwa wa Serikali uliowekwa kwa kipindi hiki angalau kila wilaya ina shule ya sekondari; na kwa kuwa Serikali katika mipango iliamua kuwa angalau kila wilaya watateua shule za sekondari ambazo zitakuwa za Kitaifa, kwa maana ya kufanya wanafunzi wachanganyike kutoka wilaya moja au nyingine. Je, Serikali imefikia wapi na mpango wake huo na itaanza lini kutekeleza ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):**Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Ni kweli Serikali kwa kutekeleza maagizo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, iliagiza kila Kata iwe na sekondari na utekelezaji huo umefanikiwa kwa asilimia kubwa sana, tunapongezana wote. La pili, kuhusu kila wilaya kuwa na shule ambayo itakuwa ni ya Kitaifa, kama nilivyojibu katika jibu langu lililotangulia kwa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir ni jukumu la kila wilaya, kuweka mikakati yao na kuileta Wizarani ili kutuelezea sisi wao wameamua ni shule ipi ambayo wangependa iwe ama ya Kimkoa au ya Kiwilaya na zile za Kitaifa ni jukumu la Wizara. Naomba tuelekee zaidi kwenye Halmashauri zetu kwa sababu sasa hivi ndiko kwenye maamuzi mengi makubwa ya kimaendeleo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, ingawa nimeletewa hapa *memo* kwamba ni kwa nini ninamruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri, kujibu maswali huku akiwa amekaa na hajasimama? Naomba niwathibitishie kwamba, alikuwa amesimama na hajakaa. Kwa hiyo, wale watu wanaofikiri amekaa, hawako sahihi. *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

Na. 287

**Ubovu wa Barabara ya Old Mwanza**

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya *Old Mwanza* toka Tabora kwenda Mwanza kupitia Bukene na Kahama kupitia Kata ya Semembela Jimbo la Bukene ni mbovu; na kwa kuwa Semembela ni eneo lenye rutuba sana, hali inayosababisha mazao kukubali; na kwa kuwa barabara hiyo itawasaidia Wananchi wa Kata hiyo jirani kufikisha mazao yao sokoni toka mashambani: Je, ni lini barabara hiyo itafufuliwa ili kuwasaidia wakulima kufikisha mazao yao sokoni, yaani Kahama, Mwanza, Burundi na Rwanda?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya *Old Mwanza*, toka Tabora kupitia Mambali na Semembela hadi Kahama, ipo chini ya uangalizi wa Wizara ya Miundombinu na TAMISEMI kama ifuatavyo: Sehemu ya barabara hiyo kutoka Tabora hadi Mambali yenye urefu wa kilometa 54.2 ni sehemu ya barabara ya Mkoa ya Kutoka

Tabora hadi Itobo, kilomita 117.2 na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Tabora. Sehemu ya barabara hiyo kutoka Mambali kwenda Semembela hadi Kahama ni barabara ya Wilaya ya Nzega. Kwa upande wa barabara ya Mkoa kutoka Tabora hadi Mambali, katika bajeti ya mwaka 2006/2007, ilifanyiwa ukarabati wa kiwango cha changarawe chini ya ufadhili wa *NORAD,* ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.14 kilitumika. Hadi sasa jumla ya kilometa 49 zimekarabatiwa na kazi itakamilika Agosti, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sehemu ya barabara hiyo kutoka Mambali hadi Kahama, inayohudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge, awasiliane na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ili kujua mipango ya Maendeleo na matengenezo waliyonayo ili iweze kutengenezwa na kuondoa kero kwa wananchi wa maeneo inamopitia barabara hiyo. Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Tabora, ipo tayari kutoka ushauri wa kitaalamu kama utahitajika.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, alipita katika sehemu hiyo wakati wa ziara yake; na kwa kuwa Wananchi wa Mambali walimwambia kuwa barabara ya kutoka Mambali kupitia Semembela ni muhimu sana kwa sababu ya mazao yanayolimwa katika Kata ya Semembela. Je, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri haoni ni wakati muafaka kufuata sauti ya Wananchi ambao ndiyo wanaojua umuhimu wa barabara hiyo ambapo sisi ni kama tunatekeleza?

Pili, kwa kuwa Halmashauri zetu tunazijua hali yake kifedha; na kwa kuwa barabara hiyo ni ya umuhimu sana kwa wakulima kupeleka mazao yao sokoni na hivyo kujikwamua katika umaskini. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuhakikisha inaichukua barabara hiyo kuipeleka *TANROADS* ili kuhakikisha wakulima wale wanajikwamua kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mimi na Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, tuliitembelea barabara hiyo na tulipofika pale Mambali, wananchi walitoa kilio kwamba barabara hiyo itengenezwe. Lakini tulipofika Itobo, mimi nikiwa na Mheshimiwa Mbunge, tulikutana na *Engineer* wa Nzega na nilishangaa nilipoambiwa kwamba, barabara hiyo wala siyo ya Wilaya ni ya Kijiji. Nilimshauri yeye na nilimshauri vilevile *DED* nilipofika Nzega kwamba, barabara hiyo angalau basi ianze kupandishwa kutoka barabara ya Kijiji kwenda kuwa barabara ya Wilaya ili ihudumiwe vizuri na Halmashauri ya Nzega. Ushauri huo sijui kama umetekelezwa. Namshauri Mheshimiwa Mbunge aendelee kufuatilia. Kuhusu kwamba ichukuliwe na *TANROADS,* kama nilivyosema, bado ni ya kijiji. Kwanza, wao waipandishe iwe barabara ya Wilaya, waanze kuihudumia na baadaye kama vigezo vitatosheleza, kulingana na Sheria ya Barabara, ambayo ilipitishwa hivi karibuni, tuone uwezekano baadaye wa kuipandisha

hiyo barabara iingie kwenye barabara za *TANROADS,* kama itakuwa imekidhi vigezo. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa katika mtandao wa barabara za Halmashauri zetu karibu zote zina mtandao mkubwa sana wa barabara kuliko mtandao wa barabara za Mkoa; na kwa kuwa Serikali inatoa fedha kidogo sana kwenye Halmashauri zetu; na kwa kuwa barabara hiyo inatoka kwenye barabara ya Mkoa na baadaye inakuwa barabara ya Kijiji; si busara sasa kuongeza kiwango cha fedha zinazokwenda kwenye Halmashauri ili ziweze kukidhi matengenezo ya barabara zote za Halmashauri na zile za Vijiji?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, mtandao wa barabara za Wilaya ni mkubwa kuliko za Mkoa, lakini matengenezo yanayohitajika kwenye barabara za Kitaifa ni makubwa, pamoja na kwamba mtandao ni mdogo na yanagharimu kiasi kikubwa zaidi kuliko matengenezo ambayo yanafanyika katika barabara za Wilaya. Hivyo, ni sahihi kabisa kwamba, barabara za Mkoa na Kitaifa, zipate fedha nyingi kuliko zile barabara za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba sasa fedha ziongezwe. Kwanza, tukubali na tutoe pongezi kwa Serikali, kwa kuongeza kiwango cha *Road Funds,* ambapo Halmashauri zetu mwaka jana zilikuwa zinapata takriban shilingi bilioni 25 kwa ajili ya barabara, lakini sasa kiwango hicho kimepandishwa mpaka shilingi bilioni 65. Tuone basi hizo shilingi bilioni 65 zitatumika vipi, kabla hatujasema tuongeze zaidi ya hapo. Tumeongeza zaidi ya asilimia 140 na ni kiwango kikubwa, kitumike vizuri na nina uhakika barabara zetu za Wilaya zitaboreshwa.

Na. 288

**Magari ya Mradi wa Maji – Ziwa Victoria**
**Kuharibu Barabara**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria ulipitisha magari ya mizigo mizito katika barabara za Mkoa na Wilaya Jimboni Misungwi na kusababisha uharibifu; na kwa kuwa Serikali kupitia Wizara husika, iliahidi kuwa ingetengeneza hasa Mkandarasi wa Mradi huo:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetolewa na Mkandarasi huyo kama fidia ya uharibifu wa barabara na madaraja?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani za kuzirudisha barabara hizo katika hali yake ili zipitike?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga, unajengwa katika Kandarasi tano. Kandarasi Namba 1 na 2 zipo katika Wilaya ya Misungwi. Katika ujenzi wa Mradi huu, vifaa mbalimbali yakiwemo mabomba ya chuma na viungio vyake, vilivyotengenezwa katika viwanda vya *TSP* na *ASP* vilivyoko Dar es Salaam na Nairobi, yalisafirishwa kwa barabara hadi maeneo ya ujenzi. Katika Wilaya ya Misungwi, Kandarasi Namba 1, inayotekelezwa na Mkandarasi *China Civil Engineering Construction Corporation,* inatumia barabara isiyokuwa ya lami inayotokea njia panda ya barabara ya Mwanza - Shinyanga kupitia - Misasi hadi Kijiji cha Ihelele na Kandarasi Namba 2 inayotekelezwa na Mkandarasi *Sinohydro Corporation,* ilitumia barabara hiyo kutoka Misasi hadi Kijiji cha Mwawile kupitia kitongoji cha Buhingo. Kazi za ulazaji wa mabomba kwa Kandarasi hizo imemalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikataba ya kazi kwa Kandarasi hizo mbili, Wakandarasi wanawajibika kuzifanyia matengenezo barabara hizo pale zinapoharibika, kutokana na wao kuzitumia kusafirishia vifaa vya ujenzi, pamoja na mabomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha shilingi milioni 143.6 zilitengwa na Wizara ya Maji kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara kwenye Kandarasi Namba 1 na 2, pale zinapoharibika kwa matumizi ya kusafirishia vifaa vya ujenzi wa mradi. Katika Kandarasi Namba 1, Mkandarasi ameshatumia kiasi cha shilingi milioni 63.5 na zimebakia shilingi milioni 46.1. Mkandarasi bado yupo eneo la mradi na kwa sasa anaendelea na ukarabati wa barabara ya Misasi hadi Kijiji cha Illujamate, pale inapoharibika kwa yeye kuitumia. Kazi za ujenzi wa Kandarasi Namba 2, zilimalizika tangu tarehe 14 Novemba, 2006. Mkandarasi alitumia kiasi cha shilingi milioni 34 katika kuifanyia matengenezo barabara aliyoitumia katika kusafirishia vifaa vya ujenzi na mabomba ya kandarasi hiyo. Hivyo, katika barabara hizo, kazi za matengenezo zilihusu pia matengenezo ya madaraja madogo (kalvati) pale yalipoharibika. Aidha, barabara hii pia ina daraja moja kubwa pekee lililopo Misasi, ambalo halikuathiriwa na upitishaji wa vifaa vya ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaratibu ujenzi wa Mradi huu, pamoja na matengenezo ya maeneo ya barabara ambazo zipo kwenye mikataba na Wakandarasi. Mhandisi Mshauri *Nor Consult International,* amekuwa akisimamia ujenzi wa mradi na matengenezo ya barabara ambazo zinaharibika kwa matumizi ya kusafirisha vifaa na mabomba ya ujenzi wa Mradi huu kwa kandarasi zote.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza, nampongeza kwa

jinsi anavyofuatilia matatizo yanayojitokeza kwenye barabara hiyo na shughuli zimeshaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wahandisi mbalimbali wa Maji na Wataalam wengine wanaofika kwenye Mradi huo, wamekuwa wakishauri kwamba, barabara hiyo ya kutoka Mwanangwa – Misasi – Buhingo – Sike - Mbalama – Ihelele, ijengwe kwa kiwango cha lami, kwa sababu ya kupitisha mizigo mingi zikiwemo dawa kwa ajili ya kuweka kwenye maji ya Mradi huo. Je, Wizara ya Maji, imeshawasiliana na Wizara ya Miundombinu kuhusu suala hilo?

La pili, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi imetengewa shilingi milioni 212 kwa ajili ya ujenzi wa barabara zake katika Halmashauri hiyo; na kwa kuwa barabara nyingi ni mbovu sana ikiwemo ya Misungwi kwenda Ngunge mpaka Mondo na ile ya kutoka Kabale - Ngobo - Mwamboko zitatumia fedha hizo; na kwa kuwa barabara hiyo ya Buhingo hadi Ihelele inasimamiwa na Halmashauri. Je, Wizara ya Maji au Wizara ya Miundombinu, itaendelea kuihudumia barabara hiyo kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi haina fedha za kuitengeneza?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ombi la barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami, kwa kuwa inatumika sana kwa kupitisha vifaa vingi na vizito kupeleka Ihelele. Naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, baada ya kumalizika kwa kazi hiyo ya ujenzi na ambapo umefikia kiwango cha zaidi 84 kwa 100, ndipo ambapo itajulikana baadaye kwamba, mizigo ya aina gani itapelekwa huko. Lakini hata hivyo, nitamwomba suala hilo nilipokee na kushauriana na wenzetu wa Wizara ya Miundombinu, kujua uwezekano gani ambao unaweza ukawepo juu ya jambo kama hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili lilikuwa linahusu barabara hiyo kwamba, kwa kuwa Halmashauri haina uwezo wa kuitengeneza hiyo barbara. Je, Wizara ya Maji inaweza kuendelea kuitengeneza? Kuhusu hilo nilikuwa napenda nimfahamishe kwamba, Mkataba wa sisi na barabara hizo ni kwa kipindi ambacho tunapitisha vifaa vyetu kwa ajili ya Mradi wa Maji. Mara mradi huo wa maji utakapomalizika, naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba, ajaribu kwa kutumia Halmashauri yake, waweze kupeleka ombi hilo na kushauriana na Wizara ya Miundombinu.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo hili katika barabara ya Wilaya ya Misungwi, linafanana kabisa na la barabara inayotoka *Old Shinyanga* kupitia Isheremangazi kwenda Sarawe. Malori yanayobeba mabomba ya maji na hasa Mkandarasi Namba 3 na 4 wapo katika Jimbo la Solwa na wameharibu vibaya sana ile barabara kutokana na malori mengi kubeba mabomba ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri, anipe maelezo au majibu mazuri kwa sababu nimemsikia amesema kwamba, Wizara imetenga shilingi milioni 212 kwa ajili ya kukarabati. Je, barabara hiyo ipo katika mpango wa kukarabatiwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Wilaya ya Shinyanga, vijiji ambavyo kwa njia moja au nyingine, barabara zake zimeathirika na vijiji hivyo ndivyo ambavyo vitalipwa fidia na baadhi ya wananchi huko wamelipwa fidia. Vijiji vilivyoharibika ni kama vifuatavyo:-

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kama vijiji viko vingi, ningeshauri labda uonane na Mheshimiwa Mbunge, uweze kumpa hivyo vijiji kwa nafasi nzuri zaidi. Maana yake nimechungulia orodha yako nimeona vipo vingi zaidi. Nafikiri mkikaa pamoja, ataelewa vizuri zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa ushauri wako, ila nimalizie tu kwa kumwambia kwamba, Solwa Kijiji cha Miseme kipo katika orodha ya fidia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ahmed A. Salum, nafikiri umefurahi kusikia angalau hivyo vipo katika mpango huo.

Na. 289

**Uchimbaji wa Visima Virefu vya Maji**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA (K.n.y. MHE. YONO S. KEVELA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, ukarabati wa Mradi wa Maji wa Wanging'ombe umechelewa na hivyo kuleta matatizo ya maji katika Vijiji vya Lyamluki, Lyadebwe na Saja. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwachimbia visima virefu vya kudumu wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, naomba kutoa maelezo mafupi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Wanging'ombe ulijengwa kwa ufadhili wa Shirika la *UNICEF,* kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 5.5 na Serikali ya Tanzania ilichangia kiasi cha shilingi milioni 15. Ujenzi wa Mradi ulikamilika mwaka 1977. Vyanzo vikuu vya Mradi huu ni Mito ya Mbukwa na Mtitafu, ambavyo kwa ujumla vinatoa maji kiasi cha meta za ujazo 12,700 kwa siku.

Mradi ulibuniwa kutoa huduma kwenye vijiji 63, lakini vijiji 60 vikiwemo Vijiji vya Lyamluki, Lyadebwe na Saja, ndivyo vilipata maji kutoka kwenye Mradi huo, baada

ya ujenzi kukamilika. Vijiji vitatu vilivyobaki, pamoja na chujio la maji, havikuweza kukamilika kutokana na fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Mradi huu kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji sita vya Kijombe, Ngamanga, Mtewele, Katenge, Ikulimambo na Uhenga, havipati maji vizuri kutokana na uchakavu wa matanki ya maji, mabomba na viungio. Aidha, vijiji vitatu vya Lyamluki, Lyadebwe na Saja ambavyo viko mwisho wa bomba kuu, kwa sasa havipati maji kutoka kwenye Mradi kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya maji katika vijiji vya njiani na upungufu wa maji kwenye vyanzo unaotokana na shughuli za kilimo cha Vinyungu, kinachoendeshwa kwenye maeneo ya vyanzo vya maji vya Mbukwa na Mtitafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye maelezo ya utangulizi, upungufu wa maji kwenye vyanzo unatokana na shughuli za kilimo cha Vinyungu usiodhibitiwa. Tathmini inaonesha kuwa, Vijiji vya Lyamluki, Lyadebwe na Saja, vinaweza kupata huduma ya maji kutoka kwenye Mradi wa Wanging'ombe kama matumizi ya maji ya mito ya Mkubwa na Mtitafu yatasimamiwa kikamilifu. Hivyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na uongozi wa Wilaya, kuweka taratibu nzuri zaidi za matumizi ya maji kutoka kwenye vyanzo. Hatua hii itawezesha maji kupatikana kwenye vijiji ambavyo kwa sasa havipati maji na kwa hali hiyo, miundombinu iliyowekwa kwa gharama kubwa inaweza kutumika badala ya Serikali kuingia gharama nyingine ya kuchimba visima virefu. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Maji, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna vijiji ambavyo vinahudumiwa na *Quick wins* na sera ya maji ni kuchangia Mifuko ya Maji, wananchi pamoja na Halmashauri husika; na kwa kuwa baadhi ya Halmashauri tumeshachangia Mifuko ya Maji, kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa tumechangia shilingi milioni 15. Je, miradi hiyo ya *Quick wins,* pamoja na Miradi ya Benki ya Dunia, itaanza kutekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwanza, napenda kumpa pongezi kwa ajili ya Halmashauri yake kuweza kufikisha mchango wa wananchi wake shilingi milioni 15, hiyo ni hatua kubwa sana. Lakini pia napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa hivi sasa miradi ya *Quick wins* imeshaanza katika Halmashauri mbalimbali, fedha tumeshatuma kwenye Halmashauri 84 na Halmashauri 37 hatukutuma fedha kwa sababu hazijatimiza masharti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, imefuzu masharti kwa kipindi cha 2007/2008. Kwa hali hiyo, mgao utakaofuatia kuanzia sasa, Halmashauri yake itapata fedha za *Quick wins* na pia itapata fedha za Benki ya Dunia, ambayo tunaita *World Bank*. Napenda pia kuzifahamisha Halmashauri za Wilaya nyingine zote kwamba, Miradi ya *World Bank* kwa sasa hivi tumekamilisha taratibu zote zilizokuwa zinatakiwa

na Mfadhili. Sasa kilichobaki, tunangoja tuweze kuingiziwa fedha ili tuweze kuzigawa katika Halmashauri mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako mazuri ya ufafanuzi ambao umewasaidia, nafikiri karibu Waheshimiwa Wabunge wote walihitaji kupata hizo taarifa muhimu.

Na. 290

**Kuwaendeleza Kitaaluma AMOs**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Madaktari Wasaidizi *(AMOs)* elimu endelevu ya *Post Graduate Diploma* na baadaye *Masters Degree* hasa ikitiliwa maanani kuwa kiutendaji, *Assistant Medical Officer* na *Medical Officer* ni wamoja na kimsingi ndio Madaktari wanaotegemewa sana katika Hospitali za Wilaya, Mikoa na Vijiji?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda, kujibu swali la Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Madaktari Wasaidizi ni wataalam wanaotegemewa sana katika hospitali zetu za Mikoa, Wilaya na hata Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa kuwaendeleza Madaktari Wasaidizi *(AMOs)*, baada ya kuhitimu mafunzo yao ya awali ya miaka miwili, Wizara ilianzisha Mafunzo Malaum ya Ubingwa *(specialities)* katika nyanja za Radiologia *(Radiology)*, Macho *(Ophthalmology),* Nusu Kaputi *(Anaesthesia),* magonjwa ya akili *(Psychiatry)* na magonjwa ya ngozi *(Dermatovenerology),* kwa kada hii. Mafunzo haya ni ya muda wa miaka miwili kwa kiwango cha stashahada ya juu.Aidha, upo mpango wa kuwaendeleza Wataalam wa Sekta ya Afya kupitia Kamati ya Ufadhili wa Mafunzo ya Wizara. Katika mpango huu, Madaktari Wasaidizi hufadhiliwa kuhudhuria mafunzo mbalimbali katika ngazi ya Shahada ya Uzamili na Shahada ya Falsafa ndani na nje ya nchi.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amekubaliana nami kwamba, ni muhimu kutoa mafunzo kwa Madaktari na hivi karibuni inatakiwa kila Kata kuwepo na Zahanati. Kwa hiyo, inaonekana ni mpango ambao unatakiwa uwe endelevu. Sasa amesema kwamba, upo mpango wa kuwaendeleza Wataalam wa Sekta ya Afya kwa kupitia Kamati ya Ufadhili ya Mafunzo ya Wizara. Hajatupa *timeframe,* huwa inatokea mara ngapi au mpango huo unaanza lini? Hilo ndilo swali langu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, nimesema upo mpango wa kuendeleza wataalam na kwa maana hiyo, mpango huo upo na umeendelea kuwepo.

Na. 291

**Utekelezaji wa Mradi wa *TASAF 1***

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa *TASAF* imeahidi kukamilisha miradi ambayo haikukamilika katika awamu ya kwanza kama ilivyowasilishwa kwenye Bajeti ya mwaka 2006/2007; na kwa kuwa katika barabara iliyoanzia Vijiji vya Mjimbini, Tanga Mkwajuni, Tanga Michikichini hadi Kukuu katika Shehia za Mjimbini na katika Shehia ya Kangani, ambapo matengenezo ya barabara Awamu ya *TASAF 1* kiliondoshwa kifusi katika barabara hiyo na kuacha udongo tu, hali iliyosababisha barabara hiyo kuwa mbovu kuliko ilivyokuwa hapo awali:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizosababisha barabara hiyo isiwekwe kifusi kipindi hicho cha *TASAF 1* kama ilivyoahidiwa katika Bajeti ya mwaka 2006/2007?

(b) Je, ni lini ufumbuzi wa kero hiyo utapatikana haraka iwezekanavyo?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Katika utekelezaji wa shughuli za awamu ya kwanza, *TASAF* ilichangia katika miradi iliyolenga kutatua kero na kuboresha hali ya maisha ya wananchi. Aidha, kwa kuzishirikisha jamii kuchangia rasilimali katika utekelezaji wa miradi husika iliyojulikana kama Miradi ya Jamii au kulipa ujira kwa kazi iliyofanywa na walengwa katika kutekeleza miradi hiyo iliyojulikana kama Miradi ya Ujenzi. Aina ya pili ya miradi ililenga kuzinusuru kaya maskini kwa kuwapatia walengwa ajira za muda mfupi ili kukuza kipato chao. Ubainishaji wa jamii lengwa *(targeting),* katika awamu ya kwanza ya *TASAF* ulifanywa na Ofisi ya Waziri Kiongozi, kwa upande wa Zanzibar au Halmashauri za Wilaya/Miji husika kwa Tanzania Bara, kulingana na vigezo vya umaskini vilivyoandaliwa *(Poverty Profile).* Baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuthibitisha ubovu wa barabara ya Kangani na ukaguzi wa daraja ambalo lilitakiwa kuvunjwa na kujengwa upya, *TASAF* iliafiki kuongeza mchango wake wa kuichonga barabara hiyo urefu wa km. 6.5 na kufukia kifusi kwenye maeneo korofi urefu wa km. 2. Mradi wa Ukarabati wa Daraja na Barabara ya Kangani ambao uliunganisha Vijiji vya Mjimbini, Tanga hadi Kangani, ulitekelezwa

kuanzia tarehe 18 Februari, 2002 na kukamilika tarehe 30 Desemba, 2002, kwa gharama ya shilingi 43,947,700 kwa kiwango cha kifusi kama ilivyoainishwa na Mhandisi husika. Katika Mradi huo, *TASAF* ilichangia shilingi 39,035,500 na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilichangia shilingi 4,912,200. Kati ya fedha hizo, walengwa walilipwa shilingi 16,855,200, kama ujira baada ya kufanya kazi katika Mradi. Mradi ulikamilika na kupewa hati ya kukamilishwa baada ya Mhandisi, yaani Wapemba kuridhika na kiwango kama ilivyopangwa. Hivyo, jukumu la kuhakikisha barabara inabaki kwenye ubora wake ni la jamii yenyewe. Walengwa 646 walipata ajira ya muda mfupi na kukuza stadi/ujuzi wa kutengeneza barabara kwa kiwango cha barabara za udongo. Kurejewa kwa ubovu wa barabara hiyo kunatokana na kukosa matengenezo ya mara kwa mara, hasa ukizingatia mvua zinazoonyesha, kiwango (udongo) na matumizi ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa viongozi husika, akiwemo Mheshimiwa Mbunge, kuihamasisha jamii kutambua kero hiyo ya ubovu wa barabara na hivyo kufanya matengenezo ya mara kwa mara, kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya Serikali na mashirika binafsi. Kufanya hivyo kutaleta ufumbuzi wa kudumu kwa tatizo hilo.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo tu la nyongeza. Tangu Serikali itangaze azma yake hiyo mwaka jana ni miradi mingapi na miradi ya aina gani na kutoka maeneo gani, imekamilishwa katika Visiwa wa Unguja na Pemba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kama utakuwa unaweza kufahamu, maana yake ni swali linalotaka idadi ya miradi mingi zaidi ya hiyo iliyoulizwa.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la takwimu namna hiyo linahitaji maandalizi. Kwa hiyo, naomba liwasilishwe kwa utaratibu unaojulikana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na tukiendelea sasa tutakuwa tunaingia kuomba kwamba, tutumie dakika nyingine za ziada. Kwa hiyo, naomba kusema kwamba, maswali ambayo tulikuwa nayo leo hapa mezani yote yamekwisha. Kabla hatujaendelea na hatua inayofuata, naomba niwape matangazo yaliyopo mezani kwangu.

Waheshimiwa Wabunge tangazo la kwanza linaniomba niwafahamishe kwamba Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii ana wageni wake wafuatao hapa ndani leo. Mgeni wa kwanza kabisa ni mke wake Mama Kudra Maghembe, ningeomba asimame tumfahamu. Karibu sana Mama Kudra kwa kushirikiana nasi na hasa kumpa moyo Professa Maghembe kwenye siku yake hii muhimu ya kusoma Bajeti. Watoto wake Namchenga na mwingine Namvumo. Mdogo wake Sekeu-Toure Mndeme, ambaye ni Mkurugenzi katika Benki ya *CRDB*. Naona huyo hayupo. *(Makofi)*

Naomba niendelee kutambulisha pia yuko Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii Bibi Blandina Nyoni, nadhani yuko tayari kwenye kiti chake kwa ajili ya kuanza kazi. Yuko pia Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro Mheshimiwa Sana Pius Msekwa, Spika Mstaafu na yeye bado hajaingia hapa ndani. Yuko Mwenyekiti wa Bodi ya *TANAPA,* Kanali Emmanuel Balele, yuko Mwenyekiti wa *TAFORI* Prof. Gabriel Mbassa, yuko Mwenyekti wa Bodi ya *TWPF,* Prof. Salome Miana na Mjumbe wa Bodi. Yuko Mjumbe wa Bodi pia Mheshimiwa Eliachim Simpassa, naona amesimama na Mwenyekiti wa Bodi. Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Eliachim Simpassa alikuwa Mbunge pia katika Bunge lililopita.

Waheshimiwa Wabunge naomba niwafahamishe kwamba wako wanafunzi wa Shule ya Jeneral Msuguri, Dodoma. Ningeomba kama wapo hao wanafunzi wasimame. Karibuni sana wanafunzi. Pia wako wanafunzi wa Shule ya Msingi Kilimani, Dodoma. Karibuni sana watoto wetu. Waheshimiwa Wabunge ningeomba nitoe tangazo lingine Katibu wa Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi anaomba niwatangazie Wabunge hao kwamba mpaka sasa ofisi yake bado haijapokea picha za Waheshimiwa Wabunge na madereva wao kwa maandalizi ya Mkutano Mkuu. Kwa hali hiyo anaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote ifikapo mwisho wa wiki hii picha hizo wawe wameshaziwasilisha kwenye Ofisi ya Katibu wetu. Ni Wabunge 56 tu ndio waliofanya kazi hiyo. Kwa hiyo naomba sana Waheshimiwa Wabunge tuwasilishe picha hizo hasa wale Wabunge wa CCM.

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine ninaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Wakumbuke leo tarehe 25 Julai, 2007 tutakuwa na kikao chetu kuanzia saa 7.00 mchana lakini kikao hicho tumekihamishia ukumbi wa *Dodoma Hotel*. Kwa hiyo tunawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Maendeleo ya Jamii mfike bila kukosa. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Mheshimiwa George Lubeleje ameniomba pia niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 25 Julai, 2007 kutakuwa na kikao maalum kwa ajili kuhariri Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria, kitakachofanyika katika ukumbi namba 133 ghorofa ya Kwanza Jengo la Utawala. Kikao hicho kitafanyika saa 5.30 asubuhi hii. Kwa hiyo, Wajumbe wote wa Kamati ile ya Katiba, Sheria na Utawala mnaombwa mhudhurie. Tunao wageni wengine pia wanafunzi kutoka Shule ya Uhuru Mjini Dodoma, naomba na wao wanafunzi wetu kama wapo kutoka Shule ya Uhuru wasimame. Karibuni sana watoto wetu Wabunge la kesho.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama anaomba kuwatambulisha wageni wake wanaotoka Shirika moja Lisilo la Kiserikali linaloitwa *Tanzania Coalition on Debt and Development (TCDO).* Makao yao Makuu ni Dar es Salaam na viongozi hao ni kama wafuatao. Kuna Bwana Chamber Max Kajege tena ni kaka yake Mheshimiwa Kajege huyo, yupo hapa ndani, Ebron Mwakagenda na Naitapa Lemea. Hao ni wageni wangu lakini pia ni wageni wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii.

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, ameniomba niwatambulishe wageni wake, Ndugu Elisha Mwenyekiti wa TUGHE Mkoa wa Tabora, Ndugu Mkwama Mratibu wa *TUCTA* Mkoa wa Tabora. Huyu Mheshimiwa Kaboyonga naona anajali sana mambo ya wafanyakazi wake huko. Lakini pia nimeombwa na Mheshimiwa Benito Malangalila anasema nimtambulishe mgeni wake ambaye cheo chake ni Naibu Kamanda Vijana CCM Wilaya ya Mufindi na Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM. Huyo mgeni anaitwa Godfrey Mosha. Karibu sana mgeni wa Mheshimiwa Malangalila.

Waheshimiwa Wabunge tangazo langu la mwisho hapa nimepata maoni kutoka kwa Wabunge takriban watano (5) wananiomba nitoe mwongozo kwa nini utaratibu wa kuondoka magari yamekuwa yakisumbua hapo mbele ya ukumbi wetu wa Bunge. Sasa naomba kuwaambie suala hili nalipeleka kwa Katibu wa Bunge yeye ataweka utaratibu mzuri wakati wa kuahirisha vikao vyetu tuweze kuondokaje kwa utaratibu mzuri hapo nje.Hayo ndiyo matangazo ambayo yalikuwa hapa mezani kwangu na baada ya kutoa matangazo hayo basi nimwombe Katibu atuongoze na shughuli inayofuata. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2007/2008
### Wizara ya Maliasili na Utalii

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira iliyowasilishwa leo asubuhi juu ya makadirio na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2007/2008, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye kupitisha Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Asasi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa kwa kuchambua, kujadili na hatimaye kupitisha makadirio ya Wizara yangu. Napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa, Wizara yangu imezingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na itaendelea kupokea mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitangulize shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuniteua kuiongoza Wizara ya Maliasili na Utalii. Nitaendelea kushirikiana kwa dhati na Waheshimiwa Wabunge pamoja na wadau wengine katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ili mchango wake katika pato la taifa uongezeke kwa kiasi kikubwa.Aidha, napenda kuchukua nafasi hii, kukupa pole, Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa misiba mikubwa iliyotupata ya kuondokewa na waliokuwa Wabunge wenzetu marehemu Juma Jamaldini Akukweti aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Masuala ya Bunge na Amina Chifupa Mpakanjia, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Vijana (CCM). Nawapa pole familia za marehemu na Watanzania wote kwa ujumla na kuziombea roho za marehemu, Mwenyezi Mungu aziweke pahala pema peponi, Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwapongeze Mhe. Mtutura Abdallah Mtutura kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Tunduru na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya Kwanza ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2006/2007, Sehemu ya Pili ni Mpango wa Utekelezaji kwa Mwaka 2007/2008 na Sehemu ya Tatu ni Hitimisho. Maelezo yaliyotolewa katika sehemu zote tatu, yamezingatia mgawanyo wa kazi kisekta, sera na sheria zinazoongoza hifadhi za rasilimali, malikale na uendelezaji utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imezingatia pamoja na mambo mengine, Maagizo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wakati alipolihutubia Bunge mwezi Desemba 2005, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika vikao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jukumu kubwa la Sekta ya Wanyamapori ni kuhakikisha kwamba wanyamapori wanaendelea kuwepo katika mazingira yao na wananchi wanashiriki katika kuwahifadhi na kuwatumia kiendelevu kwa manufaa ya nchi yetu. Katika kutekeleza majukumu hayo, mwaka 2006/2007, Wizara yangu ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukamilisha marekebisho ya Sera ya Wanyamapori ambayo ilipitishwa mwezi Machi 2007. Marekebisho ya Sera hii yatawezesha usimamizi madhubuti zaidi wa uhifadhi na matumizi endelevu ya Wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kuandaa Kanuni za uanzishaji wa mashamba ya Kufuga Wanyamapori na Kanuni za biashara ya Viumbe hai umeanza kwa kuwapata wataalam waelekezi. Vilevile, tathmini ya utekelezaji wa Kanuni za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (*WMAs)* ilifanyika na taarifa yake ilijadiliwa katika mkutano wa wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ahadi iliyotolewa kwenye Bunge la Bajeti mwaka jana kuhusu tathmini ya Uwindaji wa Kitalii, Wizara ilianzisha mchakato wa kuwezesha Taifa kufaidika zaidi na rasilimali ya wanyamapori katika sekta ya uwindaji wa kitalii. Aidha, Wizara yangu ilipitia ada mbalimbali ili kuzirekebisha zilingane na zile zinazotozwa katika nchi jirani hususan Jumuiya ya Kimaendeleo ya nchi Kusini mwa Afrika - *SADC*. Lengo ni kuhakikisha kuwa kiwango cha maduhuli kinachopatikana kinaongezeka na kuwezesha Serikali kumudu gharama kubwa za kuhifadhi maliasili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilitekeleza jukumu la kulinda rasilimali ya wanyamapori kwa kuendesha doria, kutoa mafunzo na kununua vifaa. Katika kazi hiyo jumla ya siku za doria 62,137 zilitumika ndani na nje ya mapori ya akiba. Aidha, watumishi 37 walipatiwa mafunzo maalum ya mbinu za kukabiliana na majangili hususan ulinzi wa Faru katika Mapori ya Akiba ya Ikorongo na Grumeti. *(Makofi)*

Ili kuimarisha Vikosi vya Doria dhidi ya uwindaji haramu unaofanywa na majangili, Wizara ilipata msaada wa silaha 700 za aina mbalimbali, risasi na magari ya doria 20 kutoka kwa wakereketwa wa uhifadhi wa wanyamapori. *(Makofi)*

Katika kupambana na ujangili, askari wanyamapori walikamata watuhumiwa 1,013 kwa makosa ya kuingia, kuwinda na kuvua samaki katika maeneo yaliyohifadhiwa na kupatikana na nyara na silaha kinyume cha sheria. Kesi 551 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali na kati ya hizo, kesi 211 zilimalizika kwa watuhumiwa 393 kukiri makosa na kulipa faini ya jumla ya Shs. 38,445,994 na watuhumiwa 43 kufungwa jela jumla ya miezi 423.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2006/2007, Wizara ilipokea taarifa kuhusu matukio ya watu kushambuliwa na mamba katika maeneo mbalimbali ikiwemo mito na mabwawa katika Wilaya za Mbozi na Kyela, Mito ya Ruvu, Rufiji, Malagarasi, Ugalla, Zigi, Momba, Pangani, Ruhuhu na Kilombero. Maeneo mengine ni Ziwa Nyasa, Rukwa na mabwawa ya Nyumba ya Mungu, Hokororo na Mtera. Wizara ilishirikiana na uongozi wa wilaya husika kwa kutoa risasi, magari na wataalam wa wanyamapori ili kukabiliana na matukio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuwadhibiti Kunguru weusi ambao ni kero kubwa na tishio kwa wananchi, mazingira na viumbe wengine, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kupambana na ndege hao. Katika kipindi cha kuanzia tarehe 27/10/2006 hadi tarehe 7/6/2007 jumla ya mitego 65 ya kuwakamata imetengenezwa na kusambazwa katika maeneo 36 Jijini Dar es Salaam. Kunguru 11,427 wamekamatwa kwenye mitego hiyo na kuteketezwa. Vilevile, kemikali aina ya *DRC - 1339* ilinunuliwa kutoka New Zealand na kufanyiwa majaribio na wataalamu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu katika nchi za Tropiki (*Tropical Pesticides Research Institute (TPRI).* Majaribio ya kemikali hii yameonyesha mafanikio makubwa katika kuwaangamiza kunguru hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia umuhimu wa kuhifadhi vyanzo vya maji, Wizara iliandaa Rasimu ya Mkakati wa Kitaifa wa Kuhifadhi Ardhioevu. Utekelezaji wa programu ya usimamizi endelevu wa ardhioevu katika Wilaya tisa za Mikoa ya Mbeya na Iringa na Mapori ya Akiba ya Usangu, Mpanga-Kipengele na Rukwa/Lukwati ulifanyika. Katika mikoa ya Mbeya na Iringa jumla ya Shilingi 263 milioni zilitumika katika wilaya tisa (9) kuendesha miradi isiyoharibu mazingira. Kati ya wanachama 600 wa vikundi vya ujasiriamali vilivyosajiliwa wanachama 200 kati yao wamepatiwa mafunzo kuhusu ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha miundombinu kwa ajili ya uhifadhi, Wizara ilikarabati kilomita 282 za barabara na viwanja vinane vya ndege katika Mapori ya Akiba ya *Selous,* Rungwa, Maswa, Rukwa-Lukwati, Mpanga-Kipengele, Liparamba na Lukwika-Lumesule-Msanjesi. Wizara ilichukua hatua mbalimbali kuhifadhi rasilimali za wanyamapori. Kufuatia ahadi iliyotolewa katika Bunge la Bajeti mwaka jana, Wizara iliandaa rasimu ya kwanza ya Mpango wa Usimamizi na Uendeshaji wa Pori la Akiba Maswa (*General Management Plan*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa Sera ya Wanyamapori ni kushirikisha jamii katika kuhifadhi na kunufaika na rasilimali za wanyamapori. Maeneo nane ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori *(WMAs)* kati ya kumi na sita yalipatiwa Haki ya Matumizi. Aidha, washiriki 43 kutoka Jumuiya nne walipata mafunzo ya ujasiriamali katika kituo cha ujasiriamali cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kati ya *WMA* nane zilizopatiwa Haki ya matumizi, Jumuiya tano ambazo ni; Ipole, Uyumbu, Ngarambe/Tapika, Burunge na Ikona zilinufaika na mgawo wa jumla ya Shilingi 74, 074,705. Kiasi hicho kilikuwa ni mafao yatokanayo na uwindaji wa kitalii katika maeneo yao, chini ya utaratibu wa kugawana mapato kati ya Hazina, Wizara, na Halmashauri za Wilaya.

Wizara ilitoa mafunzo kwa wananchi ili kuwajengea uwezo na ufanisi katika kushiriki kuhifadhi maliasili kwenye maeneo ya ardhi za vijiji. Mafunzo hayo yalitolewa na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi Maliasili kwa Jamii cha Likuyu-Sekamaganga katika Wilaya ya Namtumbo na Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi katika Jiji la Mwanza. Katika mwaka huu, jumla ya wananchi 143 kutoka maeneo mbalimbali nchini wamepatiwa mafunzo ya kuhifadhi maliasili katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jukumu kuu la Taasisi ni kufanya, kuratibu na kusimamia utafiti wa wanyamapori hapa nchini. Katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 utafiti ulifanyika katika maeneo yafuatayo:-

- Uchunguzi wa aina za nyuki na mimea inayotumiwa na nyuki katika Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

- Uchunguzi wa magonjwa ya wanyamapori ndani ya hifadhi za Taifa za Arusha, Serengeti, Ziwa Manyara na eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

- Mahusiano ya watu na tembo katika maeneo ya magharibi mwa Serengeti katika Wilaya za Serengeti na Bunda.

- Kufuatilia kurudi na kuongezeka kwa mbwa mwitu katika Hifadhi za Serengeti na Ngorongoro. Jumla ya mbwa mwitu 57 wameshatambuliwa na kumbukumbu zao zinafahamika kwa njia ya picha.

- Ukusanyaji wa takwimu za mtawanyiko wa aina mbalimbali za mammalia Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Sensa ya wanyamapori ni muhimu sana ili kuweza kupanga matumizi endelevu ya rasilimali hii. Katika kipindi cha 2006/2007 Taasisi iliendesha Sensa za wanyamapori zilizofanyika katika maeneo ya Hifadhi za Taifa za Katavi, Ruaha, Serengeti, Tarangire na Ziwa Manyara. Vile vile katika Mapori ya Akiba ya Kigosi, Moyowosi, Rungwa, Selous na Ugalla na kwenye maeneo yanayozunguka mapori yaliyohifadhiwa. Sensa hizo zilibaini kuwa idadi ya tembo kwa ujumla imeongezeka kutoka 121,000 mwaka 2003 hadi kufikia tembo 142,000 mwaka 2006.

Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 15, kwa nchi nzima. Matokeo haya yanadhihirisha kazi nzuri ya ulinzi iliyofanywa na wahifadhi katika maeneo yao ya kazi. Idadi ya wanyama wengine kama vile nyati, pofu, twiga, kiboko, simba, nyemera, ngiri, na pundamilia haikubadilika ikilinganishwa na sensa zilizotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** mojawapo ya majukumu ya Taasisi ni kujenga uwezo wa kitaalam kwa wananchi ili kuboresha mbinu za uzalishaji wa mazao ya nyuki hivyo kuinua vipato vyao. Kwa kuzingatia hayo, Taasisi iliendesha mafunzo ya ufugaji nyuki kwa njia za kisasa kwa wafugaji kutoka Wilaya nne ambazo ni Kiteto (6), Ngorongoro (55), Chunya (9) na Bagamoyo (84). Aidha, Taasisi ilitoa mafunzo ya ugani kwa Maafisa 26 kutoka Mkoa wa Mara na Maafisa 9 kutoka *Natural Forest Resources Management and Agroforestry Centre (NAFRAC)* Shinyanga. Pia mafunzo ya ugani yalitolewa kwa wataalamu kutoka nje ya nchi kama ifuatavyo; Uingereza (7) Uholanzi (2) na Botswana (2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu makuu ya Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* ni kutunza na kuendeleza maeneo yote yaliyotengwa kama Hifadhi za Taifa kwa manufaa ya Watanzania na jumuia ya kimataifa. Katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007, Shirika lilifanya mapitio ya mpango mkakati wake utakaotumika kuanzia mwaka huu 2007/2008 hadi 2011/2012. Mpango huo umeainisha baadhi ya maeneo yatakayopewa kipaumbele kama ifuatavyo:

- Kuhifadhi maeneo kwa kutumia mbinu za kisasa za uhifadhi na utaalamu bora;

- Kukuza na kupanua utalii katika hifadhi za mashariki, magharibi na kusini mwa nchi yetu ili kuongeza wigo wa biashara ya utalii na hivyo kuongeza ajira; na

- Kuimarisha mahusiano na ushirikiano kati ya Hifadhi na wananchi walio jirani ili kuboresha ulinzi wa rasilimali ya wanyamapori ndani na nje Hifadhi zilizopo jirani nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania lilisimamia uhifadhi wa maliasili na mazingira; kufanya doria za uzuiaji ujangili na kuangalia mwenendo wa shughuli za utalii ndani ya hifadhi ili kuhakikisha kuwa hifadhi zetu zinabakia kuwa kivutio kikubwa cha watalii.

Kati ya Julai 2006 na Machi 2007, idadi ya watalii ilifikia 557,370 na kuingizia Shirika Shilingi 58.3 bilioni. Mafanikio hayo yalitokana na juhudi kubwa za kutangaza utalii na vivutio vya utalii nje ya nchi na uboreshaji wa miundombinu, hususan barabara. Jumla ya barabara zenye urefu wa kilometa 1954 zilifanyiwa ukarabati katika Hifadhi za Taifa zifuatazo; Arusha (50 km), Katavi (67km), Kilimanjaro (37km) *Lake Manyara (70),* Mikumi, (60km), Ruaha (400), Saadani (150km), Serengeti (1000 km) ) na Tarangire (120 km)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimara wa Shirika ni pamoja na ubora wa watumishi wake na motisha mbali mbali wanazopata ili kuchochea utendaji wao na hivyo kuongeza tija kazini. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Shirika liliboresha masilahi ya watumishi kwa

kuongeza mishahara yao kwa asilimia 80. Aidha Shirika lilianzisha bima maalum ya wafanyakazi *(Group Endowment Assurance Scheme)* ili kuwawezesha watumishi wa muda mrefu (zaidi ya miaka 10) wa Shirika kupata mafao bora zaidi wanapostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudumisha ushirikiano na vijiji vilivyo jirani na Hifadhi za Taifa, Shirika linatekeleza mpango wa ujirani mwema kila mwaka. Katika kipindi cha 2006/2007, Shirika lilitumia jumla ya Shilingi 940,484,800 kusaidia miradi ya maendeleo iliyoanzishwa na wananchi. Fedha hizo zilitumika katika kazi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa madarasa, mabweni, nyumba za walimu, zahanati, barabara, ununuzi wa samani, na huduma za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mojawapo ya mahitaji ya Sera ya Wanyamapori na mwongozo wa kusimamia na kuendeleza Hifadhi za Taifa ni kuhakikisha kila eneo la hifadhi lina Mpango wa Usimamizi na Uendelezaji *(General Management Plan*). Katika kipindi cha 2006/2007, Shirika lilikamilisha kuandaa mipango ya Usimamizi na Uendelezaji wa Hifadhi za Taifa za Serengeti, Mahale, Mikumi na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka inasimamia Eneo la Ngorongoro linalojumuisha hifadhi ya wanyamapori na makazi ya watu. Katika vijiji vinavyozunguka Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, miradi ya ujirani mwema iliyotekelezwa ni pamoja na mradi wa maji wa Makhoromba (Karatu) ujenzi wa Shule za Sekondari Malambo, Loliondo na Digodigo katika Wilaya ya Ngorongoro, ujenzi wa Shule ya Sekondari Welwel katika Wilaya ya Karatu, mradi wa maji wa Shule ya Sekondari Banjika (Karatu), ujenzi wa madarasa, Shule ya Msingi Lositete (Karatu) na mradi wa *Laja Wildlife Corridor (Mbulu).* Aidha, Mamlaka ilitoa huduma mbalimbali za kijamii kwa wananchi katika Wilaya kadhaa ikiwemo Wilaya za Bukoba, Arumeru, Arusha, Monduli, Karatu, Mbulu, Ngorongoro, Musoma, Bunda, Ukerewe, Nzega na Kongwa. Jumla ya Shilingi 264,578,100 zilitumika katika miradi hiyo.

Uendelezaji wa Kreta ya Embakai ulifanyika kwa kukarabati urefu wa kilomita 12 za barabara kutoka eneo la *View point* hadi Lemala ili watalii waweze kutembelea eneo hilo. Jumla ya kilomita 331 za barabara ndani ya Hifadhi zilikarabatiwa katika mwaka 2006/2007. Ili kuboresha huduma za jamii, Shirika lilijenga madarasa matano, tanki la maji na kufanya marekebisho ya chanzo cha maji katika shule ya Sekondari Embarway.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya watalii waliotembelea Hifadhi ya Ngorongoro katika kipindi cha Julai 2006 hadi Machi 2007 ni 301,527 (watalii 221,446 ni kutoka nje ya nchi na 80,061 ni watalii wa ndani) ambao kwa pamoja waliliingizia Shirika jumla ya Shilingi 24.7 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania ulikusanya Shilingi 7.0 bilioni. Fedha hizo zilitumika katika kuimarisha doria za uzuiaji ujangili, utafiti, mafunzo ya uhifadhi na kazi za maendeleo katika Mapori ya Akiba. Aidha, Mfuko uligharamia miradi ya maendeleo

inayohusu ushirikishaji wananchi katika uhifadhi. Jumla ya shilingi 261.7 milioni zilitumika kugharamia miradi hiyo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Wanyamapori Mweka kilidahili wanafunzi 278 wa mafunzo ya muda mrefu. Idadi hii iliongezeka kwa asilimia 34 ikilinganishwa na udahili wa wanafunzi 206 wa mwaka 2005/06. Maombi ya kujiunga na Chuo yanazidi kuongezeka lakini Chuo hakiwezi kudahili zaidi ya wanafunzi 260 kwa sababu kina upungufu wa mabweni, madarasa na vifaa vya kupigia kambi kwa mafunzo ya vitendo.

Ili kuhakikisha kuwa Chuo kinakidhi mahitaji ya taaluma, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ulifanyika. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ukarabati na ujenzi wa mabweni mapya, hivyo kuwezesha chuo kupokea wanafunzi wengi zaidi. Vilevile, chuo kilichimba kisima cha maji na kununua jenereta yenye uwezo wa *KVA 200* na kompyuta 81.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Tanzania ina karibu ya hekta milioni 33.5 za misitu na misitu mataji wazi, kati ya hizi, hekta milioni 13 zimetengwa rasmi na Serikali kama Misitu ya Hifadhi. Aidha, hekta 85,000 za eneo lililotengwa na serikali ni mashamba 16 ya miti (*forest plantations*) na hekta milioni 1.6 ni maeneo ya lindimaji (*catchment forests*) ambazo zinajumuisha misitu ya Tao la Milima ya Mashariki yenye mifumo ya ikologia ya kipekee, rasilimali ya jene (*genetic resources*) na bioanuwai kubwa.

Wizara inapitia Sera ya Misitu ya Mwaka 1998. Aidha, Wizara ilitangaza Sheria za Misitu Namba 14 ya mwaka 2002 na Kanuni zake katika Mikoa ya Singida, Dodoma, Manyara, Kigoma na Tabora. Katika kutekeleza sheria hiyo, Wizara ilisitisha usafirishaji magogo nje ya nchi, kuandaa Mwongozo wa Uvunaji endelevu wa misitu na kuunda vikosi vya udhibiti wa mazao ya misitu vyenye askari 44 katika kanda tano ambazo ni Kanda ya Mashariki, Kanda ya Kusini, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini. Aidha, Wizara ilikadiria kiasi cha magogo yanayoweza kuvunwa katika wilaya 11 za Kanda ya mashariki na Nyanda za Juu kusini. Katika makadirio hayo ujazo wa magogo yaliyosimama ni meta za ujazo 55,848,888 na yanayoruhusiwa kuvunwa kwa mwaka ni meta za ujazo 2,000,000. Hivyo tuna rasilimali kubwa ya magogo lakini uwezo wetu wa kuyapasua mbao ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuwezesha upatikanaji wa mazao ya misitu na utunzaji wa mazingira, Wizara ilizalisha na kusambaza mbegu bora za miti pamoja na vipandikizi (*grafting/budding*) ambazo zoligharimu kiasi cha shilingi 32,045,200 na kuipatia Serikali jumla ya shilingi 157,459,359 hadi kufikia Mei 2007. Wizara ilikusanya kilo 10,557 za mbegu za miti na kuuza kilo 8,858 nchini na kilo 1,187 nje ya nchi pamoja na kusambaza miche 31,307 hapa nchini.

Ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mbegu bora unakuwa endelevu, Wizara ilianzisha vyanzo vitatu vya mbegu bora za miti ya Mikaratusi. Vilevile, vyanzo vitano vya miti ya kiasili aina ya Mvule na Mkangazi vilitambuliwa na kuandikishwa katika sehemu mbali mbali nchini. Wizara pia, iliendelea kutunza vyanzo 25 vya mbegu za miti ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuendeleza rasilimali ya misitu, Wizara ilitunza Mashamba ya Miti ya Serikali 16 kwa kukuza miche 8,233,740 kati ya miche 8,400,000 iliyotarajiwa katika mwaka 2006/2007. Vilevile, hekta 5,563 zilipandwa miti na hekta 3,293 zilipogolewa (*pruning*) matawi. Palizi ilifanyika katika hekta 4,419 na kutengeneza barabara zenye urefu wa kilomita 553.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Kampeni ya Taifa ya Kupanda Miti, Wizara kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, Serikali za Vijiji na wadau wengine ilihamasisha kila mkoa kupanga siku yake ya kupanda miti kwa kufuata majira ya mvua. Katika kipindi cha mwaka 2006/07, upandaji miti ulifanyika wakati wa majira ya mvua. Hadi mwishoni mwa Aprili 2007, miche milioni 18 ilipandwa nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kupanua maeneo ya Hifadhi ya Misitu, Wizara ilipima na kuchora ramani za misitu ya Serikali Kuu na vijiji zenye jumla ya hekta 183,330 katika Mikoa ya Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya, Singida na Tanga ambapo jumla ya misitu 35 ilipimwa.

Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wizara ilipima Misitu ya vijiji yenye ukubwa wa hekta 58,735 katika Wilaya za Kilosa, Mbozi, Singida, Handeni, Mkuranga, Kilombero na Rufiji. Misitu hii imepimwa kwa kusudio la kukamilisha taratibu za kuzihifadhi chini ya uangalizi wa vijiji husika. Vilevile, rasimu ya kuitangaza misitu ya hifadhi ya vijiji mbalimbali wilayani Singida, Monduli, Kiteto, Mufindi, Mkuranga na Liwale imetayarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kutangaza mazao ya nyuki kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi mwezi Septemba 2006, Wizara kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la *National Honey Show*" waliandaa maonesho ya asali yaliyofanyika katika Manispaa ya Dodoma. Maonesho hayo yalishirikisha wafugaji nyuki 150 kutoka vikundi vya Mikoa ya Mbeya, Tabora, Rukwa, Tanga, Kigoma, Manyara, Singida na Dodoma. Kwa mara ya kwanza, Wafugaji nyuki walikutanishwa na wanunuzi wa asali kama vile Kampuni ya *Fida Hussein, Honey Care* na *Traid Craft.* Aidha, wawakilishi wa vyombo vya fedha na mikopo walishiriki na kutoa miongozo ya jinsi ya kupata mikopo toka taasisi hizo. Mashirika ya nchi wahisani pamoja na wawakilishi kutoka Kenya, Uganda na Zambia walikuwa miongoni mwa washiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwezesha wafugaji nyuki kuanzisha hifadhi za nyuki, Vijiji vya Kalangasi, Lutona na Tura katika Wilaya ya Uyui; Nkonko na Mpola katika Wilaya ya Manyoni na Kijiji cha Kilimamzinga Wilaya ya Handeni viliwezeshwa kutenga maeneo na kupima Hifadhi za Nyuki za Vijiji.

Aidha, shule tano za msingi Wilayani Manyoni ziliwezeshwa kuanzisha manzuki. Mwaka 2006/2007 Wizara ilitenga hekta 1200 za Hifadhi ya Nyuki ya Taifa ya Kang'ata, wilayani Handeni na hekta 500 za Hifadhi ya Aghondi, Manyoni ambapo hatua za kuzitangaza na kumiliki Hifadhi hizi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2006/2007 kulijitokeza wimbi kubwa la uvamizi wa misitu katika sehemu mbali mbali hapa nchini. Uvunaji haramu

katika misitu pia umeathiri misitu na kupunguza pato la serikali. Biashara kubwa ya magogo yaliyovunwa kinyume cha sheria ilifanyika katika nchi za China, Japan na nchi nyingine za Kusini Mashariki mwa Asia.

Katika kudhibiti uhalifu huo ndani ya nchi, Vikosi vya doria katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora na Lindi, vilikamata mazao mbalimbali ya misitu vikiwemo vipande 50,282 vya mbao, mkaa gunia 2,288, *Gum Arabica* tani 103.9, nguzo vipande 4,600, slipa 330, magogo yenye mita za ujazo 208, samani za aina mbalimbali 2,118 na milango 560 vilivyotumia mbao na magogo yaliyovunwa kinyume cha sheria. Sambamba na mazao ya misitu, vifaa vilivyotumika katika uhalifu vilikamatwa ambavyo ni baiskeli 112, misumeno 54, bunduki aina ya gobore sita, risasi saba, bastola moja na mahema mawili. Nyara nyingine zilizokamatwa ni ngozi mbili za nyoka, ngozi moja ya simba na meno manne ya tembo. Katika doria hizo jumla ya Makambi 32 ya Wavamizi yaliharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji, Wizara ilianza zoezi la kuondoa wavamizi katika maeneo ya Shamba la Miti Kilimanjaro Magharibi na Misitu ya Hifadhi ya Kazimzumbwi na Pugu katika Mkoa wa Pwani. Vilevile, wavamizi waliondolewa katika Msitu wa Hifadhi wa Biharamulo, Hifadhi za Misitu Wilaya za Uyui na Urambo Mkoani Tabora, Misitu ya Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani na Msitu wa Hifadhi wa Nilo mkoani Tanga. Hadi kufikia Machi 2007, wavamizi wapatao 111,129 wakiwemo wafugaji wenye mifugo 79,238, wachimba madini wadogo wadogo na wakulima waliondolewa katika maeneo ya misitu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Katika kutambua wingi wa raslimali ya misitu, Wizara ilifanya makadirio ya ujazo wa miti iliyosimama katika mashamba ya miti yenye ukubwa wa hekta 8,421 ya Shume (Lushoto), Meta za ujazo 264,081 Longuza (Muheza) na Meta za ujazo 370,622 Mtibwa (Mvomero). Katika zoezi hilo, jumla ya meta za ujazo 62,924 za miti ziliruhusiwa kuvunwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kupitishwa kwa Mwongozo wa Uvunaji Endelevu na Biashara ya Mazao ya Misitu mwezi Agosti 2006, Kamati za kusimamia uvunaji wa mazao ya misitu ziliundwa katika wilaya 90 Tanzania Bara. Kamati hizo zinaendelea kuanzishwa katika Wilaya zilizobaki. Ili kufanikisha majukumu ya kamati, semina za kuboresha utaratibu wa uvunaji na biashara ya mazao ya misitu zilifanyika katika kanda saba. Kutokana na wimbi kubwa la ukataji wa magogo katika misitu ya asili, Wizara imezielekeza Wilaya 56 zinazovuna mazao ya misitu, kuandaa mipango ya uvunaji na kuwasilisha Wizarani ili ihakikiwe na kupitishwa kabla ya leseni kuanza kutolewa msimu unapoanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara iliandaa Rasimu za Mrahaba wa Mazao ya Misitu; kudhibiti Biashara ya Mazao ya Misitu kutoka Nje ya Nchi; na Kuzuia Uvunaji wa Miti ya Misandali. Rasimu hizi ni sehemu ya Sheria ya Fedha iliyojumuishwa katika Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa kwenye Bunge lako tukufu tarehe 14 Juni 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii ikolojia uliendelea kuimarishwa katika misitu ya mazingira asili ya Amani, Misitu ya Hifadhi ya Duluti, Rau, Kimboza, Shume, Magamba na Kilimanjaro. Aidha, Misitu ya Hifadhi ya West Kilombero Scarp iliyopo wilayani Kilolo na misitu ya Matundu, Nanganje, Lyondo na Iwonde iliyopo wilayani Kilombero ilipimwa kwa pamoja ili kuwezesha Misitu hiyo kupandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Kilombero (Kilombero *Nature Reserve*) yenye ukubwa wa hekta 134,511. Vilevile, Wizara iliandaa Rasimu ya kutangaza Hifadhi za Mazingira Asilia (*Nature Reserves*) za Nilo mkoani Tanga. Aidha, Wizara kupitia Sekta ya Utalii imeanza mchakato wa kuandaa Rasimu ya Mwongozo wa Kuendeleza Utalii wa Ikolojia nchini *(eco-tourism).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kuzingatia ubora na kuinua viwango kwa lengo la kukidhi soko la ndani na nje ya nchi, Wizara imeandaa mpango wa kudhibiti mabaki ya dawa katika asali (*Chemical Residue Monitoring Plan for 2007).* Katika mpango huo, sampuli za asali zitachukuliwa kutoka katika maeneo mbalimbali nchini na kupimwa kwenye maabara teule.

Aidha, wadau 100 watapewa mafunzo ya namna ya kufuatilia, kukusanya sampuli na kuhakiki ubora wa asali. Vilevile, Mwongozo wa udhibiti wa ubora wa mazao ya nyuki umetayarishwa kwa lugha ya Kiingereza na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na nakala 2000 zimechapishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ilishiriki kuandaa chombo cha kutangaza na kuunganisha nchi za Afrika katika biashara ya mazao ya nyuki kinachoitwa *ApiTrade Africa.* Kupitia chombo hiki, mazao ya nyuki yatatangazwa na kupata masoko ndani na nje ya nchi. Aidha, nchi wanachama watapata taarifa za masoko duniani na kubadilishana uzoefu na habari za kitaalam kuhusu uendelezaji wa ufugaji nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Ushirikishaji jamii katika usimamizi wa misitu kwenye wilaya 54 ulifanyika ambapo wanavijiji waliwezeshwa kumiliki misitu iliyopo ndani ya ardhi ya vijiji na kuingia mkataba na Serikali katika kusimamia misitu ya hifadhi hizo. Serikali za Mitaa zilijengewa uwezo wa kutekeleza usimamizi shirikishi kwa kupewa vitendea kazi pamoja na mafunzo mbalimbali. Aidha, Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa Jamii na Mfumo wa kukusanya na kuhifadhi kanzidata za misitu na nyuki *(National Forest and Beekeeping Data* Base (*NAFOBEDA)* umetayarishwa. Hadi sasa kuna hekta milioni 3.6 za misitu ambazo ziko chini ya usimamizi shirikishi katika vijiji 1,788 vilivyopo katika wilaya 54.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilitoa elimu ya ufugaji nyuki ili kuongeza ufahamu miongoni mwa wananchi juu ya faida za ufugaji nyuki kiuchumi, kijamii na kimazingira. Semina 14 kuhusu mbinu bora za ufugaji nyuki zilitolewa kwa wafugaji nyuki katika Wilaya za Chunya, Uyui, Nachingwea, Rufiji, Kilindi, Njombe, Simanjiro, Kiteto na Babati. Aidha, Wizara ilinunua na kusambaza mizinga na vifaa mbali mbali vya ufugaji bora wa nyuki kwa ajili ya maonyesho katika wilaya za Manyoni, Handeni, Kondoa na Kibondo. Uhamasishaji wa ufugaji nyuki uliendelezwa ambapo Wilaya ya Manyoni iliweza kuanzisha na kusajili vyama saba vya wafugaji nyuki. Aidha, wafugaji

nyuki katika kijiji cha Mswaki Wilaya ya Handeni walianzisha Chama cha Wafugaji Nyuki cha Kuweka na Kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2006/2007, Wizara ilitangaza vipindi 70 vya redio kupitia kipindi cha Maliasili na Misitu ni Uhai, Programu tano za televisheni na vipindi viwili vya mahojiano ya moja kwa moja vya televisheni.

Aidha, machapisho mbalimbali yakiwemo nakala 15,000 za vipeperushi, vijarida na vijitabu vilichapishwa. Baadhi ya machapisho na vipeperushi hivyo ni; Hifadhi Mazingira, Punguza Umaskini; Mabango ya Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki; Nyuki ni Hazina; Nishati Mbadala; na Usimamizi Shirikishi wa Misitu. Wizara pia, iliandaa na kusambaza maelezo kuhusu taratibu za Serikali za kusafirisha mazao ya misitu nje ya nchi, Mwongozo wa Uvunaji, Usafirishaji na Biashara ya Mazao ya Misitu, Ubora wa asali, Njia rahisi ya kutambua asali yenye kiwango kizuri cha maji na isiyochemshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya hivi karibuni kumetokea matatizo ya kuihusisha miti aina ya mikaratusi na kukauka kwa vyanzo vya maji nchini. Utafiti duniani umeonesha kuwa kuna aina zaidi ya 600 za miti hii na kati ya hizo zipo zinazofaa katika kuhifadhi vyanzo vya maji na zisizofaa. Kutokana na utafiti huo Taasisi imeanza kuelimisha jamii juu ya aina za mikaratusi na matumizi ya maji kupitia magazeti na televisheni. Aidha, Taasisi kwa kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha Kilimo Mseto (*World Agroforestry Centre)* imechagua maeneo ya kutafiti mikaratusi na mianzi inavyotumia maji katika Mkoa wa Iringa.

Utafiti juu ya mazao yasiyo timbao umebaini miti ya *Commiphora* huko Arusha na Manyara inayotoa manemane inayotumika kama dawa, mti wa Mnango huko Bagamoyo unaotoa gamu iliyokuwa inatumika kama malighafi kutengeneza rangi na mti wa *Boswellia* huko Mkomazi unaotoa ubani unaotumika katika ibada na sherehe za kimila. Mazao haya yana umuhimu mkubwa wa uchumi jamii na utafiti utafanyika juu ya masoko ili kubaini mchango wa mazao haya katika kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti juu ya ufanisi wa upasuaji magogo kwenye mashamba ya miti ya Rongai, Kilimanjaro Magharibi na Meru umebaini kupotea kwa kiasi kikubwa cha magogo kama vumbi kutokana na kutumia misumeno mibaya kwa upasuaji mbao. Wizara inaelekeza kuwa misumeno ya moto *(chainsaws*) na ile ya mkono (*pitsaws)* itumike tu katika kuangusha miti na si kupasulia mbao kwenye misitu yote nchini.

Mradi wa bioteknolojia ya mikaratusi inayokua haraka umeanza kupata matokeo ya aina za vyahuso *(Clones*) zinazostawi katika maeneo mbalimbali nchini na kitalu kikubwa cha kuzalisha miche kimeanzishwa huko Kwamarukanga, Korogwe. Aidha, teknologia tano za kilimo mseto zimesambazwa kwenye kaya 830 katika maeneo mbalimbali.

Taasisi ikishirikiana na Taasisi za nchi za Finland na Sweden imeanzisha majaribio darasa ya kukuza na kuhifadhi misitu ya miombo huko Kitulang'alo,

Morogoro. Matokeo ya utafiti huu yatasaidia uendelezaji na ukadiriaji wa ujazo wa misitu ya vijiji iliyoanzishwa kwa Mpango Shirikishi wa Idara ya Misitu na Nyuki.

Taasisi imeshiriki kutengeneza mikakati ya kupunguza matukio ya moto na matumizi endelevu ya misitu ya Tao la Mashariki. Aidha, spishi vamizi 18 zinazopunguza bioanuwai katika milima hii zimebainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika jitihada za kusambaza matokeo ya utafiti taasisi iliandaa Kongamano la Pili la Kilimo Mseto ambapo mada 24 ziliwasilishwa na nakala 1000 za kumbukumbu zilichapishwa. Taasisi imechapisha na kusambaza nakala 350 za Jarida la *TAFORI* na nakala 150 za bibliografia ya Milima ya Tao la Mashariki. Ili kuboresha mazingira ya kazi, *TAFORI* imeanzisha mchakato wa kupata Mtaalam Mshauri (*Consultant)* kwa ajili ya kuandaa michoro, nyaraka za zabuni na usimamizi wa ujenzi wa Makao yake Makuu huko Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina jukumu la kusimamia na kuhakikisha kuwa Maliasili ya Uvuvi inalindwa, inahifadhiwa na kuendelezwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo. Usimamizi huu unalenga kuwa na uvuvi endelevu utakoachangia kukuza uchumi wa Taifa, kuongeza kipato, lishe, ajira na hivyo kupunguza umasikini kwa wananchi.

Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 jumla ya tani 341,550 za samaki zenye thamani ya shilingi 285,718,540,350 zilivunwa katika maeneo yote ya Uvuvi nchini. Kati ya samaki waliovuliwa kiasi cha tani 50,463 zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 141,286,038 ziliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa shilingi 9,882,411,712.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Ziwa Victoria, walivuliwa samaki wenye uzito wa tani 239,340 zenye thamani ya shilingi 208.5 bilioni. Tathmini ya hali ya uvuvi iliyofanyika katika Ziwa Victoria ilibaini kwamba uvuvi haramu umekithiri katika nchi zote tatu na kasi ya uvuaji sangara ni mkubwa kiasi cha kutishia uvuvi endelevu wa samaki hao. Ili kukabiliana na tatizo la uvuvi haramu, nchi zote tatu zinazomiliki Ziwa Victoria zilikubaliana kuandaa na kutekeleza Mpango wa Kanda wa Kupunguza Kasi ya Uvunaji wa Sangara *(Regional Plan of Action for Reducing Fishing Capacity in Lake Victoria).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha uvuvi endelevu unadumu katika Ziwa Victoria na Tanzania inafaidika kikamilifu na rasilimali zake, Wizara iliitisha Kikao-kazi mwezi Juni 2007 kilichojumuisha Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Watendaji Wakuu, Vyombo vya Usalama na Wenyeviti wa Halmashauri katika maeneo hayo. Kikao kazi hiki kiliweka mkakati wa kudhibiti uvuvi haramu na biashara ya magendo ya samaki mipakani .

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa mazao ya kibiashara hutegemea Dagaa na Migebuka ambayo ni maarufu kwa ajili ya chakula na biashara ndani na nje ya Mkoa wa Kigoma. Ziwa Tanganyika kwa upande wa Tanzania linakisiwa kuwa na kiasi cha tani 80,000 za samaki ambazo zinaweza kuvuliwa bila kuathiri uwezo wa samaki hao kuongezeka. Sensa iliyofanyika mwaka 2006/2007

ilionyesha kuwa kuna wavuvi 12,574, vyombo 7,129 na mialo 134. Taratibu za kuwa na matumizi endelevu ya samaki wa Ziwa hili zinaandaliwa kwa kushirikiana na nchi jirani shiriki katika milki ya Ziwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hadi sasa uvuvi wa samaki wa mapezi kutoka bahari yetu umelenga sana soko la ndani. Hata hivyo, uvuvi wa kibiashara unahusisha mazao ya Kambamiti (*prawn*), Kambakoche (*Lobster*), na Pweza (*Octopus*). Katika mwaka 2006/2007 tani 49,838 za mazao mbalimbali zilivuliwa kwenye bahari yetu na kuliingizia Taifa shilingi bilioni 44. *(Makofi)*

Uvuvi wa Kamba miti umekuwa ukishuka kwa miaka kadhaa kutoka tani 1,027 mwaka 1994 hadi tani 307 mwaka 2006. Ukame uliotokea mfululizo ulichangia katika kupungua kwa rasilimali hii. Hatua za kuhakikisha uvuvi wa kamba unakuwa endelevu zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kupunguza msimu wa uvuvi kutoka miezi tisa hadi sita, kupunguza idadi ya meli zinazopata leseni ya kuvua na idadi ya nyavu kwa kila meli. Pia,Wizara imeimarisha ukusanyaji wa takwimu kwa kutoa vitendea kazi kwenye Wilaya za Ilala, Bagamoyo, Tanga, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwezi Aprili, 2007 Tanzania imeomba kuwa mwanachama wa Kamisheni ya Jodari wa Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Tuna Commission*) ambayo husimamia rasilimali ya samaki aina ya jodari katika Bahari ya Hindi. Samaki hawa wana tabia ya kuhama eneo moja la bahari hadi lingine kufuatana na msimu wa mwaka na katika maji yetu jodari hupatikana kwa wingi miezi ya Septemba hadi Januari. Katika Bahari ya Hindi samaki hawa huzungukia karibu nchi zote za bahari hii kufuatana na hali ya hewa ambayo huambatana na wingi wa chakula majini. Hali hii inalazimu usimamizi wa pamoja kuhusu uvunaji wa samaki hawa. Kwa sasa tathmini ya wingi wa jodari katika upande wa magharibi mwa Bahari ya Hindi ikiwemo Bahari Kuu ya Tanzania inafanywa kupita chombo hiki ili kujua wingi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu katika kikao cha mwezi Februari, 2007 lilipitisha marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority Act Cap. 388*). Kupitia sheria hii chombo cha kusimamia uvuvi katika Bahari Kuu *(The Deep Sea Fishing Authority)* kitaanzishwa kipindi cha 2007/2008. *(Makofi)*

Vile vile, Wizara imeanza mchakato wa kujenga hoja Umoja wa Mataifa kuhusu kuongeza Ukanda wa Uchumi wa Bahari kutoka *Nautical Miles* 200 za sasa hadi 350. Ongezeko la ukanda huu litatuwezesha kuwa na eneo kubwa zaidi na hivyo kuwa na rasilimali nyingi zaidi za Bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 na Kanuni zake zimeanza kufanyiwa mapitio kwa lengo la kuboresha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa faida ya Watanzania. Sababu za msingi zilizopelekea Sheria hii ifanyiwe mapitio ni kuboresha utendaji kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na pili, tuweze kwenda na mabadiliko ya kanuni za kimataifa za biashara ya mazao ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuboresha lishe, kuongeza ajira na kuinua kipato cha wananchi, Wizara inachukua hatua za kuimarisha ukuzaji wa viumbe hai kwenye maji ili kupunguza shinikizo la uvuvi katika maji ya asili.

Mafunzo ya ufugaji samaki yaliendeshwa katika Mikoa ya Iringa, Tanga, Manyara, Kilimanjaro na Mbeya ambako Wizara ilisimamia uchimbaji wa mabwawa matano ya mfano ya ufugaji samaki kibiashara (mawili katika Mkoa wa Iringa, mawili katika pwani ya Mkoa wa Tanga na moja Mkoa wa Manyara). Ukubwa wa kila bwawa ni kati ya mita za mraba 600 hadi 1,200 yanayoweza kutunza vifaranga 1,200 hadi 2,400 kila moja. Katika mafunzo hayo, wataalam 25 wa ugani na wakulima 350 walifaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha ufugaji samaki, vifaranga wa mbegu bora ya samaki 120,000 kutoka Kituo cha Kuzalisha Mbegu Bora ya Samaki vilisambazwa kwa wananchi katika Mikoa ya Iringa, Morogoro, Dar es Salaam, Tanga Manyara na Kilimanjaro. Vifaranga 44,200 vilipandikizwa katika mabwawa ya asili katika Mikoa ya Morogoro na Tanga. Aidha, vifaranga wengine 76,500 walipewa watu kupandikiza kwenye mabwawa ya binafsi majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majaribio ya unenepeshaji wa Kaa kwenye uzio (*Crab fattenning in cages*) yalifanyika katika Mkoa wa Tanga. Jumla ya *cages* 2000 zilitengenezwa na kuweza kukuza Kaa waliouzwa kwa jumla ya shilingi milioni sita.

Aidha, ufugaji wa Kambamiti kibiashara (*prawn farming*) unaofanywa na Kampuni ya Alpha Krust Wilayani Mafia umeonyesha mafanikio. Mradi una mabwawa 25 yenye ukubwa wa wastani wa hekta moja na nusu kila bwawa ambayo yamepandikizwa Kambamiti. Lengo ni kuwa na mabwawa 76 yenye uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 6 kila bwawa baada ya miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kilimo cha Mwani ni moja ya shughuli zinazochangia katika kuwaondolea wananchi umaskini. Kilimo hicho kinaendeshwa katika maeneo mbalimbali ya pwani yetu kwa kuhusisha takriban wakulima 3,000. Katika mwaka 2006, tani 320 za mwani mkavu wenye thamani ya Dola za Kimarekani 136,000 zilisafirishwa nje ya nchi. Ili kuhamasisha wananchi waweze kuendeleza kilimo hiki, ushuru kwenye zao hili umeondolewa linapouzwa nje ya nchi. Aidha, Mpango Mkakati wa Kitaifa wa kuboresha na kuendeleza kilimo hicho ulizinduliwa mwezi Februari 2007 huko Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2006/2007, Wizara iliendesha doria za nchi kavu na majini katika Maziwa Makuu na Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi. Jumla ya siku za doria 9,350 ziliendeshwa na zaidi ya watuhumiwa 6,060 walikamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria ambapo kesi 236 zilifunguliwa Mahakamani.

Watuhumiwa 129 walipatikana na hatia kati yao watuhumiwa 82 walihukumiwa vifungo vya kati ya mwaka mmoja na miaka mitatu. Watuhumiwa 47 walilipa faini za kati ya Shilingi 10,000 na 180,000. Aidha, magari 10, baiskeli 27 mitumbwi 245, samaki

kilo 46,668, majongoo bahari kilo 1,226 na injini za mitumbwi saba vilikamatwa na zana haramu 215,725 zilikamatwa. Watuhumiwa 407 kesi zao bado zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, doria za uvuvi ziliimarishwa mwaka 2006/2007, kwa kuongeza boti mpya tatu na kukarabati nyingine tatu. Boti hizo mpya zilipelekwa Kigoma, Tarime na Bukoba ili kuongeza nguvu katika kudhibiti uvuvi haramu pamoja na biashara ya magendo. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Vijijini ilipewa boti moja kwa ajili ya doria kwenye Bwawa la Mtera na katika bwawa la Nyumba ya Mungu, Wizara imeimarisha ulinzi wa rasilimali na ugani kwa kupeleka pikipiki moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bahari Kuu doria ziliendeshwa kwa kutumia ndege za kukodi. Aidha, mienendo ya meli iliweza kudhibitiwa kwa kutumia *Vessel Monitoring System (VMS)* mfumo ambao huwezesha kufuatilia mienendo ya meli kwa kutumia kompyuta. Kwa vile Tanzania ni mwanachama wa *SADC Monitoring Control and Surveillance (MCS) Network* kwa kutumia mtandao huo nchi hupeana taarifa za meli zenye sifa mbaya ili kuepuka kuzipa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inasimamia Vyuo viwili vya Mafunzo ya Uvuvi. Chuo cha Uvuvi Nyegezi hutoa mafunzo katika taaluma ya uvuvi katika ngazi ya Astashahada, ushauri wa ufugaji samaki na ni kituo cha mfano wa shughuli za uvuvi katika maji Baridi.

Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani hutoa mafunzo katika taaluma za Ubaharia, Uhifadhi, Uchakataji na Masoko, Ufundi wa Mitambo ya Baharini na Ujenzi wa Boti. Chuo pia kinatoa mafunzo kwa Wakaguzi wa mazao ya Uvuvi kwa nchi za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Vilevile, chuo kinatoa ushauri wa ufugaji samaki na ni kituo cha mfano wa shughuli za uvuvi katika maji chumvi. Napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali ya Japan kupitia taasisi yake ya '*Overseas Fisheries Commission'* kwa kutoa Wataalam na fedha takriban shilingi milioni 600 kukarabati Chuo cha Mbegani. Kazi hii pia itatekelezwa katika kipindi cha 2007/2008 kwa shilingi milioni 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatekeleza Mradi wa Usimamizi wa Bahari na Mazingira ya Pwani - *Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP)* ambao ulianza rasmi Desemba mwaka 2005. Kwa kupitia mradi huu yafuatayo yalifanyika katika kipindi cha mwaka 2006/2007:

1. Kuwezesha kukamilishwa sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing Authority).* Muswada wa marekebisho (*Amendments Bill)* ulipitishwa na Bunge lako katika kikao cha Februari, 2007.

2. Kutoa fedha za kuwezesha wanavijiji kuendesha shughuli ndogondogo za kujipatia kipato. Wizara imeajiri *TASAF* kutokana na uzoefu wake kuwa Wakala

wa kutoa fedha hiyo kwa wale watakaofaidika na mradi huo. Fedha ambayo imekwishapelekwa kwa Wadau Tanzania Bara hadi sasa ni takriban shilingi bilioni 2. Kati ya hizo, Shilingi 615 milioni zilipelekwa kupitia *TASAF* kwa ajili ya Miradi ya wanavijiji vya wilaya za Rufiji, Mafia na Kilwa. Idadi ya miradi iliyoibuliwa na wanavijiji wa wilaya za Rufiji, Mafia na Kilwa ni 248, kati ya miradi hiyo, 116 imefanyiwa upembuzi yakinifu kwa kushirikisha jamii na 82 imekwishapitishwa na Kamati za Wilaya ilipofika tarehe 30 Aprili 2007. Aidha, miradi iliyopitishwa na Kamati ya *MACEMP* ni 21 na 4 kati ya hiyo imethibitishwa kupewa fedha na *TASAF*.

3. Katika jitihada za kupiga vita uvuvi wa mabomu na nyavu zilizokatazwa, mradi umewezesha kufanyika kwa doria za Bahari na Ukanda wa Pwani. Hadi kufikia Juni 2007 doria maalum mbili zimefanyika katika maeneo ya mkondo wa Mafia, Rufiji na Kilwa, pamoja na maeneo ya bahari ya Mkoa wa Tanga. Aidha, doria nne za anga zimefanyika katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu kwa ushirikiano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

   Vilevile, mradi uliwezesha kufanyika kwa mikutano mbalimbali ya wadau ili kujadili mbinu shirikishi za kupiga vita uvuvi haramu. Wadau hawa ni pamoja na Wavuvi na Wawekezaji katika Sekta ya Utalii na Manispaa.

4. Kukuza weledi na uelewa wa wadau kwa kutumia warsha, mikutano na njia mbalimbali za mawasiliano, zikiwemo; makala mbalimbali na vipeperushi kuhusu matumizi endelevu na fursa za kiuchumi za rasilimali za baharini na ukanda wa pwani.

5. Kufanya mchakato wa zabuni na manunuzi ya vifaa mbalimbali kama baiskeli, pikipiki, boti, gari, vifaa vya ofisi, Kompyuta, ili kurahisisha utekelezaji wa mradi.

6. Kuorodhesha maeneo ya mambo ya kale na maarifa asilia *(Inventory of cultural sites and indigenous knowledge)* kwa kuwa ni rasilimali muhimu katika kuchangia uchumi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Implementation of Fisheries Management Plan (IFMP)* ulianza mwaka 2003 chini ya ufadhili wa Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)* kwa gharama ya Euro milioni 29.9 na utakamilika mwaka 2008. Lengo kuu la mradi ni kuinua uhifadhi, uendelezaji na uvunaji endelevu wa rasilimali ya uvuvi katika Ziwa Victoria kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo. Mradi unatekelezwa na nchi za Tanzania, Kenya na Uganda ambazo humiliki Ziwa Victoria. Katika kipindi cha mwaka 2006/07 Mradi umeimarisha Vikundi vya Ulinzi wa raslimali za Uvuvi *(BMUs)* vipatavyo 434, umewezesha kufanyika kwa doria shirikishi jamii katika ziwa Victoria na umetoa elimu kwa umma kuhusu uvuvi endelevu.

Aidha, mradi umewezesha kukusanywa kwa takwimu za mazao ya uvuvi (*Catch Assessment surveys),* umetoa mafunzo kuhusu usalama na huduma za uokoaji ziwani kwa Maofisa wa Uvuvi kutoka Mikoa yote mitatu; na umewezesha kufanyika kwa tathimini ya maeneo ya kujenga miundo mbinu ya kupokelea samaki na kuboresha Ofisi za Uvuvi kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uwiano wa Maendeleo wa Bonde la Ziwa Tanganyika ambao utatekelezwa na nchi za Tanzania, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na Zambia, umekubalika rasmi Aprili, 2007. Makao yake Makuu yatakuwa Bujumbura Burundi. Lengo kuu la mradi ni kuchangia katika kupunguza umaskini wa kipato katika bonde la Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Basin*) ambalo zaidi ya asilimia 65 ya ukanda mzima wa bonde uko Tanzania.

Mradi huu utagharimu Dola za kimarekani milioni 68.40; kutokana na ufadhili wa Benki ya Dunia (43.3%), *GEF (19.7%),* Mfuko wa Maendeleo wa Norway (17.6%), *IUCN (1.5%)* na mchango wa kila nchi (7.2%). Tanzania itanufaika kwa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 4.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uvuvi Kusini Magharibi ya Bahari ya *Hindi (Southwest Indian Ocean Fisheries Project*) upo katika hatua za mwisho wa maandalizi. Mradi huu unajumuisha nchi za Tanzania, Kenya, Msumbiji, Afrika Kusini, Comoro, Madagascar, Mauritius, Seychelles na Reunion utaanza mwezi Septemba 2007. Mradi huu ambao lengo lake ni kufanya utafiti ili kupata taarifa za kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika bahari kuu unahisaniwa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ubora wa Mazao ya Uvuvi hutegemea sana mazingira ya samaki wanavyotunzwa kuanzia kuvuliwa hadi kufika kwa mlaji. Katika mwaka 2006/2007, jumla ya Shilingi 400 milioni zilitumika katika kukarabati mialo 19 na kujenga mialo mipya 6 katika Pwani ya Ziwa Victoria.

Katika kuhakiki ubora wa mazao ya uvuvi, sampuli 1,564 kutoka Ziwa Victoria, Viwanda vinavyozunguka Ziwa Victoria na vilivyoko Ukanda wa Pwani zilifanyiwa uchunguzi katika maabara za ndani na nje ya nchi ili kuhakiki usalama wa afya. Wizara imesimamia na kuhakikisha kuwa ubora wa mazao ya samaki yanayouzwa ndani na nje ya nchi yanakuwa salama kwa afya za walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika kuendeleza soko na kuhakiki ubora wa bidhaa za uvuvi, Wizara imefanya ukaguzi wa mara kwa mara katika viwanda vya kuchakata samaki. Katika mwaka 2006/2007, jumla ya viwanda 15 vya kuchakata samaki, meli 15 za uvuvi, maeneo 11 ya kutunzia samaki hai na maghala manne ya kuhifadhia mazao makavu ya uvuvi yalikaguliwa. Jumla ya kaguzi 3,600 za mazao ya uvuvi zilifanyika viwandani na kwenye mialo wakati wa upakiaji wa mazao yanayosafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Tanzania huuza nje ya nchi mazao ya uvuvi toka maji baridi na chumvi katika nchi za Jumuiya ya Ulaya, Amerika, Japan na Israel. Mazao

haya yanapaswa kukidhi viwango vya ubora kimataifa. Hivyo umakini wa ubora unahitajika katika uvuaji, usafirishaji na uchakataji. Ili kukidhi viwango vya ubora vya kimataifa na kuongeza fedha za kigeni, Wizara imekamilisha ujenzi wa Maabara ya Taifa ya Uvuvi Jijini Mwanza. Maabara hii ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, mwezi Januari 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilishiriki kutoa mafunzo kwa wavuvi wadogo wadogo katika fani mbalimbali za uvuvi katika Ziwa Nyasa. Katika mwaka 2006/2007, wavuvi 32 kutoka Kata kumi za Wilaya ya Mbinga na Kata sita za Wilaya ya Ludewa wamenufaika na mafunzo ya vitendo ya kutumia ndoana katika kuvua samaki wanaoishi katika kina kirefu cha Ziwa Nyasa. Vilevile, elimu kwa jamii ilitolewa kupitia mikutano ya hadhara katika vijiji 6 vya wilaya ya Ludewa na 75 katika Wilaya ya Mbinga. Jamii ya wavuvi wanaoishi katika bonde la Mto Ruhuhu walipatiwa mafunzo kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Uvuvi pamoja na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi katika kipindi cha 2006/2007 ilifanya utafiti mbalimbali kwenye maji baridi na maji chumvi kwa lengo la kuishauri serikali kuhusu uvunaji endelevu, usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi.

Utafiti wa Silikanti, aina ya samaki anayesadikika kuishi miaka milioni 60 iliyopita, unaendelea kwa ushirikiano na taasisi za Japan, Ujerumani na Afrika Kusini. Hadi sasa samaki huyo amevuliwa katika Wilaya za Tanga, Muheza, Temeke, Kilwa, Lindi na Mtwara. Hata hivyo, kati ya Silikanti 36 waliovuliwa kwenye nyavu za wavuvi hadi sasa, 28 wamevuliwa katika Mkoa wa Tanga.

Kwa vile samaki huyo ana historia ya pekee, adimu sana na ni kivutio kikubwa cha utalii, Taasisi kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za ndani na nje ya nchi imeanza kufanya utafiti utakaowezesha kujenga hoja ya kuyatambua na kuyatenga maeneo hayo ya Tanga kuwa Maeneo Tengefu ya Bahari.

Utafiti wa samaki aina ya Sangara katika Ziwa Victoria umebaini kuwa samaki wengi wanaovuliwa ni wadogo na hawajafikia umri wa kuzaa, hivyo hawafai kuvuliwa. Vilevile, utafiti wa kuona athari za minyoo inayopatikana katika dagaa wa Ziwa Nyasa unafanyika. Taarifa za awali zimebaini kuwa minyoo aina hiyo haina madhara kwa binadamu.

Aidha, utafiti uliofanywa Bwawa la Mtera kuhusu vifo vya samaki ulionyesha kwamba vilisababishwa na uchafuzi wa mazingira uliotokana na kukauka kwa maji katika bwawa hilo. Tatizo hilo sasa halipo baada ya maji kuongezeka kwenye bwawa kutokana na mvua nyingi zilizonyesha. Utafiti wa majaribio ya ufugaji samaki aina ya mwatiko umeendelea vizuri katika Ukanda wa Pwani. Wizara inafanya utafiti ili kuondoa tatizo la upatikanaji wa vifaranga na lishe ya ziada kwa samaki hao.

Aidha, Taasisi kwa msaada wa *Lake Victoria Research Initiatives (VicRes)* imezalisha vifaranga vya Kambale na kutathmini mfumo bora wa kuzalisha vifaranga

hivi kibiashara (*Value chain Analysis*) na kubuni mfumo wa kuongeza uzalishaji wake pamoja na Sato katika bwawa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Katika kipindi cha 2006/2007, Wizara ilitangaza maeneo Tengefu mapya sita na hivyo kufikisha idadi ya maeneo hayo kuwa 13. Maeneo hayo mapya ni Visiwa Vidogo vya Sinda, Kendwa, Mwakatumbe (vilivyoko Dar es Salaam); Shungimbili, Mbarakuni na Nyororo yaliyoko Wilaya ya Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuhimiza Uhifadhi Shirikishi, Vikundi vitatu vya ulinzi wa raslimali za Bahari vimeanzishwa katika maeneo Tengefu ya Bongoyo, Mbudya na Sinda. Aidha, doria shirikishi jamii zimefanikisha kupunguza uhalifu ndani ya Hifadhi za Bahari. Mathalani, katika hifadhi ya Mafia, Kilo 250 za Simbi, magogo 22 na makokoro 22 yalikamatwa, wakati katika Hifadhi ya Mnazi Bay, boti 2, Kokoro 3 na vipande 120 vya nyavu za macho madogo zisizokubalika kisheria zilikamatwa na watuhumiwa 21 walifikishwa mahakamani. Sambamba na kuendesha doria hizo, Elimu ya matumizi endelevu ya raslimali za Baharini ilitolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jitihada za kupunguza kasi ya uharibifu wa raslimali za Bahari ziliimarishwa kupitia mpango wa kubadilishana zana haribifu kwa zana bora za Uvuvi Endelevu. Jumla ya vikundi 73 vya Wavuvi kwenye Hifadhi ya Mafia na wavuvi 90 katika Hifadhi ya Mnazi Bay walinufaika na mpango huo. Aidha, elimu ya kutengeneza majiko banifu ilitolewa kwa wanawake 25 katika Hifadhi ya Bahari kisiwani Mafia ambapo majiko 22 yalitengenezwa. Matumizi ya majiko haya yatapunguza matumizi ya kuni na hivyo kupunguza kasi ya ukataji miti kwa ajili ya kuni katika eneo la msitu wa Mlola ambao ni pekee na uliobaki, wilayani Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2006, kulikuwa na watalii 644,124 walioingia nchini ikilinganishwa na watalii 612,754 waliotembelea nchi yetu mwaka 2005. Wageni hao waliliingizia Taifa jumla ya Dola za Kimarekani 862 milioni mwaka 2006 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani 823 milioni mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha mazingira ya biashara ya utalii na kuiwezesha serikali kusimamia sekta hii kwa ufanisi zaidi, Wizara imechukua hatua ya kutunga Sheria Mpya ya Utalii. Ni mategemeo yangu kuwa Muswada wa Sheria hii utawasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu, mwezi Novemba 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupanua wigo na vivutio vya utalii, Wizara kwa kushirikisha Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na uongozi wa Wilaya na Serikali za Vijiji, imebainisha maeneo ya uendelezaji utalii wa fukwe katika Wilaya za Bagamoyo, Mafia, Mkuranga, Tanga Mjini na Pangani. Zoezi hili la kuhakiki umiliki wa maeneo ya fukwe za bahari linaendelea katika mikoa ya Tanga na Lindi, ili maeneo mazuri yatambuliwe na kuwekwa bayana kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoahidi kwenye Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2006/2007, Wizara ilianza kuandaa Programu ya Taifa ya Uendelezaji Utalii.

Hadi kufikia Mei 2007, awamu tatu kati ya nne za kuandaa programu hiyo zimekamilika kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa nchi yetu ni miongoni mwa nchi 15 duniani zilizoteuliwa kunufaika na mradi wa *United Nations World Tourism Organisation/Sustainable Tourism for Elimination of Poverty (UNWTO/ST-EP Initiative*). Lengo la mradi huu ni kuwawezesha wananchi wenye kipato kidogo kunufaika na biashara ya utalii. Katika mwaka 2006/2007, utaratibu wa kuwanufaisha wananchi wa maeneo ya Pangani na Saadani ulikamilishwa kwa kupewa dola za kimarekani 77,500 ili kuboresha miradi ya utalii wa utamaduni. Utekelezaji huo utaendelea kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kuimarisha na kudumisha ushirikiano wa kimataifa, Wizara ilihudhuria jumla ya mikutano 12 ikiwemo mkutano wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii Duniani *(UNWTO).* Katika mkutano huo, Tanzania iliteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti kwenye kamati maalum iliyoundwa ili kushirikiana na *UNWTO* na "*Federation of International Football Association (FIFA)* kutumia michezo ijayo ya Kombe la Dunia itakayofanyika Afrika Kusini mwaka 2010 kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Mikutano mingine iliyohudhuriwa ni ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* na ule wa Chama cha Wasafirishaji Watalii toka Marekani kuja Afrika *(ATA).* Aidha, Wizara ilihudhuria mkutano wa *International Institute of Peace through Tourism (IIPT)* uliofanyika Kampala, Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* lilipitisha vigezo vya kutumika kupanga hoteli katika madaraja kwa nchi zote wanachama. Katika kutekeleza makubaliano hayo, jumla ya hoteli 122 katika mikoa ya Arusha na Manyara zimefanyiwa tathimini na kuwekwa kwenye madaraja husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Utalii, Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa mafunzo unaohisaniwa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU).* Mradi huo unaogharimu *Euro 2.5* milioni unatekelezwa katika kipindi cha miezi thelathini kuanzia Januari 2007. Malengo makuu ya mradi huo ni: kuandaa Mitaala ya Kitaifa katika fani ya Hoteli na Utalii; kuinua viwango vya ufundishaji kwa kutoa mafunzo kwa walimu wa vyuo vya hoteli na utalii; kuisaidia *NACTE* na *VETA* kusimamia mafunzo ya hoteli na utalii nchini na kuweka mfumo mzuri wa utoaji tuzo; kutoa mafunzo kwa walengwa mbalimbali katika sekta; na kununua vifaa vya kisasa vya kufundishia katika Chuo cha Hoteli cha Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwezi Juni 2007, Halmashauri ya Jiji la Arusha iliikabidhi Wizara jukumu la kusimamia Chuo cha Mafunzo ya Hoteli cha Arusha kilichojengwa kwa msaada wa Shirika la *Hans Siedel Foundatio* la Ujerumani na kuwa sehemu ya Chuo cha Taifa cha Utalii. Chuo hiki kinatoa mafunzo ya Upishi *(Food Production*), Mapokezi (*Front Office Operations*) na Utoaji huduma (*Food & Beverage*

*Service*) katika ngazi ya Astashahada. Kwa sasa chuo kina uwezo wa kupokea wanachuo 120 kwa mwaka na kina eneo la hekta mbili ambazo zinaweza kutumika kwa upanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii ni biashara inayoshamiri katika nchi zenye amani na utulivu kama Tanzania. hivyo, matukio ya kuwavamia watalii huleta athari kubwa katika biashara hiyo. Kwa kutambua umuhimu wa kudumisha amani na utulivu, mwaka 2006/2007 Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Usalama wa Raia na wadau wengine imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuweka ulinzi madhubuti kwenye maeneo yanayotembelewa na watalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006/2007, Idara ililenga kukusanya Shilingi 1.124 bilioni kutokana na ada mbalimbali za Wakala wa Utalii. Hadi kufikia mwezi Mei 2007 jumla ya Shilingi 1.538 bilioni zilikusanywa ikiwa ni ongezeko la asilimia 36.8 la makadirio. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika Sekta ya Utalii na kuimarisha ukaguzi wa Wakala wa Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Bodi ya Utalii ilitekeleza jukumu lake la msingi la kutangaza nchi yetu na vivutio vya utalii ili kuongeza mchango wa sekta ya utalii katika pato la Taifa na kupunguza umaskini. Katika mwaka 2006/2007, Bodi ilishiriki kwenye maonesho ya utalii 12 nje ya nchi, 4 kwenye soko la ndani na kuratibu mengine 18 ya kimataifa. Aidha, Bodi pamoja na wadau mbalimbali wa utalii walihudhuria maonesho katika nchi za Canada, Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Italia, China, Hispania, Sweden, Australia, Ubeligiji, India, Japan, Korea ya Kusini, Zimbabwe na Ethiopía. Juhudi za kutangaza utalii kwenye soko la Marekani ziliendelea ambapo Bodi ilifanya misafara miwili ya kutangaza utalii (*Road Shows).*

Bodi ya Utalii ilitangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini kwenye magazeti ya nchi za nje kama ifuatavyo: Marekani *(Travel World News*, *USA Today, New York Times, Africa Travel Magazine); Canada (Canada Chronicle, Canada Tribune* na *Africa Travel Magazine);* Ujerumani (*Travel Africa);* Afrika Kusini (*Africa Decisions*); Mashariki ya Kati (*Travel Gazzette)* na Nchi za Ghuba (*Arabian Travel Times*). Aidha, Televisheni za Nje za *CCTV* (China), *MBC* (Korea Kusini), *ABC Goodmorning* America (Marekani) na *ARD* (Ujerumani) zilitumika kutangaza vivutio vya utalii vya hapa nchini.

Vilevile, Bodi ilikaribisha nchini vikundi 14 vya Mawakala wa Biashara ya Utalii wakiwemo waandishi na wapiga picha za televisheni. Mawakala hao kutoka Marekani, China, Qatar, Ubelgiji, Ujerumani, Afrika Kusini, Korea Kusini, Hispania, na Canada walialikwa kuona vivutio vyetu ili waweze kuwashawishi watalii kuitembelea Tanzania.

Katika jitihada za kuleta watalii wengi nchini, Bodi ilishirikiana na wadau wengine kuwezesha "*Qatar Airways*" kuanzisha safari za ndege za kila siku kati ya Doha na Dar es Salaam kuanzia mwezi Machi 2007. Shirika la Ndege la *Qatar Airways* sasa linaungana na Mashirika ya Ndege ya *Emirates, KLM*, na *Ethiopian Airlines* kuleta watalii nchini kila siku kutoka Marekani, Ulaya, Mashariki ya Kati na Mashariki Mbali. Aidha, Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini limeanzisha safari za moja kwa moja kutoka Johannesburg kwenda Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kiwango cha juu kilichoonyeshwa kwenye kutangaza vivutio vyetu vya utalii, ninayo furaha kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa nchi yetu ilitunukiwa tuzo iitwayo *GOLDEN EUROPE AWARD FOR QUALITY AND COMMERCIAL PRESTIGE* ambayo ilitolewa Berlin - Ujerumani, tarehe 29 Januari 2007. *(Makofi)*

Aidha, kwa kuzingatia utaratibu wa kutambua Maajabu Saba ya Dunia ambao unafanyika katika nyakati tofauti, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kupitia Televisheni ya *ABC Goodmorning America* na Gazeti la *USA Today* ilitangazwa kuwa ni mojawapo ya Maajabu Mapya Saba Duniani.

Vilevile, kutokana na utangazaji bora wa vivutio vyetu kwenye soko la China, Tanzania ilitunukiwa tuzo ijulikanayo kama *CHINESE TOURISTS WELCOMING AWARD* ambayo ilitolewa tarehe 14 Mei 2007 huko Beijing, China. *(Makofi)*

Kwa upande mwingine, Bodi ya Utalii ilitoa tuzo tano mwaka 2007 kwa Kampuni za kimataifa ambazo zilikuwa mstari wa mbele kutangaza vivutio vya utalii vya nchi yetu. Tuzo hizo zilitolewa mbele ya wajumbe 300 walioshiriki kwenye mkutano wa *Africa Travel Association (ATA)* uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia kuanzia tarehe 7 – 11 Mei, 2007. Kampuni zilizopata tuzo hizo ni: *Qatar Airways* -Tuzo ya Shirika ya Ndege Bora 2007; USA Today - Tuzo ya Mwandishi wa Habari za Utalii wa Tanzania; *Tauck World Discovery* - Tuzo ya Wakala Bora aliyetangaza Tanzania; Micato *Safaris na Silversea Cruise* - Tuzo ya Ukuzaji Utalii wa Meli Tanzania na *Lodge* ya Singita *Grumeti Reserves* - Tuzo ya Hoteli Bora ya Kimataifa. Hii ni mara ya saba tangu Bodi ya Utalii ianze kutoa tuzo hizi *(Annual Awards)* kwa madhumuni ya kutangaza utalii wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Ili kuendeleza Utalii wa Ndani, Wizara ilishiriki kwenye maonyesho ya Sabasaba *(DITF)* Julai 2006, maonyesho ya utalii na utamaduni Mkoani Kagera mwezi Oktoba 2006. na maonesho ya utalii ya *Karibu Travel* & *Tourism Fair* yaliyofanyika Arusha mwezi Juni, 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Wizara pia ina jukumu la kusimamia, kulinda, kuhifadhi, kutafiti na kuendeleza urithi wa utamaduni. Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara ilianza mchakato wa kuandaa Sera ya Malikale ambayo ndiyo itakayokuwa dira ya uendelezaji wa sekta ya malikale. Kwa kipindi cha 2006/2007, Rasimu ya Sera ya Malikale ilikamilishwa na inasubiri maamuzi ya Serikali ili ianze kutumika. Wizara pia ilikamilisha maandalizi ya Misingi na Mwongozo wa Uhifadhi wa Urithi wa Utamaduni pamoja na Mwongozo wa Ukarabati wa Majengo ya Kihistoria. Misingi na miongozo hiyo itakuwa na manufaa kwa wadau mbalimbali wanaojihusisha kwa namna moja au nyingine na uhifadhi wa malikale.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika kuhifadhi rasilimali za malikale, Wizara imekamilisha mipango ya kupima mipaka pamoja na kuweka umeme na maji katika Kituo cha Amboni ili kuboresha huduma kwa wageni wanaotembelea kituo hicho. Aidha, hatua za kuchimba kisima cha maji na kuweka umeme wa nguvu ya jua katika Kituo cha Bonde la Olduvai zimeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Mwaka 2006/2007, Wizara ilitekeleza kazi ya kuhifadhi na kulinda Urithi wa Dunia eneo la Kilwa Kisiwani na Songo Mnara kwa kuyanusuru baadhi ya magofu katika maeneo hayo. Lengo ni kuhifadhi maeneo haya na kuyatoa kutoka katika Orodha ya Urithi ulio hatarini kutoweka.

Katika utekelezaji wa kazi hiyo, Wizara imekamilisha ujenzi wa kinga maji, birika za maji na tanuru la kuchomea chokaa Songo Mnara pamoja na kuotesha mikoko karibu na lililokuwa Gereza katika maeneo ya Kilwa Kisiwani ili kuzuia mmomonyoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliwasilisha *UNESCO* maombi ya kuuwezesha mji mkongwe wa kihistoria wa Kilwa-Kivinje kujumuishwa pamoja na Kilwa-Kisiwani na Songo-Mnara katika Orodha ya Urithi wa Dunia. Aidha, maombi yamewasilishwa kuliweka eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuwa eneo la Urithi wa Dunia Mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika kutekeleza ahadi iliyotolewa kwenye Hotuba ya mwaka jana, Wizara imekamilisha rasimu ya kabrasha litakalowasilishwa *UNESCO* kwa ajili ya kuiwezesha Njia Kuu ya Kati ya Biashara ya Utumwa meno ya tembo kuwekwa kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia. Sanjari na rasimu hiyo, Wizara imekamilisha upimaji na uchoraji wa ramani ya Njia Kuu ya Kati ya Biashara ya Utumwa na meno ya tembo.

Vilevile, katika kuhifadhi mji wa kihistoria wa Bagamoyo, Wizara imepima viwanja, kuandaa mchoro wa mpango wa mji huo mkongwe pamoja na ukarabati wa jengo la kihistoria la *Tea House*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutambua wingi wa rasilimali za malikale, mwaka 2006/2007 Wizara ilichukua hatua ya kuandaa mfumo na fomu itakayotumika kuweka kumbukumbu mbalimbali za maeneo ya Urithi wa Utamaduni hapa nchini. Fomu hiyo itasaidia kupata kumbukumbu na kujua idadi kamili ya maeneo yenye kumbukumbu za malikale ambazo zitawekwa pamoja katika kanzidata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za kuhifadhi na kutangaza maeneo ya kale kitaifa na kimataifa zilichukuliwa, ambapo Eneo la Michoro ya Miambani Kondoa liliingizwa katika Orodha ya Urithi wa Dunia. Wizara pia imeanza kuandaa mpango wa kuweka vionyeshwa katika Vituo vya *Caravan Serai (Bagamoyo),* Isimila (Iringa) na Kolo (Kondoa) kwa lengo la kuviboresha vituo hivyo na kuwezesha wageni wanaotembelea vituo hivyo kupata taarifa kwa usahihi zaidi. Wizara pia iliwasilisha maombi *UNESCO* ili njia iliyotumika katika biashara ya Watumwa na Meno ya Tembo kutoka Ujiji kupitia Ulyankulu, Kwihala, Kilimatinde, Mpwapwa, Mamboya hadi Bagamoyo. Njia hii tayari imewekwa kwenye orodha ya awali ya Urithi wa Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Utangazaji Tanzania *(TUT)* ilianza rasmi kurusha kipindi cha *ZAMADAMU* fikiri juu ya urithi wa Mtanzania/malikale zetu tarehe 16/11/2006. Kipindi hiki hurushwa na TVT kila siku ya Alhamisi saa 1.30 hadi 2.00 usiku na kurudiwa

Jumapili saa 5.30 - 6.00 mchana. Hadi kufikia mwezi Mei 2007, Idara imeweza kurusha jumla ya vipindi 26 kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu malikale.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea na utafiti wa akiolojia *(archaeology*) mkoani Kilimanjaro kuhusu "mireshe" katika eneo la Mweka kwa lengo la kujua matumizi yake na pia kutoa taaluma ya uhifadhi wa mahandaki hayo.

Aidha, Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia tafiti za akiolojia zilizofanywa na watafiti mbalimbali toka ndani na nje ya nchi kwa mujibu wa sheria. Vibali tisa kwa ajili ya tafiti za akiolojia, usafirishaji wa masalia, na ukarabati wa majengo ya kihistoria vilitolewa kwa watafiti tisa. Utafiti huo ulifanyika katika maeneo ya Bonde la Olduvai, Bonde la Mandawa - Lindi, Masasi, Kisiwa cha Mafia, Laetoli, Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, na Sanje ya Kati - Kilwa. Aidha, Wizara ilishirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania kufanya sorovea kwa ajili ya kuyatambua makambi, makaburi, majengo, maeneo mbalimbali yaliyotumiwa na wapigania uhuru toka nchi mbalimbali za Afrika. Kazi hiyo ilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mwanza, Mtwara, Lindi, Morogoro, Dodoma, Mbeya na Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza na kutunza kumbukumbu za Muasisi wa Taifa letu, Wizara ilikarabati kituo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kilichopo Magomeni, Dar es Salaam. Lengo ni kuboresha huduma za wageni wanaotembelea kituo hiki ambacho ni nyumba aliyoishi Mwalimu Nyerere akiwa Waziri Mkuu wa Kwanza wa Tanganyika. Vilevile, Wizara ilianza ujenzi wa kituo cha taarifa na kumbukumbu cha Dr. Livingstone kilichopo Ujiji Kigoma.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania lina jukumu la kukusanya, kuhifadhi, na kutafiti vitu vyote vinavyotambulika kama urithi wa Tanzania wa utamaduni, kihistoria, kisayansi na kiteknolojia.

Mwaka 2006/2007, Shirika liliandaa maonesho ya ikolojia katika Makumbusho ya elimu viumbe wakiwemo Tembo, Nyati na Kifaru. Aidha, Shirika lilichukua hatua za kuboresha Kijiji cha Makumbusho ili kiweze kuvutia watalii zaidi. Miongoni mwa kazi zilizofanyika ni ukarabati wa nyumba za jadi za jamii za Wakwere/Wadoe, Wamwera, Wafipa na Wangoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni ilifungua tovuti na kuandaa maonesho kuhusu biashara ya utumwa. Maonesho haya yalitembezwa katika Wilaya za Ilala, Kinondoni na Temeke katika Mkoa wa Dar es Salaam kuanzia tarehe 28 Agosti hadi 2 Septemba 2006. Katika Makumbusho ya Azimio la Arusha yaliandaliwa maonesho ya siku moja tarehe 5/2/2007 kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 40 ya Azimio la Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Shirika lina jukumu la kuhamasisha na kushirikisha jamii katika uhifadhi wa rasilimali za utamaduni, kwa kutekeleza Programu ya Siku ya Utamaduni wa Mtanzania, ambapo jamii ya Wakerewe ilifanya tamasha la kabila hilo katika Kijiji cha Makumbusho tarehe 19 - 20 Agosti 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na uvumi ulioenea miongoni mwa jamii kuhusiana na mnyama aina ya Nguva kufananishwa kimaumbile na binadamu, Shirika lilielimisha Umma kuhusu mnyama huyo kuwa, huyu ni mnyama anayezaa, anayenyonyesha na kula majani kama wanyama wengine. Kimaumbile ana mapezi mawili, hukumbatia mtoto na hutoa machozi kama binadamu tofauti na samaki wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kama ilivyoahidiwa katika Bunge lako mwaka jana, Shirika limechukua hatua ya kuandaa mchanganuo wa mradi wa kuongeza ghala za uhifadhi katika Makumbusho ya Elimu ya Viumbe na mchanganuo wa matengenezo ya magari ya kihistoria aina ya *Rolls-Royce* na juhudi za kutafuta wafadhili wa kutengeneza magari hayo zinaendelea. Aidha, ukarabati wa jengo lililokuwa likitumiwa na *Malihai Clubs* ulikamilika katika makumbusho ya Elimu ya Viumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kutekeleza jukumu la kulinda, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za maliasili na malikale pamoja na utalii, Wizara iliendelea kuboresha mazingira ya kazi na kuendeleza watumishi ikiwemo kuimarisha ustawi wao.

Mwaka 2006/2007, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka mbalimbali ilipandisha cheo watumishi 587, iliajiri watumishi wapya 268 na kujaza nafasi mbadala 44. Ili kuwaendeleza Watumishi kitaaluma, watumishi 712 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 84 walipata mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwawezesha watumishi wake kupata mafunzo, Wizara pia iligharimia mafunzo ya watumishi wa Serikali za Mitaa katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada za Uzamili. Aidha, iliendelea kugharimia mafunzo ya wanafunzi watarajali katika taaluma ya misitu na ufugaji nyuki kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo watendaji na wataalam wa kutosha katika soko la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea kuzingatia Kanuni za Utawala Bora kwa kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati wa Kuzuia Rushwa 2006-2010. Katika kipindi hicho, Wizara ilishughulikia tuhuma mbalimbali zilizotolewa kupitia magazeti na barua ambapo jumla ya malalamiko 18 yalipokelewa na kushughulikiwa. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa baadhi ya Maafisa Wakuu na Waandamizi juu ya misingi ya Utawala Bora katika kutekeleza mkakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, UKIMWI bado ni janga linaloendelea kuangamiza nguvukazi ya Wizara na Taifa kwa ujumla. Kwa kuzingatia tatizo hilo mwaka 2006/2007, Wizara ilishirikiana na Tume ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI kuhamasisha watumishi kupima afya zao, kununua chakula chenye virutubisho na dawa za kurefusha maisha. Aidha, Wizara ilifanya tathmini ya hali halisi ya UKIMWI sehemu za kazi na kukagua matumizi ya dawa za magonjwa nyemelezi na utendaji kazi wa waelimishaji rika. Tathmini hiyo ilifanyika katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Mara, Mwanza, Kagera, Kigoma, Mtwara, Morogoro, Pwani na Tanga.

Vilevile, Wizara iliteua Wataalamu Washauri kufanya tathmini ya hali halisi ya UKIMWI, kuingiza masuala ya UKIMWI kwenye Mitaala ya vyuo vilivyoko chini ya Wizara na kuandaa kanzidata kuhusu UKIMWI. Matokeo ya awali yanatarajiwa kupatikana katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuimarisha afya, ustawi na ushirikiano kati ya watumishi na wale wa wizara mbalimbali, Wizara ilishiriki michezo ya Shirikisho la Michezo ya Wizara (SHIMIWI) iliyofanyika Mkoani Tanga na ya Mei-Mosi iliyofanyika Kitaifa Mkoani Mwanza. Jumla ya watumishi 80 walishiriki katika michezo hiyo na kushinda medali mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea kusimamia na kuboresha vyuo vya mafunzo vilivyo chini yake kwa lengo la kuimarisha taaluma zinazohusu maliasili na utalii. Vyuo hivyo ni Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - Mweka (Moshi), Chuo cha Misitu Olmotonyi (Arusha), Chuo cha Mafunzo ya Viwanda vya Misitu (Moshi), Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi (Mwanza), Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi-Mbegani, (Bagamoyo), Chuo cha Uvuvi Nyegezi (Mwanza), Chuo cha Taifa Cha Utalii (Dar es Salaam) na Kituo cha Elimu ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii cha Likuyu-Sekamaganga (Namtumbo). Katika kutekeleza mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara imelenga kutoa kipaumbele kwa maeneo matatu yafuatayo:-

- Kutekeleza programu za uendelezaji, uhifadhi na usimamizi wa maliasili, malikale na utalii;
- Kukuza na kuendeleza utalii; na
- Kusimamia mafunzo na utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Wanyamapori utawasilishwa Bungeni mwaka 2007/08. Aidha Kanuni za uanzishaji wa Ranchi na Mashamba ya Kufuga Wanyamapori na Kanuni za Biashara ya Viumbe Hai zitakamilika katika mwaka 2007/08.

Maeneo nane kati ya 16 ya majaribio ya Kanuni za *WMA* yalikamilisha mchakato na kutangazwa kuwa *WMA* na jumuiya zao kuidhinishwa. Aidha maeneo hayo yalipata Haki ya Kutumia raslimali ya wanyamapori (*user rights*). Mchakato wa kuyatangaza maeneo mengine matano kati ya nane ambayo hayajapata haki ya kutumia wanyamapori utakamilishwa mwaka huu wa fedha. Aidha, Serikali itawezesha maeneo matatu yaliyobaki ili yaanze mchakato wa kuanzisha *WMA* pindi migogoro ya ardhi baina ya vijiji na matumizi ya ardhi baina ya wanavijiji itakapotatuliwa.

Taarifa ya Wataalam waelekezi (*Consultants*) kuhusu tathmini ya Utekelezaji wa Kanuni za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori *(WMAs)* itakayojumuisha maoni ya wadau itapokelewa na ushauri utakaotolewa utawezesha Wizara kuwa katika

nafasi nzuri zaidi ya kuanzisha na kuwahamasisha wananchi juu ya kuhifadhi na kutumia Mali Asili ya Wanyamapori kwa mtindo wa *WMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaimarisha ulinzi wa raslimali ya wanyamapori katika maeneo ya uhifadhi kwa kufanya doria, kutoa mafunzo maalum kwa askari wanyamapori na kuwapatia vitendea kazi muhimu. Aidha, Wizara itanunua ndege moja aina ya *Grand Caravan* yenye uwezo wa kubeba abiria (askari) 14 kwa ajili ya kurahisisha operesheni za kukabiliana na ujangili kwa kuwezesha askari wanyamapori kufika kwenye maeneo ya matukio ya uhalifu haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina jukumu la kulinda wananchi na mali zao dhidi ya wanyama wakali na waharibifu. Idadi ya mamba nchini inakadiriwa kuwa 72,000. Kutokana na idadi hii kubwa mamba wamekuwa tishio kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara itatoa vibali vya kuwinda mamba 1500 katika maeneo hayo kwa lengo la kupunguza tatizo hili.

Zoezi la kuangamiza kunguru weusi kwa kutumia kemikali aina ya *DRC – 1339* iliyonunuliwa kutoka New Zealand litaanza rasmi mwaka huu wa fedha. Kazi ya kuharibu mayai na makinda ya kunguru hao itaanza mwezi Septemba, 2007 ambacho ni kipindi cha majira ya kunguru weusi kutaga mayai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina raslimali kubwa ya Wanyamapori nje ya hifadhi zetu za Taifa. Katika maeneo haya yaliyopo kwenye mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo ya wazi, Wizara imepanga matumizi endelevu ya maliasili ikiwa ni pamoja na kuendesha biashara ya uwindaji wa kitalii. Hata hivyo, mapato kutokana na shughulii za uwindaji wa kitalii yamekuwa chini sana. Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 serikali iliunda Kamati ya kuangalia upya namna ya kuboresha uendeshaji wa tasnia ya uwindaji wa kitalii. Kamati ililinganisha uendeshaji, mapato, taratibu za ulinzi na uhifadhi hapa nchini na ule wa nchi za Afrika Kusini, Zimbabwe, Mozambique na Botswana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kutekeleza sehemu ya mapendekezo ya ripoti kwa kubadilisha ada ya kukodisha vitalu vya uwindaji kwa mwaka na ada za kuwinda wanyama mbalimbali. Wakati ada ya kukodi eneo la kujenga hoteli au tented camp lenye ukubwa wa Hekta 1–5 katika Pori la Akiba Selous ni *USD 36,000* kwa mwaka, vitalu vya uwindaji vyenye ukubwa wa kilometa za mraba 500 mpaka 1,500 (katika Pori la Akiba Selous) ada yake ni *USD 10,000* tu. Kutokana na kasoro hiyo, Serikali imepanga vitalu vya uwindaji katika kategoria A na B. Kategoria A ni vile vitalu vinavyopakana na hifadhi za taifa na vile vilivyopo kwenye mapori ya akiba, ambavyo ada yake imeongezwa kutoka *USD 10,000* za sasa hadi *USD 50,000* kwa mwaka. Kategoria B ni vitalu vyote 74 vilivyobaki na ada yake kwa mwaka imebadilishwa kutoka *USD 10,000* mpaka *USD 40,000.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hatua hii ya Wizara itaongeza mapato ya Serikali kutoka *USD 1,580* milioni na kufikia *USD 7,160* milioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeongeza ada za wanyamapori (*game fees*) ili ziwiane na zile za nchi za *SADC.* Kwa mfano, ada ya kuwinda Simba hapa nchini kwa sasa ni *USD 2,500* wakati ada ya kuwinda mnyama huyo huyo nchini Afrika Kusini ni *USD 18,000.* Hivyo, ada ya kuwinda Simba imeongezwa kutoka *USD 2.500* za sasa na kufikia *USD 12,000*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia imezingatia kuwa ada ya kuwinda Tembo nchini Botswana ni *USD 25,000* wakati ada ya kuwinda Tembo hapa nchini ni *USD 5,000.* Wizara imerekebisha ada ya kuwinda Tembo na kufikia *USD 15,000.*

Ada ya kuwinda Chui imerekebishwa kutoka *USD 2,500* sasa na kufikia *USD 12,000* na ada ya kuwinda Kiboko kutoka *USD 1,050* na kufikia *USD 2,500.* Marekebisho haya ya ada za wanyama yataiongezea mapato Serikali kutoka *USD 6.0* milioni mwaka 2006/2007 na kufikia *USD 16.*milioni katika mwaka huu wa fedha. Katika marekebisho haya gharama nyingine kama vile:-

(i) Ada ya uhifadhi (*Conservation fee;*

(ii) Ada ya utunzaji nyara (*Trophy handling fee);*

(iii) Ada ya wawindaji Bingwa (*Professional Hunter's License Fee);*

(iv) Ada ya Mtihani wa Wawindaji Bingwa *(Professional Hunter's Examination Fee*); na

(v) Ada ya kibali cha kuwinda (*Permit fee*) zimebakia kama zilivyokuwa mwaka jana. Ada hizi zitailetea Serikali jumla ya USD 3.2 milioni katika mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya hatua hizi za Wizara ni kuongeza mapato ya Serikali kutoka Shs.11 bilioni mwaka 2006/2007 na kufikia Shs.33.355 bilioni katika mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, Wizara itaimarisha miundombinu ili kukidhi mahitaji ya utawala; ulinzi; na matumizi endelevu katika mapori ya akiba kwa kufanyia matengenezo barabara zenye urefu wa kilometa 500; kufyeka na kuweka alama mipaka katika Mapori ya Akiba ya Liparamba, Mpanga-Kipengele na Mkungunero; kuboresha viwanja vya ndege vya Mtemere, Matambwe, Kingupira, Rungwa na Burigi; hivyo kuimarisha shughuli za ulinzi, kufanikisha uwindaji wa kitalii na utalii wa kutazama wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya mahitaji ya Sera ya Wanyamapori na mwongozo wa kusimamia na kuendeleza maeneo yaliyohifadhiwa ni kuhakikisha kila eneo lina Mpango wa Usimamizi na Uendelezaji (*General Management Plan (GMP).* Katika mwaka huu wa fedha Wizara itatayarisha *GMP* mpya za Mapori ya Akiba ya Lukwika-Lumesule-Msanjesi, Ugalla, na itakamilisha *GMP* ambazo zimeshaanzishwa za Mapori ya Akiba ya Maswa na Moyowosi-Kigosi. Aidha itapitia *GMP* za Pori la Akiba

la Selous, ili kubaini maeneo mapya ya uwekezaji katika huduma za utalii ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kambi za mahema, loji, kuimarisha mawasiliano, viwanja vya ndege na barabara. Hatua hii inachukuliwa kwa makusudi, ili kukidhi ongezeko linalotarajiwa la mahitaji ya vitanda, kutokana na kuimarisha utangazaji wa vivutio vyetu vya utalii nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa uvamizi haujirudii katika Bonde la Usangu, Azimio la kuunganisha Pori hilo na Hifadhi ya Ruaha litawasilishwa Bungeni mwaka huu wa fedha. Aidha, maeneo muhimu ya Ardhioevu ya Ihefu na maeneo nyeti ya vyanzo vya maji vya Bonde la Usangu yataunganishwa na Hifadhi ya Ruaha. Hatua hii itaongeza eneo la Hifadhi ya Ruaha kutoka kilometa za mraba 10,300 na kufikia 20,226. Hatua hii itaifanya Hifadhi ya Ruaha kuwa ya pili kwa ukubwa Barani Afrika kufuatia Hifadhi ya Taifa ya Kafue iliyoko Zambia (kilomita za mraba 22,400). Aidha kiasi cha maji yatakayohifadhiwa katika Bonde la Usangu kitaongezeka na kuhakikisha maji kutiririka kwenye Mto Ruaha kwa mwaka mzima. Vilevile, kina cha maji katika Bwawa la Mtera kitaongezeka, hivyo kuongeza uzalishaji wa umeme wa uhakika katika Bwawa hili.

Pamoja na hatua hizo, Wizara yangu itawasilisha Bungeni Azimio la kuanzisha Hifadhi mpya ya Taifa Mkomazi kwa kuyapandisha hadhi Mapori ya Akiba ya Mkomazi na Umba, na vilevile kuanzisha Hifadhi Mpya ya Kisiwa cha Saanane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara itaandaa mipango huishi ya usimamizi na uendeshaji wa Bonde la Ziwa Natron (*Lake Natron Basin Ramsar Site)* na Ziwa Jipe, na itaanza kutekeleza mpango huishi wa uendeshaji na usimamizi wa Eneo la Ardhioevu la Malagarasi-Muyovozi *(Malagarasi-Muyovozi Ramsar Site).* Vilevile, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Usimamizi Endelevu wa Ardhioevu katika mikoa ya Iringa na Mbeya, na mradi wa kuandaa na kutekeleza mpango huishi wa usimamizi na uendeshaji wa Ardhioevu ya Bonde la Mto Kilombero *(Kilombero Valley Ramsar Site).* Aidha, Wizara itaanza kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Ardhioevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za kuelimisha jamii zitafanyika kwa kutumia majarida na kampeni mbalimbali kwa wananchi waishio karibu na maeneo ya hifadhi. Vilevile, Wizara itaendeleza utaratibu wa kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo itaanzishwa na wananchi walioko kwenye maeneo hayo. Aidha, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori *(WMA)* yatakayoshiriki katika matumizi endelevu ya wanyamapori yanatazamiwa kupewa mgao wa mapato kutokana na matumizi hayo kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* katika kute *Smart Cards* na *Credit Cards* badala ya kukusanya fedha taslimu. Aidha, hatua za kuhakiki na kuandikisha watalii wote wanaoingia katika hifadhi za Taifa zitachukuliwa ili kuhakikisha usalama na ukusanyaji mapato ya serikali. Shirika limeingia mkataba wa kukusanya mapato na mabenki ya *CRDB* na Exim. Kwanza benki hizi zitaanza kukusanya mapato katika Hifadhi za Mlima Kilimanjaro, Arusha, Tarangire, Ziwa

Manyara na Serengeti. Baada ya hapo huduma hii itasambazwa kwenye Hifadhi nyingine zilizobaki. Aidha mikataba na benki husika itakuwa inafanyiwa mapitio mara kwa mara na kutathmini utendaji wa mabenki hayo. Hatua hii inalenga kuziba mianya ya upotevu wa maduhuli ya Shirika, na kuingia kwenye mtandao wa matumizi ya tekinolojia mpya ya malipo, hivyo kukidhi mahitaji ya soko la utalii. *(Makofi)*

Shirika pia, litadadisi njia na kubuni mkakati wa kuboresha makusanyo ya fedha za pango (*concession fees)* toka kwa kampuni zinazomiliki kambi za mahema za kitalii na loji katika Hifadhi za Taifa. Aidha utaratibu wa kutunza mahesabu ya Shirika kwa kompyuta (*Computerization of Accounts)* ambao umeshaanza kwa awamu utaendelezwa katika maeneo yote yanayoingiza mapato na unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za Shirika kujitangaza nje ya nchi zimeanza kuzaa matunda. Idadi ya wageni waotembelea Hifadhi za Taifa inaongezeka kila mwaka. Inatarajiwa kuwa ifikapo mwaka 2010 idadi ya wageni watakaotembelea Hifadhi za Taifa itafikia 850,000 hadi 900,000. Ili kukidhi mahitaji ya ongezeko la vitanda, Shirika litakamilisha mapitio ya *GMP* za Hifadhi za Taifa za Serengeti, Ruaha, Katavi, Mikumi na Tarangire, hivyo kupanua wigo wa uwekezaji katika huduma za utalii na kuwezesha ujenzi wa kambi za mahema, loji na kuboresha miundombinu ya mawasiliano na usafiri. Kipaumbele kitawekwa kwenye kuimarisha barabara zilizopo na kufungua mpya ili kuhakikisha kwamba vivutio vya utalii vinafikiwa kwa urahisi kwa kipindi cha mwaka mzima. Vilevile, Shirika litaboresha viwanja vya ndege katika Hifadhi za Taifa na kuimarisha hali ya usalama hadi kufikia viwango ambavyo vinakubalika na kusajiliwa na Mamlaka ya Usalama wa Anga (*Civil Aviation Authority*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** nchi yetu imekuwa ikiweka juhudi kubwa katika kutangaza utalii wa nchi yetu. Kampeni hii ya kuitangaza Tanzania imeanza kuzaa matunda na watalii wengi sana wanakuja nchini kutoka Marekani, Uingereza, Canada, Ujerumani, Italia, Ufaransa, Spain, Brazil, Urusi na Mataifa mengine.

Nia ya Serikali ni kuongeza watalii kutoka 700,000 wa sasa na kufikia 1.2 milioni itakayopatikana mwaka 2012; pamoja na kuongeza mapato kutoka katika sekta hii kuanzia Shs.1.2 Trilioni ya sasa na kufikia 2.5 Trilioni katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Mapato ya sekta ya utalii yanatokana na kuwauzia watalii huduma za usafiri, huduma za malazi, vyakula na vinywaji, ada za kuingia kwenye hifadhi na watalii kununua bidhaa mbalimbali. Hivi sasa wageni wengi wanaotaka kuja Tanzania wanavunja safari zao au kwenda nchi zingine za jirani kwa sababu hatuna Hoteli za kutosha. *(Makofi)*

Suala la kuwa tusijenge kabisa hoteli katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na katika hifadhi zetu zingine limeshabikiwa sana ndani na nje ya nchi na watu ambao ama hawana takwimu sahihi au hawana nia njema na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Hifadhi ya Serengeti ina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 16,000. Eneo hili ni kubwa kuliko nchi ya Ubelgiji, au sawa na eneo

lote la Jamhuri ya Ireland. Ni eneo kubwa la mbuga ya majani *(savannah*) na miti michache, lenye mawe makubwa (*Iselbergs)* yaliyopo, katika sehemu chache za hifadhi.

Mbuga hii ya Serengeti imeungana na Mbuga ya Masai-Mara ya Kenya. Mbuga ya Masai-Mara ina ukubwa wa kilometa za mraba 3,000. Eneo hili ni asilimia 18.7% tu ya Serengeti. Aidha, mzunguko wa wanyama wa Serengeti hususan nyumbu, umetangazwa kama moja ya maajabu mapya ya dunia. Kwa kipindi cha miezi miwili, mzunguko wa nyumbu unakuwa Masai-Mara huko Kenya na kwa miezi 10 iliyobaki unakuwa Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi mahitaji ya wageni na watalii katika Hifadhi ya Masai-Mara nchini Kenya, wamejenga Hoteli 340 zenye vyumba 7,400. Kwa upande wa Tanzania, hoteli zote Serengeti zina vyumba 940. Hii ni katika eneo ambalo lina ukubwa karibu mara 6 ya Masai-Mara. Kutokana na tofauti hii, Masai Mara ilikusanya *USD* 750 milioni mwaka wa 2006 wakati mbuga yetu ya Serengeti imekusanya *USD* 30 milioni mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ipo haja kwa Serikali kuhifadhi mbuga zetu za Taifa kwa makini kwa kufanya utafiti wa kina kuona kuwa kila hatua tunayochukua ya kuwekeza katika Hifadhi zetu haiathiri hali ya hifadhi hizo miaka ijayo. Serikali itatumia matokeo ya utafiti wa kisayansi kuelekeza uwekezaji na kuhakikisha unazingatia sera yetu ya Taifa ya Wanyamapori. Aidha, Serikali inataka kila hoteli inayojengwa itanguliwe na utafiti wa mazingira *(Environmental Impact Assessment* au *EIA)* na kuwa ujenzi wa hoteli yoyote ufanane na mazingira yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia hayo, Serikali imeangalia upya *General Management Plan (GMP)* ya Serengeti na kuamua kuongeza hoteli za nyota 5 au zaidi ili zifikishe jumla ya vitanda 4,500 ifikapo mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Katika Hifadhi ya Serengeti inapita barabara kuu kutoka Musoma mpaka Arusha. Barabara hii yenye urefu wa 214 Km inapitisha mabasi makubwa, malori makubwa ya mizigo na magari aina ya Fuso mengi sana. Aidha, ndani ya mbuga hii ndege za abiria 15 zinatua kwa siku katika kiwanja cha Seronera, 15 kwa siku katika kiwanja cha Fort Ikoma na 15 zingine katika viwanja vya Lobo na Kirawira. Serikali imefanya utafiti wa kina juu ya madhara kwenye mazingira ya hifadhi na wanyama, na kuangalia njia za kupunguza usumbufu huo.

Hivyo, Serikali imeamua, badala ya kuweka lami barabara ya Kilometa 214 inayopita katikati ya hifadhi ya Serengeti, ijenge barabara ya lami ya kilometa 45 kuanzia Tabora B Wilaya ya Serengeti, kupitia Kaskazini mwa Hifadhi ya Serengeti mpaka Mto wa Mbu, kupitia Loliondo, Lake Natron na Engaruka. Serikali pia imeamua kujenga kiwanja kimoja cha ndege katika mji wa Mugumu ambao uko kilometa 16 kutoka ukingo wa magharibi wa Hifadhi ya Serengeti ili kuondoa usumbufu wa ndege nyingi zinazotua kila siku ndani ya Hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Miradi hii itapunguza magari ndani ya hifadhi kwa watalii wanaotoka Arusha, kutumia usafiri wa ndege wanapofika Mugumu badala ya kurudi Arusha wakipitia ndani ya hifadhi. Wasiotutakia mazuri wanasema barabara iliyopangwa itaathiri hifadhi, wakisahau kuwa hivi sasa tunayo barabara ya kilometa 214 inayopita ndani ya hifadhi hiyo.

Aidha, wanasema kiwanja cha Mugumu kitakuwa na madhara kwa wanyama, huku wakijua kuwa kiwanja cha Skukuza katika Kruger National Park, Afrika ya Kusini kinapokea ndege kubwa na kiko katikati ya hifadhi hiyo. Aidha, kiwanja cha Jomo Kenyatta Nairobi kipo kilometa 5 tu kutoka *Nairobi National Park.* Kwa hiyo viwanja hivi havina madhara yaliyobainika kisayansi. Mashabiki haohao wanatangaza kuwa kiwanja cha Tanzania kilichoko kilometa 16 kitakuwa na madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika jambo hili ni vyema tuwe makini na tutetee maslahi ya nchi yetu. Tanzania itajengwa na watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majukumu ya Mamlaka inayosimamia Hifadhi ya Ngorongoro yanajumuisha kuhifadhi wanyamapori, kusimamia shughuli za utalii na kuendeleza jamii ya wafugaji wa Kimasai ambao wanaishi ndani ya hifadhi kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro.Kufuatia uamuzi wa kupunguza msongamano wa idadi ya wakazi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka itaimarisha miundombinu katika Kijiji cha Oldonyosambu kilichoko nje ya Hifadhi kwa kutengeneza barabara yenye urefu wa kilomita 24 kati ya kijiji hicho na eneo lililotengwa. Kazi hii itafanyika kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika litakarabati barabara za ndani ya Hifadhi zenye jumla ya kilomita 281, kufungua barabara moja mpya kutoka Loonguku-Olbalbal-Lemuta na kukarabati kiwanja cha ndege cha Ndutu. Katika kuboresha huduma Shirika litakamilisha ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Vile vile ujenzi wa nyumba za watumishi utaanza katika kiwanja kilichoko nje ya Hifadhi, Eneo la *Kamyn Estate* katika Wilaya ya Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idadi ya wageni wanaotembelea Hifadhi ya Ngorongoro inaongezeka mwaka hadi mwaka. Ili kukidhi mahitaji ya vitanda Mamlaka inakaribisha wawekezaji kujenga kambi za kitalii *(tented camps)* zenye uwezo wa vitanda 40 na loji *(Lodges)* zenye uwezo wa vitanda 100 katika maeneo ya Empakaai, Nainokanoka, Esirwa, Naibataat na Ziwa Masek. Aidha, Mpango wa Kusimamia na Kuendeleza *(GMP)* Hifadhi ya Ngorongoro utafanyiwa mapitio ili kubaini maeneo zaidi ya kuwekeza kwa huduma za kitalii.Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2007/08, Shirika limepanga kuongeza vivutio vya utalii katika maeneo sita (6) ambayo ni: (a) Maeneo ya kimila katika *Crater* (b) Maeneo ya safari za miguu *(Nature trails)* ( C) Vianzo vya chemi chemi katika Msitu wa Nyanda za Juu Kaskazini (d) Miinuko na Mabonde ya Ziwa Eyasi (e) *Crater* ya Olmoti, na (f) Utamaduni wa Wahazabe na Watatoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania ni muhimu sana katika kuwezesha Idara ya Wanyamapori kulinda kikamilifu rasilimali ya wanyamapori katika mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo ya wazi yenye wanyamapori, kuchangia gharama za mafunzo na miradi ya maendeleo ya wananchi wanaoishi jirani na maeneo yaliyohifadhiwa.

Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Mfuko unatarajia kukusanya Shilingi Bilioni 7.5. Mfuko utawezesha Idara kufanya doria ndani na nje ya mapori ya akiba kwa kugharamia siku za doria 20,000, kuendesha operesheni maalum, kununua vifaa vya kazi ikiwa ni pamoja na magari ya doria 15, mahema 100, radio za upepo 10, simu za *satellite* 20, bunduki na risasi na sare za askari 1,400. Aidha mfuko utagharamia ujenzi wa ukarabati wa nyumba za watumishi, majengo ya ofisi, barabara na viwanja vya ndege katika Mapori ya Akiba, Vyuo vya Mafunzo ya wanyamapori na Kanda za Kikosi Dhidi ya Ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maeneo mengine yatakayogharamiwa na Mfuko ni pamoja na utekelezaji wa Mikataba ya kimataifa (kama vile Mkataba wa Lusaka, *CITES, Ramsar, AEWA* na *CMC),* usimamizi wa uwindaji wa kitalii, utafiti na sensa za wanyamapori, uratibu wa kuhifadhi wanyamapori waliopo katika hatari ya kutoweka duniani, hususan tembo na faru weusi na mafunzo ya uhifadhi.

Katika kutekeleza Sera ya Wanyamapori kuhusu kushirikisha wananchi katika uhifadhi, Mfuko utachangia katika kuendeleza *WMAs* pamoja na miradi ya maendeleo ya wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 itatekeleza yafuatayo:-

1. Kutafiti mwenendo wa magonjwa ya wanyamapori hasa ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa. Magonjwa ya muhimu yanayoangaliwa ni pamoja na sotoka, ndigana, mafua ya ndege na *African swine fever*.

2. Kuendeleza utafiti wa tatizo la tembo waharibifu katika Wilaya za Serengeti na Bunda. Utafiti unalenga kupunguza madhara ya uharibifu wa tembo kwenye mashamba kwa kutumia njia zisizosababisha vifo vyao.

3. Kuendeleza utafiti wa mbwa mwitu katika Hifadhi za Serengeti na Ngorongoro.

4. Kuendeleza utafiti wa wanyama wa jamii ya wanyama wanaokula nyama *(Carnivores*).

5. Kuendesha mafunzo ya ufugaji nyuki kwa njia za kisasa.
6. Kufanya sensa 10 za wanyamapori katika Mapori ya Akiba ya Ugalla, Muhesi-Kizigo, Burigi-Biharamulo, Ibanda-Rumanyika na Hifadhi za Taifa za Serengeti na Mkomazi, pamoja na eneo la wazi la Ziwa Natron.

7. Kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Taasisi Arusha.

Aidha, Taasisi itapitia Mwongozo wa kusimamia na kuratibu tafiti za Wanyamapori nchini. Sambamba na hilo, Taasisi itakamilisha mapitio ya ada za utafiti ili kuongeza mapato ya Taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Wanyamapori Mweka ni kituo cha Umahiri (*Centre of excellence*) cha mafunzo ya uhifadhi katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pamoja na kuendeleza mafunzo ya kawaida katika fani ya uhifadhi, mwaka huu 2007/2008 Chuo kitaendesha kozi ya Wawindishaji Bingwa. Watanzania wenye taaluma ya uhifadhi wa Wanyamapori, pamoja na wale wanafunzi wa masomo ya kawaida ya uhifadhi wanakaribishwa kujiunga na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2007/2008 wizara yangu itaweka mkazo katika kudhibiti uvunaji haramu wa mazao ya misitu; kuongeza mapato yatokanayo na mazao ya misitu; kuongeza kasi ya upandaji miti; kudhibiti uharibifu wa misitu na kuanza mchakato wa kufufua sekta ndogo ya ufugaji nyuki. Nchi yetu inayo rasilimali kubwa ya misitu. Faida kuu ya misitu yetu ni kulinda mazingira yetu; kutupatia hewa safi na kutunza vyanzo vya maji. Misitu yetu inalinda hali ya hewa na kutupa uhakika wa misimu ya mvua na kiangazi kutobadilika mara kwa mara. Aidha, misitu yetu ni makazi ya bainuai muhimu ya mimea na wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma hizo za mazingira, uvunaji wa mazao ya misitu lazima uwe endelevu. Wizara yangu inafanya uhakiki wa miti na kupima ujazo wa mazao ya miti hasa magogo na kukadiria kiwango tunachoweza kuvuna kila mwaka bila kuathiri mazingira. Katika mashamba ya miti laini ya *Pine* na *Cypress,* Wizara imekadiria kuvuna kiasi cha meta za ujazo 669,000, miti ya mikaratusi meta za ujazo 12,000, mitiki mita za ujazo 41,000, na miti mingine meta za ujazo 38,000.Katika misitu ya asili, uhakiki na kukadiria ujazo wa magogo yaliyopo unaendelea. Kazi imekamilika katika Wilaya 11. Katika Wilaya hizo, uhakiki umeonyesha kuwa kuna magogo yenye ujazo wa miti iliyosimama wa meta za ujazo 55.8 milioni. Kati ya ujazo huo, Wizara imekadiria kuvuna magogo yenye ujazo wa meta 790,000 kati ya miti yenye ujazo wa meta 11.5 milioni. Ujazo huo na ule utakaovunwa kwenye mashamba ya miti ndio uwezo halisi wa Viwanda vyetu vya ndani. Hivyo, Wizara yangu inakaribisha wawekezaji katika viwanda vya kisasa vya kupasua mbao *(sawmills*); viwanda vya kukoboa magogo (*veneer factories*), viwanda vya *fibre* na *particle boards* na karakana za kutengeneza *furniture (Furniture and Household goods).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kupiga marufuku usafirishaji nje ya nchi wa magogo yatokayo kwenye misitu yetu ya asili. Aidha, bei ya $M^3$ ya magogo ya daraja la kwanza (mpingo, mvule, mninga) katika soko la dunia ni *USD 2,000 – 10,000* na sisi tunawauzia kwa *USD 50* mpaka 70. Tunahamishia Ajira nje ya nchi na kuhamisha Kodi ya ongezeko la thamani nje ya nchi. Nchi yetu haiwezi kwenda mbele kwa mtindo huu. Magogo yatakayoruhusiwa kusafirishwa ni yale tu yatokanayo na mauzo kupitia

katika zabuni za wazi (*open tender process*) na hata hayo, kibali cha kusafirisha nje kitatolewa tu baada ya serikali kupokea malipo yote ya magogo yaliyohusika katika zabuni hizo. Hatua hizi ni muhimu kwa kuwa hatuwezi kuwavuta wawekezaji wakaja Tanzania kujenga viwanda vya mazao ya misitu kama tutakuwa tunawapelekea magogo huko kwao kwa bei ya kutupa kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa muda mrefu sana, bei ya magogo ya miti nchini Tanzania ni ya chini kupindukia. Kwa mfano, bei ya meta ya ujazo wa magogo ya *Pine* na *Cypress* ni Shilingi 4,800. Bei hii ni chini ya gharama ya miche mitano ya Pine ambayo gharama yake ni Shilingi 5,000. Ukizingatia kuwa miti hii imekuzwa kwa uwekezaji wa Serikali kwa miaka 25 – 30; na ukazingatia kuwa uwekezaji wa Serikali unategemea riba ya 8%; bei ya magogo hayo ni kama sifuri kwa mwekezaji (Serikali).

Aidha, pamoja na thamani ya magogo ya mitiki katika soko kuwa kati ya *USD 750* mpaka *USD 1,000,* bei ya magogo ya mitiki katika mashamba yetu ni kati ya Shilingi 50,000 mpaka Shilingi 70,000 *(USD 50 – USD 70)* kwa meta ya ujazo. Kutokana na kasoro hizo, Serikali imepitia bei za mazao ya misitu hususan magogo kutoka kwenye mashamba ya miti (*Forest Plantations*) na Misitu ya Asili; lengo likiwa kufikia angalau asilimia 30% za bei ya soko.Kufuatia marekebisho haya, inakisiwa kuongeza mapato ya Serikali kutoka Shilingi 11 bilioni mwaka 2006/2007 na kufikia Shilingi 45 bilioni katika mwaka wa 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uvunaji wa Magogo bila kufuata Sheria. Tangu mwaka wa 2004, kumekuwa na uvunaji wa magogo usio endelevu katika misitu yetu ya asili. Miti inakatwa kwa wingi bila leseni na kusafirishwa nje ya nchi kinyume cha sheria. Serikali inachukua hatua kali sana za kinidhamu kwa wafanyakazi waliohusika.

Aidha, Kamishna Mkuu wa *TRA* akishirikiana na Makamishna wenzake wa China, India, Japan, Korea, Indonesia na Thailand wanafuatilia kujua ni nani alipeleka magogo katika nchi hizo kutoka Tanzania; amepewa kibali na nani na amepeleka magogo kiasi gani na amelipia mangapi ili hatua stahili zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaipitia Sheria ya Misitu ili kuanzisha Baraza la Ithibati na Nidhamu la wataalamu wa misitu ili wataalamu wote wa misitu waandikishwe upya. Baada ya kuandikishwa Baraza litafuatilia nidhamu na maadili ya wataalamu hao na kuwafuta kwenye rejesta wanapoonekana kwenda nje ya maadili. Ni wataalamu wale tu walioandikishwa ndio wataruhusiwa kufanya kazi Tanzania. Aidha, Wizara itashirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ili kuangalia upya mitaala ya Shahada za Misitu kwa nia ya kufundisha wahifadhi wa Misitu *(Forestry Conservators)* badala ya hali iliyopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuendeleza Mashamba ya Misitu. Mashamba 16 ya miti ya *Pine, Eucalyptus, Cypress* na Mitiki tuliyonayo yatahudumiwa kikamilifu na maeneo yote ya wazi kwenye mashamba hayo yatapandwa. Uvunaji utafuata utaratibu wa kuwauzia magogo wale tu ambao wana Viwanda vya Misitu. Ili kudhibiti wizi, viwanda vyote vinavyohamishika vitaondolewa katika maeneo ya Hifadhi ya Misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua umuhimu wa nishati ya mkaa katika matumizi ya nyumbani na haijakataza biashara ya mkaa. Kinachosisitizwa katika biashara hii ni wahusika wafuate sheria na kanuni zilizowekwa na serikali. Aidha, Mwongozo wa Uvunaji Endelevu wa Biashara ya Mazao ya Misitu lazima ufuatwe. Kwa kuwa 80% ya miti yote inayokatwa sasa hukatwa kutengeneza mkaa, na kwa kuwa katika kila kilo 100 zinazokatwa kutengeneza mkaa ni kilo 20 tu za mkaa hupatikana; Wizara yangu:

(i) Itakamilisha mpango wa kuboresha utengenezaji mkaa;

(ii)Itahamasisha wananchi hasa wa mijini kutumia mkaa mbadala (*briquttes*) unaotengezwa na uchafu wa organic katika miji; na

(iii)Itakamilisha mpango wa kila Jiji, Manispaa na Miji kuwa na mashamba yake ya miti ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ulinzi wa Rasilimali. Ili kudhibiti uvunaji na biashara haramu ya mazao ya misitu, mwaka 2007/2008, vikosi zaidi vya Doria vitaanzishwa katika Kanda ya Ziwa (Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara), Kanda ya Kati (Dodoma, Manyara na Singida) na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya na Iringa). Vikosi hivi vitahusisha askari Polisi, *TRA* na *Anti Poaching Unit*. Wizara itawaondoa wavamizi ndani ya Misitu ya Hifadhi katika Mikoa 10 na itapima upya mipaka ya misitu yenye kilomita 1,602 na kusafisha na kuimarisha barabara za moto zenye urefu wa kilomita 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Carbon Sequestration* (Kunyonya hewa ya *Carbon).*Nchi yetu ina misitu mingi, yenye uwezo wa kunyonya hewa ya *Carbon dioxide* kwa matumizi yake na kutoa *Oxygen* tunayohitaji kwa maisha yetu. Kwa kuwa, kiasi hiki cha kuondoa hewa chafu na kuchangia hewa safi kwa sasa kinalipiwa chini ya Itifaki ya Kyoto, Wizara imeunda Kamati ya Wataalamu waliobobea katika taaluma za Misitu, Ikolojia, Wanyamapori, Maeneo chepe chepe, Sayansi ya Udongo, Sheria na Mazingira ambayo itaandaa mapendekezo ya namna ambavyo Tanzania inaweza kulipwa chini ya mpango huu. Matarajio yetu ni kuwa mradi huu utakamilika katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendelezaji Utalii Ikolojia. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara itasimamia Upimaji wa Misitu ya Hifadhi yenye ukubwa wa hekta 134,511 ya *West Kilombero Scarp* iliyopo Wilayani Kilolo na Misitu ya Matundu, Nanganje, Lyondo na Iwonde iliyopo Wilayani Kilombero ili misitu hiyo iweze kupandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Kilombero *(Kilombero Nature Reserve)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikishaji Jamii na Elimu kwa Umma. Katika kuendeleza elimu ya Misitu na Ufugaji Nyuki kwa jamii, vipindi 74 vya Redio na Televisheni vinavyohusu Maliasili na Misitu ni Uhai vitarushwa hewani. Vile vile,

nakala 5,000 za vipeperushi, Jarida la Misitu ni Uhai nakala 12,000; mabango 30,000 na vitabu 3,000 vya Ufugaji wa Nyuki wasiouma vitachapishwa na kusambazwa. Uhamishaji kuhusu upandaji miti, kuthibiti moto, matumizi ya majiko sanifu, kilimo mseto, ufugaji nyuki na uhifadhi wa vyanzo vya maji pia utafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti wa Misitu. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 ujenzi wa Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu, utaanza katika kiwanja cha Kingolwira mjini Morogoro. Aidha, taasisi itafanya utafiti juu ya hifadhi ya vyanzo vya maji hasa katika Milima ya Tao la Mashariki. Mawasiliano yanafanywa kati ya *TAFORI* na Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Kilimo Mseto *(World Agroforestry Centre)* ili kushirikiana katika utafiti huu. Kazi hii itaanza kwa kuchunguza miti inavyotumia maji hasa mikaratusi na mianzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utafiti wa matumizi endelevu ya mazao ya misitu yaliyo na yasiyo timbao ili kukuza uchumi wa jamii na kupunguza umasikini utafanyika. Aidha, taasisi itaanzisha matanuru darasa ya kuchoma mkaa katika maeneo machache ili kutoa elimu ya uchomaji mkaa unaozingatia hifadhi ya mazingira. Kazi hii itachangia utekelezaji wa maagizo ya Wizara juu ya njia bora za kuchoma mkaa.

Aidha, utambuzi wa miti inayostawi katika maeneo mbalimbali kijiografia hapa nchini utafanyika ili kuwezesha wananchi kupanda aina za miti sahihi katika maeneo sahihi kwa matumizi ya aina mbalimbali. Vilevile, Taasisi itaanza kuzalisha vyahuso (*clones*) vya mikaratusi inayokua haraka katika kitalu cha bioteknolojia kinachojengwa huko Kwamarukanga Korogwe.Aidha, Taasisi itaimarisha Utumishi na Miundombinu ili kuendeleza utafiti misitu utakaochangia katika hifadhi na matumizi endelevu ya misitu nchini. Jarida la *TAFORI* litachapishwa mara mbili kwa mwaka na kusambazwa kwa wadau kama sehemu ya elimu ya misitu kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafunzo ngazi ya Astashahada na Stashahada Katika mwaka wa 2007/2008 Chuo cha Misitu cha Olmotonyi na kile cha Viwanda vya Misitu cha Moshi vinategemea kudahili jumla ya wanafunzi 186. Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 69 watasomea Astashahada ya Misitu na Ufugaji Nyuki, 84 Stashahada ya Misitu na Ufugaji Nyuki na 33 Astashahada ya Viwanda vya Misitu. Hata hivyo idadi hiyo ya wanafunzi ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji ya Taaluma hizo katika soko la ajira kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uhifadhi na Usimamizi wa Misitu Tanzania (*TFCMP*). Madhumuni ya mradi huo ni kuboresha huduma za Misitu, kuhusisha jamii katika usimamizi shirikishi wa Misitu; kuboresha ukusanyaji wa maduhuli ya misitu na nyuki kwa kuongeza vituo 10 vya ukaguzi. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Mradi utakamilisha jengo la Misitu Makao Makuu; na kuwezesha Wilaya 25 katika utekelezaji wa Mpango Shirikishi wa Misitu kupitia Mradi wa *TASAF II.* Aidha, boti mbili (2) za doria zitanunuliwa ili kukabiliana na usafirishaji wa magogo kupitia bandari bubu. Vilevile, Mradi utafanya tathimini ya Misitu ya Asili na ya kupandwa kitaifa na

kutayarisha mkakati wa matumizi endelevu ya nishati ya miti kwa kupanda miti na kutumia kiendelevu rasilimali za miti, nishati mbadala, majiko sanifu na *Briquettes*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ufugaji wa Nyuki. Kwa kutambua umuhimu wa ufugaji nyuki katika kuchangia juhudi za kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa Tanzania, Wizara itaanza mchakato wa kufufua sekta ndogo ya ufugaji nyuki.Hatua ya kwanza ya kufufua sekta hii itakuwa kuanzisha upya Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora. Kiasi cha Shilingi milioni 400 zimetengwa katika bajeti hii kwa ajili ya kukarabati majengo ya Chuo ili yaweze kurejea katika hadhi yake na kuweza kupokea wanafunzi katika mwaka 2008/2009. Aidha, katika kipindi cha matayarisho Mitaala ya mafunzo ya Astashada na Stashahada ya nyuki itaanza pamoja na kuboresha Chuo ili kiwe Kitovu cha Ufanisi (*Centre of Excellence).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuna aina kuu mbili za nyuki ambao ndiyo wanaotupatia mazao ya asali, nta, gundi ya nyuki, chavua, maziwa ya nyuki, majana na sumu ya nyuki. Aina hizo ni Nyuki wanaouma *(Apis Melliffera)* na nyuki wasiouma *(Trigoma na Melliponula).*

Inakadiriwa kuwa uzalishaji wa mazao ya nyuki nchini Tanzania unaweza kufikia takriban tani 138,000 za asali na tani 9,200 za nta kwa mwaka zenye thamani ya Shilingi 147 bilioni. Hivi sasa wastani wa tani 4,860 za asali na tani 360 za nta huzalishwa kwa mwaka. Hii ni sawa na asilimia 4 ya uwezo uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ili kuhakikisha kuwa nchi inafaidika na rasilimali hii muhimu itaanza kutekeleza mpango wa kufufua ufugaji nyuki katika wilaya 30, kwa mwaka 2007/2008. Wilaya hizo ni:- Kahama, Mpanda, Sikonge, Urambo, Uyui, Chunya, Manyoni, Bukombe, Nachingwea, Kilindi, Ulanga, Mpwapwa, Namtumbo, Geita, Kondoa, Simanjiro, Same, Kilombero, Bagamoyo, Njombe, Kongwa, Tunduru, Mtwara, Hanang, Monduli, Longido, Kwimba, Iramba, Mwanga na Masasi. Utekelezaji wa mpango huo kabambe utawawezesha wakulima kuzalisha Asali na Nta kibiashara na kuimarisha Taasisi zinazotoa huduma katika ufugaji nyuki. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 mradi huu utaenezwa nchi nzima ili kuongeza mapato ya wananchi.

Lengo ni kuwawezesha wananchi 200,000 wajiajiri kupitia mpango huu na kulipatia Taifa zaidi ya Shilingi 80 bilioni kwa mwaka ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuboresha sekta hii ya nyuki, Wizara inatarajia kusambaza teknolojia sahihi ya ufugaji nyuki, kuongeza idadi ya wafugaji na wafanyabiashara wa mazao ya nyuki na kuwatafutia wafugaji masoko. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara itaandaa maonyesho ya Asali na Nta katika mwaka 2007/2008 ili kuwakutanisha wafugaji na wanunuzi wakubwa wa Asali na Nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utalii; Kutangaza Utalii. Tanzania ni nchi iliyojijengea mazingira mazuri sana ya utalii. Chini ya sera madhubuti ya Chama cha Mapinduzi; Tanzania imejenga nchi ya Amani na Mshikamano unaopigiwa mfano

duniani kote. Aidha, Tanzania imejenga Demokrasia nzuri na ya kuigwa, ni nchi ya watu walio na utamaduni uliosheheni ubora wa kila aina na ukarimu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi huu wa amani, mshikamano, Demokrasia na watu wakarimu unaviuza vivutio vyetu vya pekee vya Mlima Kilimanjaro, Serengeti, Ngorongoro, Selous, Ruaha, Katavi, Mahale, Gombe na vinginenvyo. Aidha Tanzania ina visiwa vilivyo na sifa za pekee vya Zanzibar; na fukwe za bahari zenye mchanga mzuri na maji maangavu. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, tutavitangaza vivutio hivi kupitia kwenye magazeti makubwa na majarida ya safari ya nchi za Marekani, Uingereza, Italia, Ujerumani, India, China, Korea, Japani na Urusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuanzia mwezi Agosti mwaka huu tutaanza kuitangaza Tanzania na vivutio vyake katika Televisheni ya *CNN* kupitia *CNN* America; *CNN Headline News*, kupitia tovuti ya *CNN Travel* na katika viwanja vya ndege 54 vya kimataifa vya Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa kuitangaza Tanzania kupitia *Televesion* ya *Africa Channel* ya California na kupitia kipindi cha *Africa Channel* kinachorushwa na *Sky News* ya Uingereza unatayarishwa. Mategemeo yetu ni kuwa mkataba huu utakamilika na matangazo haya kuanza kurushwa mwezi Oktoba 2007. Vile vile, Wizara inazungumza na *Television* za *BBC World*, *Euronews* na *Aljazeera* ili kuongeza matangazo ya utalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watalii wengi wanakuja nchini kwetu kwa kushawishiwa na wakala wa usafiri *(Travel Agents).* Hivyo, ni muhimu wakala hao wakaijua Tanzania vizuri.Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008. Wizara yangu inaandaa mafunzo kupitia kwenye mtandao kwa ajili ya mawakala wa utalii wa Marekani na Canada. Mafunzo haya yanaandaliwa na Jarida kubwa la Safari la Marekani la *Travel Agent* na washirika wetu katika kuitangaza Tanzania nchini Marekani wa *Bradford Group wa New York.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika juhudi zetu za kuitangaza Tanzania na vivutio vyetu; kwa pekee nimshukuru na kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi kubwa anayoifanya katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwezi Agosti mwaka huu, Mheshimiwa Rais atakuwa Mtoa Mada Maalum (*Keynote Speaker)* katika Tamasha la watengenezaji wa Filamu linaloitwa *WildTalk Africa* mjini Durban, Afrika Kusini. Tamasha hilo litatangazwa moja kwa moja (*Live*) na *Televisheni* ya *CNN*, *BBC* na *Super Sports* na kuangaliwa na watazamaji zaidi ya 100 milioni. Aidha, mwezi Oktoba 2007, Rais amealikwa kuwa Mgeni Rasmi katika mkutano wa pili wa Wakuu wa nchi wa kutangaza Utalii Duniani huko Beijing China (*2nd World Tourism Marketing Summit). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mkutano wa China, Mheshimiwa Rais atatangazwa Rasmi kuwa Mwenyekiti wa Dunia wa Mkutano wa Dunia wa Wakuu wa nchi wa kutangaza utalii. Wakati wa hafla hiyo Mheshimiwa Rais atapokea rasmi ombi

la Chuo Kikuu cha Biashara cha Dunia *(World Trade University)* la kujenga Chuo Kikuu cha Dunia cha Utalii hapa Tanzania (*World Tourism University)* kwa niaba ya Bara la Afrika .(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uko usemi wa Kiswahili unaosema kuwa: Kuona ni Kuamini. Ili mawakala wa usafiri wengi waijue Tanzania, watu na vivutio vyake, Serikali imeandaa kuwa mwenyeji wa mikutano mikubwa ya *(i) Africa Travel Association, Annual Congress* mwezi Mei, 2008 *(ii) The Leon Sullivan Summit, June 2008* na *(iii) Africa Diaspora Trail Conference* mwezi *April 2009.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka huu wa fedha, Wizara itaweka mazingira mazuri ili sekta binafsi ishiriki kwa nguvu zaidi katika masoko Makuu ya utalii ya London, Berlin, Milan, Moscow, Madrid, New York Times, Beijing, Dubai, Korea na kwingineko. Aidha, Serikali imeandaa *Road Show* katika miji ya Frankfruit, Stutgart, Berlin, Vienna, Zurich na Geneva mapema mwezi Septemba mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa utangazaji wa utalii una gharama kubwa, Serikali imeyaomba mashirika yanayofaidika na biashara hii kuchangia katika kazi hii. Hivyo, ninayo furaha kulieleza Bunge lako tukufu kuwa katika mwaka huu wa fedha, mashirika ya *Singita Lodge* wanaomiliki *Grumeti Reserves* na *Sasakwa Lodge* wamekubali kuchangia *USD 3* Milioni; *TANAPA* Shs.1.5 bilioni, Ngorongoro Shs.500 milioni na *TWPF* watachangia Shs.500 milioni.Aidha Serikali imetenga Shs.3.2 bilioni kupitia *TTB* katika mwaka huu wa fedha ukilinganisha na Shs.1.5 bilioni katika mwaka wa fedha wa 2006/2007. Ili kufikia walengwa katika masoko makuu na mapya, Wizara itashirikiana kwa karibu na Balozi zetu nje ya nchi na kuteua wawakilishi wa utalii kwenye nchi za China, Ujerumani, Scandinavia na Mashariki ya Mbali. Vilevile, tovuti ya Bodi ya Utalii *(www.tanzaniatouristboard.com)* itatafsiriwa katika lugha nne za kimataifa ambazo ni Kiswahili, Kifaransa, Kijerumani na Kichina (Mandarin). Wizara pia itashirikiana na Balozi zetu za nje ya nchi ili kutekeleza Sera ya Diplomasia ya Uchumi *(Economic Diplomacy)* katika eneo la kutangaza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UN-WTO* na Utalii wa Tanzania. Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii Duniani *(United Nations World Travel Organisation (UN - WTO)* limeunda Kamati ya pamoja na *FIFA World Cup* 2010. Kamati hiyo, imemchagua Waziri wa Michezo wa Afrika Kusini kuwa Mwenyekiti na Waziri wa Maliasili na Utalii wa Tanzania kuwa Makamu Mwenyekiti. Jukumu la Kamati hiyo ni kuutangaza utalii wa nchi za *SADC* na Afrika kwa ujumla pamoja na matangazo ya *FIFA World Cup* 2010.

Aidha, kamati hiyo itaweka mkakati wa kuwaonyesha vivutio vyetu vya utalii washiriki wa fainali za *World Cup 2010* kabla ya michuano kuanza, wakati wa michuano na baada ya fainali hizo. Tanzania inajiandaa kikamilifu kufaidika na matangazo hayo.

Meshimiwa Mwenyekiti, Changamoto zinazotukabili katika Sekta ya Utalii. ia ya nchi yetu ni kuongeza idadi ya watalii wanaoitembelea nchi yetu kutoka 640,000 mwaka 2006 na kufikia watalii milioni 1.2 ifikapo mwaka 2012 na kuongeza mapato ya jumla ya *USD 850* milioni mwaka 2006 na kufikia lengo hili ni muhimu sana tuboreshe huduma za utalii. Moja ya changamoto kubwa sana za kukabiliana nazo ni kuongeza idadi ya Hoteli za nyota tano na kupandisha madaraja ya Hoteli tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuwakaribisha wawekezaji wenye uwezo wa kujenga hoteli za nyota tano katika Mbuga zetu, katika maeneo yanayozunguka mbuga zetu na katika miji yetu mikuu. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Edward Lowassa Waziri Mkuu kwa kulielezea suaala hili kwa ufasaha mkubwa wakati wa majumuisho ya hotuba yake ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuboresha huduma zitolewazo kwa watalii, Wizara itapanga hoteli katika madaraja katika Mikoa ya Mwanza, Mara, Kilimanjaro, Pwani, Dar es Salaam, Tanga na Dodoma. Aidha, Wizara itahakiki hoteli kwa ajili ya kuziweka katika madaraja kwenye Mikoa ya Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Lindi, Mtwara, Kigoma, Kagera na Shinyanga. Ni nia ya Wizara ni kufanya zoezi hili kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuhakikisha kuwa watanzania wenye Hoteli ndogo wanafaidika na ongezeko la watalii, Serikali imekubaliana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*) kuanzisha mkopo maalumu wa muda mrefu utakaowawezesha wenye hoteli ndogo na zenye kiwango cha chini ili wakarabati hoteli zao kufikia kiwango cha nyota 2 mpaka 3. Chini ya utaratibu huo utakaoendeshwa kati ya *AFD* na Benki ya *CRDB*:-

(i) Shirika la *AFD* litaweka dhamana katika Benki ya *CRDB* ambayo itatoa dhamana ya 40% ya mikopo yote.

(ii) Mkopaji naye atatoa dhamana ya 60% ya mkopo anaochukua.(iii)Mkopo utakuwa wa muda mrefu, miaka mitano mpaka kumi.

(iv)Riba itakuwa sehemu ya majadiliano ili wakopaji waweze kulipa mkopo na kufaidika na ongezeko la watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto nyingine kubwa ni kuongeza idadi ya ndege zinazotua Dar es Salaam na Kilimanjaro moja kwa moja kutokea Ulaya, Marekani, Mashariki ya Mbali na Mashariki ya Kati. Aidha, ni muhimu sana kwa Shirika la Ndege la Tanzania *(Air Tanzania Ltd.)* liwe na nguvu na kushiriki kikamilifu katika kazi hii kubwa ya kuleta watalii Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sambamba na kazi hii, ni muhimu sana tuvishughulikie na kuvitangaza viwanja vya ndege vya Sumbawanga, Mafia, Mbeya, Kigoma na Arusha. Vilevile, ni muhimu sana tujenge uwanja wa ndege wa Mugumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Taifa cha Utalii. Katika zoezi la kuboresha huduma zinazotolewa kwenye Sekta ya Utalii, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa itaanza rasmi ujenzi wa Chuo kipya cha Utalii mwezi Agosti 2007 ambao utachukua mwaka mmoja kukamilika. Chuo hicho kitakuwa na uwezo wa kudahili

wanachuo 500 kwa mwaka mmoja na kutoa mafunzo ya hoteli na utalii katika ngazi ya Astashahada na Stashahada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sambamba na ujenzi wa Chuo, Wizara yangu itatekeleza Mradi wa Mafunzo unaogharamiwa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU)*. Katika mwaka 2007/2008 yafuatayo yatatekelezwa chini ya mradi huo:-

(i) Kuinua viwango vya ufundishaji katika fani ya hoteli na utalii kwa kutoa mafunzo kwa wakufunzi.

(ii) Kuandaa mitaala ya kitaifa ya mafunzo ya hoteli na utalii itakayotumiwa na vyuo vyote nchini Tanzania. Kazi hii itafanywa kwa ushirikiano na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE),* Mamlaka ya Elimu ya Ufundi *(VETA)* na Chuo cha Taifa cha Utalii *(NCT)*.

(iii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa sekta katika sehemu zao za kazi *(Mobile Training)* ili watumishi wengi waweze kufaidika na mafunzo hayo na kuongeza ufanisi kazini.

(iv) Mradi huo pia umelenga kutoa vifaa vya kisasa vya kufundishia kwenye Chuo cha Hoteli Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi. Ili kuboresha maisha ya Watanzania kupitia Sekta ya Uvuvi, Wizara itakamilisha kazi zilizoanza katika mwaka wa fedha 2006/2007 na kuanza kutekeleza kazi mpya. Katika mwaka 2007/2008, Wizara itakamilisha ununuzi wa vifaa vya maabara katika sehemu ya Kemikali katika maabara ya Taifa ya Uvuvi, Mwanza. Lengo ni kuiwezesha Maabara hiyo kufanya kazi kikamilifu na kulipunguzia taifa matumizi ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuchunguza sampuli kama ilivyo sasa. Aidha, maabara itakuwa na uwezo wa kuzisaidia nchi za jirani kupima sampuli zao na hivyo kuliletea Taifa fedha za kigeni. Pia, Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani kitakarabatiwa kwa gharama ya dola za kimarekani 400,000 kupitia msaada wa Shirika la Uvuvi la Japan *(Overseas Fisheries Cooperation of Japan).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itashirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na wadau wengine kuandaa kanuni za kusimamia Uvuvi kwenye Bahari Kuu na kuharakisha uanzishaji wa Mamlaka ya Uvuvi katika Bahari Kuu.

Katika mwaka 2007/2008, Wizara inategemea kufanya Sensa ya Uvuvi katika Bahari ya ndani na Ukanda wa Uchumi wa Bahari chini ya miradi ya *Marine and Coastal Environmental Management Project (MACEMP), Western Indian Ocean Tuna Tagging Project (WIOTTP) na South West Indian Ocean Fisheries Project (SWIOFP).* Aidha, sensa hii itafanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ya Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 ufugaji wa samaki utaanzishwa chini ya *MACEMP* baada ya kukamilisha mradi wa ufugaji viumbe hai na kuanza utekelezaji

wake. Aidha, mafunzo ya kuongeza thamani ya mwani yataendeshwa ndani na nje ya nchi. Wizara itaendesha mafunzo ya ufugaji samaki aina ya Mwatiko katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga pamoja na kuandaa vipeperushi vya ufugaji huo. Aidha, mradi huu utaanza kutekelezwa kwenye wilaya 11 za pwani ambako ulikuwa bado kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majaribio ya Ufugaji na Unenepeshaji wa Kaa yataanzishwa katika Chuo cha Mbegani na kusambazwa katika Wilaya za Pwani. Lengo ni kuweza kushawishi wajasiriamali wengi kuingia katika shughuli hii. Aidha, mchakato wa kuandaa programu itakayosaidia kuinua kiwango cha ufugaji samaki nchini unaohisaniwa na *FAO* utakamilika katika mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Wizara itaimarisha ulinzi wa rasilimali ya uvuvi kwa kushirikisha jamii, vyombo vya Dola na wadau wengine. Kupitia mradi wa *MACEMP*, vituo vya doria vitaanzishwa katika wilaya za Kilwa, Lindi na Mtwara kwa kuvipatia vitendea kazi ili kutekeleza majukumu ya doria kwa ufanisi. Aidha, usimamizi wa rasilimali ya uvuvi katika Wilaya zote za ukanda wa pwani utaimarishwa kwa kuanzisha *Beach Management Units (BMUs )* na kupewa vifaa vya doria. Lengo ni kupambana na uvuvi haramu hasa ule wa kutumia mabomu, na kuthibiti uvuvi haramu na biashara ya magendo mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Mradi wa *MACEMP* utatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuwezesha uanzishwaji wa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, ikiwa ni pamoja na kujenga Makao Makuu ya Mamlaka.

(ii) Kuwezesha kufanyika kwa majadiliano na kufikia muafaka wa mpaka wa Bahari Kuu kati yetu na Visiwa vya Ngazija *(The Comoros)*.

(iii) Kuwezesha kufanyika kwa majadiliano na kufikia muafaka juu ya kuanzisha hifadhi ya bahari ya pamoja kati ya Tanzania na Msumbiji katika eneo la maingilio ya Mto Ruvuma.

(iv) Kuwezesha ushiriki wa Tanzania katika kutekeleza majukumu ya mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa.

(v) Kuwawezesha wanavijiji wa pwani kujenga uwezo wa kuibua miradi ya kuwaongezea kipato, na kuhifadhi miradi mingine ya wananchi itakayoibuliwa kuendeleza ufugaji wa mwatiko na kunenepesha Kaa.

(vi) Kuwezesha uhamasishaji wa jamii za pwani juu ya kuanzisha na kuendesha vikundi vya ulinzi vya rasilimali *(Beach Management Units)*, utaratibu ambao umeonyesha mafanikio katika Kanda ya Ziwa Victoria.

(vii) Kuwezesha kuanzishwa kwa mtandao wa maeneo ya hifadhi katika bahari ya ndani na ya kitaifa, kwa kuzingatia kwamba maeneo ya hifadhi yana nafasi kubwa ya kuleta matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

(viii) Kusimamia mchakato wa kuanzisha mfuko wa kuendeleza usimamizi wa rasilimali za bahari baada ya mradi wa *MACEMP* kumalizika.

(ix) Kupanua wigo wa utekelezaji wa miradi, ili kuhusisha wilaya zote 14 za pwani.

(x) Kununua vyombo vya doria kwa ajili ya kudhibiti uvuvi kwenye Bahari. Katika mwaka huu Boti 12 zitanunuliwa kwa hatua za mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchakato wa kuanzisha eneo la usimamizi wa pamoja wa hifadhi ya Bahari (*Trans Frontier Conservation Area)* mpakani na Msumbiji umeanzishwa kwa kufanya tathmini ya eneo husika. Mchakato huo utakamilishwa 2007/2008.

Kwenye kanda ya Ziwa Victoria, kazi kubwa itakuwa kuwezesha ujenzi wa mialo 13 ya kisasa yenye thamani ya shilingi Bilioni tatu zitakazotoka mradi wa *EU* wa *Implementation of Fisheries Management Plan* (*IFMP*). Aidha, Mradi utasaidia katika utekelezaji wa mpango wa kuimarisha uvuvi endelevu na kupunguza kasi ya Uvuvi katika Ziwa Victoria. Mradi pia, utajenga uwezo wa jamii wa kushiriki katika ulinzi wa rasilimali kwa kuwezesha *BMUs*, na kuboresha huduma za jamii hususan ujenzi wa Zahanati mbili na kuchangia ujenzi wa vyumba sita vya madarasa ya shule za msingi.Wizara kwa kushirikiana na asasi zingine za Serikali itajikita katika kupambana na biashara ya magendo ya samaki mpakani katika Ziwa Victoria, Tanganyika, Rukwa na Baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2007/2008 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (*TAFIRI*) itafanya utafiti wa silikanti ambao utalenga kubaini makazi ambayo samaki huyo anaishi na kwa nini wameibuka kwa kasi kubwa tangu 2003. Utafiti wa samaki huyo utafanyika mwezi Septemba na Oktoba,2007 katika maji ya kina kirefu eneo la Kigombe Tanga kwa kutumia meli na vifaa maalum. Shirika la Umoja wa Mataifa *UNESCO* na Serikali ya Japan zitagharamia utafiti huo.

Aidha, Taasisi itaendesha utafiti wa ufugaji wa samaki aina ya mwatiko katika wilaya zote 14 za pwani ya bahari ya Hindi na pia itaratibu sensa ya Uvuvi katika Ziwa Victoria, chini ya mradi wa *Implementation of Fisheries Management Plan for Lake Victoria (IFMP).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuendelea kuboresha uhifadhi wa raslimali za Uvuvi yafuatayo yatatekelezwa katika kipindi cha mwaka 2007/2008.

(i) Mipango ya Jumla ya Usimamizi *(General Management Plans)* ya Maeneo Tengefu mapya itaandaliwa ili kuweka kanda za matumizi kwa lengo la kuboresha uhifadhi wa bioanuai na kukuza utalii.

(ii) Kwa kushirikiana na wananchi ndani ya Hifadhi za Bahari za Mafia na Mnazi Bay zana haribifu zitaondolewa kwa kubadilishana na zana bora za uvuvi na Miradi mbadala itaibuliwa ili kupunguza kasi ya uvuvi haramu.

(iii) Mpango kabambe wa mtandao wa maeneo ya hifadhi za Bahari utaandaliwa. Maeneo anamokutwa Silikanti yatatambuliwa na kuhifadhiwa kisheria. Aidha maeneo ya hifadhi pamoja yatatambuliwa na mpango wa kuyahifadhi kwa ushirikiano na nchi jirani utatekelezwa kwa kuanzia nchi ya Msumbiji.

(iv) Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ya 1994 itafanyiwa marekebisho ili kuimarisha uhifadhi shirikishi jamii na utendaji wa Taasisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale. Sera na Sheria. Ili kukabiliana na changamoto mbalimbali katika kuhifadhi na kuendeleza malikale, Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2007/2008, inatarajia kukamilisha Sera ya Malikale. Vilevile, itafanya marekebisho ya Sheria za Mambo ya Kale ili ziendane na Sera. Aidha, Miongozo ya Uhifadhi wa Urithi wa Utamaduni itachapishwa na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Mambo ya Kale. Katika mwaka 2007/2008, Wizara itawasilisha *UNESCO* kabrasha la Njia Kuu ya Kati ya Biashara ya Utumwa na Vipusa ili kuiweka njia hiyo katika orodha ya urithi wa dunia na kukamilisha ukarabati wa jengo la kihistoria la *Tea House* ambalo liko Bagamoyo. Pia, itaendelea kukarabati na kuimarisha magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara kwa lengo la kuendeleza jitihada za kulinusuru eneo kutoka katika orodha ya urithi ulio hatarini. Aidha, Tanzania itakuwa nchi ya kwanza Afrika kuwa mwenyeji wa Mkutano wa *Africa Diaspora Trail Conference* ambao utatumia njia kuu ya kati ya Biashara ya utumwa na vipusa kama urithi wa waafrika wote Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kutopoteza kumbukumbu ya mchango wa nchi yetu katika historia ya ukombozi wa Bara la Afrika, Wizara itayatambua makambi, makaburi, majengo, maeneo mbalimbali yaliyotumiwa na wapigania uhuru kwa kuyawekea kumbukumbu na kuyalinda kisheria. Maeneo hayo yatawekewa mabango yatakayokuwa na nembo ya urithi wa ukombozi wa bara la Afrika na kuwekwa kwenye ramani ili yajulikane. Tathmini ya Rasilimali za Mambo ya Kale. Katika kuhifadhi na kuweka kumbukumbu za malikale, Wizara itatumia mfumo uliondaliwa wa kukusanya taarifa mbalimbali za maeneo yenye urithi wa utamaduni nchini kwa lengo kuanzisha kanzidata ya urithi wa utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendelezaji na Utangazaji Utalii katika maeneo ya Kale. Katika kutekeleza jukumu la kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya Mambo ya Kale kiutalii mwaka 2007/2008, Wizara itaweka vioneshwa katika Vituo vya Caravan Serai

(Bagamoyo), Isimila (Iringa) na Kolo (Kondoa). Aidha, umeme na maji katika kituo cha Amboni na Olduvai vitawekwa kwa lengo la kuviboresha zaidi. Pia, Wizara itakamilisha ujenzi wa kituo cha taarifa na kumbukumbu cha Dr. Livingstone kilichopo Ujiji-Kigoma. Wizara itaendelea na ujenzi wa Kituo cha Taarifa na Kumbukumbu cha Dr. Livingstone kilichopo Ujiji-Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikishaji Jamii na Elimu kwa Umma. Ili kuhakikisha jamii inapata elimu stahili juu ya historia na urithi wa utamaduni, Wizara imekamilisha Mpango wa Uhamasishaji Jamii. Mpango huo ambao utaanza kutekelezwa mwaka 2007/2008, utatoa fursa kwa jamii kuifahamu historia ya nchi yetu na urithi wa utamaduni, kukuza utalii na kuhamasisha jamii kuendelea kutunza urithi wetu kwa faida ya vizazi vijavyo. Aidha, Wizara itandaa vipeperushi 600 kuhusiana na vituo vya Malikale. Pia, itaendelea kurusha kipindi cha ZAMADAMU kuelimisha jamii kuhusu vivutio vya malikale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utafiti wa Mambo ya Kale. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara itaendelea na uchimbuzi wa akiolojia katika ‘Mreshe’ wa Chuo cha Mweka kwa lengo la kuwezesha mreshe huo kutumiwa na watalii wa ndani na nje na kujifunza utamaduni ambao ulikuwa ni sehemu muhimu sana katika historia ya Wachagga. Aidha, wizara itaendelea kuratibu na kusimamia tafiti za akiolojia zitakazofanywa na watafiti mbalimbali wa ndani na nje nchi. Mwaka 2006/2007, Wizara kupitia Idara ya Mambo ya Kale iliweka lengo la kukusanya shilingi 205,501,000.00. Hadi Mei 2007, Idara ilikusanya Shilingi milioni 214,479,385.89 sawa na asilimia 104.5. Katika mwaka 2007/2008, Idara ya Mambo ya Kale inatarajia kukusanya shilingi 229,201,000.00. Matarajio hayo yanaonyesha ongezeko kubwa kutokana na mapendekezo ya kuongezeka viwango vya ada zinazotokana na viingilio kwenye vituo vya Mambo ya Kale na tafiti mbalimbali za Mambo ya Kale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Makumbusho ya Taifa. Katika mwaka 2007/2008, Shirika la Makumbusho ya Taifa litatekeleza majukumu yake ya kuhifadhi, kutafiti na kuhamasisha jamii katika uhifadhi wa raslimali za utamaduni. Shirika litaanza ujenzi wa jengo la Nyumba ya Utamaduni. Aidha, Wizara itaendelea na juhudi za kutafuta wafadhili kwa ajili ya matengenezo ya *Rolls-Royce*. Vilevile, Shirika litatekeleza jukumu la kuhamasisha na kushirikisha jamii katika uhifadhi wa rasilimali za utamaduni kwa kuzishirikisha jamii za Mikoa ya Morogoro na Tabora. Aidha, nyumba za jadi za jamii ya Wamasai, Wahaya, Wasambaa, Wazaramo na Wamakua zitafanyiwa ukarabati katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utafiti na ukusanyaji vifaa vya urithi wa utamaduni utafanyika katika fani ya mila na Elimu ya Viumbe. Katika kujenga uwezo wa wilaya wa kuhifadhi urithi wa utamaduni hususan uanzishaji na uendelezaji wa makumbusho, ushauri utatolewa kwa Wilaya za Maswa, Njombe na Masasi ambazo ziko katika mchakato wa kuanzisha na kuboresha makumbusho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ajira na Kupandisha Watumishi Vyeo. Mwaka 2007/08, Wizara itaendeleza jitihada za kuboresha rasilimali watu, kwa kuajiri watumishi

wapya 415 na watumishi 40 watakaojaza nafasi zilizoachwa wazi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za ajira inatarajia kupandisha vyeo watumishi 1,214. Katika juhudi za kuimarisha utawala bora, mwaka 2007/08, Wizara itaendelea kuboresha utendaji kazi unaozingatia sheria na taratibu zilizowekwa. Semina kuhusu misingi ya utawala bora zitatolewa kwa watumishi wa Makao Makuu na Vituoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo na Ustawi wa Watumishi. Mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea kupambana na janga la ukimwi kwa kuhamasisha watumishi kupima ili kujua hali zao na hivyo kupunguza maambukizi mapya. Vilevile, watumishi wataendelea kushiriki michezo na kushauriwa kuunda vyama vya kuweka na kukopa kwa lengo la kuboresha afya zao na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukusanyaji Maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara ilitarajia kukusanya shilingi 37,017,336,000. Hadi kufikia mwezi Mei 2007, Shilingi 40,445,190,637.45 zilikuwa zimekusanywa. Ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.26. Matarajio ya Wizara katika mwaka wa fedha 2007/2008 ni kukusanya Shilingi 74,757,324,000. Matarajio hayo yanaonyesha ongezeko kubwa kutokana na mapendekezo ya kuongezeka viwango vya mrahaba, ada na ushuru wa mazao mbalimbali ya maliasili.

Licha ya matarajio hayo kutakuwa na upungufu wa makusanyo ya maduhuli kwa upande wa uvuvi kutokana na kupungua kwa rasilimali ya kamba na kuondolewa leseni za uvuvi katika Bahari Kuu ambazo zitakusanywa na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu.

Hitimisho. Nachukua nafasi hii kuwashukuru wadau wa Sekta ya Maliasili kwa kushiriki kwao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu kwa njia moja au nyingine. Aidha, natoa shukrani kwa washirika wetu wa maendeleo ambao ni Serikali za Ufaransa, Ujerumani, Norway, Denmark, Japan, Sweden, Finland, Ubelgiji, Marekani, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, *AWF*, *FAO*, *FZS*, *GTZ*, *IUCN*, *KfW*, *Trade Aid*, *AFRICARE*, *UNESCO*, *UNDP*, *GEF*, *UNWTO*, *World Bank*, *WWF*, *ICCROM* na wengineo kwa mchango wao mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara yanatokana na kazi nzuri na ushirikiano wa Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Zabein M. Mhita, (Mb) Jimbo la Kondoa Kaskazini na Katibu Mkuu Bibi. Blandina Nyoni na Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara pamoja na Asasi zake. Aidha, napenda niwashukuru waliokuwa Mawaziri wa Maliasili na Utalii kabla yangu Mheshimiwa Zakia Meghji na Mheshimiwa Anthony Mwandu Dialo kwa kuweka msingi mzuri wa maendeleo ya wizara ya Maliasili na Utalii. Napenda pia niwashukuru Ndugu Philemon Luhanjo, Ndugu Solomon Odunga na Ndugu Saleh Pamba waliokuwa Makatibu Wakuu wa Wizara yangu kwa kazi nzuri sana waliofanya katika kipindi cha miaka 11 iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mwaka 2007/08, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Asasi zake inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 55,493,625,000 kwa ajili ya Matumizi yake. Kati ya fedha hizo Shilingi 30,817,624,000

ni kwa ajili ya Matumizi ya Mishahara na Matumizi Mengineyo na Shilingi 24,676,001,000 kwa ajili ya kugharimia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge Hoja imetolewa na imeungwa mkono nadhani ni busara kabla hatujaendelea na wasemaji wa Kamati kwa maana ya Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji wa Kambi ya Upinzani; nitangaze orodha ya majina ambayo Waheshimiwa Wabunge watakuwa wa mwanzo kuchangia kwa hiyo kama wapo nje ya ukumbi wa Bunge warudi ndani ili wajiandae. Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Mheshimiwa Aloyce Kimaro, atafuata Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo na Mheshimiwa Lucy Owenya wajiandae. Hao ndiyo watakuwa wasemaji wetu ambao watakuwa wa mwanzo na baada ya hapo nitawapa orodha ya watakaofuata.

Nimepokea tangazo jingine kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba Kamati yake nayo itakutana saa tisa alasiri katika chumba namba 23i. Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kamati inayohusika na Wizara hii, namwona Mheshimiwa Lucy Mayenga Mbunge wa Vijana.

**MHE. LUCY T. MAYENGA – ( K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA UTALII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 pamoja na Maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyokwa mwaka wa fedha 2007/2008

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu Na. 81(1) ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004) nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 69-Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa salamu za rambirambi kwa ndugu, jamaa na familia ya Mzee Chifupa kutokana na kifo cha kijana wao mpendwa, aliyekuwa Mbunge wa Vijana kupitia tiketi ya CCM, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Kilichotokea tarehe 26 Juni 2007. Msiba wa marehemu Amina Chifupa umepokelewa kwa masikitiko makubwa kwa Watanzania wengi kila pembe ya Nchi. Katika uhai wake, Marehemu alionyesha umakini mkubwa wa kazi yake kama Mbunge. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Waziri, alielezea kwamba maandalizi ya mpango na Bajeti ya Mwaka 2007/2008 chini ya

Mpango wa Muda wa kati wa Bajeti (*MTEF*) yamezingatia maelekezo mbalimbali ya serikali yanayolenga katika kutekeleza Sera na Mikakati ya utekelezaji wa MKUKUTA na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Aidha maelekezo ya Kamati na miongozo mbalimbali pia imezingatiwa. Pia Kamati ilielezwa malengo na kazi za kila idara na taasisi kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Ushauri na Maagizo ya Kamati kwa Mwaka 2006/2007. Katika Mwaka wa Fedha uliopita Kamati yangu ilitoa ushauri na maagizo katika maeneo mbalimbali hasa yanayohusu Uvuvi, wanyamapori, Misitu na Nyuki, Mambo ya kale, Utalii na Utafiti katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Wizara kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika imeshauri na kutoa maagizo ipasavyo. Katika Mwaka wa Fedha 2006/2007, wizara iliidhinishiwa na Bunge Bajeti ya Shilingi 59,789,045,500/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Fedha za Miradi ya Maendeleo. Hadi mwezi Aprili 2007, Wizara ilikuwa imetumia jumla ya shilingi 33,067,467,567/=. Kiasi cha Shilingi kilichobaki kilitarajiwa kutumika mwishoni mwa mwezi Juni, 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi 37,017,336,080/=, mwelekeo wa makusanyo unaonyesha lengo la kiasi cha shilingi 38,852,116,403.03/= limefikiwa mwishoni mwa mwezi Juni 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafanikio na Matatizo katika Utekelezaji wa Bajeti 2006/2007; Mafanikio baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na:- (i)Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa Sera zake, kuandaa Sera ya Taifa ya Malikale na kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sera ya wanyamapori ya mwaka 1998.

(ii) Kumekuwepo na ongezeko la makusanyo ya maduhuli ambapo hadi Aprili 2007 kiasi cha shilingi bilioni 38.8 zilikuwa zimekusanywa ukilinganisha na shilingi bilioni 37.017 zilizokadiriwa kwa mwaka mzima.

(iii) Elimu ya uhifadhi na mafunzo kwa viongozi na watumishi ilitolewa ili kujenga uwezo wa kiutendaji.

(iv) Doria 18,924 zilifanyika ndani na nje ya mapori ya akiba, hifadhi za taifa na maeneo ya udhibiti wa wanyamapori. Doria 1,724 zilifanyika katika Bahari ya Hindi, doria 6,677 katika Ziwa Victoria na doria 749 katika maeneo mengine ya Ziwa na Mabwawa.

(v) Sheria ya Mamlaka ya kusimamia Uvuvi Bahari kuu iliwasilishwa na kupitishwa na Bunge (*The Deep Sea Fishing Authority (Amendment) Act, 2007).*

(vi) Mwongozo wa uvunaji wa mazao ya Misitu ulitayarishwa, Pia Mwezi Septemba 2006 hapa Dodoma, Wizara iliandaa maonesho ya kitaifa ya asali yaliyoshirikisha Wadau mbalimbali.

(vii) Wizara imeendelea kutangaza vivutio vya Utalii ndani na nje ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matatizo yaliyojitokeza wakati wa Utekelezaji wa Majukumu. Pamoja na mafanikio hayo Kamati iliainisha matatizo mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Uhaba wa Watumishi na vitendea kazi;
(ii) Uvunaji haramu na matumizi yasiyokuwa endelevu ya raslimali; na
(iii) Ufinyu wa fedha zilizotengwa kwenye Bajeti ya Serikali na uamuzi wa kupunguza fedha za Bajeti katikati ya mwaka, hivyo kuathiri mpango wa kazi na malengo yaliyowekwa. Fedha za Serikali na zile za wahisani kwa ajili ya miradi kutotolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati. Sekta ya Maliasili na Utalii ni Sekta inayokua kwa haraka sana hapa nchini. Takwimu zinaonyesha kuwa sekta hii inachangia wastani wa asilimia 16 kwenye Pato la Taifa.

Wizara ya Maliasili na Utalii ina miradi mikubwa takribani kumi na mbili (12) ambayo yote inafanya kazi chini ya Idara mbalimbali za Wizara, miradi hii inasaidia katika dhana nzima ya MKUKUTA, kwa kuzingatia hayo Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Kuhusu Uvuvi ni kwamba jamii nyingi za Pwani ni maskini zaidi ingawa zimezungukwa na utajiri mkubwa wa rasilimali ya Bahari na Pwani, miradi mingi ya Wizara inayofanya kazi katika Ukanda wa Pwani haitekelezi malengo yake ipasavyo, fedha nyingi za miradi hiyo mikubwa haziwafikii walengwa. *(Makofi)*

Mfano mzuri ni mradi wa usimamizi wa mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (*MACEMP)* wenye mtaji wa Dola milioni 61 za Kimerekani ambao unatekelezwa kwa miaka sita (2005-2011). Kamati yangu haijaridhishwa na matumizi ya fedha za mradi mkubwa kama huu ambao fedha zake haziwafikii walengwa, Aidha kasi ya ufanyaji kazi wa mradi huu ni ndogo mno ukilinganisha na fedha iliyopo na matokeo ya kazi zilizofanyika katika Kipindi hiki cha miaka miwili. Mradi huu ulilenga wilaya kumi na nne (14) za Pwani na hadi sasa unafanyakazi wilaya tatu (3) tu, Mafia, Kilwa na Rufiji. Kamati yangu inashauri Serikali kufuatilia kwa umakini mkubwa utendaji kazi wa miradi mikubwa kama hii ambayo ndiyo vyanzo vikuu vya MKUKUTA ili wananchi waishio maeneo ya Ukanda wa Pwani wafaidike.

Kamati inaridhishwa na juhudi zinazofanywa na Serikali katika hali ya ukuzaji viumbe hai kwenye maji na mikakati ya kuinua kiwango cha uzalishaji. Hata hivyo Kamati inaishauri kutoa elimu ya ufugaji wa viumbe hivyo (Samaki, Kamba, Mwani n.k)

kwa shule za msingi na sekondari na wadau mbalimbali ili mikakati hiyo iweze kufanikiwa.

Kamati ilipata fursa ya kutembelea taasisi ya Hifadhi za Bahari na baadhi ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu yaliyopo Dar es Salaam, Kamati iliridhishwa na kazi za taasisi hiyo hasa katika masuala ya ushirikishwaji wa wananchi katika kulinda, kusimamia na kuendeleza usimamizi wa hifadhi na maeneo tengefu. Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi za uhamasishaji wa Jamii juu ya uhifadhi na Usimamizi endelevu wa rasilimali hii ya Bahari, Pia taasisi hiyo iongezewe uwezo ili ifanye kazi zake kwa ufanisi. Idara ya Misitu na Nyuki. Kwa kuwa Wizara imeandaa marekebisho ya viwango vya mrahaba na ada mbalimbali za mazao na huduma za misitu, Kamati inaishauri Serikali kudhibiti ipasavyo mapato yatokayopatikana kutokana na ushuru na ada za mazao ya misitu, na ni mategemeo ya Kamati kuwa mapato hayo yatakuwa mara mbili zaidi ya kiwango cha awali.

Kamati inaipongeza Wizara kwa kuandaa maonesho ya Kitaifa ya Asali ambayo yalifanyika hapa Dodoma mwezi Septemba 2006. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuharakisha Uundwaji wa Idara ya Ufugaji Nyuki pia, kukamilisha hatua ya kukirudisha chuo cha ufugaji Nyuki Tabora ili kuimarisha Sekta hii ya Ufugaji Nyuki na Utafiti wake, pamoja na uhifadhi wa mazingira. Bado kuna ukataji mkubwa wa magogo na uchanaji wa mbao hasa katika mapori ya akiba ya Moyowosi, kigosi Magharibi mwa Tanzania na selous kusini mwa Tanzania. Kamati ina wasiwasi na uwezo wa Wizara na Halmashauri za Wilaya katika kushughulikia utoaji wa vibali na usimamizi mbovu wa ukataji wa magogo. Kamati inaishauri Serikali ifanye mabadiliko kwa idara ya Misitu kwa kuhamisha Watumishi, kufukuza wabadhirifu na kuweka maofisa wachapakazi na waadilifu.

Mojawapo ya malengo ya sera ya Utalii ni kuongeza uchumi na kuleta hali nzuri kwa wananchi kwa kupunguza umaskini na kuendeleza utalii ulio endelevu wenye kuzingatia mazingira mazuri. Sera hii bado haijakidhi kutangaza na kuendeleza Utalii uliopo Mikoa ya Kusini na Magharibi mwa Tanzania. Kamati inasisitiza Serikali kuzingatia Utalii uliopo katika Mikoa ya Kusini na Magharibi mwa Tanzania pia kuchochea uwekezaji kutoka Ndani na Nje ya nchi wa miundombinu na huduma za Utalii katika Mikoa ya Kusini na Magharibi mwa Tanzania. Kamati inaishauri Serikali kufuatilia kwa umakini mgogoro uliopo unahusu majengo ambayo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (*NCAA*) imeyanunua toka Shirika la Nyumba ya Taifa (*NHC*). Mgogoro huu unahusu Mamlaka na Wapangaji ambao wameng'ang'ania kwenye majengo hayo na kesi ipo mahakamani kwa takribani miaka minne.

Kamati inaridhishwa na Serikali katika kuendeleza juhudi za kulinda wanyamapori. Kamati inampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuongeza maduhuli ya uvunaji wa Wanyamapori, takwimu zinaonyesha Serikali itapata mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 49.6 kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008. Sheria ya Wanyamapori imechelewa sana, ije ikiwa na muundo bora wa usimamizi wa raslimali ya Wanyamapori, aidha Kamati yangu bado inaisisitiza Serikali kuunda Wakala mpya wa kushughulikia masuala ya Uwindaji wa Kitalii (*Agency*). Idara ya Wanayamapori itapata fursa nzuri

zaidi ya kushughulikia Sera, Sheria na Uhifadhi kwenye mapori ya Akiba na Hifadhi za Wananchi. Kamati inaishauri Serikali kuwa na utaratibu wa kuwahamisha Mameneja wa Mapori ya Akiba, Hifadhi za Taifa na vituo vya Malikale ambao wamekaa sehemu moja kwa muda mrefu hii itasaidia kuwa na mawazo mapya, kuboresha kazi na kuongeza ufanisi kwa Watendaji husika. Suala la ujenzi wa hotel za kitalii hasa katika maeneo ya kaskazini *(Nothern Circuit)* na maeneo mengine ya hifadhi yazingatie tathmini ya athari kwa Mazingira (*EIA*) na *Management Plans* za hifadhi husika. Kamati inashauri umuhimu wa hoteli kujengwa maeneo yanayofaa kimazingira na ramani zake ziwe maalum kabisa kwa utalii wa mbugani kama ilivyojengwa *Lobo Wildlife Lodge.* Tusiige ujenzi holela wa hoteli kama uliofanywa na wenzetu wa Nchi jirani.

Kwa kuwa Uwindaji wa Kitalii ni burudani, na uwindaji huu unafanywa katika maeneo maalum ”vitalu”, bado kuna ukiukwaji mkubwa wa Sheria za Uwindaji mfano mzuri ni kama vile nyara zinazowindwa kutolingana na kibali kilichotolewa na utoroshwaji wa nyara. Kamati inaishauri Serikali kufuatilia kwa umakini mkubwa uwindaji wa Kitalii unaofanywa hapa nchini, pia kuchukua hatua kali kwa wanaohusika pindi wanapogundulika kuwa wamekiuka Sheria za Uwindaji.

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Mambo ya Kale. Nchi yetu ina urithi na rasilimali nyingi za utamaduni, inazo kumbukumbu nyingi na muhimu zenye sifa za Kitaifa na Kimataifa, ambazo baadhi zimeitangaza sana nchi yetu nje ya mipaka yake. Uhifadhi wa malikale na makumbusho ni fani muhimu za urithi wa utamaduni ambazo zinatakiwa kupewa kipaumbele na Serikali. Idara inasimamia maeneo ishirni tu ya Mambo ya Kale, kati ya maeneo zaidi ya mia tano yaliyoainishwa. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Idara hii hasa katika masuala ya ajira mpya, fedha na elimu kwa Watumishi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati inataka kujua hatua zilizochukuliwa kwa watumishi wakorofi wa kule *Olduvai Gorge* na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

(v) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya masuala ya utafiti kwa taasisi za *TAWIRI*, *TAFORI* na *TAFIRI,* pia Serikali isambaze matokeo ya utafiti huo kwa Wadau mbalimbali ili kuendeleza matumizi endelevu ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2007/2008 ya Wizara ya Maliasili na Utalii, yameandaliwa kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yanayotarajiwa kufikiwa katika utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Wizara, Fungu 69, jumla ya shilingi 55,493,625,000; kati ya hizo, shilingi 24,676,001,000 ni kwa ajili ya fedha za maendeleo na shilingi 30,817,624,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha fedha zinazoombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, ambao ndio waliochambua Bajeti hii nao ni Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mheshimiwa Profesa Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Emanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Abdukarim E. Shah, Mheshimiwa Salim Khamis Salim, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Juma S. Nh'unga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura na mwisho mimi wenyewe, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Katibu Mkuu wake, Ndugu Blandina Nyoni na Watumishi wote wa Wizara hii na Taasisi ama Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Tumepata elimu wakati wa semina mbalimbali na tulipotembelea shughuli zao. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za Ujenzi wa Nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu, kwa ushauri na busara zao, zilizomwezesha Mwenyekiti kuiongoza Kamati hii, michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge Ndugu Damian Foka na Makatibu wake Wasaidizi wa Kamati hii; Ndugu Lawrence Makigi na Ndugu Michael Kadebe, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2007/2008, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1), Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii pia kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Marehemu Amina Chifupa. Namwomba Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuwepo hapa tena leo na kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa. Namwomba Mwenyezi Mungu, atujaalie afya njema na hekima ili tuwatumikie vyema Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakishukuru Chama changu cha Wananchi *(CUF),* kwa kuendelea kunipa ushirikiano ndani na nje ya Bunge. Naendelea pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mkoani Pemba, kwa kunichagua na ndio wao walioniwezesha kuwepo hapa leo. Ninawaahidi kuendelea kuwa pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti mwenzako, kwa kazi nzuri sana mnayoifanya. Aidha, natoa pongezi na shukrani kwa Uongozi wa Kambi ya Upinzani, chini ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, kwa imani yao kubwa kwangu na kuniteua kuwa Msemaji wa Wizara hii. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na baadhi ya Watendaji. Narudia tena na baadhi ya Watendaji wa Wizara hii, kwa kazi kubwa wanayoifanya hivi sasa, lakini bado wanayo kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uvuvi Bahari Kuu ni moja ya maeneo ambayo kama Serikali ingelikuwa makini na kuchukua maamuzi tunayopendekeza, mapato ya Serikali yangaliongezeka marudufu bila kugusa maeneo mengine. Nchi ya Namibia imeimarisha uvuvi kwa kuwa na bandari za samaki na viwanda vya samaki *(Fish Ports and Fish Processing Plants).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakadiriwa mapato yatokanayo na uvuvi nchini Namibia kwa mwaka ni dola za Kimarekani milioni 52, wakati nchi yetu ni chini ya dola milioni tisa. Ukiangalia tofauti ya kimapato utabaini kuwa, Namibia inapata dola milioni 43 zaidi ya Tanzania. Mbali na hilo, Namibia ina bandari za samaki na viwanda vya samaki vinavyoajiri watu wasiopungua 14,000 katika sekta hii ya uvuvi. Kwa nini Tanzania yenye maeneo mengi ya uvuvi kuzidi yale ya Namibia, ishindwe na Namibia iweze? Kwa nini Tanzania iliyopata Uhuru takribani miaka 29 kabla ya Uhuru wa Namibia, ishindwe na Namibia iliyochelewa kuwa huru, ifanikiwe?.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina viwanda vya kusindika samaki kwenye Ziwa Victoria wakati ukanda mzima wa bahari hakuna bandari ya samaki wala viwanda vya samaki, jambo ambalo linatukosesha ajira kwa vijana wetu. Serikali ikifanya mambo yafuatayo, mapato yatokanayo na uvuvi yataongezeka zaidi:-

- Kuongeza ada ya leseni kwa meli za nje zinazovua katika Bahari Kuu hadi kufikia *USD* 100,000 kutoka inayotozwa sasa ambayo ni *USD 18*,000 kwa mwaka. Somalia ambako kwa muda mrefu hakukuwa na Serikali, wanatoza *USD* 100,000 kwa leseni. Kulingana na takwimu zilizopo ni kuwa, kuna meli 140 (*Hansard* ya Februari 5, 2004),

Serikali ilisema kuwa imetoa leseni 193 za meli za uvuvi za nje katika Bahari Kuu ya Tanzania. Kwa maoni haya mapato yatakuwa Sh. 19 bilioni.

- Kuongeza tozo la mrabaha wa mauzo la asilimia kumi katika bidhaa za samaki zinazovuliwa katika Bahari Kuu. Kila meli kwa mwezi inavua wastani wa tani 2,000 za samaki, kwa makisio ya chini sana, japo kwa kawaida wanavua tani 1,500 kwa siku. Bei ya soko kwa kilo ya samaki ni *USD* 2.5. Kwa wanaojua biashara ya sekta hii, kiwango cha uvuvi ni kikubwa zaidi. Kwa maoni, haya mapato yatakuwa Sh. 740 bilioni ambayo sasa hayakusanywi na Serikali. *(Makofi)*

- Katika kuhakikisha kuwa sekta hii ya uvuvi inaleta mabadiliko ya kiuchumi kwa nchi na wananchi kwa ujumla, Bandari za Mtwara, Dar es Salaam na Zanzibar, zinashauriwa zitenge maeneo ya bandari za samaki *(Fish Ports and Fish Processing Plants),* ili meli zote za uvuvi wa Bahari Kuu zilazimike kununua mahitaji yao yote ya mafuta, maji, chumvi na vyakula, zinapokuja kukaguliwa kwa ajili ya kukusanya mapato. Vyombo vyetu vya ulinzi, vikishirikiana na *TRA* na Mamlaka ya Uvuvi, kudhibiti mapato haya. Kwa uamuzi huu, mapato yatakuwa shilingi bilioni tatu, ambayo nayo sasa hayakusanywi na Serikali. *(Makofi)*

- Uvuvi katika Ziwa Victoria na Tanganyika, haujadhibitiwa vizuri. Hivi sasa kuna uvuvi haramu wa wastani wa tani 36,000 kwa mwaka katika maziwa hayo, matokeo yake viwanda vyetu vinakosa malighafi. Tunashauri hatua ya dharura ichukuliwe, kuikabili hali hii kwa kutumia vyombo vya ulinzi na *TRA* ili kuongeza mapato na ajira. Zoezi hili litaongeza wingi wa samaki hivyo, viwanda vya samaki vitaongeza uzalishaji na kodi itaongezeka. Hatua hii ni ya kuongeza uwezo, haitegemewi kwa kuingiza mapato. Serikali imeshindwa kushughulikia jambo hili hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni haya ya Kambi ya Upinzani si tu yanapanua wigo wa kodi, lakini pia kwa hatua hizo, tutakuwa tumedhibiti uvunaji wa rasilimali zetu ambapo sasa hazivunwi kikamilifu au zinavunwa na kuwanufaisha watu wengine na si Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani *(Marine Coastal Environmental Management Programme - MACEMP),* unakusudia kuimarisha usimamizi wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani na kuongeza mapato ya wavuvi wanaoishi maeneo hayo yote Tanzania Bara na Zanzibar. Kambi ya Upinzani inatambua kuwa, Mradi huu unaendeshwa kwa thamani ya dola za Kimarekani milioni 61; kati ya hizo dola milioni 51 zimetoka Benki ya Dunia na dola milioni 10 zimetoka kwenye Mfuko wa Mazingira wa Kimataifa. Mgawo wa dola milioni 51 za Benki ya Dunia unaipa Tanzania Bara 60% na Zanzibar 40% ya fedha hizo na pande zote hizi mbili Bara na Zanzibar, zinapata mgawao wa 50% kwa 50% ya dola milioni 10 kutoka Mfuko wa Mazingira wa Kimataifa, kwa ajili ya Mradi huu wa *MACEMP*. Mradi huu unatekelezwa kwa majaribio kwa maeneo machache tangu Desemba, 2005 mpaka Desemba, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunafuatilia kuhusu Mradi huo ili fedha inayokusudiwa kwa Mradi huo iende kwa walengwa badala ya kuitumia fedha kwa semina, kongamano magari na shughuli nyingine za kiofisi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuupa uwezo Mradi huo unaotakikana ili uweze kujiendesha hata pale muda wa ufadhili utakapomalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Misitu, pamoja na kuwa ni chanzo kingine kikubwa cha mapato, bado mapato yake hayakusanywi ipasavyo na Serikali hasa katika bidhaa za magogo na mbao. Upotevu wa mapato umeelezwa vyema katika ripoti ya Shirika la *TRAFFI,C* baada ya kufanya utafiti ulioruhusiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii Tanzania, na kuwezeshwa na wadau wa maendeleo wa Tanzania. Ripoti pia inaelezea jinsi sera ya sasa ya misitu kama inavyoelezewa kwenye sheria na kanuni zinazohusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali hizi, unavyoyumbishwa kwa taratibu kwa maslahi ya wawekezaji wa ndani na nje, kwa kushirikiana na Watendaji Wakuu wa Serikali ya Tanzania na wa Serikali za nje kwa kuvuna misitu kwa njia isiyo endelevu na kuwepo uwezekano wa kuimaliza kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakadiriwa kwamba, upotevu wa mapato ya taifa ya Idara ya Misitu na Nyuki ulifikia dola za Kimarekani milioni 58 kwa mwaka kutokana na makusanyo ya maduhuri chini ya kiwango kwenye Halmashauri za Wilaya. Upotevu wa mapato ya Serikali Kuu na Halmashauri za Wilaya, unaotokana na makusanyo chini ya kiwango unafikia asilimia 96 ya jumla ya makusanyo halisi. Baadhi ya bajeti ya baadhi ya Halmashauri za Wilaya, zingeweza kuongezeka mara nne kama mapato halisi ya mazao ya misitu yangekusanywa vizuri. Ni hasara iliyoje hiyo kwa nchi maskini kama yetu, wakati tunaomba msaada, mapato ya rasilimali zetu yanapotea. Katika utafiti huo wa *TRAFFIC* imekadiriwa kuwa, kama hatutakuwa na uvunaji endelevu kwa magogo ya Kusini mwa Tanzania, ndani ya miaka 20 misitu hii itatoweka eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebainika pia kuna upotevu mkubwa wa mapato wakati wa usafirishaji wa magogo nchi za nje. Kwa mfano, wanunuzi wakubwa wa magogo yatokayo Tanzania ni China, Japan na India. Kwa rekodi za ushuru wa forodha Tanzania, China peke yake ilinunua *cubic metre* 18,316 za magogo na mbao kwa bei ya *USD* 150 kwa cu.mita moja, ambayo jumla ni *USD* 2.7 milioni, sawa na shilingi bilioni 3.5 za Tanzania. Lakini kwa rekodi zilizoko Forodha ya China kwa kipindi hicho, bidhaa za magogo na mbao kutoka Tanzania zilikuwa ni *cubic metre* 108,605 na bei halisi ya cu.mita moja ni *USD* 450. Takwimu hizi zinabainisha yafuatayo:-

- Kulikuwa na upotoshwaji wa kimahesabu wa cu.mita elfu 90,289 za magogo na mbao;

- Tofauti ya bei halisi waliyotozwa China na ile bei ndogo iliyooneshwa na serikali ni *USD* 300 kwa cu.mita 1; na

- Kwa sababu ya rekodi hizi, ni dhahiri kuwa Taifa lilipoteza jumla ya *USD* 40.6 millioni sawa na shilingi bilioni 52.8 za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upotevu huu wa mabilioni ya fedha, unahusu mbao na magogo haya yaliyotoka katika Mikoa ya Kusini tu. Huu ni ufisadi, hali hii inatisha na ikiendelea hivi, lengo la kuleta "Maisha Bora kwa Kila Mtanzania" litabakia kuwa ndoto tu. Serikali makini ni Serikali inayosimamia rasilimali za watu wake, viongozi mahiri ni viongozi wanaotumia vyema rasilimali za nchi kwa manufaa ya watu wake na sera makini ni zile zinazotengeneza na kudhibiti upotevu wa mapato kwa maendeleo ya watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii hatuwezi kunyamaza, ni jukumu letu kuhakikisha rasilimali za Watanzania, zinalindwa ama zinatumika vyema kwa manufaa yao. Hivyo basi, tunaitaka Serikali itueleze wahusika waliofuja ama kusababisha upotevu huu mkubwa wa mapato, wamechukuliwa hatua gani na kama bado, Watanzania wenye uchungu na nchi yao, watapenda kujua wahusika hawa watachukuliwa hatua gani, kwani wanajulikana na bado wengine ni Watumishi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, ili kuboresha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato katika Sekta hii ya Misitu, Kambi ya Upinzani tunaishauri Serikali ichukue hatua zifuatazo:-

- Halmashauri za Wilaya zilizo katika maeneo ambayo bidhaa hizi zinapatikana ziwe mawakala wa kukusanya mapato kutokana na bidhaa za maliasili. Uamuzi huu utapunguza kwa kiasi kikubwa, ufisadi uliopo sasa katika Wizara ya Maliasili. Kila Halmashauri inayokusanya kodi, ipatiwe gawio kutoka sehemu ya makusanyo;

- Mapato yote yakusanywe na *TRA* kwa kutumia stakabadhi za *TRA* kupitia Halmashauri za Wilaya kama ilivyoelezwa hapo juu;

- Mtu yeyote atakayekamatwa kwa kutorosha maliasili, afilisiwe kwa mujibu wa sheria na kama haipo itungwe;

- *TRA* mbali na kukusanya mapato, ishirikiane na Bodi ya Mauzo ya Nje kuhakiki bei za Bidhaa zetu zinazouzwa nje ili kupata mapato halali ya Rasilimali zetu; na

- TVT ianzishe kipindi cha "Bei za Bidhaa Zetu" kila siku, ili wananchi na wafanyabishara, waelewe wastani wa bei za bidhaa zetu hasa zile zinazosafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa toka Serikalini ni kuwa, wawekezaji katika Sekta ya Misitu toka nje, wanatakiwa kuwekeza kwenye viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya misitu na sio kuingia katika uvunaji na upasuaji wa mbao. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, ilieleze Bunge hili ni makampuni mangapi ya kigeni mbali na Kampuni ya Afrika ya Kusini ya *HOLTANI*, yanafanya kazi kuongeza thamani ya mazao ya misitu na ni kiasi gani makampuni hayo ya wawekezaji wa kigeni yameliingizia Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya Mheshimiwa Waziri ya kupandisha bei ya bidhaa za misitu na leseni, kuna madai ya wadau kuwa ongezeko hilo watakaoumia zaidi ni wananchi wa kawaida.

Mfano, thamani ya kitanda kimoja kinachochukua mbao sita sawa na mita za ujazo $0.5m^3$ kabla ya ongezeko, ubao mmoja ulikuwa ukiuzwa Sh. 35,000 x 6= 210,000. Kwa ongezeko la bei na ada utauzwa kwa Sh. 90,000 x 6 =540,000. Baada ya kuweka gharama za ufundi kitanda cha kawaida kinaweza kufikia Sh. 700,000. Kambi ya Upinzani inaomba ufafanuzi kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu wa kawaida, watumishi wa Wizara ndio wanaotoa *grade certificates* na *Inspection Certificate*. Mbali ya hapo, wakati wa kupakia katika makontena ni lazima Maafisa wa Ushuru wa Forodha wawepo, kufanya uhakiki wa mzigo unaopandishwa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieze Bunge; kwa nini Serikali inashindwa kuwa na takwimu sahihi za mazao yanayosafirishwa nje ya nchi, wakati vyombo husika vinatakiwa vifanye kazi yake? Kwa kushindwa huko ni kwa nini Watanzania wasiwe na dhana kwamba, wanaofanya hujuma hiyo ni Viongozi wa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Serikali itoe *returns of exports* kutokana na makampuni hayo ya wawekezaji wanaosafirisha mazao ya misitu, kwani ni njia nzuri ya kuelewa wawekezaji matapeli na wale wasio matapeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri, atueleze Kitengo cha Utafiti na Masoko kuhusiana na mazao ya misitu, kimepata vipi masoko ya mazao hayo nje ya nchi na kama hakipo bei za soko zinatafutwa na wafanyabiashara na kama ndivyo ukweli wa bei hizo ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua hizi, mapato ya maliasili ya misitu yataongezeka kwa asilimia 90 ya mapato ya sasa, makusanyo halisi yatakuwa shilingi bilioni 100, ambazo hivi sasa hazikusanywi. Kwa hali hii, hoja ya miaka mingi kuwa Serikali haina pesa, haina nafasi tena, Watanzania tumechoshwa na hoja hii inayotumika mara kwa mara, kuhalalisha umaskini wetu wakati tuna rasilimali nyingi kuzidi mahitaji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Kambi ya Upinzani ilipokea taarifa inayobainisha kuwepo kwa mbinu chafu ya ukwepaji kodi na rushwa katika usafirishaji wa magogo aina ya mi-*Teak* kutoka katika Shamba la Serikali lililoko Mtibwa – Morogoro. Taarifa hiyo inazungumzia kufunguliwa kwa *Letter of Credit* katika *Exim Bank of Tanzania. Letter of Credit* hiyo iliyofunguliwa na wanunuzi wa India, ilifunguliwa kuwezesha magogo hayo ya mi-*Teak* kusafirishwa kwenda Dubai, lakini ukweli ni kuwa, magogo hayo yalisafirishwa moja kwa moja kwa wanunuzi wa India na hivyo, kusababisha ukwepaji mkubwa wa kodi. Jumla ya *cubic metre* 42, 947 za magogo ya mi-*Teak* ziliuzwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa utaratibu wa *Central Tender Board Tender No. 26* ya 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi juu ya kumbukumbu za *TRA* na *Exim Bank,* unaonesha kuwa malipo yote yaliyofanywa kwa *Teak* iliyosafirishwa na Kampuni ya *Fibreboards 2000 Ltd.,* yalifanywa kupitia Kampuni ya *Natvar & Co Dubai*, wakati mipango yote ilifanywa na wanunuzi wa India. Hapa kuna harufu ya rushwa! Karibu *cubic metre* 25,000 za magogo ya mi-*Teak* zilisafirishwa kwa meli kati ya mwaka 2005 na 2006.

Matokeo yake mamilioni ya dola za Kimarekani kutokana na uuzaji wa magogo ya mi-*Teak* uliofanywa hadi kufikia sasa, yamekuwa yakipotea kwa ujanja huu wa kupitia Kampuni ya Dubai wakati wanunuzi ni India. Ukwepaji kodi unaofanikishwa na mtu au kampuni ni kinyume cha sheria za nchi hii. Benki yoyote Tanzania inapaswa kuelewa sheria, kanuni na taratibu kama zilivyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Fedha na kadhalika.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliambia Bunge hili ni adhabu gani itakayotolewa kwa benki iliyohusika katika kupindisha sheria zinazohusu mteja wake kuficha bei halisi ya bidhaa nje ya nchi *(declaration of under-price in the market for the purpose of avoiding proper taxation).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mamilioni kadhaa ya dola za Kimarekani yanakadiriwa kupotea kutokana na ukwepaji huu wa kodi katika usafirishaji wa *Teak* unaofanywa na kampuni ya *Fibreboards 2000 Ltd.* kwa kutumia kampuni tajwa ya Dubai. Ikumbukwe kuwa ni watu hawa hawa wa *Fibreboards,* waliodiriki kuomba punguzo la kodi kwa Mheshimiwa Rais katika biashara yao ya mbolea kule Arusha. Hii ni sawa na tajiri kumwomba maskini amkopeshe fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ipo Wizarani, *TRA* na TAKURU, lakini hatua hazijachukuliwa hadi leo. Jambo la kusikitisha, wahusika wanaendelea kuinyonya nchi bila wasiwasi na huku Watanzania rasilimali zao zinatumiwa vibaya wakiambiwa kuwa ni wavivu na si wazalendo. Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali ileleze Bunge lako Tukufu ni kwa nini uchunguzi wa tuhuma hizi nzito haukufanyiwa kazi? Taifa makini halipaswi kukabiliwa na ufisadi kama huu, kana kwamba nchi hii haina wenyewe. Ni wajibu wetu sote kupambana na vitendo vya kifisadi na hili halina itikadi na hatimaye kuwachukulia hatua wahusika na kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa, adhabu zinazohusika zinachukuliwa kwa wahusika na kuwa fundisho kwa wale wote wenye mawazo ya kufanya ufisadi kama huu. Sisi ni mahodari wa kuwabana Watanzania, wanaoleta bidhaa zao hapa nchini, ambazo zinatuongezea urari wa biashara, badala ya kufuatilia kupata bei muafaka kwa bidhaa zetu tunazo safirisha nje, hatua ambayo itatuongezea fedha za kigeni na kuufanya urari wa bishara baina ya *Export* na *Import* kuwa na uwiano mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za Maliasili, kuna vitalu 158 vya uwindaji. Kwa kipindi kirefu, Serikali imekuwa ikikodisha kitalu kwa wastani wa *USD* 7,500 kwa mwaka na imekuwa ni kawaida kwa wamiliki nao kukodisha vitalu hivyo kwa wenye fedha kwa wastani wa *USD* 100,000 kwa mwaka. Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 159 la juni 29, Serikali imepandisha ada za vitalu ambapo katika kundi la kwanza ada imekuwa ni dola 50,000 kutoka dola 10,000 na kundi la pili

ada imekuwa dola 40,000 kutoka dola 10,000. Kwa mabadiliko haya, Serikali itaingiza kati ya dola milioni 2.96 na dola milioni 4.2 kwa mwaka. Ushauri wa Kambi ya Upinzani siku zote umekuwa ni kuona Serikali inapata mapato zaidi kwa maendeleo ya wananchi. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua hiyo. Pamoja na hatua hiyo, bado Kambi ya Upinzani tunaishauri Serikali kuzingatia yafuatayo ili kuongeza mapato:-

- Ipitie na kuangalia mwenendo wa sekta hii na uwezekano wa kuongeza ada ya vitalu ifikie *USD 100*,000 kwa kitalu;

- Kuwajasirimisha Watanzania vitalu vyote vya uwindaji;

- Ili kupata thamani halisi washauriwe kuingiza Vitalu hivyo katika soko la mitaji kwa kutumia *eletronic commerce;* na

- Kutoza asilimia 30 ya mapato yatokanayo na Mtanzania atakayekodisha kwa mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua hii, Watanzania watakuwa wamewezeshwa kumiliki rasilimali zao wenyewe na pia kwa kuongeza viwango vya kodi ya uwindaji. Makusanyo yanakisiwa kuwa shilingi 85 bilioni, ambayo hayakusanywi hivi sasa. Ushauri huu ukitekelezwa sio tu utaongeza Pato la Taifa, bali pia utaongeza tija na Watanzania watafaidika na rasilimali zote ambazo Mwenyezi Mungu, amewabariki nazo. Ni vyema sekta hii ikaangaliwa kwa ungalifu na pia kusaidia kuimarisha na kuboresha huduma zinazotolewa na sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ndogo ya uwindaji wa kitalii, kumetokea malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi. Sekta hii imekuwa ni chanzo cha mapato mengi ya Serikali kupotea. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa ili Serikali ifanikiwe kukusanya fedha za kutosha kutoka katika sekta hii ndogo ya uwindaji wa kitalii, hatua zifuatazo ni lazima zichukuliwe:-

- Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 1974 kupitiwa upya na kufanyiwa marekebisho makubwa na au kuifuta na kuitunga upya. Sheria mpya itoe kipaumbele kwa Watanzania katika TASNIA ya uwindaji wa kitalii.

- Ifikapo mwisho wa kipindi cha umilikaji, vitalu vyote virudishwe Serikalini kwa ugawaji mpya na kampuni za uwindaji za Watanzania zipewe fursa na nafasi ya kwanza kushindania umiliki wa vitalu.

- Taratibu za ugawaji wa vitalu ziwe wazi ikiwa ni pamoja na kutangaza vitalu vilivyo wazi na biaonuwai zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaona kuwa inakusanya mapato mengi katika Sekta hii ya Maliasili na Utalii hadi kuchangia asilimia 16.8 ya Pato la Taifa. Hata hivyo, Serikali imeshindwa kufikia malengo ya watalii milioni moja kwa mwaka, kama

ilivyokuwa imepanga. Idadi ya watalii wanaokuja nchini ni wastani wa 644,124. Ni vyema tunapoweka malengo yetu tukaangalia. Hivi kweli Serikali yenye kutilia maanani umuhimu wa utalii nchini, inaweza ikajiwekea malengo kama haya? Kwa nchi yenye vivutio vya utalii lukuki kama Tanzania, yaani ongezeko la watalii takriban laki mbili kwa mwaka hadi 2010, kweli linaingia akilini mwetu! Ni aibu iliyoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe, Serikali imekuwa ikipoteza mapato kutokana na watalii kulipia gharama za safari zao na baadhi ya huduma kwa *Tour Operater* huko huko kwao kwa wastani wa *USD* 200 - 300 kwa mtu mmoja kwa siku. Mtalii anapofika Tanzania, huwa analipa wastani wa *USD* 80 - 150 tu. Hivyo, kuzipunguzia mapato hoteli zetu na kwa maana hiyo na Serikali. Kama nusu ya watalii hawa 322,062 huwa wanakuja katika *Package Tour* na kuwa tunakusanya wastani wa *USD* 100 kwa siku kwa kila mmoja, kwa muda wa siku saba ukiacha mapato yasiyo ya moja kwa moja, katika eneo hili Serikali ingelikusanya kama kodi ya mapato 30% sawa na shilingi 67.5 bilioni, ambazo hazikusanywi hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalii wengi hupenda kutembelea mbuga za kaskazini *(Northern Circuit).* Hali hiyo husababisha msongamano mkubwa wa watalii katika mbuga zetu. Umefika wakati sasa kuwe na Mkakati Maalum wa kutangaza na kukuza utalii Kusini na Magharibi mwa Tanzania. Sambamba na hatua hiyo ni vyema yale makosa yaliyofanywa huko nyuma, yakasahihishwa kabla ya kuingia mikataba mipya, kama Serikali inavyofanya kwenye Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlima Kilimanjaro unaingiza fedha nyingi za kigeni kutokana na watalii. Kinachosikitisha ni kuona bado waongozaji wasaidizi wa njia *(Tour Operators),* hulipwa fedha ndogo na makampuni ya utalii. Ni wajibu wa Serikali inayojali wananchi wake, kuingilia kati uonevu huu ili watu hawa wasidhalilishwe ndani ya nchi yao, vinginevyo, biashara hii haitanyanyua kipato cha watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na utangazaji wa vivutio vya utalii ndani ya nchi yetu, ipo haja ya kuimarisha uwingi na ubora wa hoteli zetu. Ndani ya hoteli kadhaa, baadhi ya vyakula vinavyopikwa vinatoka nje ya nchi, licha ya kuwa vyakula hivyo vinapatikana ndani ya nchi. Suala hili si jema kwa maendeleo ya wakulima wetu, ambao hukabiliwa na tatizo kubwa la kukosa masoko ya kutosha ya kuuza bidhaa zao. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa ni vyema Wizara hii na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kuanza kuainisha wakulima na mahoteli ambayo yatatumia mazao yetu badala ya kuagizia nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imebainika kuwa, nafasi muhimu katika hoteli nyingi za kitalii huchukuliwa zaidi na wageni kwa hiyo, ipo haja ya kuimarisha taaluma kama tatizo ni elimu. Kama tatizo si elimu, basi uangaliwe utaratibu wa kuzifanya hoteli hizi kuajiri wazalendo katika nafasi muhimu. Malipo ya huduma kwenye baadhi ya hoteli hizi hufanywa kwa dola badala ya kulipwa kwa fedha yetu. Suala hili ni vyema likahakikiwa na kurekebishwa vyenginevyo, njia hii inaweza kutumika kuhalalisha fedha chafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania mpaka sasa haijaweka Chuo cha Kimataifa cha Utalii. Ni jambo la kushangaza kwamba, hata chuo tulicho nacho ilibidi tukihamishe kutoka kwenye eneo la kitalii Jijini Dar es Salaam na kukipeleka kwenye mazingira ya huduma za magengeni. Halafu tunakaa tunalalamikia kazi bila kuwa na chombo cha kutoa wafanyakazi wenye sifa zinazotakikana na hili linachangaia kuweka malengo ya chini kabisa ya kuleta watalii hapa nchini. Hivi kwa nini Chuo cha Uvuvi kiwekwe kando kando ya bahari na sio sehemu kama Mkoani Kilimanjaro au Morogoro? Kwa nini tusihamishie vyuo vya misitu baharini? Huko Afrika Kusini, kuna Chuo cha Utalii kinachoendesha Hoteli ya Utalii ya Nyota Tatu. Sisi ni kweli hatuna watendaji wanaoona hali kama hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa nchi yetu haina chuo kinachotoa shahada *(Degree)* ya utalii, isipokuwa vyuo vichache vinatoa stashahada ya juu *(Advanced Diploma)*. Utalii bila watu walioelimika, maendeleo katika sekta hii hayatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi na uvunaji endelevu wa maliasili lazima viendane na utafiti. Ni utafiti ndio utakaotufanya tuelewe mwelekeo wa hifadhi zetu na viumbe vinavyoishi katika hifadhi hizo, pamoja na bahari na maziwa. Baadhi ya taasisi zinazofanya utafiti katika sekta hii ni *Tanzania Wild Research Institute (TAWIRI)* na *Tanzania Fisheries Research Institute (TAFIRI)*. Licha ya umuhimu wa utafiti katika samaki, bado *TAFIRI* inakabiliwa na changamoto nyingi, fedha za utafiti zinazotegemewa ni za wafadhili. Mradi unapokwisha basi tafiti nazo huwa hazifanyiki. Hilo ni tatizo kubwa, ipo haja ya Wizara kulishughulikia na kulitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia watafiti na wasaidizi wao wa *TAFIRI*, wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu mfano, kuelea kwenye maji kwa kipindi kirefu, kukusanya takwimu bila ya kuwa na bima ya maisha au posho ya kufanya kazi katika mazingira magumu *(risk allowance)*. Pia mishahara ya wafanyakazi wa *TAFIRI* hailingani na ile ya wafanyakazi wa *TAWIRI* na *TAFORI,* licha ya *TAFIRI* kufanya kazi kwenye mazingira magumu zaidi. Ni wajibu wa Serikali kuondoa changamoto hizi zinazoikabili *TAFIRI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nisisitize kuwa, ushauri tuliotoa ni wa kujenga na si kubomoa. Tumezingatia maslahi ya Mtanzania na mustakabali mwema wa Taifa letu. Taifa lina uwezo mkubwa wa kirasilimali hususan katika Sekta hii ya Maliasili na Utalii, ambazo zikitumiwa kimkakati kama nilivyoeleza, tunaweza kupata mapato ya kutosha ya kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu wa kiufundi si tu ni ujumbe kwa Watanzania kwamba, Wapinzani tunaweza lakini pia ni funzo kubwa kwa Serikali kuwa, nchi haiongozwi kwa maneno matamu bali kwa sera na mikakati yakinifu, makini na zinazotekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa heshima na taadhima ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia mjadala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kuandaa hotuba ambayo ameiwasilisha sasa hivi mbele yetu. Pamoja na hotuba nzuri, nadhani upandishaji wa bei ya maliasili zetu, umechelewa kuwasilishwa hapa Bungeni. Wabena wanasema *"Alikwina"* maana yake ulikuwa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandishaji wa bei hasa maliasili mbao, tungetofautisha kati ya wale wanaouza nje na wale wanatumia hapa nchini, maana sisi wananchi tutaathirika sana na upandaji wa mali asili mbao. Hizo nyingine naafiki ni sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna methali inayosema "ada ya mja hunena, muungwana ni vitendo." Ninaishauri Serikali hasa Mawaziri, yale maneno wanayotamkwa hapa Bungeni, wayatekeleze kwa vitendo. Uungawana ni vitendo, sisi viongozi yale tunayosema tuyatekeleze kwa vitendo na kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Kabla sijaendelea kuchangia, naomba ni-*declare interest* kwamba, mimi ni mfanyabiashara na hasa mfanyabiashara wa utalii. Mimi ni mdau ndani ya Sekta ya Utalii. Kwa hiyo, ninayozungumza mengi nayaelewa kwa ufasaha na mengine nashiriki kwa vitendo. Sekta ya Utalii ni sekta ambayo inaweza kuingiza mapato mengi na makubwa ndani ya nchi hii. Mheshimiwa Waziri, amesema 17 ingeweza kufika mpaka asilimia 40 kama tungesimamia vizuri. *(Makofi)*

Mfano mimi nizungumzie utalii ndani ya Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro ni kivutio, Mlima Kilimanjaro ni urithi wa Watanzania, ni urithi wa Wananchi Kilimanjaro na ni urithi wa dunia. Mlima Kilimanjaro unavutia watalii wengi duniani na unatangazwa duniani. Lakini wageni wanaokuja Kilimanjaro, hawaji tu kwa sababu wanakuja kuona theluji iliyoko Mlima Kilimanjaro, wanakuja kuona utalii wa Wananchi wa Kilimanjaro, mila na desturi za wote wanaozunguka Mlima Kilimanjaro, pamoja na Wamasai na Wachaga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha wale vijana ambao ndiyo kitovu cha utalii, wanyanyasika sana wakati wanapokuwepo Mlimani Kilimanjaro, wakiongoza watalii wanakuwa nao siku tano mpaka saba, mtalii mmoja akiingia Kilimanjaro kwa siku tano, mtalii mmoja analipa dola 550 pale kwenye geti ya *KINAPA.* Lakini wale wanaomhudumia wanalipwa kati ya shilingi 5,000 mpaka 20,000. Hali hii inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme hawa vijana wamenituma nilete kilio chao hapa Bungeni. Mwaka jana wakati wa Bajeti, nilileta kilio cha hawa vijana, Serikali ikatamka kwamba ni kweli hawa *Guides and Porters* wananyanyasika sana na itachukua

hatua. Nasikitika mpaka leo hii ninavyozungumza, hakuna hatua iliyochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Bunge hili mwaka huu kwenye kikao hiki, niliuliza swali, hawa vijana hatua gani itachukuliwa ili waweze kulipwa vizuri maana wananyanyaswa sana na *tour operators*. Nilijibiwa kwamba, hawa vijana ili waweze kulipwa vizuri, waende wakafungue Chama cha Wafanyakazi. Maana yake waende Wizara ya Kazi. Wizara ya Maliasili inakwepa wajibu, inapeleka Wizara ya Kazi. Hawa vijana wana vyama vyao, kuna Chama cha *Kilimanjaro Guides Association*, kingine ni *Kilimanjaro Porters Association,* walishakubalina kwa siku moja *guide* alipwe dola 20, mpishi alipwe dola 18 na *porter* alipwe dola 15, hayo ndiyo yalikuwa makubaliano na vyama vyao. Fedha hizi hazitoki kwenye Bajeti ya Serikali, wale watalii ambao wanakaa nao vijana kule mlimani kwa siku tano mpaka saba, wako tayari kuwalipa pasipo na kipingamizi chochote. Lakini wakilipa kupitia kwa *tour operators,* wale *tour operators* hawawalipi hawa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nashauri na nasema sitaunga mkono hii hoja mpaka nipate jibu sahihi na la kudumu kwamba, hawa vijana watalipwa kwa usimamizi wa *Kilimanjaro National Park,* pamoja na *Tanzania National Park,* kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii. Hawa vijana wakilipwa ndiyo ile *empowerment* tunayosema, ndiyo uwezeshaji wa Watanzania. Fedha ile itasambaa kwenye familia. Unapokataa kusimamia maana yake ile fedha ambayo wangekuwa walipwe, inabaki kwa *tour operator*. Yeye yuko Ulaya, anatuma fedha kidogo huku kwa sababu sisi hatuna mpangilio sawa sawa, ile fedha nyingi anabaki nayo kule Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali iliwekee kipaumbele wale vijana ni wengi wamenituma na mimi naungana nao, hatutakubali tena kuendelea kunyanyasika. Uwezo wa kusimamia tunao, kwa nini tunakwepa wajibu wetu? Narudia tena, sitaunga mkono hoja hii mpaka tukubaliane kwamba, hawa vijana watalipwa vizuri kama walivyopanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlima Kilimanjaro unaingiza fedha nyingi, naomba nisome: “Mwaka 2004 kwa kutumia hawa vijana Mlima Kilimanjaro ulizalisha shilingi 10, 649,586,720. mwaka 2005 bilioni 14,232,000,000, mwaka 2006 shilingi bilioni 14; jumla ya miaka mitatu ni shilingi bilioni 44.” Sasa kama hawa vijana wanazalisha shilingi bilioni 44; kwa nini wanyanyasike? Naomba Serikali ilitilie maanani hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hii ni yetu sote. Mawaziri wamepewa dhamana, Mawaziri wanapaswa wawawezeshe Watanzania, siyo Mawaziri wakaribishe wawekezaji tu. Mawaziri wawawezeshe Watanzania, Watanzania wana uwezo na wako wengi wa kutosha na uwezo wanao. Tukiendelea na hii dhana ya kukaribisha wawekezaji kutoka nje, hii nchi haitajengeka. Nakwambia mtakuja kuwa kama Zimbabwe, wakati wanaondoka tutabaki hatuna kitu. Wawezeshaji toka nje wanachoweza kufanya ni kuwekeza lakini kwa kiwango kikubwa wataendelea kuharibu nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu, Waziri Mkuu alitamka maneno yafuatayo nanukuu: "*If you want a brighter view of life, help somebody else to get the solution of her or his problem.*" Kama unataka mtazamo mzuri wa maisha, msaidie mwenzako aweze kutatua kero zake. Sasa nawaomba na nawashauri wenzetu, Mawaziri na viongozi wengine, saidieni Watanzania watatue matatizo yao kwa utaratibu unaoeleweka ili waweze kupata maisha bora kwa wote. Narudia tena, hii nchi ni yetu sote, lazima tuwezeshwe twende pamoja, tujenge Taifa lenye haki, lenye kupendana ili tufikie lile lengo Rais alilolisema "Maisha bora kwa kila Mtanzania." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, tutakutana jioni kwenye vifungu ili tuweze kuona ni vipi vijana wangu watasikilizwa. Asante. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi hii leo katika kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Watumishi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri waliyoifanya, lakini bado kuna dosari. Chochote kilichokuwa kizuri, hakikosi kuwa na dosari.

Nataka nichukue fursa hii, niwatangazie wananchi wangu, wapiga kura wangu wa Kilwa Kusini kwamba, msimu wa kilimo umeanza na matrekta yatakwenda huko mwezi wa nane ili waweze kuanza kuboresha kulima kwa kutumia matrekta kama ilivyokuwa mwaka jana. Kwa hiyo, naomba wananchi wangu wa Kilwa Kusini, wajiandikishe kwa Watendaji wa Vijiji ili waweze kulimiwa kwa bei nafuu, kwa punguzo maalum kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tangazo hili, univumilie, nataka niingie moja kwa moja kwenye hoja iliyoko mbele yetu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magogo tunazalisha sana Wilaya ya Kilwa na Rufiji, magogo asilia. Miti hii inachukua muda mrefu sana kwa takriban miaka 50 mpaka 70. Waziri hajaniambia habari zozote kuhusu *plantation* ya miti asilia katika hotuba yake. Ana mikakati gani, amevuna miti mingapi na atapanda miti mingapi na mikakati gani atakayofanya kuipanda hiyo miti? Kibaya zaidi tuna wawekezaji wa Kichina, hawa wamepewa fursa ya kwenda maporini. kienda huko utawakuta wanachagua magogo, hili silitaki hili nalitaka. Sisi kama tutakwenda kwao tutaweza kwenda kwenye hazina zao jamani? Hatuwezi kwenda kwenye hazina zao huko kwao. Wana haki gani ya kuingia kwenye misitu na kuchagua gogo hili nalitaka, gogo hili silitaki. Tutamaliza misitu yetu jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuwa mchungu sana kwa sababu naona Kilwa na Rufiji tunakwisha sasa. Kila siku ya Mungu, magari 20, 30 yanabeba magogo yanatoka pale. Wengine wanafanya ujanja wao, unaweza kumwona mtu ana *cubic meter* 300, bado hazijaisha miaka miwili jamani! *Cubic meter* 300 leseni ile inatumika mara mbili mara au tatu. Hatuna takwimu, misitu inakwisha na *plantation* hakuna. *(Makofi)*

Namshukuru sana Waziri, amesimamisha kabisa zoezi hili la kusafirisha magogo nchi za nje. Asante sana Waziri kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nigusie kidogo upande wa mbao. Tumeanza na 70,000 kwa *CBM* kutozwa, sasa hivi Waziri kwenye hotuba yake anasema tozo ni shilingi 250,000 kwa *CBM* moja, ongezeko la asilimia 350 limeongezeka. Mheshimiwa Waziri, atuonee huruma sisi wenye maliasili hii, bei ni kubwa sana angalau kutoka Sh. 70,000 tufanye iwe Sh.100,000 jamani. Itakuwa kitanda hatuwezi kununua, kitanda kitafika Sh. 400,000, mlango wa nyumba utafika Sh. 500,000. Naomba sana toka Sh.70,000 iwe Sh.100,000. Tuwabane wale wanaosafirisha ndio tuwapige bei ya Sh.250,000. Mheshimiwa Waziri, tafadhali tutazuia ugomvi, wananchi wangu wananisikiliza huko wamenitumia *SMS* Mheshimiwa kachangie hilo. Hatuwezi kuwa na nyumba bora, kenji zetu tutapigia nini huko juu, mbao hizo zitakuwa ghali sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujumuisha, nataka jibu la Waziri kuhusu ombi letu sisi watu wa Rufiji na Kilwa ili Tanzania nzima tupunguziwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ombi hilo, nataka niende moja kwa moja kwenye tembo. Wenzangu wa Zanzibar wataniwia radhi, kuongelea tembo nina maana sana. Tembo Kilwa, Liwale na Rufiji, limekuwa tatizo kubwa sana. Leo tembo anatozwa dola za Kimarekani 15,000, yule yule tembo anayeingia kwenye mashamba ya watu anafanya uharibifu mkubwa. Kila siku Kilwa kuna tokio moja la tembo, mpaka naongea na Mkurugenzi anasema sina fedha sasa Mheshimiwa Mbunge, siwezi. Naomba Wizara, tuongezewe magari Kilwa, Rufiji na Liwale. Huyo huyo tembo anayetuingizia dola 15,000, amekuwa tatizo kwetu. Tuna tatizo kubwa sana, wanakuja kuvuna wao, tunapanda sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri wakati anajumuisha anitamkie kwamba, Kilwa anaiwezesha vipi kuhusu tatizo kubwa sana la tembo, kila siku tuna tatizo hilo? *(Makofi)*

Baada ya kusema hilo la tembo, nataka niende moja kwa moja upande wa utalii. Kilwa kuna vivutio vizuri sana vya utalii. Kimoja nikitaje lakini sioni kwamba, Wizara inaitangaza Kilwa upande wa Maliasili. Tuna viboko ambao wanaitwa viboko wa maajabu, ukifika pale kwenye bwawa wakiambiwa viboko wasalimie wananchi au wageni, wanasimama wanatoka nje wote kwa pamoja wanakuja kuwasalimia wageni. Sijawahi kuona Tanzania nzima viboko kama hao, lakini Wizara haijui habari hiyo, sisi tunataka vigezo hivyo watalii nao wajue. Tuna mipango Kilwa Kipatimo, ambako walikuwa wanajificha Wandereko wakati wa Vita ya Majimaji, sijawahi kusikia gazeti lolote, kitabu chochote, makabrasha au chochote kuongelea kuhusu mapango yale. Mapango yanayotajwa ni yale ya *Amboni Caves*, lakini hakuna *Kipatimo Caves*. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Rais, atakwenda kule kuzindua Sherehe ya Majimaji, atayona yale mapango 100 yako pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naingie kwenye (RUMAKI) Rufiji, Mafia na Kilwa. *MASEM* inasuasua haifai. Nina maana nikisema utaniwia radhi sana, huu Mpango ulikuwa mzuri sana, tulipata semina pale Dar es Salaam, tukaitwa Waheshimiwa Wabunge wote, lakini hakuna mazingira yanayoboreka katika fukwe za bahari zetu. Kilwa, Rufiji na Mafia hakuna. Dola milioni 65 zimetumika katika Mpango huu, lakini mpaka leo nikikwambia ni *patrol boat,* hakuna imetajwa humu hazijafika *patrol boats* hazipo. Sehemu za Pande kule bado wana tabia ya kutupa mabomu ili wapate samaki kwa haraka sana.

Wanachafua bahari yetu kwa mabomu, mazingira yako machafu, walituahidi ule mpango kwamba, kila sehemu kutakuwa na soko la samaki, hakuna soko la samaki, hakuna vyoo, hakuna chochote kilichofanyika kwenye Mpango huu. Sijui nasikia Mpango huu mwaka mmoja na nusu baadaye utakwisha. Kwenye makabrasha sasa mpira unatupiwa *TASAF,* wanasema tuombe fedha *TASAF*. Naona ajabu kabisa, *MASEM* ilikuwa na dola milioni 65, sasa *TASAF* ndiyo itachangia itasaidia hiyo miradi ya mabwawa ya samaki. Sijui Waziri atatujibu kuhusu hilo la *MASEM*, kwa sababu Mpango huu Kilwa sijauona kama umenufaisha sana. Kuna vikundi vichache vilivyonufaika kwa ajili ya mikopo midogo midogo ya shilingi 500,000, 600,000, lakini mvuvi mwenyewe hajafaidika kwenye Mpango huu. Mazingira siyo mazuri, fukwe bado zinachafuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilwa tuna *open areas* kama mbili/tatu, ambazo Halmashauri yetu inapata kipato lakini wale wawekezaji wamekuwa wajeuri sana. Wanachoma moto, wakichoma moto unakuja mpaka kule kijijini unaunguza mikorosho ya watu, ukiwaita Wilayani hawaji wawekezaji hao. Mimi nasema uwekezaji gani huu kwenye uwindaji, rasilimali gani, rasilimali zetu wenyewe? Kwa nini huu uwekezaji wa kwenye vitalu, tusipewe wenyewe, tunaweza kulipa hizo dola 50,000? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Ningependa nianze kwa kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Lakini la pili, nataka nimpe pole sana Waziri. Nampa pole Waziri kwa sababu kuwemo ndani ya Wizara hii, basi inabidi kama Mkristo utembee na Biblia, kama Muislam utembee na Quran, muda wote unamwomba Mungu mambo yasiende kombo. Mimi ningewaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa jitihada hizi ambazo ameanza nazo Mheshimiwa Waziri, tumuunge mkono pale ni pagumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwezi Machi na Aprili, nilikuwa katika Tume ambayo Waziri aliiunda kuhusu masuala ya misitu. Ndiyo maana leo nampa pole kwa sababu nilikuwa siyafahamu yayolimo ndani ya Wizara hii. Utendaji katika Idara ya Misitu na Nyuki kuanzia ngazi ya Wilaya mpaka Makao Makuu, una matatizo makubwa kweli kweli. Yaani watendaji wetu hawa, wanawaonea wivu wakazi wa Jangwa la Kalahari na

Sahara. Wanataka sisi tufikie kiwango kile haraka iwezekanavyo, badala ya kuwahurumia sisi tunawaonea wivu, tunatamani na sisi tuishi katika jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue mfano tu wa usafirishaji wa magogo na mimi ningependa kuanza na mbao. Hizi mbao za *pines* zinazotoka Njombe kule mpaka zinafika Horohoro kwenda nchi jirani, kuna vituo hapa vya ukaguzi wa maliasili sijui vingapi kutoka Njombe mpaka kule Horohoro. Lakini lazima sisi kama Tume, siku moja tulikaa kati ya Tanga na Horohoro pale Chumbageni, kwa muda wa saa nne, tuliokoa shilingi milioni nne ambazo hazikulipiwa ushuru, kwa muda wa saa nne tu. *(Makofi)*

Unaweza ukaangalia kwa siku moja zinapotea shilingi ngapi na kwa mwaka basi shilingi ngapi. Tukamwita *Regional Catchment Officer* aje atoze zile pesa na tukampa maagizo. Siku ya tatu, tulikaa Maweni tukampigia tena simu njoo, magari mawili nayo yalitoka huko hayana kibali cha kusafirishia, ujazo ulioandikwa kwenye fomu siyo sahihi, utendaji wa namna hii kama Waziri hana Biblia mfukoni ama *Quran,* hautufikishi tunakotaka kwenda. *(Makofi)*

Kutoka Ikwiriri magogo haya Mbunge mwenzangu, jirani yangu, ninayepakana naye ametaja sana Kilwa na Rufiji. Lakini nafikiri anafahamu kwamba, matatizo haya tunayapata sana vilevile na watu wa Lindi, Nachingwea na Liwale. *(Makofi)*

Ukipita njia ile unakutana na malori yamebeba magogo, yamebeba mbao, hakuna kibali cha kusafirishia. Kule Lindi Kijiji cha Nyengedi, Jimbo la Mheshimiwa Bernard K. Membe, tumekuta magogo yamekaa pale, lakini mwenye magogo anashindwa kuyasafirisha yale bado amekwenda kukata mengine kule Nachingwea, kwa Mheshimiwa Mathias M. Chikawe. Tunamwita Afisa Maliasili anasema niko Dar es Salaam. Lakini kwa sababu na mimi ni mtu wa Lindi, ilibidi tukamchukue nyumbani kwake. Wewe bwana hapa siyo Dar es Salam hapa Mikumbi, twende tukafanye kazi kule ya Taifa. *(Makofi)*

Hata Tume iliyochaguliwa na Waziri bado Mtaalam wa Wizara hiyo hiyo haithamini, niko Dar es Salaam wakati yuko Lindi. Tunasema utendaji ni mbovu. Uvunaji wa misitu ndiyo balaa. Mkinga hakuna mti sasa. Pangani hakuna mti sasa. Wachongaji wa vinyago kutoka nchi jirani, wamehamia Handeni na Kilindi. Sasa ni zamu ya Handeni na Kilindi kuwa jangwa. Tukiwa kule tulifanikiwa kukamata vinyago vyenye thamani ya shilingi milioni kumi vya mti wa Mkarambati. Vinyago hivi vimetengenezwa ndani ya kijiji hicho hicho kimoja. Mimi napenda sana kumpongeza Mkuu wa Mkoa, *DED* na *DC.* Mkuu wa Mkoa wa Tanga, *DED* wa Handeni na *DC* wake, waliamua kumchukua na Mwenyekiti wa Kijiji na Mtendaji wake na wao kuunganishwa na yule Mkamba. Maana haiwezekani vinyago vinachongwa vyenye thamani ya shilingi milioni kumi wewe Serikali uko hapo hapo hujui!

Hao nao wasingekamatwa kama si huyu Mkamba kuamua kwenda kuchukua mke wa mtu. Yule mtu akawa na uchungu ndiyo akaenda kuripoti na Watendaji tunao mpaka Wilayani. Bukombe kule Shinyanga, hawana msitu lakini wamemwongopea

Mwenyekiti wa Kamati ya Ugawaji, ambaye ni *DC* wetu na wakatoa kibali kwenda kuvuna miti katika Hifadhi ya Taifa, maana msitu hawana. *(Kicheko/Makofi)*

Tukamwambia *DC* wamekuongopea vijana hebu wakakuoneshe katika huo msitu uliotolea kibali watakuoneshe visiki. Tusingeenda sisi pengine asingejua. Tumekamata mbao 10,000 zote hazina kibali na misumeno 100. Tukashauri mbao zisije zikapinda wapeni wananchi wajengee sekondari, mbao zile mpaka leo ziko Halmashauri. Kazi kweli kweli. *(Makofi)*

Ukija Rufiji, Kilwa, Lindi, Nachingwea na Liwale, inatisha. Watu wanakata magogo bila huruma. Mbao kama vile Mninga, ili ukatwe lazima uwe umeishi kati ya miaka 70 na 100. Unaukata mti huu halafu wengine kwa uharibifu tu hawachukui, wanaangusha miti halafu wanasema huu nachukua, huu nachukua, huu hapana. Unaoza unakuwa mali ya mchwa.

Sasa wanafikia mahali wanatuambia eti tuna-*add value* katika magogo. Siyo tume-*add value,* sasa ndiyo tumefanya mchezo wa hatari. Maana bora walivyokuwa wanafasirisha magogo vilevile yalivyo, yalikuwa yanachukua nafasi ndogo kwenye kontena. Sasa yanapigwa randa sehemu nne, tume-*add value,* ndiyo yanapangika vizuri kweli kweli. Yanapangika vizuri, yanaingia mengi. Miti ya kupandwa usiseme, kwa upande wa mashamba ya Serikali kwa kweli hali ni ngumu. Kule Ukerewe hakuna mti sasa wa kukata. Rongai hakuna mti wa kukata, Buhindi kama taratibu zitafuatwa tutavuna kwa miaka saba ijayo. Baada ya hapo tutakaa miaka tisa bila kuvuna. Maana tunavuna tu hatupandi. Hii si kazi ya Waziri, hii ni kazi ya Wataalam wetu waliokaa vyuoni miaka minne, mitano, wanasomea miti. Wao badala ya kuitibu miti, wanaiharikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la bei, sina matatizo kwa bei za nje. Maana hapa tumefananisha, Mkuruti kwa mfano, nje unauzwa dola 500 hivi sasa. Sisi kabla ya kupanda bei hii, tulikuwa tunauza kwa dola 50 mpaka 70 kwa mita moja ya ujazo. Hii ilikuwa tunajipunja sana. Lakini kwa matumizi ya ndani, mimi nafikiri tuna haja ya kuangalia upya na wale wanaosafirisha tu ndiyo wapigwe bei hii. Maana kwa laki mbili na nusu hajafikia hata nusu ya bei ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viboko waliozungumzwa wa Kilwa, si jambo la uongo. Tulimpeleka Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib. Ningeomba Waziri aende pale, kwa sababu siyo kila mtu atawaamrisha wale viboko watasimama. Kuna mzee fulani na vijana wake wakifa wale tutafanyaje. Tunatakiwa wataalam waende ili wakapate siri kwa yule mzee na wale vijana wake, mambo haya yaendelee. Hawezi kwenda Mheshimiwa Dewji akasema viboko salimieni, hawanyanyuki wala hawatoki mle kwenye maji. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, mimi nimempenda sana Msemaji Mkuu wa Upinzani leo, amejitahidi sana kuunga mkono baadhi ya maneno. Amenifurahisha sana pale mwishoni aliposema ujumbe huu tunaoutoa ni kwa wananchi kufahamu kwamba,

Wapinzani tunaweza; asiyeweza nani? Sisi pia tunaweza. Maana Viongozi wa Vyama vyote vya Upinzani walikuwa Viongozi katika Serikali hii. Ndiyo katika nchi hii hii. Kiongozi Mkuu wa Chama cha Msemaji wa Upinzani leo aliwahi kuwa mshauri wa uchumi wa Rais Mwinyi, hakuweza siku zile anataka kuweza leo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanadamu wanajikwaa kwa sababu ya kufikiria mambo ya miaka 50 ijayo. Maana unakuta mtu hana matatizo ya macho anajikwaa jiwe la kilo moja mpaka anatoa ukucha. Badala ya kuwaza pale alipo anataka kuwaza miaka 50 mbele. Ndiyo mtu anajikwaa anatoa ukucha. *(Makofi)*

Sasa mimi nakubali mnaweza. Lakini kuweza kwenyewe ni kwa fikra zaidi kuliko vitendo. Hatua inayofanywa na Waziri sasa, inapaswa kuungwa mkono na kila mtu na huku ndiyo kuweza. Wananchi sasa wataamua haya yanayofanywa kwa vitendo au yale yanayozungumzwa kwa ndoto tu za alinacha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy F. Owenya.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Nachukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, kwa hotuba nzuri, pia Naibu wake Mheshimiwa Zabein M. Muhita, kwa kazi nzuri na kwa hotuba nzuri.

Pamoja na hayo yote, ningependa kuwapongeza Wabunge wenzangu waliotangulia kwa hoja hii. Labda la ziada kwa upande wa misitu ni kwamba, hawa wanaokata misitu au wanaokata magogo, wanatumia magari makubwa mno kiasi ya kwamba, yanaharibu barabara za vijijini na hata zile za Mkoa. Kwa hiyo na hilo lizingatiwe ili kuona umuhimu wake, kukata magogo au kuharibu barabara. *(Makofi)*

Liwale ina eneo la *square* kilomita 39,000, asilimia 53 ya eneo hilo ni mbuga za wanyamapori za *Selous* au hifadhi ya wanyamapori. Idadi ya wanyamapori, nitatumia neno tembo, imeongezeka. Idadi ya simba na wanyama wengine pia imeongezeka. Kwa bahati mbaya kabisa, wanyama hawa malisho yao aidha ni wanyama wengine au binadamu. Tofauti na ng'ombe ambao Serikali imewaona wananchi wafugaji kwa macho yote mawili. Sijui tufanye baada ya muda, hawa wanyamapori watakapokuwa wamekosa malisho kwa mfano wengine, kama tembo au ndovu wanaharibu mazao yetu. Hivi sasa hawa tembo au ndovu pia huharibu mikorosho kiasi ya kwamba, kuwafanya wananchi wa maeneo ya Liwale washindwe kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiomba Serikali iweke mikakati mizuri, pamoja na ku-*support* utalii wa uwindaji pamoja na kuangalia vizuri zaidi wanyama, pia wachukue mkakati wa kuangalia hawa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kwa usalama wao na kwa usalama wa mazao zao. Hivi sasa utakuta Serikali pakitokea janga

la ina yoyote kwa mfano, wanaita wenyewe janga, tmbo watatu, wanne, watano wamekufa au wameuawa, wanatuma ujumbe mzito sana wa Serikali ikibidi ndege mbili au helkopta. Lakini Serikali hiyo hiyo, wakisikia wananchi mahali fulani Liwale au wapi, wameuawa na simba au mnyama mwingine wa aina yoyote, hakuna ujumbe wa ngazi hiyo unaotumwa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Sisi hatuchaguliwi katika majimbo yetu kwa kutumia wanyama hao, tunachaguliwa kutokana na wananchi wale ambao ndiyo wafugaji wakuu wa wanyama hao. Naomba Serikali itusaidie kuwa karibu sana kwa usimamizi wa wanyama hawa ili isiendelee kutoa madhara katika maeneo yetu.

Sasa hivi ng'ombe ambaye hata mfugaji anaweza akalala naye ndani, anatafutiwa *alternative* ya sehemu ya kwenda kula, nako ni huko Kusini, sasa wale simba watakapoongeza na tembo tutawapeleka wapi? Maana yake ninyi mko wengi huku Kaskazini huku labda tuwalete maeneo hayo halafu tuone kama hali itakuwa ni nzuri. Vinginevyo, Serikali ina umuhimu kabisa kuwajali wananchi wanaokaa katika eneo ambalo kuna wanyamapori wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilijaribu kuuliza swali Bungeni, ambalo lilihusu kutaka kujua vitalu vingapi vipo katika Wilaya ya Liwale. Jibu nililopata ni kwamba, vitalu vilikuwa 14, lakini kuna vitalu ambavyo tuna-*share* na maeneo mengine, hivi havikuhesabiwa. Kiasi kile tulichokipata cha asilimia 25, kinakuwa kila wakati hakibadiliki. Naomba Serikali iangalie, hii asilimia 25 sasa hivi imepitwa na wakati. Kwanza, kama ni kusakidia wananchi katika maendeleo, gharama za kufanya maendeleo zimeshaongezeka. Kwa hiyo, hiyo asilimia 25 sasa ingeongezeka ikafika hata 30 au zaidi.

Swali langu lingine lilikuwa kuhusu *GTZ,* ilikuwa ni shirika au ilikuwa ni *NGO* ambayo ilikuwa inasaidia sana wananchi wa Liwale kwa kuwasaidia wale wanaokaa katika mbuga za wanyama na pia kwa misaada mbalimbali.

Kabla hawajatoka, waliahidi kukarabati Boma la Liwale awamu kwa awamu. Walishaji-*commit* wangeweza kutoa milioni nane za kuanza kukarabati awamu kwa awamu ili jengo lile liendelee kutumika. Walivyotoka katika swali langu, niliuliza shughuli zile sasa zitafanywa na nani? Jibu ambalo nililipata mimi hapa ilikuwa ni kwamba, Wizara itashughulikia. Lakini tangu mwaka jana wakati nilipata jibu hilo mwezi wa sita, hadi leo hii sijaona Wizara, *Selous* wala Kurugenzi, kufuatilia suala hilo na sisi wenyewe tumewahi kuunda Tume yetu tukaenda mimi, Mkuu wa Mkoa, pamoja na *DC* wa Liwale, kwenda kumwona Mkurugenzi, kujua nini kinachoendelea. Lakini hatukupata jibu sahihi mpaka leo hii. Sasa naihimiza Serikali kwamba, yale yaliyokuwa yanaahidiwa na *GTZ*, ambayo pia mliahidi kwamba, mtayatekeleza, basi naomba muanze kuyatekeleza kwa Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali, kwa kuongeza kifuta machozi mpaka kufikia laki mbili. Lakini hawa wanaopewa kifuta machozi hiki ni wale tu ambao ni ndugu za wale marehemu waliouawa na wanyamapori. Naomba pia kiasi

hicho hicho kifikiriwe kwa majeruhi waliojeruhiwa na wanyamapori. Baadhi yao wana ulemavu wa kudumu, hawawezi kujishughulisha tena kimaendeleo. Kwa hiyo, ingekuwa vyema, tukaona umuhimu wa hawa ili waendelee kupata dawa au kujitibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili likikamilika pia, utatusaidia sana sisi ambao tunaendelea kufuga wanyama wenu kwa ajili ya utalii. Naomba kabisa Serikali ielewe kwamba, mwananchi anapouawa na mnyamapori au anapojeruhiwa na mnyamapori, isifanywe kama ni sehemu ya utalii. Kwa hiyo, kuna umuhimu kabisa mnapotoa kifuta machozi kama hicho cha laki mbili au zaidi, kwa waathirika na wanyamapori, naomba sana fedha hizo zitoke haraka. Sababu tukio linaweza kutokea leo ikabidi kazi ya Mbunge afuatilie wakati mwingine miaka miwili. Sasa inakuwa haiwezi kuwa kifuta machozi.

Kwanza, tayari hata walioathirika sasa idadi imeongezeka na si hivyo tu inakuwa ni kitu kama unadai. Sasa kama kweli kuna utaratibu huo, basi na ninyi wenyewe muwe macho kwa ku-*keep record.* Maana yake mimi rekodi ya wananchi walioathirika na wanyamapori katika Wilaya yangu ya Liwale ninayo. Lakini sidhani kama Mkurugenzi wa Wanyamapori anaelewa hivyo. Kwa kuwa hakuna hata siku moja yeye mwenyewe amekuja kufuatilia kwa karibu kama anakuja kufuatilia labda akisikia tembo wameuawa huko maporini. Kwa hiyo, kile ndiyo kinamkera zaidi kuliko maisha ya wananchi, kuliko mashamba ya wananchi. Naomba *atitude* hii ibadilike, ili nasi tuwe wachungaji wazuri wa wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Serikali iliangalie vizuri sasa suala la barabara. Katika swali langu tarehe 13 Juni, 2006, niliuliza swali la nyongeza kuhusu barabara ya kutoka Ulanga South mpaka kuja Liwale kupitia Ndapata. Jibu nililolipata niliambiwa kwamba, barabara hiyo itatengenezwa na Maliasili. Sijui anaweza kunieleza tumefikia hatua gani kutokana na jibu hilo ambalo mlinipa kwa wakati huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoamini ni kwamba, hakuna kilichoendelea. Basi bado naiomba Serikali, ijaribu kufuatilia zile ahadi au majibu ambayo yanatolewa hapa Bungeni na wanayasikia na tunapojaribu kufuatilia tunakuta tatizo au tunakuta utata unajitokeza mbele. Kwa hiyo, naomba kabisa aidha kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu au ninyi wenyewe kama mlivyoji-*commit,* naomba barabara kutoka Ndapata ambayo inatokea Liwale hadi Ulanga, ianze kushughulikiwa mapema iwezekanavyo vinginevyo, ku-*support* kwangu huku kwa 100% kutakuwa na mushkili.

Pia kwa upande wa uwindaji, naomba kabisa Serikali iwe macho, hawa wawindaji kinachofanyika wakati mwingine wanakwenda kwa wanavijiji na kuwapa fedha fulani kwa ajili ya ujenzi wa mambo fulani. Hizi fedha zinakuwa hazina rekodi maalum na wakati mwingine wana-*over invoice* wakati matumizi waliyofanya ni kidogo. Sasa mimi ningeomba kabisa pawe na sababu za makusudi kabisa, Serikali kuona kwamba, uongozi wa Wilaya, Mbunge, *DC* na uongozi mzima katika Wilaya husika, washirikishwe kikamilifu vinginevyo, wananchi watakuwa wanasaidiwa kiujanja ujanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Halmashauri yenyewe inakuwa haijui, naomba sana Serikali ilifuatilie hilo na tuko tayari kushirikiana nanyi kwa haya yote ili mradi tu pawe na utaratibu mzuri.

Nachukua fursa hii, pia kumpongeza Naibu Waziri, kwa kuwa aliwahi kutembelea Liwale na sasa hivi namwomba Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, achukue hatua kama hiyo. Ili uje ujumuike nasi tunaopata shida kutokana na wanyamapori ambao wewe ndiyo Wizara yako, wewe ndiyo mdhamini mkuu. Utatupa ushauri zaidi na pia unaweza kutoa jicho la huruma kwa yale ambayo utayaona maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo yote, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia tena. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Kabla sijasahau, naomba kueleza kwamba, mimi ni mdau wa utalii na nime-*specialize* kupandisha watu Mlima Kilimanjaro. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nimshukuru Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa hotuba hii. Vilevile napenda nimpongeze Msemaji Mkuu wa Upinzani, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mungu, Tanzania tumejaliwa rasilimali nyingi sana ambazo ni *unique.* Hivyo, Sekta ya Utalii ni mojawapo yenye vivutio vingi vya utalii na vilevile inabidi ili tuweze kuendeleza utalii huu, lazima uwe endelevu na kutunza mazingira yetu.

Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, alipokuwa anachangia aliongelea kuhusu Mlima Kilimanjaro na mimi nitauzungumzia Mlima Kilimanjaro lakini kwa upande mwingine wa tofauti. Mlima Kilimanjaro pamoja na watafiti wengi wamekuwa wakisema kwamba, barafu inayeyuka, hili siyo jambo ambalo litafanya watalii wasije kupanda ule mlima. Bado historia itakuwa pale pale, watalii mimi nafikiri tena watakuwa ni wengi kwa sababu watakuja kutembelea mlima ambao ulikuwa na barafu na sasa hivi hauna tena barafu. Kwa hiyo, kazi yetu tuendelee kupanda miti kwa wingi, tutunze mazingira ya Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoongelea mwanzoni, Mlima Kilimanjaro unaliingizia Taifa fedha nyingi sana. Kutokana na Ripoti ya Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa ukurasa wa 120, Kilimanjaro kwa mwaka jana iliingizia Taifa shilingi 26,600,169,523. Hizi ni fedha nyingi sana. Lakini cha kusikitisha katika Mlima Kilimanjaro *rescue service* siyo nzuri kabisa. Mawasiliano ni mabaya. Kwa mfano, mtu akipanda mlima, bahati mbaya akaanguka kule kwenye barafu akavunjika mguu, kupata *rescue* inaweza ikachukua zaidi ya hata saa kumi. Gari inabidi itoke Marangu ije mpaka kule Shira II.

Pamoja na fedha nyingi wanazozipokea *KINAPA*, nashangaa kwa nini wasinunue helkopta ya ku-*rescue* watu hawa? Inabidi sisi *tour operators* tujaribu kupiga simu Nairobi kupata helkopta wanakodisha kwa dola mpaka 4,000. Je, *KINAPA* haiwezi kununua hiyo helkopta na ikawa inapakia pale *Airport* ya Moshi iweze ku-*rescue* hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kusema kwamba, itatangaza *CCN* watakuwa wengi. Kuhusu kupanda Mlima Kilimanjaro, zipo njia za Rongai, Machame, Marangu, Londrosi na Limosho. Watalii watakuwa ni wengi sana. Kuna ile njia ya kupitia Old Moshi imefungwa. Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuifungua njia ile pia wageni waweze kutumia ile njia ya Kilimanjaro na vilevile barabara zinazokwenda mpaka *Gate* hizi za Umbwe, Londrosi, Machami na Rongai ni mbaya sana. Kwa nini sasa Serikali isitengeneze barabara zile ziweze kupitika wakati wote na wazitengeneze kwa lami si changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Madini tumeona kwamba, wananchi wa Halmashauri husika huwa wanafaidika na zile fedha wanapata dola 200,000 kwenye zile Halmashauri. Lakini sasa kwenye Mlima Kilimanjaro, ningependa Waziri atueleze wale wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro kwenye Halmashauri husika, wanafaidika vipi na fedha zinazopatikana kutokana na mlima ule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia kuhusu wawekezaji. Sasa hivi kuna *tour operators* wanaotoka ng'ambo wanakuja kuwekeza kwenye Mlima Kilimanjaro, sijui wanawekeza nini pale. Kwa sababu unakuta mtalii ana-*package* ya watu labda 50, anawachukua kutoka Marekani au *Europe* anakuja anawapandisha mlima. Fedha anazipokea kule kule Marekani, anachokileta hapa ni *park fees* tu na fedha kidogo za kulipia mafuta na *guides,* lakini pesa nyingine zile zilizobaki zote zinabaki kule kule kwenye nchi yao. Sasa hata kule Himalaya, biashara kama hii inafanywa na wale *local tour operators;* kwa nini *local tour operators* wasifanye kazi hii halafu wale wanaotoka ng'ambo wakawapa *local tour operators* na Serikali itakuwa inapata mapato zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu sasa hivi wameleta mtindo mwingine, walikuwa wakija wananunua vyakula hata wale akina mama sokoni Mbuyuni na wapi wanafaidika, wanunua matunda wananunua kila kitu kutoka kule sokoni. Sasa hivi kwa sababu ya kubana *porters* wale wachache, wanaleta vyakula vya makopo, wanaleta hata hizi *energy bars* wanaleta kutoka huko. Kwa hiyo, unakuta hata wale wanawake wa pale Moshi Mjini hawafaidiki na watalii wanaokuja pale Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na msisitizo wa kuendeleza utalii zaidi kule *Northern Circut* na kwa sababu watalii watakuwa ni wengi, nafikiri Serikali ni wakati muafaka sasa kuhakikisha kwamba, hii Wizara inashirikiana na Wizara ya Miundombinu ili waweze kutengeneza barabara huku *Sourthern Circut,* hata barabara za kwenda mpaka Kilwa, Kigoma, kuna *Gombe National Park* waende mpaka Bagamoyo kuna sehemu nyingi tu. Sasa hivi kuna hii *Beach* ambayo ni Saadan, unaweza ukaona wanyama mpaka

kwenye *beach;* kwa nini kule kusiendelezwe? Mheshimiwa Waziri, atakapojibu naomba atueleze kuhusu hiyo.

*Tanzania Tourist Board,* kwa kweli wanajitahidi sana, wakati tunakwenda kwenye *exhibition* nje wanatoa *promotion materials*. Wanatoa hizi *tarrif*, vipeperushi, lakini bado fedha wanazotengewa ni chache sana. Hawawezi ku-*exhibit* kwenye maonesho yote duniani. Unakuta kwenye *pavilion* nyingine hata zile *material* unakuta mgeni anakuja unampa vitabu, unampa *information* kuhusu Tanzania, anakuuliza sasa niweke kwenye begi gani?

Mwingine anatoa bahasha, mwingine anatoa mfuko wa rambo, mwingine hivi, haiwi *uniform.* Lakini hawa wengine unakuta wana *uniform,* hata akitoka nje na lile begi limeandikwa Tanzania, kila mtu anajua hapa tunauza Tanzania. Kwa hiyo, nafikiri *Tanzania Tourist Board,* waongezewe fedha zaidi ili waweze kutangaza na tuweze kuwa na banda lenye hadhi na nzuri kwa wateja kuweza kulitembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia kuhusu *local tourism.* Zinatakiwa zifanyike jitihada nyingi sana ili tuweze ku-*promot local tourism.* Watu wengi sana wako hapa Tanzania, lakini hawavitambui vivutio vyetu. Ningependa Mheshimiwa Waziri na mimi nikiwa kama mdau, tuangalie ni jinsi gani kwa kuanzia tu, tuwapeleke Wabunge kutembelea mbuga zetu, pia waje wapande mlima. Kupanda mlima mimi nitaweza kuwapandisha kwa bei nafuu kabisa.

Kwa sababu ninao *well trained and experience guides* na mapota wangu tunawalipa vizuri sana. Kwa hiyo msiwe na wasiwasi kuhusu *safety,* mkija tutawapandisha na Waziri atanisaidia, ili wakiweza kurudi kwenye majimbo yao, wakahamasishe watu kutembelea vituo vya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kidogo kuhusu magogo, tumeona kwenye vyombo vya habari kila mtu anazungumzia kuhusu ukataji wa magogo. Sasa pia Mheshimiwa Waziri, amekubali kwamba, kuna wafanyakazi ambao wako kwenye Wizara, wanahusika na biashara ya magogo, sisi hii si itakuwa ni *conflict of interest* kwa nini Wizara isishirikiane na Wizara ya Biashara, hawa watu wanakata magogo na kusafirisha nje kwa nini wasitengeneze hivyo viwanda hapa Tanzania? Wahamasishwe wajenge viwanda vyao hapa Tanzania, *furniture* zinaweza zikatengenezewa hapa Tanzania, hata huku ndani ya Bunge hizi *furniture* zote hizi zimetoka China, pengine magogo haya yalipelekwa China yakarudi hapa. Kwa hiyo, naomba wajaribu kuwahamasisha wafungue viwanda hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda nimpongeze Waziri kwa dhati kabisa, kuweza kufuata ushauri wetu tulioutoa mwaka jana na mwaka huu hotuba yake ikawa nzuri sana. Wachangiaji waliopita wamesema wanaweza, lakini tangu mwanzo wa kuchangia mpaka mwisho wa kumalizia kuchangia, alikuwa analalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu, juu ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilipokuwa nikichangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii, nilianza mchango wangu kwa kuonesha wasiwasi kwamba, bajeti ya mwaka jana ya Wizara hii, ilikuwa ni ndogo kiasi kwamba, utekelezaji wa kazi wa baadhi ya idara kama Idara ya Wanyama Pori na taasisi kama vile Bodi ya Utalii Tanzania, *TAWL* na *TAFOL,* zisingeweza kufanyika kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu nitaanza mchango wangu kwanza kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, Naibu wake, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Katibu Mkuu, Ndugu Blandina Nyoni, Wakuu wote wa Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa kufikisha mbele ya Bunge lako Tukufu, bajeti nzuri inayoeleweka na inayoleta matumaini ya utekelezaji mzuri na wa tija wa kazi za Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utangulizi huu, napenda kuunga mkono asilimia mia moja na zaidi bajeti hii. Pamoja na kuunga mkono bajeti hii, napenda nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kupandisha viwango vya ada za uvunaji wa maliasili wa nchi yetu hasa za mazao ya misitu na wanyama pori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka nimpongeze kwa dhati kabisa, Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe na Naibu wake, kwa kuonesha ujasiri katika suala hili. Baadhi ya watu wa hapa ndani ya nchi na nje ya nchi, walishaifanya nchi yetu kichaka cha kuvuna maliasili zetu kwa bei ya kutupa na kuiacha nchi hii ikiendelea katika kundi la nchi maskini duniani na wao wakiogelea katika dimbwi la utajiri uliokithiri. Mheshimiwa Waziri, amedhihirisha dhamira ya kuhakikisha maliasili ya Tanzania sasa inavunwa kwa heshima na kwa kiwango cha fedha kinachostahili. *(Makofi)*

Jambo ambalo wengi walishajaribu wakashindwa na kukumbwa na misikukosuko mingi, hapa naomba ninukuu usemi wa Baba wa Taifa, alioutoa mwaka 1961 kabla nchi yetu haijapata Uhuru. Kwa ridhaa yako naomba ninukuu: “Kudumisha uhai wa wananyamapori wetu ni suala linalotuhusu sisi sote katika Afrika. Viumbe hao wa porini pamoja na mapori wanamoishi, sio kwamba ni muhimu kama mambo ya kustaajabisha bali pia kwamba ni sehemu muhimu ya maliasili na ustawi wa maisha yetu siku za baadaye. Kwa kukubali dhamana hii ya kuhifadhi wanyama wetu, tunatoa tamko la dhati, kuwa tutafanya kila tuwezalo, kuhakikisha kuwa wajukuu wa watoto wetu, wataweza kufaidi utajiri na thamani ya urithi huu.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, ada hizi mpya zilizotangazwa hazitoshi, zinatakiwa kuongezwa, nchi hii imekosa mabilioni ya pesa kwa muda mrefu sana. Lakini kinachostaajabisha, baadhi ya watu ndani ya Serikali ambao wamo ndani ya Serikali kwa muda mrefu sana, walikuwa wakipinga kupanda kwa bei hizi. Leo hii wapo

humuhumu ndani ya Serikali na wanatuletea ongezeko la hizi bei. Mimi ningeshauri wale wote waliohusika kwa namna moja au nyingine, mwaka jana tulichangia hapa na walipinga na kutoa sababu lukuki. Leo wamo humo humo ndani wanaleta mapendekezo mapya na ambayo kwa kweli tunayapongeza lakini ni wajibu wawajibike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine ambalo ningependa nimshauri Mheshimiwa Waziri, alishughulikie haraka iwezekanavyo, nalo ni la wawekezaji wenye mahoteli na *camps* katika Hifadhi za Taifa, Ngorongoro na baadhi ya mapori ya akiba. Watu hawa wamekuwa wakilipa *concession* kwa taasisi hizi za ajabu sana. Wakati wao waki-*charge* mathalani chumba shilingi laki tatu au dola 270 au 300, lakini wamekuwa wakilipa si chini ya dola kumi kwa kila mgeni anayelala kwenye hiyo hoteli. Wakati huo hawagharamii kitu chochote, si barabara zinazoelekea kwenye hoteli zao, si kuondoa maji machafu katika hoteli zao. Sasa hii ni biashara ya namna gani, taasisi hizi zimejitahidi kwa muda mrefu sana kuhakikisha kwamba, wanalipa kiwango kinachostahili lakini kwa kigezo kwamba wao ni wawekezaji wamekuwa wakikikataa. Sasa jambo hili namwomba Mheshimiwa Waziri, alishughulikie haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichangie suala la maendeleo ya utalii hapa nchini. Sekta ya Utalii nchini ikipewa umuhimu unaostahili, inaweza kuliingizia taifa letu Pato kubwa la Taifa zaidi ya asilimia 16 inayochangia hivi sasa. Ninaipongeza Serikali kwa mara ya kwanza, kwa kuongeza bajeti ya Bodi ya Utalii Tanzania. Mwaka huu walau inakaribia shilingi bilioni tatu, nina hakika bodi ina uwezo wa kufanya hiyo kazi na chini ya uongozi wake Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, mambo yatakuwa mazuri. Lakini wasiwasi wangu ni ule msisitizo wa Serikali kwamba, tutumie balozi zetu kutangaza vivutio vyetu vya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili haliwezekani, watumishi wengi wa balozi zetu, *training background* haikuwa kwenye biashara ya utalii na biashara ya utalii ni biashara nyeti, ambayo inahitaji mtu anayeifahamu na kutoa *proper ethics.* Nimezunguka balozi nyingi, mambo ya utalii hawana habari, wapo kwenye *diplomatic*. Sasa hili tutaimba hapa, hakuna kitakachofanyika. Mimi ningeshauri pesa hizi zilizopatikana, zifanyike *road shows* nyingi katika nchi ambazo zinaleta watalii Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nizungumzie suala la uwekezaji na hususan wa mahoteli katika hifadhi zetu. Kimsingi naunga mkono kwa asilimia mia moja, wazo la kujenga hoteli za nyota tano katika mbuga hizi. Lakini hakuna nchi duniani ambayo imejenga utalii endelevu kwa hoteli za nyota tano, kwa sababu hoteli za nyota tano, zinalenga wageni. Nchi yoyote hapa duniani ambayo imefaulu katika utalii, imetegemea sana utalii wa ndani na kwetu sisi Watanzania na majirani, hoteli za nyota tano nani atakwenda kukaa huko? Likitokea tatizo dogo sana la watalii kutoka nje wasije hapa nchini, hifadhi zetu zitakufa na pato letu litakwenda chini. Zitolewe nafasi kwa Watanzania wenye uwezo, mbona tukienda Arusha tunalala Kibo Paris, hii ni ya Mtanzania lakini hapati nafasi ya kuwekeza ndani ya *National Park*, ndani ya pori la akiba kwa sababu gani? Sasa hivi Arusha lipo tatizo kubwa, Mawakala wa Utalii wa Tanzania hawana nafasi kwenye biashara ya utalii, kwa sababu hoteli zote za nyota tano zilizoko Serengeti zimekuwa *booked* na watu wa nje. *(Makofi)*

Tunawasaidia vipi, turuhusu Watanzania wapewe kipaumbele, ijengwe hoteli moja ya nyota tano, tatu za nyota mbili au tatu hizi zitakaa hata kwa ajili ya Watanzania na Wazungu ambao hawana uwezo kulipia nyota tano. Tuwasaidie Watanzania wapate nafasi ya kuwekeza, Arusha pale wapo akina *Leopard Tours*, wana uwezo wa kuweza kujenga, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro hapa ana uwezo anaweza kujenga; kwa nini wasipewe? Watanzania wengi wataenda kuishi watakaa kwenye Hoteli ya Mtanzania mwenzao kwa sababu wanamfahamu, wanazungumza lugha moja na chakula wanaweza kutengenezewa cha Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Namwomba Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, atakapokuwa anahitimisha bajeti yake, anieleze ni mkakati gani wa makusudi, Wizara inauweka katika ku-*balance* uwekezaji ndani ya maeneo ya Hifadhi za Taifa na Pori ya Akiba. Lengo ni kuhakikisha kwamba, tunajenga utalii endelevu, ambao hautegemei tu Wazungu na watalii kutoka nchi za nje. Nchi zote hizi, South Africa, hata Kenya hiyo Masai Mara, ambayo watu wanaizungumzia, si kitu chochote ukifika kule ndio maana hata hao wanyama hawaendi kule kwa sababu wamejaza mahoteli. Mimi nimefika Masai Mara zaidi ya mara tatu, wanyama hawaendi kule kwa sababu kila sehemu *five star hotel,* mataa kibao, wanyama wanaogopa taa usiku. Sasa tuendeleze yale ambayo Mwalimu alituachia, Serengeti ni ya kwetu *and Serengeti should not die during this time.* Serengeti ni kubwa, ina kilomita za mraba 14,000, zaidi ya Wilaya inahitajika kupanuliwa, lakini tupanue kwa utaratibu ambao itafanya iendelee kuishi miaka yote na wajukuu zetu waishi. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii, niweze kuchangia mawili, matatu. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu mpya, Mama Blandina Nyoni, karibu sana kwenye Wizara yetu ya Maliasili, Wizara yenye mambo mengi na wewe akili iwe timamu katika kufanya shughuli zako, usije nawe ukaingia kwenye malumbano, fanya kazi zako kulingana na taratibu na sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, naomba kwanza, niungane na maelezo yote na mapendekezo yote, pamoja na maoni tuliyotoa katika Kamati yetu ya Maliasili na Mazingira. Naomba Wizara iyaangalie na iyafuatilie sana, kwa ukaribu na taratibu zote. Yale yaliyoongelewa na Waheshimiwa Wajumbe wenzetu, yenye kuweza kunufaisha Wizara hii kwa maslahi ya Watanzania, basi naomba sana waweze kuyafuatisha.

Nataka kuanza kidogo tu, nitaanzia kwanza kwenye Idara ya Wanyamapori. Naomba niipongeze Serikali kwa kuweza kupandisha viwango hivi vya ada ya mazao yote yanayotokana na maliasili zetu. Kidogo tu nilikuwa nataka kusema, bahati mbaya hili wazo nimelipata hivi karibuni kwamba, katika ukataji wa leseni, sisi Tanzania tuna hulka ya kutoa *package* leseni kwa *package* kwamba, leseni unapewa wanyama wanane, sita au kumi. Nilichokuwa naomba, hivi hatuwezi kufanya kila mnyama akawa na leseni ili kuongeza mapato, hebu wataalam wakae waliangalie hili ili waweze kulitafakari kama linawezekana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye masuala yetu hususan ya uvuvi, Mafia ni eneo ambalo limezungukwa na bahari na bahati nzuri, tuna ukanda mzima nusu ya eneo la Wilaya ya Mafia, limezungukwa na hifadhi ya bahari. Hivyo, basi naomba niipongeze Serikali kwa kutumia hata vyombo vingine vya dola, kuweza kudhibiti uvuvi haramu uliokuwa unaendeshwa na baadhi ya watu ambao wanatoka nje ya Wilaya yetu ya Mafia. Naomba kuiomba sana Serikali na wale waliokuja kufanya *operation* zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Mradi wa Maseno, bahati nzuri wao wenyewe katika taarifa zao na makongamano na warsha walizokuwa wakitoa na sisi tulikuwa tunapita kuwaeleza wananchi kwamba, sasa unakuja mradi mzuri, mkubwa, wenye fedha nyingi, ambao unazaidi dola milioni 61, ambazo zitakuja katika kuhakikisha kwamba, zinawasaidia wavuvi na kuwasaidia wengine wote ambao wanakaa katika eneo la ukanda wa Pwani, pamoja na Visiwa vya Uguja na Pemba, kuweza kuondokana na umaskini na kuweza kuwasaidia kuwapatia zana ambazo wao walikuwa kama wananchi, hawana uwezo nazo, basi mradi huu ungekuja kuwasaidia. Ninaamini kwamba, pesa hizi ni nyingi sana, zaidi ya shilingi bilioni 70, nafikiria kwa wilaya 14 zilizokuwa katika Ukanda wa Pwani huu, basi umaskini ungeondoka katika eneo hili na watu wakaweza kujifananisha na hao wanaoambiwa wanatoka katika maeneo tajiri. Kwa hiyo, naomba sana huu Mradi, Mheshimiwa Waziri uuangalie, leo una miaka miwili na umefanya kazi katika Wilaya tatu, Mafia, Kilwa na Rufiji. *(Makofi)*

Lakini hebu tuangalie katika matumizi yaliyotumika katika kuwasaidia, yale ambayo wao wameyasema hivyo ni kweli katika miaka miwili hii ambayo kigezo kimetumika katika wilaya tatu, wananchi wamefaidika kweli kweli kupitia pesa hizi au tumekuja kudanganywa, maana hivi tunavyokaa na kuongea, sisi viongozi haswa wa kuchaguliwa tunaonekana kwamba, tuliwalaghai wananchi kwa ajili ya kutafutia kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa zilizotumika ni nyingi, dola milioni 51 ukijumlisha dola 10 ni dola 61; ukitoa hizo *percentage* kwamba, pengine sisi upande wa Tanzania Bara zingefika zaidi ya milioni 45 na nyingine zikaenda katika maeneo ya Uguja na Pemba. Lakini je katika zile wilaya tatu zilizokuwa zimefanyika majaribio ya mradi huu, hivyo kwa nini tumeshindwa kuwasaidia wale walengwa ambao ni wavuvi, wangeweza kuondokana na sasa hivi labda tuseme katika kumwondolea mtu uwezo wa kuweza kununua zana kamili za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kukusanya bei ya zana kamili ya uvuvi, thamani yake ni shilingi milioni 13 mpaka 15, unampatia mashine, unampatia boti, unampatia na nyavu zilizokubalika kisheria ili aweze kumudu kwenda katika maeneo yaliyokubalika na atapata samaki wakubwa aweze kuvua kila seti hiyo inaweza ikatumika kwa watu zaidi 30 ambao wanaweza na wao kuwalisha watu waliokuwa nyuma yao zaidi ya mia. Sasa hebu tuangalie jinsi umaskini utakavyoondoka, lakini hebu uliza mimi ninafahamu katika Wilaya yangu katika pesa hizi zilizotumika, maana yake

ukijumlisha milioni 50 ina maana kila mwaka zimetumika dola milioni 10, kwa maana miaka miwili ni dola milioni 20.

Sasa watuambie katika dola milioni 20, wilaya tatu hizi Mafia imefaidika kwa kuondoa umaskini na wananchi wameondokana na umaskini kwa kiasi gani, hali kadhalika Rufiji nao wameondoka na umaskini na wamesaidiwa kiasi gani na Kilwa imepata nini? Je, watakapoenea katika Wilaya nyingine watafaidika vipi kwa hizi pesa zilizobakia? Mimi mradi huu unatia mashaka na ninaona haya kwa sababu wale waliokuwemo katika Mradi huu ni watu mahili, wataalam na wanaelewa adha inayotupata watu wa Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana sana Mheshimiwa Waziri, aliangalie suala hili, sisi tunahitaji kuondokana na umaskini, pesa mmetuletea ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, ninyi Serikali ndiyo mtakaolipa kwa maana ya mapato wanayolipa Watanzania wote. Sasa isije ikawa kwamba, pesa hizi zitumike kwa watu wachache na wale walengwa wasije wakafanya jambo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hifadhi za bahari, nashukuru sasa hivi wameweza kuongeza maeneo yametamkwa hapa katika Visiwa vya Singa, Dar es Salaam na maeneo mengine ya Mafia na tunataka kuelekea pia katika visiwa vingine. Lakini naomba wakati tunakwenda kuangalia na kupeleka wataalam wetu, kupeleka maelezo kwa wananchi. Sasa hivi Mafia hifadhi ya bahari inachukiwa, ukienda Kilwa inachukiwa na ikitamkwa kwamba sehemu nyingine inakwenda inachukiwa kwa sababu gani, kwa sababu yale yanayotumika kuwaeleza wananchi yanakuwa wananchi wazuri lakini baadaye hakuna kinachofanyika. Mwisho wake, watu wanaambizana na kusema kwamba, Mradi huu hauna maana yoyote, unakuja kuzuia maeneo yetu ambayo tumezoea kuvua. Sasa naomba sana tutumie lugha nzuri na tuweze kuhakikisha kwamba, yale tunayoyasema sasa Serikali itoe pesa hizo kuweza kuwapatia wale walengwa. *(Makofi)*

Nimesikitishwa kwa taarifa za ghafla, ambazo nimezipata haswa wakati huu tukiwa tunaendelea kuweka maeneo haya ya hifadhi ya bahari kwamba, nini kinachoendelea baada ya kumwondoa Meneja wa Bahari, Ndugu Lunisha. Nasikia ameondolewa pale kwa nini tusiambiwe sisi kwanza kama Kamati, tukaweza kulielewa hili jambo na tuweze kufanikisha? Nini kilichosababisha; kuna tatizo gani? Mimi kama Mjumbe Bodi, sielewei na bahati nzuri nipo katika Kamati Ndogo ya ajira na Nidhamu, kwa nini msitueleze? Nimesema nitayaongea hapa ili jambo liwe la wazi na kama ana madhambi, basi tuweze kuyafahamu. La kama amesema ukweli lakini watu wanataka kulinda tuweze kuyajua. Naomba sana jambo hili tuweze kulifanyia kazi, tusioneane haya katika kuijenga nchi yetu hii. *(Makofi)*

Sina mengi ya kusema, ninachoomba Mradi wa Masemu, leteni pesa tuwape Wananchi wa Mafia, Kilwa, Rufiji, ukanda mzima wa Pwani, Visiwa vya Uguja na Pemba na sisi tuweze kuondokana na umaskini. Pesa ni nyingi na ninaamini nyingine zitabaki, magari yatanunuliwa, majumba yatajengwa na watu watafanya mikutano na pesa bado hata ukisema kwamba, zimebakia mwisho wa mwaka zitaweza tena kurudi Serikalini, tuleteeni bilioni moja tu, Mafia tutaondoa umaskini kwa Wilaya zima.

Hizo nne ambazo tumesema kama kila Wilaya ipate nne nne tu, basi moja itaweza kutusaidia na kuondoa umaskini, hizo tatu nyingine fanyeni makongamano, wekeni mawarsha, nunueni magari, jengeni ofisi, tuleteeni milioni 800 tu vijiji 20 tutaweza kununa seti 60 za uvuvi na kwa kila kijiji vitatoka vikundi vitatu vyenye 90 na umaskini utaondoka Mafia. Watu watavua kwa zana zilizokubalika na wataacha kuvua katika maeneo ya hifadhi na kwenda katika bahari kuu, ambayo ndiyo tunayopigia kelele kwamba, wageni watakuja kutumaliza sisi wenyewe tunawakodolea macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Wizara hii asilimia mia, lakini nataka nipate maelezo ya Mradi wa Masemu na Meneja wa Hifadhi ya Bahari, Ndugu Lumisha, nini kilichosababisha aweze kuondolewa pale ghafla. Asante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru wachangiaji wote waliochangia toka leo asubuhi, wametoa changamoto ya kutosha. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kutuletea hotuba nzuri leo hapa Bungeni.

Sasa ninaomba tu niseme Waheshimiwa Wabunge, nimekuwa nikipokea maombi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wengine, kila mtu akionesha umuhimu kabisa wa kutaka kuchangia mada hii kuwawakilisha wananchi wake. Sasa ninaomba nizungumze kitu kimoja, Waheshimiwa Wabunge wengi, wamekuwa wakiniambia mimi nimechangia mara moja tu, niseme tu kwamba, orodha ya waliokwishawahi kuchangia mara moja tu hapa Bungeni ni ndefu sana katika mada hii ya leo.

Sasa mpaka hapo tu tulipofikia, bado nimebakiwa na wasemaji kumi ambao wamechangia mara moja tu. Waliochangia mara mbili bado nina orodha ya wasemaji kama saba na kuna waliochangia mara tatu nao wanahitaji kuzungumza kwenye hotuba hii.

Sasa nilitaka kuweka wazi kwamba, baadaye tutakaporudi mchana, tutakuwa na wachangiaji wawili, lakini hebu nisome hao waliochangia mara moja waliobakia, halafu nitawaomba sekretarieti na nitaomba Meza ya Katibu, inisaidie kuniletea wachangiaji wawili ambao wataanza mchana na baadaye tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri.

Tunaye Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyacha, Mheshimiwa Luhanga J. Mpina, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi na Mheshimiwa Janeth Massaburi.

Waliokwisha kuchangia mara mbili kuna Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

Waliochangia mara tatu, Mheshimiwa Zitto Z. Kabwe na Mheshimiwa Michael L. Laizer.

Kwa hiyo, naomba tu mpate hiyo picha Waheshimiwa Wabunge na muone kwamba, labda tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri, mchana aweze kutoa ufafanuzi wa kina ili yale yote ambayo yangehitaji kufafanuliwa, yaweze kusikika kwa Wabunge wote. Vinginevyo, orodha ni kama hivyo nilivyoisoma.

Baada ya kusema hayo maneno machache, basi naomba Waheshimiwa Wabunge, nisitishe shughuli hizi mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 1 1.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kipindi chetu cha jioni. Kwa leo tutakuwa na wasemaji watatu na tutaanza na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi na tunamalizia na Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo jioni hii. Pili, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yao ya Wataalamu, ikiongozwa na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara moja ambayo kama kazi aliyoianza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, itasimamiwa vizuri, ninaamini uwezo wa kuchangia kwenye Pato la Taifa utakuwa mkubwa sana, hautapungua asilimia 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishukuru Wizara kwa kiwango kikubwa, ilizingatia ushauri ambao tuliutoa katika Bunge Tukufu, pamoja na kwamba, pengine viwango havikufika kule tulikofika, lakini nasema mwanzo ni mzuri na huo ndio uzalendo tunaouhitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1990 wakati wa Awamu ya Pili ya Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, tulikuwa na matatizo mengi sana, kwa ushauri alioupata Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, alianzisha neno ruksa na ndio mafanikio haya tuliyonayo. Kwa hiyo, washauri hawa waliomshauri tukapata neno ruksa, ndio leo sera hizi tunaziendeleza na hapa tulipo nafikiri ni kutokana na ushauri na kazi aliyoifanya Mzee Mwinyi wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefungua Kitabu cha *Revenue*, kwa bahati mbaya sana kwenye eneo la *fisheries,* bado mapato ni madogo mno na cha kusikitisha zaidi ni

kwamba, tulitegemea zile *economic zones* za *fisheries licenses* basi angalau zitakuwa zimebadilika, lakini mwaka juzi Serikali ilipata mapato ya shilingi bilioni 1.09 na mwaka jana wakapata shilingi bilioni 1.187, mwaka huu ambao tulitegemea kutakuwa na mabadiliko makubwa kuna *token figure.* Sasa hiki ni kichekesho kikubwa sana, mahali ambapo tuna meli zisizopungua 140 za uvuvi na tumetoka kutoka *one billion* tukafika 1.1 *billion,* leo tuna *token figure* ya 100. Nafikiri kuna tatizo la msingi katika mapato ya *fisheries*, ndio Kitabu cha *Revenue* hiki hapa kinavyosema. Sasa mimi naomba kama kuna mashahihisho, nitaomba yafanywe hayo masahihisho kwa sababu bado *Finance Bill* haijafika, mnaweza mkafanya masahihisho na Katibu Mkuu, bahati nzuri anafahamu sana mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika kitabu hicho hicho, kwa takwimu alizotoa Waziri kwa upande wa misitu, inaonekana kutapatikana kama 45 bilioni lakini kwenye kitabu cha *revenue* mapato yanaonekana kama ni 15.6 bilioni, napo nafikiri kuna matatizo au kutokea *adjustment* wakati wa *Finance Bill* tutaweza kuelewa. Haya aliyoeleza Waziri katika hotuba na yaliyoko katika Kitabu cha *Revenue* ni vitu viwili tofauti na hilo nafikiri linahitaji kurekebishwa au tupate ufafanuzi. Sasa ukiacha mapungufu hayo kwenye *revenue,* ningeomba hata kwenye *game licenses* vilevile kumeteremka kumekuwa na 122 milioni, sasa hivi tuna *estimate* 60 milioni, nafikiri hapa kuna matatizo ya kimsingi ya mapato kunahitaji kurekebishwa, hilo lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sisi tulikuwa tunashauri kwamba, Wizara hii ya Maliasili inaelekea kuna matatizo ya msingi ya watendaji na tunapata matatizo kwa sababu hata yale maamuzi yanayotolewa na Serikali, ukiona namna yanavyotekelezwa unapata ushahidi wa kutosha kwamba, kuna matatizo ya msingi na mimi ninawaonea huruma sana, Naibu Waziri na Katibu Mkuu. Kama Serikali haitakuwa *serious* kuwasaidia Mawaziri na hasa nasema *serious* kwa maana ya kichwa, Rais mwenyewe akaangalia na kuifumua Wizara hii, mapato hayawezi kuongezeka hata siku moja na ndio maana inafika mahali, tunatamka matamshi makubwa makubwa lakini utekelezaji unakuwa mdogo sana. Sasa mimi nilitaka kushauri mambo yafuatayo; la kwanza katika suala la ongezeko la bei za magogo, nakubaliana kabisa na wazo la Waziri, pendekezo aliloiletea hapa Serikali, lakini kuna vitu viwili lazima waangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Zanzibar, ukitaka kununua karafuu ukiwa mwenyeji utauziwa Sh.2,000 na ukiwa mgeni utauziwa Sh.4,000. Hapa Tanzania Bara tunahitaji kufanya hivyo hivyo, mbao anazonunua mgeni bei yake iwe tofauti na mbao anayonunua Mtanzania. Pengine gharama za uendeshaji wa Serikali zitakuwa kubwa, uwezo wa wananchi wetu kumudu maisha yao ya kila siku utakua mkubwa hivyo, kuna haja ya kutofautisha bei ambazo Mtanzania atanufaika nazo kwa matumizi ya ndani ya nchi na bei ambazo tutawauzia wageni kwa kupeleka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo itasaidia kuondoa huo utata unaotokea hivi sasa, kuona kitanda kitafika Sh.700,000, lazima tufike mahali tuwe na *identification,* tuseme haya ni kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi na kwa maendeleo yetu na haya ni kwa

ajili ya kusafirisha nje. Mimi nafikiri hilo litaweza kusaidia likifanyiwa kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tunarudia sisi kusema kwamba, kuna haja ya kufanya tathmini, huu uvunaji wa magogo tunaoufanya, tukiangalia na hali ya mazingira na joto linavyopanda katika Dunia ya leo, hivi tukiona manufaa na faida kuiacha hii miti yenyewe ikaendelea kuwepo na kuivuna; ni lipi bora? Hasa tukiangalia utaratibu tunaotumia hivi sasa kuivuna, ukisoma taarifa ya trafiki, kwa Wilaya ya Nachingwea au Mikoa ya Kusini, hali sio nzuri hata kidogo, watu wamevuna zaidi na matokeo yake, uwezekano wa kupata jangwa Tanzania upo karibu mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri ni vizuri tukafanya tathmini, tunahitaji kweli pesa za kigeni kutokana na mbao, lakini tunahitaji kutunza mazingira yetu ili vizazi vyetu vya kesho na kesho kutwa, viweze kuishi kwa usalama. Sasa nafikiri hili linahitaji vilevile kufanyiwa utafiti ili tujue kama kuvuna kwetu tunavuna kwa kiwango gain. Naelewa mnasema kwamba, tunatoa leseni wavune kiasi Fulani, lakini kuna *over harvesting* kila wakati, hata wale wanaochukua *tender,* upo ushahidi wa kutosha mtu amepata *tender* ya *cubic meter* 2,000 lakini anavuna 5,000, tunaielewa *corruption* ilivyo katika nchi yetu au ufisadi ulivyo. Sasa nasema kuna tatizo hilo la msingi linahitaji kuangaliwa kwa upande huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la nne ambalo ninataka kulisema ni suala la uvuvi. Ninasikitika sana katika Hotuba ya Waziri, uvuvi wa baharini amezungumza kidogo mno kana kwamba, haupo na kwa kweli haupo, hata viwanda unavikuta vingi viko kwenye ziwa haviko kwenye ukanda wa bahari. Sasa suala la kuanzisha *fish ports* wakati umefika, tuna Bandari ya Mtwara kubwa na nzuri, maji kina kubwa tu imekaa *idle* haina kazi na meli kubwa zote ziko ukanda huo. Ukiya-*call* pale ukawaambia lazima mje hapa tufanye tathmini mlichokivua ili tupate *reality* ndani yake, hiyo ni *income* kubwa na watu wa Mtwara watakuwa wamefaidika sana. Sioni sababu kwa nini hilo linashindikana, tumelisema na tunaendelea kulisema na tumetoa mifano ya nchi mbalimbali, wenzetu wanafanya na wanafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli hizi zinavua zinaondoka na bidhaa hatujui wanapouza, hatuna habari yoyote, sisi *charge* yetu ni leseni ya dola 18,000 ni aibu sana kwa nchi yetu, tunakosa mapato bila sababu ya msingi. Kwa hiyo, nilifikiri Waziri alifanyie kazi, wenzenu Zanzibar wana meli 70, Bara kuna meli kama mia moja na kitu, zinahitaji kufanyiwa kazi tupate *revenue* za kutosha, bahari yetu inakaushwa kabisa. Wavuvi wetu wadogo wadogo sasa hivi walikuwa wanavua kwenye *shell water,* wakapata samaki sasa hivi inabidi waende ndani zaidi kupata samaki, kwa sababu meli kubwa zinavua zaidi kiasi kwamba, hata wavuvi wetu wadogo wadogo kuwakosesha samaki. Ninafikiri hili lingeangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni lile alilosema Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah kwamba, fedha nyingi zinatolewa za misaada mbalimbali lakini fedha hizi nyingi zinamalizikia kwenye warsha, semina, matembezi na magari, haziwafikii walengwa hata kidogo. *Billions* nyingi zinazotolewa hizi, ukichukua hesabu tu

aliyofanya Mheshimiwa Shah hapa ya milioni 13 kwa chama cha ushirika cha uvuvi wa kukabidhiwa, tungekuwa vyama vingi vya ushirika vya uvuvi wakavua samaki tukaondoa tatizo la lishe, tukaondoa tatizo la ajira, lakini fedha inamalizikia kwenye misafara, semina, pamoja na manunuzi ya magari na vifaa vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza, naomba kuunga mkono hoja, asante sana. *(Makofi)*

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nishukuru kwa kunipa nafasi adimu ili kuweza kuchangia katika Wizara hii. Kwanza, nawapongeza Mawaziri, kupata nafasi hii pamoja na Katibu Mkuu, nakuomba Katibu Mkuu, umeingia katika Wizara ambayo ina matatizo mengi, lakini mdogo wangu shika uzi ule ule, uweze kufanya kazi zako vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na tatizo la Wakurugenzi katika Wizara hii, Kurugenzi ziko nyingi lakini mimi nafikiri Wakurugenzi wanakuwa kama ndio wenye Wizara. Ikiwa Mkurugenzi anaweza akakataa amri ya Wizara mpaka kwenye magazeti ameandika kwamba, sing'oki ng'o, hivi kweli kuna Wizara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana Wizara hii sote ni kambare, mkubwa na mdogo wote wana ndevu. Utawala Bora uko wapi? Nilishtuka sana kuona hali hii inajitokeza na ndio maana Wakurugenzi katika Idara hiyo ya Wanyamapori, wengi wana *degree* lakini hawana utaalamu wa wanyamapori. Kwa sababu kisheria tunasema hivi, *knowing the law is one thing, practicing is another*. Sasa kama hawa wangeweza kupelekwa katika Chuo cha Mweka, wakaenda wakaona kazi inayofanyika wakapata mbinu za kufanya hiyo kazi, pamoja na *degree* walizonazo lakini wakiwa wana utaalamu hasa wa kazi yao, nafikiri hizi idara zingeendeshwa vizuri. Naomba maelezo kama kweli huu ubabe upo, kazi itaenda vipi katika Wizara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana, hata nchi za nje wanasoma haya magazeti wanaona kwamba, hii Wizara inashindwa kweli kuweza kumdhibiti Mkurugenzi, watu wakaa miaka 20 tunakuja kugomba hapa Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata. Tulizungumza kwenye TAMISEMI, Watendaji wa Kata wengine wamekuwa wenyeji mno, hawa maafisa wa kilimo wamekuwa wenyeji mno, waondoke kwa sababu wanazoeana na wanavijiji, hapo tukashambulia kweli kweli Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba, angalau mtu akikaa miaka minne au mitano, aondoke ili asijenge mazingira ya kuzoea mahali, kwani ufanisi wa kazi unapungua lakini Kurugenzi za Wizara ya Maliasili ndio kwao, anakulia pale pale atakuwa na ufanisi kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana huu ubabe wameuonesha, sing'oki ng'o na kweli hajang'oka, sasa sijui Wizara watatuambia nini? Sina matatizo na Waziri, nina matatizo na utendaji wa kazi, tunaenda vipi, kuna sera gani, kuna utaratibu gani, *good governance* iko wapi kwa ufanisi? Naomba maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu magogo, wamerudia sana wenzangu. Jimbo langu la uchaguzi, magogo yanabebwa lakini manufaa ya wananchi kuhusu magogo haya, haionekani. Naomba anifafanulie pale wanapochukua haya magogo, *output* na *input* inakuwaje? Tunaathirika sana na magogo mwisho kutakuwa jangwa, tutakosa hata kuni za kuchomea tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu *claims* za wawindaji, mimi naziunga mkono sana hizi *claims* kwa sababu wanatuletea hela za kigeni na wawekezaji wanatusaidia katika *revenue* yetu. Lakini tatizo la kusikitisha linalojitokeza katika jimbo langu la uchuguzi ni kwamba, kuna Mbuga ya Nyahuwa, ambayo tunaambatana na Sikonge na Manyoni Magharibi kidogo na Uyui kwa maana ya Jimbo la Igalula. Mbuga hii kibali walipata Wizarani, wamekuja kuripoti Wilaya ya Sikonge, Kambi yao iko katika eneo langu la Jimbo la Igalula katika Kijiji cha Malongwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi waliyoifanya hawa wawindaji wamefika pale hawana habari na Mwenyekiti wa Kijiji, wala Mwenyekiti wa Kata na wala mtendaji, wakaanza kuweka kambi zao. Sasa bahati mbaya, kwa wao bila kujua kwamba, kule wamekuta watu lakini bahati nzuri uchumi wa Jimbo langu la Igalula moja ya kupata pesa ni asali na miti hii ndio inatoa asali *the best* katika nchi. Ukipata asali nzuri yenye rangi nyekundu nyekundu hivi, ndio asali nzuri inayotoka Jimbo langu la Igalula. Wametundika mizinga yao bila kuathiri miti, bila kuathiri wanyama, ndio uchumi wao ambao wanautegemea Tura, Malongwe, Kizengi, Nyahuwa, lakini matokeo yake hawa wawekezaji wameingia pale wakafika wakakuta watu wanaingia katika kutengeneza mizinga yao basi wanaondolewa tokeni.

Wale wanashangaa kuona Wazungu wameingia pale hawana taarifa, wakauliza kwenye Serikali yao ya kijiji hawana taarifa basi Mtendaji wa Kata alipokwenda pale alifukuzwa kama mbwa *get out, get out,* bila hata heshima kwamba, huyu ni binadamu kasoro rangi tu tunatofautiana. Hawa ndio wenye nchi, hawa ndio wenye ardhi pale, hawa ndio wakazi wa hapa; waende wapi? Hatukatai kabisa kwamba, Serikali muweze kuwapa maeneo hayo, lakini kwa nini hatufuati utaratibu, *good governance* iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema madaraka kwa wananchi, yako wapi madaraka yao katika uwekezaji huu wa hawa wawindaji, wamepigwa viboko, wamepigwa na matako ya bunduki, wamebomolewa midomo, wamevunjwa miguu mpaka wananifuata hapa watu 20, mama tunakufa, nakuja kuulizia wana kibali kutoka Wizarani wameripoti Sikonge. Sikonge pale wanaripoti wanaingia hawajui mipaka ya Wilaya iko wapi na sisi tunaingiliana katika shughuli za uwekezaji, lakini ingawa hatuendi kulima wanawekeza mizinga hii. Wananchi wangu si chini ya 30 au 40 wamepata maumivu hayo. Anakuta huyu Mzungu anapiga risasi mzinga na asali inamwagika, anakuta debe la asali limewekwa pale, anachukua anamimina asali anaondoka nayo, wanafukuzwa na kuitwa kama mbwa kwamba, sisi ni wawekezaji, hivi kweli tunafika wapi ikiwa mwananchi huyu tunataka kumsaidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Wizara inieleze baada ya matatizo haya, ingawa Kamati ya Ulinzi na Usalama ilienda, wale Wazungu ilisadikiwa waliomba radhi,

kuomba radhi lakini athari iliyopatikana nani atakayeilipa? Naomba Serikali iwalipe wananchi wangu mizinga yao iliyoharibiwa na inisaidie wale wote ambao wamepata maumivu waweze kutibiwa kwa gharama ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ndugu zangu inanisikitisha, hawa ndio wapiga kura na wapiga kura hao ndio ambao wamesaidia tukapata Serikali, wameongeza kura kwenye Serikali na leo tunaringa wana-CCM tuko hapa, lakini hao ndio ambao wamefanyiwa madhara haya. Ninaomba sana, sina matatizo na Waziri, Naibu na wala Katibu Mkuu, nina matatizo na kazi iliyofanyika katika Wizara yake. Kwa sababu ya kuogopa hawa Wakurugenzi, nafikiri labda Wizarani mambo ni yale yale, kama Mkurugenzi anaweza kutoa tamko la ajabu ajabu; je, hapo Wizarani si ndio hakuna mtu anayepumua kila mmoja anaenda kivyake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba ndugu zangu mimi nipate jibu, wapiga kura wangu wamekuja wapo hapa wananisubiri; nani atawalisha? Wapate jibu leo la Wizara hii. Sasa hivi hizi *claims* zimewekwa, wananchi wetu hawana namna ya kupata faida na mapori yao kwani mbao kuna watu wenye *license*, nyama hawawindi kwa hiyo, hata wananchi hawali nyama ya porini, kwa sababu wamewekwa pale, ng'ombe wenyewe ni matatizo kama hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu mwananchi ana faida gani na pori lile hana faida ya mbao, hana faida ya wanyama, anafukuzwa kwamba *claims* inaleta fedha za Serikali lakini yeye mwenyewe hafaidiki wala haoni faida ya kuwa na pori lile katika eneo lake, sasa wakale wapi? Kwa sababu wengine siyo wafugaji, ina maana wale mlenda kila siku, nyama za pori; ndio *claim* imeshawekwa na wanafukuzwa kwa mtutu wa bunduki, inasikitisha kwenye jimbo langu. Jimbo la Tabora Vijijini, Jimbo la Uyui na Jimbo la Igalula. Ninaomba nipate majibu la sivyo, hawa wapiga kura kesho ninawaleta ofisini, muweze kuwapa namna ya kuwatibu na muweze kuwapa namna mtakavyolipa hasara waliyoipata, kuombwa radhi si suala, suala ni manufaa ya hawa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba kuwasilisha haya lakini kabla hatujamaliza, mnieleze ili angalau nikalale usingizi na hawa wapiga kura wangu nione wamepata faida gani ya kutibiwa maumivu yao na kulipa asali ambazo wameibiwa na nyingine mizinga kupigwa, kwa sababu ya uwekezaji, *claims* za wawekezaji hazina faida kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hayo yajibiwe, asante. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu, akifanya majumuisho ya bajeti yake, aliweza kutoa maamuzi matatu muhimu sana kuhusu mambo ya maliasili zetu. Kwanza, alisema kwamba, hakuna cha mjadala, barabara ya Musoma

na hata Mugumu, Tabora, Loliondo na Mto wa Mbu, zitajengwa na wanaosema watasema lakini zitajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, alisema Kiwanja cha Ndege cha Mgumu wanaosema waseme kitajengwa, akasema *Five Star Hotels* zitajengwa katika Mbuga za Serengeti ili kuongeza viwanja toka 950 mpaka 4,500. Kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya Wananchi wa Serengeti, napenda kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kusema kauli hiyo. Kwa sababu mara nyingi tukiwa tunataka kuchukua hatua, majirani wanasema hivi tunarudi nyuma. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametoa uamuzi na kwa kweli tunampongeza sana na sisi Wanaserengeti tunangojea hayo yafanyike. Ninawashukuru sana Waziri Mkuu na Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wake, kwa hotuba nzuri waliyotupatia. Ninampongeza kwa sababu kwanza, katika makusanyo ya mwaka huu alifikia lengo na akavuka kwa asilimia tisa, Wizara chache zinaweza kufanya hivyo. Ninampongeza sana na vilevile mwaka wa fedha unaokuja amesema mapato yataongezeka kutoka bilioni 40 kufikia bilioni 110.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo itakuwa ni kazi nzuri sana na sasa Wizara itaanza kujitegemea, mwaka huu ameomba karibu bilioni 55 kwa ajili ya kazi maendeleo na mishahara. Sasa, kama watafika bilioni 110, ina maana kwamba, wataweza kupata hela za kujitegemea kwa *OC* na vilevile za maendeleo na watapata hela za kusaidia sekta nyingine, kwa hiyo, napenda kumpongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie katika upande wa utalii. Tanzania, kwa miaka mitano. Mwaka 2001 tulipata dola za Kimarekani milioni 9.4, mwaka 2002 tulipata milioni 9.1, mwaka 2003 tulipata 9.3, mwaka 2004 tulipata 9.8, mwaka 2005 tulipata 9.8, kinachoshangaza ni kwamba, Zimbabwe ambao wana hifadhi chache sana na sehemu za kuwindia, ilikuwa inapata milioni 30, sasa inakuwaje sisi tuna eneo kubwa hivyo tupate milioni 9 halafu Zimbabwe wapate milioni 30, lakini ukiangalia *South Africa,* Majimbo matatu tu ya *North West,* kwa Zulu na Limpopo, walikuwa wanapata wastani wa *US dollars* milioni 50. Sisi tunaambulia milioni 9 na Tanzania ina eneo kubwa kuliko nchi zote Ulimwenguni kwa kuwinda?

Kwa hiyo ni dhahiri kwamba, tumekuwa tukipoteza mapato. Katika ushauri huo, wataalamu walikuwa wanasema tungeweza kupata dola milioni 46 na leo ndio Mheshimiwa Waziri wa Maliasili ameonesha kwamba, kwa kupandisha bei hizi tutaweza kufikia karibu bilioni 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kumpongeza kwa uamuzi wa kijasiri alioufanya. Sasa inaonekana Serikali ya Awamu ya Nne, inafanya maamuzi ambayo watu walisema kwamba, hayatawezekana sasa yatawezekana. Napenda kumpongeza sana. Ni lazima tutumie mali zetu za asili, zituletee faida na watu wasije

kusema kwamba, bei zinapanda, anayesema bei zinapanda aende akawinde kwingine, ambako anajua atapata wanyama kwa bei rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti*,* nilienda kuitembelea Kenya mwaka jana nikakaa wiki mbili, nikaenda Zimbabwe nikakaa wiki mbili, nikaenda *South Africa,* bei ya vitalu kule inafika dola 250,000 kwa mwaka kwa kitalu kimoja; sasa inakuwaje bei yetu nchini? Mimi nasema kwamba, anaanza vizuri, tulikuwa tunapata kwa ajili ya vitalu 1.6 milioni sasa sasa hivi tutaenda milioni 7.16, *that is a good start*. Lakini nasema kwamba, mwaka kesho Mheshimiwa Waziri, *go further, go further* lete kabisa bei ya kitabu cha *SADC* tuainishe, watu wasikimbilie Tanzania kuja kupata vitalu vya bei rahisi.

Hatuna vitalu vya bei rahisi hapa kwanza, tunavyotaka mtu kama mimi sitaki hata wanyama wawindwe, kwa sababu simba unapomsikia yuko Serengeti anazaa, kila siku kamera zinapita tunapata pesa, kwa hiyo, hata asipokuja kamera zitapita tutapata pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tembo, sasa hivi tunasema atauzwa kwa dola 15,000 lakini *SADC* ni dola 25,000 kwa hiyo, ninakushukuru kwamba, umefika kwa dola 15,000 mwaka kesho tulinganishe na Botswana. Hatuwezi kuuza tembo wetu kwa bei rahisi, kwani tembo wa Tanzania ndio wanaotisha, ukienda huko kwenye *game reserve* ukaangalia tembo tulionao, ufafanishe na wa Botswana, wale ni wadogo wala hawana maana, wanauzwa dola 25,000.

Sisi tembo mkubwa wa kutisha tunauza kwa 15,000 ni sawa mimi nashukuru kwamba, umefika hapo lakini naomba *move forward* tufike 25,000 tuoanishe. Hakuna simba wa maana kama wa kwetu hapa, nenda *South Africa* ukaangalie wao ni wadogo wameshakwisha, wamekondeana, wana chawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi simba wa kwetu ni simba kweli kweli, sasa kwa nini auzwe dola 12,000 na wale wauzwe dola 18,000? Tunataka tufikishe bei hiyo hiyo, asiyetaka kuja kuwinda aende zake na wasitutishe. Watanzania hatuwezi kutishwa na wageni hata siku moja. Nchi hii ni yetu na tutaisimamia, hatuwezi kutishwa na wageni, *this is our country,* asiyetaka abebe virago aondoke.

Wamekuja ku-*lobby lobby*, sisi hutudanganyi, *they are in a wrong place and they are meeting wrong people,* hatuwezi kuondoka na hakuna mtu anayeweza kutushawishi kwa hilo. Lazima bei zipande na nina hakika *next year,* watafanya vitu vyao. Mimi nakufahamu, miaka mingi umenifundisha, tumefanya kazi pamoja, pia una uwezo wa kuamua, naomba mumsaidie Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uwezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naenda Wilaya ya Serengeti. Wilaya ya Serengeti kuna hoteli nyingi kama Serena *Hotel*, Robo *Hotel* na hata Soronela *Hotel* na kadhalika lakini kampuni hizo hazitusaidii sisi wananchi wa Serengeti. Kuna kampuni moja tu inaitwa *V.I.P Grumet* ambayo imejenga *Five Star* ndiyo imetuletea maji, imetujengea madarasa, barabara zinatengenezwa na kazi nyingine wanafanya. Tunaomba hizo hoteli

nyingine zitusaidie na Serikali mzikabe na tungelipenda tupewe ada ya kitanda kama nchi nyingine zinavyofanya. Halmashauri kama hoteli za kitalii zipo pale zinatakiwa zipewe ada ya kitanda. Tunaomba dola 10/= kwa kila mgeni anapokuja ili tuweze kufanya maendeleo hatuwezi tukachunga wanyama, tunazuia majangili halafu tunaona mgeni anakuja anachuma anaondoka tu na sisi anatuacha na umasikini. Serikali itusaidie kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye magogo. Mheshimiwa Waziri amesema *cubic metre* ya gogo tunalipwa shilingi 4,000/=. Juzi nilikuwa *West* Kilimanjaro, nikakuta kampuni zinasomba magogo, wanapata magogo at *subsidised price.* Sisi Tanzania tunaweza kuwapa watu *subsidised price whether* ni makampuni kutoka Kenya na sehemu nyingine. Sisi hakuna kitu, hatuwezi ku – *subsidise* mbao zetu, kama mtu atakuja alipe bei ambayo ni ile ya *production*. Kwa hiyo, naunga mkono kwamba bei ya magogo ipande.

Kuhusu ubadhirifu, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, ameshachukua hatua kwa kuunda Tume, na Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir leo ametudhihirishia na ameona mambo mabovu yanavyotendeka, hivyo ameshaunda Tume ya kudhibiti na ameahidi ukisoma Mtanzania ya leo kwamba atawafuatilia. Tunaomba Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe panga lako lifyeke.

Kwanza, tusivumilie, mimi ni mwanamisitu, naona aibu kusikia wanamisitu wanatuibia, tufanye tuwe na *contact or professional ethics* hata kabla mtu akifanya mambo hayo kabla hajaenda Mahakamani tuitane Tanzania *Forestry Association,* tumfukuze halafu ndiyo aelekee Mahakamani. Hatuwezi kuvumilia kuwa na viongozi ambao ni wabadhirifu. Siwezi kutumia jina wahuni labda Mwenyekiti ataniambia nikae lakini hatuwezi kuvumilia watu wabadhirifu katika nchi hii, mambo ya kusema fulani ni kigogo kwani ni kigogo gani hicho? Wasitutishe, mimi mbele ya Mheshimiwa Kikwete na hata Mheshimiwa Lowassa hakuna kigogo kinachoweza kuwashinda mikono yao ni safi. Mikono ya Mheshimiwa Rais wetu ni safi na mtu msafi hawezi kushindwa kudhibiti kigogo kinachotuibia mali. Ninaamini kufikia kama kesho hii hali itakuwa imedhibitiwa.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali (*climatical change*), mwaka jana mliona tulivyohangaika hapa, ukataji wa miti unatuletea *climatical change* na hiyo husababisha ukame. Tunapenda hatua zichukuliwe kuhakikisha kwamba miti haikatwi ovyo kwani gesi ya Songosongo ipo, tunaomba ile gesi itumike kwa ajili ya kupikia na mkaa wa mawe utumike na tupande miti, bila hivyo tutakwisha kwani tutapata mafuriko, vimbunga na njaa zitakuja kila mwaka. Tunaomba idhibitiwe hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kusema kwa leo, napenda niseme kwamba tumeanza kuona nuru katika Wizara ya Maliasili, tunasema Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe na Naibu Waziri wako, na Mama Nyoni, kwanza karibu Wizarani, *we know what you do*……….!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa James M. Wanyancha, naomba uongeee na Kiti, huruhusiwi hapo ulipo kualika watu kinyume na utaratibu wa Kanuni.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawasawa! Sasa naomba mwendeleze uzi huohuo na ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumza katika maeneo machache ili kutoa pongezi na ushauri kwa kazi kubwa inayofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe pongezi zangu kwa uongozi wa Wizara kwa kazi nzuri inayofanywa kulinda maliasili yetu na kukuza utalii. Kitendo cha Wizara kupandisha viwango vya uwindaji wa wanyama pori ni kitendo kinachostahili pongezi kwa kila mwenye kuitakia mema Serikali, naomba kuwashauri viongozi wa Wizara kutokubali kuyumbishwa na wale wanaodai kuwa gharama hizo ni kubwa sana.

Kuhusu uvuvi, nchi yetu ina eneo kubwa sana la bahari lakini hali ya uvuvi kwa wananchi wetu ni duni sana, ni vyema yatolewe maelezo kuhusu mipango ya Wizara kuboresha uvuvi na pia kuinua hali ya uchumi ya wavuvi katika ukanda wa bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta utalii imeendelea kukua vizuri sana na kulileta Taifa fedha nyingi za kigeni. Lakini hadi sasa bado macho ya watalii ni katika Ukanda wa Kaskazini *(Northern Circut).* Bado utalii katika *Southern Circut* haujapewa uzito mkubwa, maeneo ya Kusini mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ina historia kubwa, miji ya Kilwa na Mikindani ni miji yenye historia kubwa. Mikoa hiyo ndiyo inayobeba historia nzima ya vita ya Majimaji. Aidha, pori la Selous limeambaa katika eneo kubwa la mikoa hiyo.

Napenda kufahamu mipango ya Wizara ya kuendeleza utalii *Southern Circuit.* Aidha, historia yingine ambayo itabadili kabisa mwelekeo wa utalii katika Ukanda wa Kusini ni kurejeshwa nchini mjusi mkubwa duniani *Dinnossor* ambaye mabaki yake yapo Ujerumani hadi hivi sasa. Napenda kufahamu Serikali ina mpango gani wa kurudisha mabaki hayo ya *Dinnossor* katika eneo lake la asili mkoani Lindi ili kuimarisha utalii katika mkoa wa Lindi. Namalizia kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru mola kwa kunipa uzima na uwezo wa kuweza kuchangia walau machache tu juu ya Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba suala la *Marine Parks,* nchini ni moja kati ya taratibu za hifadhi za mazalio ya samaki katika eneo la bahari husika. Lakini mimi

najiuliza ni kwa kiasi gani *Marine Parks* hizi zinasaidia kukuza uchumi wa wananchi wa maeneo ambayo sehemu ya bahari imewekwa *parks* hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisiwani Mafia katika kijiji kidogo cha Jibondo ipo *Marine Park* ambayo amesababisha matatizo makubwa ya kufika hadi ya baadhi ya wananchi kushtakiwa mahakamani kwa tuhuma ya kuvua ndani ya hafidhi hiyo. Naomba kujua yafuatayo:-

(i) Inasemekana wananchi hao wa Jibondo walioshitakiwa hawakuona ndani ya hifadhi husika na kwamba ni kesi ya kubambikiwa, je, Serikali inasemaje kuhusiana na hili?

(ii) Kama kesi hiyo ni ya kubambikiza, je, ni lini kesi hiyo itafutwa maana ni zaidi ya karibu miaka miwili sasa.

(iii) Je, Serikali itawachukulia hatua gani wale ambao waliwabambikiza kesi wenzao wa Jibondo? Naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Waziri Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana hasa kwa kuratibu na kusimamia mambo yote muhimu yahusuyo maliasili ya nchi yetu na shughuli zote za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu Tanzania tumejaliwa na Mwenyezi Mungu kwa kuwa na vitu vingi ambavyo ni asilia, vyote vinahitajika kuendelezwa kwa maslahi ya kuiletea nchi yetu pato na hivyo kukuza pato la uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo misitu, bahari maziwa, wanyama wa kila aina, ndege wazuri wa kujivunia na vionjo vingine kadha wa kadha, vyote vikiwa ni maeneo ya kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi zote za Wizara katika kuhakikisha sekta ya utalii nchini inaboreshwa ikiwa ni pamoja na kuenzi maliasili ya nchi yetu, bado maeneo mengi ya kiutalii hayajafanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie baadhi ya maeneo ambayo naamini yanahitaji kupewa kipaumbele kwa mwaka huu wa fedha. Kwanza maliasili, misitu ni kitu muhimu sana, mistiu inaleta mvua, misitu inatunza vyanzo vya maji, misitu inatunza mazingira, kumekuwepo na uharibifu wa misitu asili, kuharibiwa huku kumeleta athari kubwa yakiwemo yale ya kufanya wanyama watoweke, kuna vyanzo vya maji na kuleta athari ya mmomonyoko wa udongo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Bajeti ya mwaka huu Wizara iangalie na iwe makini kwa kutunza misitu yakiwemo mapori tengefu. Jimbo langu la Iramba Magharibi, eneo lote la Mlima Sekenke lilitengwa kama eneo la hifadhi lakini bado hakuna juhudi zinazofanywa na Wizara kulitunza eneo hilo ambalo ni muhimu kwa misitu mizuri na kuwa na vyanzo vingi vya maji. Kadhalika tabia ya uvunaji wa miti hovyo ipigwe marufuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia eneo hili linachangiwa na ubovu wa watendaji wa idara hii ya misitu kutokuwa waaminifu na pengine kujiingiza katika vitendo vichafu vya kuuzia baadhi ya wananchi maeneo ya misitu kwa ajili ya matumizi binafsi, watumishi hawa wadhibitiwe na Wizara na ikiwezekana wachukuliwe hatua za kisheria ikiwemo uhamisho kikazi ili kukutana na mazingira mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miti kama mipingo ni muhimu sana maeneo ya msitu wa mipingo katika jimbo langu yapo katika kijiji cha Msai kata ya Mtoa naomba eneo hili lipewe kipaumbele na Wizara kushirikiana na Halmashauri ya Iramba itenge eneo kwa ajili ya kulinda miti hii ya mipingo isitoweke kama ambavyo wavunaji haramu kuhitaji miti aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Kitangiri linatoa mapato na mchango wa ajira katika jimbo langu la Iramba Magharibi, utunzaji wa Ziwa hili umetupwa mkono na Wizara na hivyo uendeshaji wa shughuli Ziwani kutokueleweka vizuri, Ziwa linaweza kuleta watalii, wapo ndege wa kila aina mbali na hilo Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho naomba anifafanulie juu ya namna ya kuwapatia boti ya doria kwa ajili ya shughuli za uvuvi Ziwani, kadhalika maombi juu ya kutoa semina kwa wavuvi wadogo wadogo ili wawe na mipango endelevu kwa shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mheshimiwa Waziri kutupa ongezeko la uwindaji kwa wanyama kama vile Simba, Tembo, Chui na kadhalika, bado naamini gharama hizo ndogo hasa kulingana na umuhimu wa wanyama hao katika sekta ya utalii na kadhalika. Pia elimu inahitajika kwa wafugaji nyuki kwa ajili ya kujipatia asali.

Mwisho shughuli za utalii katika mbuga za wanyama ziongezwe ili kuvutia watalii wengi kwa nia ya kutangaza nchi yetu na pia Wizara itumie matangazo sehemu mbalimbali majarida tovuti, *CD* zisambazwe kote duniani kutangaza sekta hii muhimu, naunga mkono hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujirani mwema na mahusiano kati ya wananchi waishio kandokando ya hifadhi, picha ya matatizo mengi wanayopata wananchi waishio kandokando ya hifadhi ni pamoja na kukosa eneo la kilimo, malisho, wanyama, tembo, kuuwawa na wanyama wakali kama simba na chui, kutokuruhusiwa kuwinda wala kuingia kwenye hifadhi na kukamatwa na kuwekwa mahabusu kwa muda mrefu sana au kufungwa jela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mazao kuharibiwa na wanyama kama tembo bila msaada wa haraka na kusababisha njaa katika vijiji vya kando kando. Mfano, Semu,

Bugayabahya, Mwamashimba, Mwanindwa, Ming'ongwa, Buturi, Malale Mwamchoyo na Mwasengela huko Meatu jimbo la Kisesa.

Kwa kuwa msimu wa tembo unajulikana, kwa nini Serikali isipeleke askari moja kwa moja kipindi kinapofika badala ya kusubiri kupewa taarifa wakati tayari uharibifu mkubwa umefanywa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zinazopakana na hifadhi hupata 25% ya mapato yatokanayo na ada za vitalu na za uwindaji wakati mwingine fedha kukatwa na kuletwa pungufu katika mwaka wa fedha 2006/2007 Halmashauri ya Wilaya Meatu ilitengewa shilingi milioni 32, zilizotolewa ni shilingi milioni 27. Je, fedha zilipunguzwa na nani na lini pungufu italetwa?

Kuhusu barabara za vijijini. Vijiji vingi vinavyopakana na hifadhi hazina barabara na hivyo hakuna shughuli zingine za kiuchumi na badala yake wananchi huenda kwenye hifadhi kuwinda mfano Semu, Bugayabhya, Nyanza, Ming'ongwa, Buturi, Mwamhongo, Mwasegela barabara zake hazipitiki. Je, Waziri haoni kwamba sasa ni muda muafaka wa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na TAMISEMI kuchonga na kujenga barabara za vijiji vya kando kando?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi maalumu, Waziri atafute fedha za dharura kuchonga na kujenga barabara ya kutoka Sakakasa – Buturi (Makao Makuu ya *Maswa Game Reserve).* Hivi sasa wageni wa ndani na nje wanapata taabu sana kufika ofisini hapo na mara nyingi kulazimika kutumia helkopta. Naomba sana Waziri ashughulikie tatizo hili mwaka wa fedha 2007/2008. Kuhusu sheria ngumu, kwa kuwa sheria zinawakataza kuingia kuwinda na kuchangia kwenye hifadhi, je, Serikali haioni kuwa wananchi wanapata mateso makubwa kuwakataza kuwinda kwa ajili ya kitoweo?

Katika mgodi kuna wachimbaji wadogo wadogo, haki na maslahi yao yamekuwa yakiboreshwa kila siku, je, ni lini Serikali itaruhusu wawindaji wadogo wadogo watakaowauzia nyama kwenye *butchery* wananchi wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukosa maeneo ya kuchungia na maji, ni lini Serikali itatenga maeneo ya kuchungia kwa vijiji kando kando ya hifadhi? Serikali ina mkakati gani wa dharura kuchimba malambo na mabwawa kwa vijiji vya kando kando.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Hongera Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Mlima Kilimanjaro umezungukwa na Halmashauri za Wilaya kama ifuatavyo; Longodi, Monduli, Siha, Hai, Moshi Vijijini na Rombo. Halmashauri hizi ndio zinazotunza huu mlima lakini cha kushangaza uzalishaji ndani ya huu mlima kwa miaka mitatu (2003 hadi 2006) ni shilingi 44,606,204,346/= lakini Halmashauri hizo zimepata shilingi 303,816,548 tu. Hata 1% haifiki. Naomba Halmashauri hizi zipewe 25% ya mapato ya *KINAPA* kama wapatavyo Halmashauri zenye vitalu vya uwindaji.

Pili, Mheshimiwa Waziri kuna njia ya kupanda Mlima Kilimanjaro kwa kupitia Kilema Maua. Naomba njia hiyo sasa itumike kwa kupandisha watalii kwa *camping*. Isiwe *administrative route* tu. Utalii Mlima Kilimanjaro utaongezeka kwa mujibu wa

matangazo tunayofanya, naomba *route* hii iongezwe, ni nzuri naifahamu na itapendwa na watalii maana mandhari yake ni nzuri

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja, kule Ruangwa kuna misitu mingi na ardhi yenye mvuto kwa ufugaji wa nyuki, je ninaweza kupata muda wa kuonana na Mkurugenzi wa Nyuki ili aje kutembelea kule akatusaidie ili nasi tulingane na wana Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu hatuna kitoweo je, Bwana Samaki ana muda wa kuonana nami ili angalau tupatiwe siku ya yeye kutembelea Ruangwa ili atuelekeze namna ya kuanzisha mradi wa kufuga samaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabwana *(game)* wa kule kwetu hawana usafiri. Kuna matukio ya wapiga kura kuliwa na samba, je, niwaombee gari au pikipiki au baiskeli? Ukiwauliza kule Ruangwa kile wanachokitaka watakueleza gari kama ninavyowaombea mimi Mheshimiwa Waziri wanashindwa kuwahi matukio kwa sababu ya ukosefu wa usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkona hoja hii asilimia mia kwa mia, kwa kuwa Tarafa ya Mwaya Wilayani Mahenge, Mkoa wa Morogoro ni maarufu kwa kilimo cha pamba na mazao mengine; kwa kuwa uzalishaji wa pamba umedorora sana kwa sababu ya barabara inayoingia Tarafa hii kwa urahisi ukitokea Ifakara/Morogoro kuwa na milima mikali na mbovu sana; kwa kuwa barabara ya mkato kabisa kuelekea Tarafa hii ni ile ya Chikuti - Lukande – Mwaya; kwa kuwa barabara hii haipo chini ya *TANROADS* wala Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga bali ni barabara ya Wizara ya Maliasili na Utalii na kwa kuwa pia kuna daraja muhimu ambalo limebomoka hivyo kuzuia magari kupita kabisa. Je, Wizara ya Maliasili na Utalii ina mpango gani wa haraka wa kuitengeneza barabara hii pamoja na daraja ili iweze kuhudumia watalii, wananchi na hasa wakulima wa pamba kama ilivyokuwa huko nyuma?

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya misitu ni muhimu sana nashauri kuwepo na utaratibu wa kushirikisha jamii kulinda misitu (Ulinzi Jamii Shirikishi). Aidha, suala la kupanda miti ni la msingi sana. Ni muhimu Serikali ikatenga pesa za kuwatika miti ya kulinda mazingira na bei ya miti hiyo iwe karibia na bure. Nchi nzima bei ya miti ikiwa juu wananchi watashindwa kupanda miti maana ni gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itangaze utalii maeneo ya Kusini mwa nchi hasa Iringa ambako kuna *Ruaha National Park,* Kalenga na Isimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua kwa nini wageni waliotembelea Isimila na Kalenga kwa mujibu wa Jedwali SA mwaka 2006/2007 wamepungua ukilinganisha na mwaka 2005/2006 sababu ni zipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majibu na ufafanuzi wa masuala tajwa hapo juu naomba kuunga mkono hoja.

Aidha, bei za vibali ziwepo bei za Watanzania na wageni, vinginevyo bei zikifanana Mtanzania mwekezaji atashindwa kuwekeza.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi bei za maliasili zetu zimekuwa haziendani na hali halisi ya bei za dunia. Naunga Serikali mkono kwa hatua iliyochukua kuzirekebisha bei zetu angalau ziendane na hali halisi ya bei za dunia. Wafanyabiashara wengi wanapinga kwa nguvu zao zote ongezeko hili, lakini ushauri wangu kwa Serikali wasiwasikilize hata kidogo kwani kama ni faida, wamekwishapata na sasa wachunge pato la Serikali. Ongezeko dogo tu kwenye mkaa, sio sababu ya kupandisha bei ya mkaa kufika shilingi 30,000. Bei hizi ni wizi kwani ongezeko ni shilingi 2,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magogo, kwa muda mrefu magogo yamevunwa bila utaratibu na cha kushangaza japokuwa Serikali imekataza usafirishaji wa magogo nje ya nchi, bado kuna wajanja wanasafirisha. Ili kudhibiti biashara hii, tuweke doria nzuri katika Pwani zetu na mipaka yetu na kukataza kabisa usafirishaji wa magogo. Huu ni urithi tuliorithi kutoka kwa wazee wetu na ni vizuri tulinde kwa ajili ya kizazi kijacho. Kuna magogo kama ya *Sao Hill,* haya ni sawa yauzwe na sio magogo ya asili. Narudia kuomba, kupiga marufuku kabisa uvunaji wa magogo katika misitu yetu ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitalu vya uwindaji naunga mkono Serikali kupandisha bei ya vitalu vya kuwinda. Kwa muda mrefu bei tulizokuwa tunatoza, ni kama tulikuwa tunazotoa bure ukilinganisha na nchi jirani. Tusibabaishwe na wawindaji wachache wanaotutishia kuwa wataondoka kuliko waendelee kutuibia ni heri waondoke, lakini ni hakika watakuja wengine watakao heshimu maamuzi yetu. Naunga mkono pia kupandisha bei ya kila mnyama anayewindwa na huu ni mwanzo tu, baada ya muda tuangalie upya kupandisha bei zetu ili tuendane sambamba na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa ndege *(birding)*. Kwa sasa hivi biashara ya utalii wa ndege haupo hapa Tanzania. Tunao ndege wa kila aina hasa katika milima, chini ya mlima Kilimanjaro. Ningeiomba Serikali kufikiria na kukubali uanzishaji wa utalii wa ndege kwani kwa sasa dunia ndio utalii unavutia matajiri wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapato ya Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro, unaingiza pesa nyingi kuliko hifadhi zetu zote. Kufanikiwa huku, kunawezekana tu kwa uwezo na kazi nzuri inayofanywa na *porters* na waongozaji wanao wahudumia hao watalii. Kilio cha *porters* na waongozaji ni kuwa malipo ya kazi ngumu wanayofanya hawapati, wanabakia na *tip* tuu toka kwa wageni. *Tour operator* hawaweki pesa za *porters* na waongozaji kwani wakifanya hivyo bei zao zitakuwa juu na watakosa kazi na hata hao *porters* na *guides* wanakubali kwani hawana kazi. Kama pesa za *Porters and Guides* zikiwekwa mapato ya nchi kwa ujumla utakuwa juu. *Tour Operators* wakubwa wote wanaonyesha na kuwalipa *Porters and Guides* kama hawa *Tour Operator*

wadogo wataongeza hizi bei, watafikia bei za *Tour Operator* wakubwa kwa hiyo, wanaogopa kukosa kazi.

Maombi yetu ni kukuomba, *Tour Operator* wanapolipa *Park Fees* hapo hapo walipe malipo mengine ya kuwalipa *porters*. Hawa sio wafanyakazi wako, lakini hii ni msaada, tunaomba ili tunusuru hawa *porters* na kuhakikisha kila mtalii analipa malipo halisi.

Pia tofauti ya bei utakuwa haupo, kwani kwa mfano, mtalii mmoja kupitia *Tour Operator* mdogo asiyelipa *porters* anamtoza mtalii *U$D 600* ambazo ni za kulipia *Park Fee* tu, na kumlazimisha kujinunulia chakula na kutoa *tip.* Lakini *Tour Operator* mkubwa kwa mtalii huyo huyo humtoza *U$D 1200* ambazo zinalipia *Park Fees, Transport* kwenda *Gate* na kumrudisha hotelini, chakula kwa muda wote akiwa mlimani pamoja na chakula cha *porters.* Pia pesa hizi zita-*cover two nights* hotelini. *Tour Operator* na *porters* wako tayari kukatwa % fulani kwa ajili ya huduma hii.

Kuhusu ulinzi wa watalii. Watalii wamekuwa wakishambuliwa mara kwa mara na majambazi, tungeomba, uwepo utaratibu wa kuwa na kikosi cha polisi, kama ilivyo *Railways* na Bandari kwa ajili ya ulinzi wa watalii. Kwa sasa Kanda ya Kaskazini ndio ina tatizo hili japokuwa kila hoteli ina walinzi, lakini kikipatiwa na polisi mara kwa mara itasaidia sana kupunguza kama sio kukomesha kabisa tatizo hili. Naunga mkono hoja.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mikakati mizuri ya kudhibiti wanyama wakali na waharibifu. Suala hili litaangaliwa wakati wa sheria inayopitiwa na katika kutekeleza programu ya ushirikishaji wananchi *(WMA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu boma ambalo lilikuwa likarabatiwe na *GTZ* ni suala la mambo ya kale na halikuwa kwenye mpango wa kati wa Wizara. Hata hivyo Wizara itaangalia suala hili kwenye Bajeti zijazo, kulingana na Bajeti ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matengenezo ya barabara ya Ndapata hadi Ulanga, pamoja na nia nzuri ya Wizara kusaidia matengenezo ya barabara hiyo, lakini kutokana na *budget cuts,* Wizara haina uwezo wa kutengeneza barabara hiyo mwaka huu wa fedha. Hata hivyo *TWPF* inaweza kuchangia kidogo Halmashauri za Wilaya na *TANROADS.*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiit, Serikali ieleze mikakati ya kuongeza idadi ya watalii katika hifadhi ya Taifa ya Kitulo iliyopo Wilayani Makete. Idadi ya watalii kwa mwaka 2006/2007 ilikuwa ni watalii 74 tu na mapato ya shilingi 11,493,750 tu, hili ni pato dogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ieleze ni lini itajenga hoteli ya kitalii katika hifadhi hii ya Kitulo. Hifadhi hii tangu ianzishwe haina hoteli na hii husababisha watalii kupata usumbufu na kulazimika kusafiri muda mrefu kwenda kulala Mbeya, umbali wa zaidi ya kilometa 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mikakati gani ya kuitengeneza kwa kiwango cha lami barabara ya kitalii iendayo *Kitulo National Park* yaani barabara ya Chimala – Matamba – Kitulo? Barabara hii inapita kwenye mlima wenye kona zaidi ya 54 ambazo pia ni utalii wa kuvutia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiit, pia Serikali iangalie uwezekano wa kutumia eneo zuri lililopo kwenye hifadhi hii ya Kitulo kutumika pia kwa michezo ya *golf* ambayo pia inaweza kuwa kivutio kikubwa kwa watalii. Naunga hoja mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kwa hotuba yake nzuri sana, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Zabein Mhita na Katibu Mkuu Bibi Blandina Nyoni, kwa jinsi walivyo makini katika kufanya kazi vizuri, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu upo kwenye mambo ya kale, kijiji cha jadi cha Nyumba Nitu kilichopo Kata ya Mdandu Wilaya ya Njombe. Kijiji hiki ni muhimu sana kwa utalii na ni muhimu sana kwa utunzaji wa mimea na hifadhi ya mazingira. Msitu huu ni wa maajabu sana kwani miti yake na mimea yake iko pale kwa karne nyingi na hata wanafunzi wetu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine huenda pale kwa kujifunza aina za mimea. Mbali ya msitu kuna kuku weusi wa ajabu na kuna mapango makubwa pale Nyumbanitu ambayo watu zaidi ya mia moja wanaweza kuishi kwenye mapango hayo yalikuwa yanatumika wakati wa vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maajabu hayo ni sawa kabisa kama yalivyo nchini Japan. Nashauri Wizara yako itembelee na iweke vitega uchumi pale kijini cha Mlevela - Nyumbanitu - Njombe. Endapo tutawekeze pale kijiji cha Mlevela na Nyumbanitu kitapata unafuu wa kupata huduma muhimu za zahanati, shule na maji ya bomba kwani huduma hizo ni muhimu sana kwa maendeleo. Pia kuna ramani ya Afrika pale Lwivala – Igodivaha, Kata ya Imalinyi, Njombe. Tunaomba kibali cha kutoza ushuru wageni kwa kushirikiana na Halmashauri ya Njombe ili kuweza kuinua uchumi wa Halmashauri ya Njombe na kijiji cha Igodivaha kupata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa vile *Mpanga Game Reserve/*Kipengere iko Tarafa ya Wanging'ombe. Nashauri kile kiwanja cha ndege cha Ilembula - Usetule Handula (Wanging'ombe) kifufuliwe wenzetu wa *TANAPA* na Wizara ya Maliasili na Utalii na sasa tayari pale Ilembula ambako ni mji mdogo wa Njombe Magharibi kama mahoteli ya kitalii mfano *H-Hotel,* pia kuna hospitali na Chuo cha Uuguzi cha Ilembula, Njombe ambacho ni nyenzo za kuvutia wageni na watalii. Fedha zipelekwe kwenye eneo husika siyo kupeleka Njombe mjini ambako ni mbali na eneo husika siyo kupeleka Njombe mjini ambako ni mbali na eneo husika.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu walionitangulia kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Simanjiro kumuombea kwa Mwenyezi Mungu roho ya ndugu yetu Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia ili mola aiweke mahali pema peponi. *Amin.*

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Jumanne Maghembe, kwa hotuba yake nzuri yenye maamuzi mazito na magumu. Nasema maamuzi mazito kwani kiwango cha ushuru alichokitangaza leo asubuhi kwa upande wa vitalu vya uwindaji na bei ya kuwinda wanyamapori ni bei ya kuwinda wanyamapori ni tofauti sana na kile ambacho kinatumika sasa na siku zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo kabisa na kupanda kwa viwango hivyo kwani kufanya hivyo kunaiweka nchi yetu kwenye nafasi nzuri kimapato na hivyo kuwezesha utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kuwa huu unafanyika wakati ambapo wageni kwa maana ya watalii wapo na wanaendelea na shughuli zao sasa, kwani kipindi chao kuanzia mwezi Julai, tarehe moja ya kila mwaka na kuishia Desemba. Kwa kuzingatia kuwa wageni hao pengine watakuwa wamekwishafanya malipo kwa viwango vilivyokuwa vinatumika kabla ya hotuba ya Waziri, je, Waziri wakati wa kujibu hoja anaweza kulieleza Bunge lako Tukufu kuhusu utaratibu utakaotumika kufanikisha zoezi hilo? Ni vizuri pia tukafahamishwa kama uamuzi huo unatekelezeka katika mwaka huu wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Waziri yatatuweka mahali pa kujua iwapo palikuwepo na ushirikishwaji wa wadau kabla ya uamuzi wa Serikali, lakini kujua iwapo tuko salama kwa mujibu na sheria au mikataba ya Serikali na wawekezaji hao wa ndani na wa nje. Hii itasaidia kurudisha heshima na imani yetu ya wageni kwa nchi yetu. Aidha, ningependa kufahamu asilimia zinazopelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya zenye vitalu vya uwindaji kama zitaongezeka kwa uwiano huo huo wa kupanda kwa viwango vya ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Simanjiro kwa upande Magharibi inapakana na hifadhi ya Taifa ya Tarangire na *Mkungunero Game Reserve,* kwa muda mrefu sasa pamekuwepo na mgogoro wa mipaka kati ya vijiji vinavopakana na maeneo hayo. Pengine imefika wakati wa Serikali kwa kushirikiana na wananchi wa Simanjiro kumaliza mgogoro huo, aidha, nashauri Waziri atueleze ni lini hasa mgogoro huo utamalizika na hivyo kuendeleza mahusiano mazuri baina ya hifadhi yetu na jamii inayoizunguka. Itakumbukwa kuwa wakati wote wa masika sehemu kubwa ya wanyamapori wa Tarangire wanahamia kwneye mbuga za Simanjiro na hivyo kuyafanya maeneo ya Simanjiro kuwa *clinic* ya kuzalia wanyama hao hususan nyumbu, pundamilia na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri pia Bunge lako lifahamu kuwa bila huruma ya wana Simanjiro ya kuyalinda maeneo yao nje ya hifadhi kwa ajili ya mifugo na wanyamapori hifadhi ya Taifa ya Tarangire isingekuwepo wala *Mkungunezo Game Reserve.* Naiomba Serikali itenge fedha za kutosha kwa maendeleo ya Wilaya hiyo kwani kwa sehemu kubwa maeneo ya malisho ya mifugo ndiyo hayo hayo yanayotumika na wanyamapori. Hii ni pamoja na uharibifu mkubwa wa mazao unaofanywa na wanyama hao bila fidia yoyote.

Mhesihmiwa Mwenyekiti, umefika wakati sasa wa kuweka wazi vigezo vinavyotumika na *TANAPA* katika kuunga mkono miradi ya maendeleo ya fani katika maeneo yanayozunguka hifadhi za Taifa kwani hali ilivyo sawa katika baadhi ya Wilaya ikiwemo Simanjiro ni mbaya sana. Ni wajibu wa *TANAPA* kusaidia miradi ya jamii kulingana na mahitaji ya wananchi ili kuendeleza suala zima na mahusiano mema.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kimaandishi. Napenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na wataalamu wa Wizara kwa utekelezaji mzuri wa shughuli za mwaka 2006/2007. Ni dhahiri kwamba utekelezaji huu ndio uliopelekea ongezeko la Pato la Taifa. Nawapongeza pia kwa mikakati mizuri ya utekelezaji wa mwaka 2007/2008 utakaopelekea ongezeko la ukusanyaji maduhuli kutoka zaidi ya shilingi bilioni 40 mwaka 2006/2007 hadi zaidi ya shilingi bilioni 74 mwaka 2007/2008. Mapato haya yatasaidia Taifa kujitegemea kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Serikali kwa kufanya kazi zake kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuna suala la kufufua sekta ndogo ya ufugaji nyuki pia kuboresha maisha ya Watanzaia kupitia sekta ya uvuvi kwa njia mbalimbali kama mradi wa *MACEMPT* na ununuzi wa vifaa vya Maabara ya Taifa ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, kuiomba Wizara ielekeze nguvu zake kwa vikundi vya uvuvi na kuviwezesha kupata nyenzo za uvuvi zilizokamilika ili kuweza kupambana kikamilifu na uvuvi haramu na kutekeleza MKUKUTA. Wavuvi wanahitaji boti imara yenye injini ili kuhakikisha usalama wa maisha yao hivyo wasaidiwe kupata mitaji mikubwa. Ikumbukwe kwamba semina pekee kwa gharama kubwa kwa wavuvi wengi haitasaidia sana kama vile semina kwa vikundi vichache kwa gharama ndogo na gharama zingine zisaidie upatikanaji wa nyenzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie matumizi endelevu ya maliasili. Hili linamuhusu kila mwanadamu kwani kila mmoja ni mtumiaji wa maliasili ikiwa ni pamoja na ardhi, misitu, hewa, maji na wanyamapori. Kwa Watanzania kuna ile dhana ya kwamba maliasili ni ya Watanzania wote hivyo kila mtu anaweza kuitumia anavyotaka. Kwa upande wa ardhi na misitu kumekua na ile tabia ya wananchi kwenda popote porini, kufyeka eneo kubwa na kuyachoma magogo waliyofyeka ili kuanzisha makazi na kufanya shughuli za kilimo. Napenda kuishauri Serikali/Wizara itoe miongozo juu ya matumizi ya aina hii kwani haya si matumizi endelevu. Ukiachia uharibifu wa misitu kwa uvunaji magogo, pia upo uharibifu wa maliasili hii kwa kilimo cha kuhamahama na uchomaji moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali au Wizara ikachukua fursa ya kuwaeliewesha wananchi wote kwa ufasaha juu ya mahusiano ya maliasili zote tulizonazo. Kwa mfano, ya ardhi, misitu na wanyamapori pia misitu na hali ya hewa katika ustawishaji mazao yanayostawi katika eneo la Bariadi pia milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa misitu hausababishi *global warming* kwa ghafla bali huanza kwa kuathiri joto la eneo husika. Hivyo, ongezeko la joto katika eneo linalostawisha maharage ni wazi kwamba baada ya muda fulani uzalishaji utaathirika. Vile vile wadudu na magonjwa mengi ya mazao hupendelea hali ya joto zaidi kuliko baridi. Hivyo wananchi waeleweshwe juu ya uhalisi wa athari za matumizi yasiyo endelevu ya maliasili yetu na jinsi yanavyomuathiri kila mtu moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuiomba Wizara imalize matatizo ya upungufu wa watumishi kwa kuajiri wahitimu wa vyo vyetu kama Mweka, Olmotonyi na *Sua*. Naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Wizara hii ili kujua mambo muhimu. Napenda nifafanuliwe kwa kina ni kwa nini Serikali isifanye au Wizara, pori au maporini tuliyonayo ya mkoa wa Kagera kuwa hifadhi, tuna sehemu nyingi ambazo zinaweza kuwa ni hifadhi nzuri na kutuingizia kipato na kupata ajira. Mapori yenyewe ni Buligi Kimisi, Kajunguti na Rwasina yapo mengi hayo ni mojawapo.

Naomba nipate majibu, tuna visiwa vizuri tu na vyenyewe vipo vingi tu, nipatiwe majibu, nijue kinachozuia ni nini na kwa nini haiwezikani. Nilitembelea sehemu ya Kigoma/Ujiji kwa *Livingstone* nikamkuta mzee mmoja aliyekuwa akitunza sehemu ile, kwa kweli nilifurahi sana alivyokuwa akitoa historia ya pale, alikuwa anafurahisha sana. Mimi juzi nilipata taarifa kwamba ameacha kazi, nimesikitika sana kusikia kwamba ameondoka kwa ajili ya kukosa fedha, alituambia kwamba mjukuu wake *Livingstone* alikuja pale akamwambia atamtumia msaada na kweli akatuma dola, hawakumpa wakazila, mimi ninachotaka kujua ni kwa nini Serikali isitengeneza sehemu kama hizo kujua kwamba mkoa wa Kigoma ulivyo nyuma, kimaendeleo. Naomba jibu au majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la magogo bado ni mgogoro mkubwa. Swali lingine naomba kujua wanyama waliouawa kwenye pori la Biharamlo walienda wapi, waliuawa au waliuzwa au walikufa? Naomba kujua mambo yote niliyoyauliza au kuchangia kwenye maandishi, naomba majibu. Nawatakia Bajeti njema.

Naomba wavuvi wakumbukwe wapewe zana kuliko kuwa wanatumia zana haramu, hivi Serikali haioni kwamba wavuvi wanapata shida kukamatwa kila siku na huku zana hizo wanazinunua madukani. Je, wanazitoa wapi, naomba zidhibitiwe kuliko kosa kuwakamata wavuaji tu, naomba majibu.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Pongezi. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa maandalizi mazuri ya Bajeti na uwasilishaji mahiri. Nawapongeza watendaji wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na kushauri, endeleeni kufanya *evaluation* ya kila eneo ili nchi yetu iendelee kufaidika na mali asili zetu. Kuhusu uvuvi, pamoja na bahari yote, sekta hii haijachangia kwa njia ya kutosha katika Pato la Taifa. Serikali

haifanyi biashara, lakini iweke mazingira mazuri, Watanzania wavue baharini na ku-*export* nje. Nategemea kuwa na shughuli za biashara ya samaki Pwani ya Tanzania kuliko Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipangusa machozi cha shilingi 200,000/= ni kidogo mno, hata kwa matibabu ni kidogo mno. Kuhusu nishati mbadala, jitihada ifanywe kueneza nishati mbadala ili kuokoa misitu. Hii ifanywe kwa kuhakikisha bei ya vifaa kama *cookers* na kadhalika vipungue bei. Gesi *(cooking gas)* isambazwe na kwa bei nafuu. Naunga mkono hoja.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Taasisi zake kwa kazi nzuri ya kusimamia na kuiendeleza sekta hii muhimu katika uchumi wetu.

Kwa mtazamo wangu, sekta hii ni miongoni mwa sekta viongozi katika uchumi wetu. Nchi nyingi duniani zinapata fedha nyingi za kigeni kutoka kwenye sekta kama hii. Miongoni mwa nchi hizo ni pamoja na Kenya, Sycheles na Mauritius ambazo hazina vivutio vingi vya utalii na maliasili kama Tanzania! Hivyo, ni dhahiri kwamba tukijipanga vizuri, nchi yetu itaweza kupata fedha nyingi za kigeni kutoka kwenye sekta hii. Miongoni mwa mambo ambayo Serikali inapaswa kufanya ni pamoja na kuihimiza sekta binafsi, kuongeza ujenzi wa hoteli zenye hadhi za Kimataifa katika maeneo yanayopata watalii wengi, kuanzisha maeneo mapya ya kutembelewa na watalii sambamba na kuboresha maeneo yaliyopo, kwa mfano kufungua maeneo mapya yenye vivutio vya utalii upande wa Kusini na Magharibi ya nchi. Kwa kufanya hivyo Serikali itaondoa msongamano wa watalii katika eneo la Kaskazini ya nchi na hivyo kuwezesha sehemu nyingine za nchi kufaidika kiajira na kwa kipato kutokana na sekta hii muhimu katika uchumi wetu.

Kuhusu uendelezaji wa viwanda vitakavyotumia masiliasili zetu, Taifa litafaidika zaidi kiajira na kimapato kama Serikali itahimiza uanzishwaji wa viwanda vinavyotumia mali zetu za asili hapa nchini badala ya kuendelea kuuza maliasili zetu katika hali ghafi. Viwanda kama vya samani, karatasi, *hard and soft boards,* nyara za wanyama (kama sanamu za simba, chui na kadhalika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ya watalii wanaokuja hapa nchini wanalipia huduma zao za hoteli kwa utaratibu wa *package fees* na fedha hizi hulipwa kwa mawakala wa utalii nje ya nchi. Utaratibu huu hautusaidii sana kuongeza mapato yetu ya utalii. Nashauri Serikali ibadilishe utaratibu huu ili watalii wote waje kulipia gharama za hoteli na kadhalika hapa hapa nchini.

Kuhusu ada za watalii wawindaji, naipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua katika kubadilisha viwango vya ada za kuwinda wanyama wetu mbalimbali. Hata hivyo naishauri Serikali iendelee kuzipandisha ada hizi mpaka zifikie viwango vinavyotozwa na nchi nyingine za *SADC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei za magogo yanayopelekewa nje ya nchi, naipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua ili kuhakikisha kwamba bei za magogo yetu inafanana na bei za bidhaa hii katika osko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wafanyakazi wakorofi na wala rushwa, Serikali isiwaonee haya wafanyakazi wakorofi na wala rushwa. Wafanyakazi wa namna hii wasivumiliwe waondolewe haraka kila wanapobainika.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa maandishi Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na Naibu Waziri na watalaam wa Wizara hii kwa kazi nzuri na mipango ya kuboresha Wizara hii muhimu kwa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mambo ya kale, historia hii ni muhimu mfano Bagamoyo jumba ambalo lilikuwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ambalo sasa hivi limekuwa bovu, halifai tena kutumika kutokana na uchakavu. Ningeomba hivi ni nani anayehusika kukarabati jengo lile ambalo ni kivutio kikubwa katika historia ya nchi yetu, kuna hatari ya kudondoka saa yoyote, hivi Wizara haioni hilo na wahusika wakalikarabati jengo lile na kunusuru kupotea historia na magofu mengine yaliyopo Bagamoyo pamoja na Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanyakazi vizuri ya kupandisha bei ya vitalu vya uwindaji pamoja na kuongeza vitalu hivyo na bei hizo bado Wizara iwe na mpango endelevu wa mara kwa mara kupandisha gharama mbalimbali za maliasili na utalii ili kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu kwa Wizara pamoja na jitihada kubwa za kuhamasisha wananchi wa Tanzania kuelewa umuhimu wa kutembelea maeneo ya utalii ni vyema somo hili sasa liongezewe umuhimu na matangazo ya mara kwa mara katika vyombo vya habari na kuongeza wananchi kuchangia uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvunaji wa magogo napongeza kwa kusimamisha uvunaji. Baadhi ya uvunaji huo wa magogo kwa upande wa Kusini yanavunwa sana na kupelekwa nje ya nchi na kumaliza rasilimali hii liende sambamba na upandaji miti hasa misitu asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gunia la mkaa katika jiji la Dar es Salaam ni shilingi 20,000 ningependa kujua ushuru wa gunia moja ni kiasi gani kulileta mjini?

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kushiriki kikao cha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza na viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu ni moja katika sekta muhimu za maliasili ambayo ikisimamiwa vizuri inaweza kuchangia kwa kasi kubwa Pato la Taifa letu.

Usafirishaji wa mbao na magogo unapoteza fedha nyingi kutokana na kutosimamiwa vizuri usafirishaji wa bidhaa hii ya maliasili. Tunaiomba Serikali iwe makini zaidi katika kusimamia usafirishaji wa magogo hasa kwa njia haramu unaofanywa na baadhi ya walanguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi hasa katika bahari kuu unaoweza kuongeza Pato la Taifa kwa kiwango kikubwa sana iwapo Serikali itakuwa makini sana katika kusimamia bidhaa zitokanazo na maliasili hii hasa samaki. Serikali inapaswa kujenga viwanda vya kusindika samaki. Hii itasaidia kuongeza pato na pia ajira kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada ya leseni kwa mali za nje za uvuvi hapa nchini ni vyema ikaongezeka kutoka *USD 18,000* za sasa hadi *USD 100,000.* Hii itawezesha Serikali kukusanya pato kubwa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uvuvi unaweza kuongeza Pato la Taifa, ni vyema kwa Serikali kuwa makini katika kudhibiti uvuvi haramu ambao unaharibu mazalia na makazi ya samaki na hivyo kusababisha aina fulani ya samaki kuweza kupotea kabisa. Hii inapoteza kiasi fulani cha mapato kutokana na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kuna vivutio vingi vya utalii kama vile misitu, wanyama wa aina mbalimbali ambao nchi nyingine hawaonekani, fukwe zilizo safi hasa kule Zanzibar Mlima Kilimanjaro na kadhalika. Hivyo ni vema Serikali ikawa makini sasa kuvitumia vivutio vilivyopo vya utalii ili viweze kuchangia kwa kiasi kinachostahili katika Pato la Taifa letu. Ahsante.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ili kukuza maliasili Misitu, tunashukuru Serikali kuwezesha vikundi vya wafugaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea kupata mizinga 50 *complete* ya ufugaji wa nyuki kwa mtindo wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, tunaomba sana sasa vikundi hivyo vyenye mizinga vipatiwe sasa mafunzo maalumu ya ufugaji na hatua nyingi na zote za utengenezaji bidhaa za nyuki kwa teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji samaki, kwa kuwa mabwawa ya mbegu za samaki ya Luhira unamilikiwa au kuhudumiwa na Halmashauri ya Wilaya Songea, ambapo mara zote Serikali kuu imekuwa ikitoa fedha za kuendeleza uzalishaji mbegu bora katika mabwawa hayo. Lakini mabwawa hayo ni machakavu na hayajafanyiwa ukarabati muda mrefu ingawa umuhimu wa mabwawa hayo ni mkubwa sana. Tunaomba Serikali itusaidie kuyakarabati na kuongeza fedha za kuyaimarisha ili kuongeza tija katika maliasili samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tunaomba vikundi vya wafugaji samaki wafirikiwe kuwezeshwa kimafunzo na kirasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu Waziri na watendaji wake wote. Wizara hii ni ya umuhimu mkubwa sana katika kuchangia uchumi wa Taifa. Serikali imekuwa ikipoteza mapato mengi ama kwa kukusanya ushuru na ada ndogo au kutokukusanya kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na mkakati mpya wa kuongeza ushuru wa uwindaji wa simba, tembo, chui na kadhalika kwa kiwango japo kisichofikia cha nchi nyingine lakini kilicho kikubwa zaidi ya ilivyo sasa. Kwa namna hiyo napongeza uongezaji wa ushuru wa magogo, sasa naamini Serikali imeona mapendekezo ya Kambi ya Upinzani juu ya namna ya kukusanya mapato katika Wizara hii inawezekana.

Kuhusu sekta ya madini, Wizara hatukatai kufanya utafiti wa samaki mbalimbali lakini rasilimali zaidi zitumike kuwaendeleza wavuvi wadogo wadogo kiuwezo na kiutaalamu kwa kuwapatia zana mbalimbali za uvuvi na mtaji wa kujiendeleza.

Lakini vile vile Wizara itumie fursa ya meli za nje zinazovua katika bahati yetu kwa kutoza ada kubwa za leseni za uvuvi na pia kodi/ada kwa wingi wa samaki wanaovumiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magogo, hongera kwa kupandisha ada ya kusafirisha magogo baada ya kugundua wizi uliokuwa unafanywa katika usafirishaji wa magogo na mbao hata hivyo Wizara iwe makini katika kupanga bei za mbao ndani ya nchi. Bei ya mbao ikizidi kutawafanya Watanzania wapate kwa njia haramu na hii itawakosesha Serikali ada kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii, bado idadi ya watalii wanaoingia nchini ni ndogo sana lakini ni muhimu sana watalii wanaoingia nchini wawe wa daraja la juu watakaoingiza pato kubwa nchini. Baadhi ya watalii hulipia kila kitu kule kwao na hapa wanakuja kutembea tu, hao wasipewe nafasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mlima Kilimanjaro, ni *symbol* ya Tanzania. Watanzania tunajivunia. Lakini mapato ya utalii yaongezeke kulingana na hadhi ya mlima huu. Kilio chetu ni kwa wenye makampuni ya utalii kutothamini *tour operators* kwa kuwalipa fedha ndogo sana. Wizara ilione hili na iwasaidie vijana hao. Ahsante.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Jumanne Maghembe, kwa kazi nzuri kwa muda mfupi aliokaa hapo Wizarani mipango ya mwaka 2007/2008 ni ushahidi tosha kwani amegusa maeneo ambayo yalikuwa yanalindwa. Nampongeza pia Naibu Waziri Mheshimiwa Zabein Mhita pamoja Katibu Mkuu mpya mama Blandina Nyoni, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu nimekuwa nikieleza kero ya wapigakura wangu wa Kata za Sepuka na Mwaru haja vijiji vya Ighombwe na Msosa

kwa kusakamwa na wanyama wakali hasa tembo na simba ambao wamekuwa wakiua wananchi kadhaa. Pamoja na taarifa kupelekwa Wilayani, lakini askari wanyamapori wanachelewa kufika katika matukio. Narudia wananchi kadhaa wameuawa kijiji cha Ighombwe. Aidha, tembo wanaharibu sana mazao ya wananchi mwaka hadi mwaka na hakuna fidia yoyote kwa wananchi hao. Tatizo hili linakosa kushughulikiwa kwa sababu ya upungufu wa askari wanyamapori *(Game officers)* kwani Halmashauri yangu ina askari hao wawili tu *(only two)* na maeneo yenye wanyama wakali ni mengi Singida.

Mheshimiwa Mwenuyekiti, mara kadhaa nimeshauri askari hao waongezwe ili walau kila tarafa iwe na askari hao hasa Tarafa za Sepuka, Ikungi na Ihanja. Suala la fidia nalo linafaa kuangaliwa kwa viwango vya sasa kuboreshwa. Tatizo lingine ni ndege wajulikanao kama Kasuku (Silingu). Wanaathiri sana mazao kiasi kwamba wananchi wamekata tamaa ya kulima na hivyo kusababisha njaa. Nashauri ndege hawa waangamizwe kwa kutumia ndege. Serikali ilikuwa inaomba kibali cha kusafirisha ndege aina ya kasuku kwenda nchi za nje. Jambo ambalo litahamasisha wananchi hasa vijana kwa kuwatega na kuwakamata na kasha kuwasafirisha nchi za nje. Serikali imefikia wapi? Naomba maelezo na naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa hotuba hii nzuri inayotoa elimu na kuleta matumaini mapya ya maendeleo kwa nchi yetu kupitia Wizara hii.

Aidha, nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na watumishi wengine wote walio chini yake kwa kazi nzuri wazifanyazo kila leo ili mradi kuhakikisha kuwa Wizara hii inaendelea kustawi. Ni imani na matumaini kuwa chini ya Katibu Mkuu huyu mzalendo, makini na mchapakazi Wizara hii mapema iwezekanavyo itaelekea katika nafasi. Naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya pongezi hizo hapo juu naomba sasa nifanye maombi machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa ufugaji wa samaki, Wilaya ya Kwimba ndiyo Wilaya pekee isiyopakana na Ziwa. Wilaya hii ni kame, hivyo katika kipindi kirefu cha miezi 4 hadi 5 kitoweo kikuu huwa ni mboga za majani zilizokaushwa au samaki wakavu wakiwemo panki, samaki hawa wakiwemo wabichi watokao Ziwani huwa ni ghali sana kutokana na gharama za usafiri. Ni kutokana na kero hiyo ndipo umuhimu wa mradi tajwa umeingia kati kwa Wilaya ya Kwimba hasa jimbo la Kwimba mradi huu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba ni kupewa utaratibu wa kuanzisha miradi hiyo, mazingira ya kuanzisha mradi huo na nani Wizarani ninayaweza kuonana naye akanielekeza hatua muhimu. Maeneo ninayoyaombea miradi hiyo ni pamoja na Kata ya Mwakilyambiti na Mwamala, je, Mheshimiwa Waziri au mtaalamu yeyote mhusika anaweza kutembelea jimbo la Kwimba kufika katika maeneo hayo ili kusaidia katika kutoa ushauri wa kuwezesha uanzishwaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kibali cha kuvuna magogo katika pori la Butundwe kilichokuwa kimetolewa kwa Chama cha Mapinduzi – Kwimba, taarifa kuwa kibali hicho kilitolewa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi, Mkoa wa Mwanza. Taarifa ziliendelea kubainisha ya kuwa kutokana na uzembe wa Chama Wilaya kibali hicho alipewa mtu asiyejulikana na kukitumia kuvuna kiasi cha miti kilichokuwa kimetajwa katika kibali hicho.

Hata hivyo Chama Wilayani hakikuwa na taarifa yoyote juu ya kibali hicho na kuanzia muda tuliopewa taarifa hiyo ufutiliaji wa ukweli huo umekuwa nyuma licha ya ukweli kuwa kweli kiasi hicho cha miti (hadi leo Chama na Halmashauri) kinahitajika katika ujenzi wa shule na utengenezaji wa madawati katika shule za sekondari na msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kumwomba leo Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho au kwa njia nyingine iwayo yote anipatie taarifa juu ya ukweli kuhusiana na kibali hicho hususan taarifa ya kibali kilitolewa lini, kwa maombi yapi na ni nani alichukua kibali hicho na kiasi gani cha magogo kilivunwa kutokana na kibali hicho? Bado naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba nzuri sana yenye dira nzuri na mipango uliyogusa maeneo yote yatakavyosaidia kukusanya mapato au kuongeza mapato. Nampongeza Mheshimiwa Zabein Mhita, Naibu Waziri kwa kazi nzuri anazofanya, Katibu Mkuu bibi Blandina Nyoni kwa kuteuliwa katika Wizara hii hatuna wasiwasi naye kwani umuhimu wake wa kazi na mkubwa, ni imani yangu kuwa matunda mazuri yataonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze watendaji wote wa Wizara hii kwa jitihada zao kubwa za kuhakikisha kuwa mipango mkakati yote iliyopangwa na Serikali inatekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwashukuru *TANAPA* Idara ya Wanyama kwa kutuunga mkono kwa upande wa elimu kwa njia ya ujirani mwema. Tumefanikiwa kuwa na sekondari nzuri na hosteli ya kisasa ya wasichana katika Kata ya Madibira, Utengule Usangu na Ubariku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache ambayo nahitaji kupata ufafanuzi kuhusu upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kuunganisha la bonde la ardhi Oevu la Usanga. Lengo la Serikali ni zuri sana la kuzuia uvamizi katika bonde hili na sehemu vyanzo ya maji.

Mimi pamoja na wananchi wa Mbarali na uongozi wa Mkoa wa Mbeya tukiunga mkono na tulikubaliana kupitia kikao cha *RCC* vijiji saba na vitongoji viwili ndivyo vinavyohusika ambavyo ni Ikoga, Solowambo, Idunda, Mpayama, Msanyaji, Mhwele, Mkuuheri na kitongoji cha Aimike, Nyaluhanja, elimu ilikwishatolewa na wananchi wanachosubiri ni fidia na maandalizi ya sehemu wanayohamia.

Ufafanuzi ninaomba ni kuhusu barua ya tarehe 27 Aprili, 2007 iliyosainiwa na Mheshimiwa Waziri kuwa kuna vijiji vingine vilivyosahaulika vinatakiwa kuongezwa jambo ambalo sasa limeleta wasiwasi kuwa inawezekana kuwa wananchi hawa wakakosa kabisa sehemu za kuishi na kulima. Unaposema vijiji vingine viongezwe yaani Madundiasi, Luhanga, Iyola, Muhongole, Msongia, Lusaka, Kapurunge, Ifushirio, Ukwevila, maeneo yanayotegemea kwa kilimo itakuwa tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza uongozi wa Wilaya ushirikishwe ili tufikie muafaka katika kuweka mipaka. Vijiji ambavyo elimu ilishapitia naomba zoezi la kuwahamisha au kuwaandalia maeneo wanayopaswa kwenda uanze mapema. Kwa vile azimio la kuongeza hifadhi hii litaletwa Bungeni mwezi Novemba, 2007, wananchi wajulishwe kama wanaweza kuendelea na ulimaji wa mashamba yao na kufanya shughuli zao za maendeleo kwani kwa sasa hawaruhusiwi kufanya chochote cha kuongeza kipato chao.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa kazi nzuri wanayoifanya na kuhakikisha maendeleo yanapatikana. Wizara hii inafanyakazi kubwa ya kulinda maliasili zetu ili ziwe endelevu na ziendelee kutuletea kipato kinachoendana na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maliasili ya magogo bado Serikali haijaweka utaratibu mzuri wa uvunaji kwani hakuna utaratibu unaoeleweka, ukija kwa hawa wanaojiita wazawa ndio waharibifu wakubwa wa misitu hii lakini pia hawa wageni wanapoingia wakikuta vurugu hii huwa wanakuwa wanashirikiana na wananchi kuzidisha uharibifu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leseni/vibali vya ukataji wa magogo naomba wale wote waliopewa leseni/kibali cha ukataji wa magogo viangaliwe upya ili Serikali iweze kujiridhisha na wafanyabiashara ya magogo na pale akigundulika mbababaishaji aweze kunyang'anywa kibali na kuchukuliwa hatua zinazofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kupandisha kodi na mauzo ya maliasili zetu ili zikaribiane na soko la nchi nyingine, ushauri wangu huu ni mawazo tu, ipo haja sasa kuangalia uingiaji wa watalii nchini ili kuendelea kuangalia tena kuongeza bei ya kodi na mauzo kufikia sawasawa na nchi nyingine hii itategemea watalii watakavyoweza kuingia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa watalaamu wa Serikali wanaweza kuishauri Serikali ni mambo gani ya kale yanaweza kuwa ni ya kitalii. Je, kwa nini hawafanyi hivyo pamoja na makumbusho mazuri makubwa ili tukaweza kuyatangaza kitalii ili tukaweza kuongeza mapato zaidi kwenye utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuwa watalaamu wetu wapelekwe nchi zilizoendelea kwa utalii ili waweze kujifunza na kuweza kuongeza kuimarisha utalii nchini na ongezeko la mapato litaonekana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo maliasili nyingi na nzuri ila hatujajipanga vizuri, tutoe elimu mara kwa mara kwa watendaji wetu elimu ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi, azma ya Serikali ni kumsaidia mvuvi kwani wavuvi wengi ni maskini wenye kipato cha chini. Serikali ilipoleta mradi huu wa *MACEMP* wenye mtaji wa dola milioni 61 za Kimarekani azma ni mazingira ya bahari pamoja na kumsaidia mvuvi mpaka hii leo fedha hizi zimefanya nini kwa kule Zanzibar hata kule Mkoa wa Kaskazini Unguja ni miradi mingapi wananchi wa kule wamefaidika au mipango ya fedha hizi kwa Zanzibar ikoje ili kuwaweka vizuri kwa upokeaji mradi huu wananchi, basi Wabunge wote tunaotokea maeneo hayo ya mradi huu tupatiwe semina ili tuweze kuwaweka vizuri wananchi kwa utekelezaji wa mradi huo hata kama mradi huu si wa siasa ni wananchi viongozi ndiyo wahamasishaji wakuu wa wananchi.

Naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote kwa kazi kubwa wanazofanya na zenye mafanikio makukbwa, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utafiti wa wanyamapori na kadhalika, nashauri taasisi za utafiti ziongezewe fedha, maalumu ni Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania *(TAWIRI);* Bajeti yake bado ni ndogo ukilinganisha na taasisi zingine za Wizara, licha ya *TAWIRI* kuwa na kazi nyingi, kubwa na muhimu sana kwa uhifadhi wa wanyamapori. Si lazima *TAWIRI* ikategemea fedha za Bajeti ya Serikali pekee. Utaratibu urejewe wa mamlaka za usimamizi wanyamapori kuchangia kila mwaka fedha za utafiti kwa *TAWIRI.* Utaratibu huu uwe wa kudumu na unaoeleweka kwa wahusika wote.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, miti ni maliasili kama rasilimali nyingine ni lazima ivunwe na iuzwe ili Serikali ipate mapato kwa ajili ya kuwaletea wananchi maendeleo. Ushauri wangu ni kwamba Serikali itilie mkazo katika mambo yafuatayo; kwanza, wananchi wahimizwe kumiliki mashamba ya miti. Aidha, zoezi la upandaji miti liwe endelevu na pili umakini mkubwa uwepo katika kutunza misitu asilia, misitu asilia isivunwe au kuuzwa maana kuirudisha misitu asilia ni zoezi la muda mrefu sana na si rahisi kurudisha uoto wake wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misitu ya Mfwemela, misitu hii ipo katika Wilaya ya Mpwapwa, Jimbo la Kibakwe katika Kijiji cha Mbuga, misitu hii ipo katika milima Tao la Mashariki, ni misitu ambayo ina Bioanuai *(Biodiversity)* ya aina yake na imetangazwa kama *one of the World Heritage Site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 48 wa hotuba ya Waziri ameyataja maeneo tengefu kwa mwaka 2006/2007, katika orodha hiyo sijasikia kama Mafwemela imetajwa, naomba maelezo au nieleweshwe Wizara ina mpango gani wa kulitunza eneo hili ambalo lina viumbe na mimea ambayo haipatikani sehemu nyingine. Naomba maelezo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali kupitia *GN. NO 161* ya 29 Juni, 2007 imetangaza upandishwaji wa bei ya mazao ya misitu. Japokuwa dhana nzima inaonekana ni ya kutaka kupandisha mapato kwa Serikali, kuna malalamiko mengi hasa kutoka kwa wavunaji wadogo wadogo kwamba kwa kipindi cha miaka mitano kumekuwa na ongezeko la zaidi ya 300% ya kwamba ongezeko husika linapelekea Tanzania kuwa na gharama kubwa zaidi kulinganisha na gharama za nchi za *SADC* hali itakayopelekea wanunuzi wadogo wa ndani kushindwa katika ushindani hali ambayo yaweza kusababisha uagizwaji wa mbao toka nje hasa nchi za jirani kukua kwa kasi zaidi. Kwa mantiki hiyo naomba nipate ufafanuzi ni kwa kiasi gani mabadiliko haya yatamnufaisha mfanyabiashara mdogo wa mbao wa mtumiaji wa bidhaa za mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitalu, kumekuwa na malalamiko mengi juu ya suala zima la umiliki wa vitalu vya uwindaji na kwamba kumekuwa na malalamiko mengi juu ya umiliki husika na kwamba hakuna njia madhubuti za kudhibiti usafirishaji wa wanyama. Kwa kuwa kumekuwa na utata katika suala zima la vitalu, naomba nipatiwe majibu yafuatayo; kuna idadi ngapi ya vitalu vya wanyama nchini, nani ni wamiliki wa vitalu husika, ni wastani wa wanyama wangapi wanavunwa kwa mwaka na udhibiti unafanyika vipi hasa ukizingatia kuna taarifa zinazoonyesha kwamba idadi ya wanyama wanaochukuliwa kinyume na makubaliano, ni mapato kiasi yamepatikana kutokana na vitalu husika na ni ajira kiasi gani zimepatikana kutokana na vitalu husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipatiwe ufafanuzi tafadhali.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kuwasilisha Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2007/2008 ya Wizara yake kwa umahiri na ufasaha mkubwa. Naiona hotuba hii ya Waziri kuwa mwanzo wa ukombozi wa sekta ya maliasili na utalii kutoka kwenye hali ya uduni na udhaifu wa kujitakia wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hatua zote ambazo Wizara imependekeza kuchukua katika mwaka mpya wa fedha zikiwemo ongezeko la ada ya kuwinda wanyama, ada za kukodi maeneo ya kujenga hoteli na ada za vitalu vya uwindaji, ukusanyaji wa mapato kwenye hifadhi zetu kwa *smart cards* na *credit cards,* ongezeko la bei za mazao ya misitu hususan magogo kutoka kwenye mashamba ya miti na misitu ya asili na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hatua hizi, ninayo mapendekezo machache ambayo ningependa Wizara iyatupie jicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ongezeko la *game fees* na ada zingine kwa upande wa wanyamapori, limezingatia ada zilizopo nchi za SADC. Je, ongezeko hili imezingatia vile vile kuwa nchi zingine za *SADC* zina msururu wa ada za ziada tulizonazo na kama vile *conservation fees, trophy handling fees, professional hunters license fees*, *professional hunters examination fees* na *permit fees* ambazo Waziri amezitaja ukurasa wa 74 wa hotuba yake? Ikiwa ada hizo za ziada hazikuzingatiwa au

hazipo katika nchi hizo tunazojilinganisha nazo, basi upo umuhimu wa kuzipitia upya ili zisiwe kikwazo kwa wateja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uanzishaji wa matumizi ya *smart cards* katika hifadhi zetu ni mzuri ingawa umechelewa sana. Kwa kuwa nchi kama Kenya ilianza kutumia *smart cards* miaka kadhaa iliyopita na miaka ya mwanzo ya matumizi ya utaratibu huo iliwasababishia hasara kubwa kutokana na wizi wa kielektroniki ni vema kwa *TANAPA* kutuma watendaji wake nchini Kenya hujifunza kuhusu *loopholes* zilizopo katika mfumo huo mpya ili tusije tukalizwa, hii ni tahadhari tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara ielekeze nguvu zake sasa katika kuleta mapinduzi kwenye uendeshaji wa biashara ya uwindaji kwa kuweka utaratibu wa kisheria ambapo wananchi wawe na hisa ya asilimia zaidi ya 30 katika makampuni ya wageni. Hakuna sababu yoyote ya msingi kuendelea kuruhusu wageni kutawala biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kabisa kwa niaba ya wananchi wangu wa Wilaya ya Hai, naomba mpokee pongezi na shukrani za dhati kabisa kwa kazi nzuri sana mnayoifanya na kwa viwango vya hali ya juu kabisa tangu kuundwa kwa Wizara hiyo nikianzia kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote wale wenye moyo wa uzalendo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mnatenda kwa viwango kwa sababu ya mageuzi makubwa sana mliyoyafanya na mnayoendelea kuyafanya hapo Wizarani ambayo yameanza kuwarudishia imani wananchi kwa ujumla kwani wengi walishaona kwamba wageni ndio wenye nchi na Watanzania ni wananchi kwa maana ya wageni kupewa kila kilicho kinono tena kwa bei poa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi naomba nitoe ushauri ufuatao. Kuhusu utambuzi wa vivutio na maeneo ya utalii, nashauri kuwepo na mkakati wa Kitaifa kwa kila Mkoa kuyatambua maeneo yote yaliyopo kwenye kila mkoa kwani naamini hakuna mkoa utakaokosa vivutio vya kitalii kwa mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuutangaza utalii wetu nje ya nchi, nashauri tuutangaze utalii wetu nje ya nchi kwa bidii zaidi na kwa mbinu nyingi zaidi kwa mfano kwenye Balozi zetu wawepo watu wenye kuufahamu utalii wetu vizuri na waliobebea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii wa kitamaduni/kiasili, nashauri dhana ya *cultural tourism* ienezwe kwa nchi nzima kwa maana ya utalii kwenye vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitalu vya uwindaji, nashauri vitalu vyote vya uwindaji vikodishwe kwa wazalendo tu ambao ndio watakaoingia mikataba na wageni na siyo wageni kukodishiwa vitalu kwa maana ya kuwawezesha wazalendo kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za watalii, nashauri tujielekeze kutoa huduma zenye viwango vya hali ya juu kwa sababu ya ushindani uliopo duniani ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha Watanzania wengi zaidi katika vyuo vyetu vya utalii pamoja na huduma nyingine kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite Wilayani/Jimboni Hai, kule Wilayani kwetu tunavyo vivutio vingi sana vya utalii nikianza upande wa tambarare yale maji ya joto yanayotoka ardhini katika Kijiji cha Chekimaji, Mingurumo na sauti mbalimbali katika eneo hilo, kule uwanda wa mlimani yapo mapango mengi yaliyotumika na babu zetu wakati wa vita kwa mfano Kijiji cha Ngira na Masama Mashariki.

Sasa kikubwa na kizuri sana kwa ajili ya wananchi wa Hai pamoja na kwa Taifa zima ni njia mpya ya kupanda mlima Kilimanjaro inayoanzia umbali mfupi sana kutoka kiwanja cha ndege cha *KIA* yaani pale Kwa Sadala, Masama Mula hadi Nguni msituni kuingia mlimani.

Mheshimiwa Mwenyekiit. *added advantage* ya *route* hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete wakati wa kampeni ya kujengwa kwa kiwango cha lami kipande korofi cha barabara hii yaani kuanzia Kwa Sadala, Masama Kati Kanisani, Masama Mula, Salali, Sonu. Nimeongea na Balozi wa heshima wa Hungary na ameonyesha uwezekano wa nchi anayoiwakilisha kukubali kusaidia kufungua *route* hii na kuleta watu wa kufundisha vijana wetu kazi za kusaidia wapanda mlima na kutangaza *route* hii mpya nje ya nchi kwa sababu ya utofauti wake na njia zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa maeneo yenye migodi ya madini hapa nchini ambapo wawekezaji hulipa Halmashauri katika maeneo husika kiasi cha *USD 200,000* kwa mwaka, basi nami napendekeza na kushauri kwamba Halmashauri zote zinazozunguka Mlima Kilimanjaro zipewe pesa kwa mwaka kiasi fulani kutokana na mapato ya Mlima Kilimanjaro badala ya hiki kinachofanyika na *TANAPA* hivi sasa kama vile ni hisani tu na wala siyo lazima, hivyo tukae na kukubaliana gawio kamili kwa kila Halmashauri japo kwa kuanzia *USD 200,000* kwa mwaka kwani huu mlima na sisi ndio mgodi wetu Mwenyezi Mungu aliotujalia. Wananchi wanaouzunguka mlima huu ndio wanashiriki kuzima moto utokeapo, kulinda rasilimali zilizopo mlimani pamoja na kuuhifadhi, Mlima Kilimanjaro huingiza mapato makubwa kushinda chanzo kingine chochote cha utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongezeni kwa hatua zote mlizoanza kuchukua na mnazoendelea nazo, hongereni sana na tutaendelea kuwaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima wa afya na kunijalia kuchangia hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuwasilisha hotuba hii yenye dira na mwongozo, pia niwapongeze watendaji wote

wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kushirikiana vyema na viongozi wao na kufanikisha kitabu cha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara hii kwa ujumla kwa kazi nzuri na hasa kwa kuwajali wazalendo wa nchi hii kwa kuwapa vibali kuanzisha *zoo* na kuwasaidia kwa kila hali kwa kufanikisha azma zao. Hali hii ni ya kupongezwa kwani hali hii pia imeongeza ajira kwa vijana na kutumiza ahadi ya Rais na Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimebahatika kutembelea *zoo* iliyopo Kisarawe juu katika Jimbo la Kigamboni na kutokana na misaada wanayopatiwa na Wizara pamoja na Serikali wameniomba nitoe salamu zao kwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa yale yote mazuri na wanaomba wasichoke kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa na Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na wadau wengine kuandaa kanuni za kusimamia uvuvi kwenye bahari kuu, huu ni mwanzo mzuri wa kuondoa migogoro inayotokea mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara hizi pamoja na Serikali zetu mbili pia kushughulikia wavuvi wadogo wadogo ambao hufanywa na wananchi wetu wa nchi hii mara kwa mara hutokea matatizo kwa wavuvi hawa hasa wanapoweka dago katika fukwe na visiwa vidogo vidogo vilivyoko katika bahari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko ya wavuvi hao kutazwa fedha na kusingizia ni lazima akate leseni mpya ya sehemu alikokwenda kuvua na wakati mwingine kufukuzwa na kupoteza vifaa na mali yao na pia husababisha mapigano na hatimaye vifo na majanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara hii na Wizara ya Kilimo, kuziondoa kasoro hizi kwa kuwaelimisha wahusika na kipi kifanyike kwa anayetaka kwenda kuvua katika sehemu moja ya nchi hii na taratibu gani zifuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchango huu mdogo ambao lengo langu ni kuondoa migogoro naunga mkono hoja hii.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipongeze Wizara hii kwa kusimamia vizuri pamoja na Waziri Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na Naibu wake Mheshimiwa Zabein Mhita pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kwenda awamu ya nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maliasili za bahari, kwa kweli maliasili za baharini zipo nyingi lakini bado Serikali inahitaji kutoa elimu na kutafuta wataalamu hata wa nje ya nchi ili kuweza kutumia mali hizo na kuuza ili kupata fedha za kigeni. Maliasili za nchi kavu vile vile zitunzwe na tuzitumie kwa uzuri na kujali hali ya mazingira kwa Pato la Taifa, wanyamapori waendelee kutunzwa, maendeleo yake yawepo kwa aina ya

wanyama na mapori ya kuhifadhi ili tufaidike kwa yote na watalii waweze kuingia kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii, utalii utakua na kuleta fedha nyingi ndani ya nchi lakini naomba sana Wizara kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Elimu itolewe, bahari zitumike vizuri na fukwe zetu zote za mwambao zihifadhiwe, kuwekwe vivutio na huduma za utalii viwepo na vijana wa kutembeza wageni *(guide tour)* na waelimishwe kujua lugha nyingi au zote za wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa rasilimali uwepo na sekta ya uvuvi wa samaki iendelezwe ili kuhifadhi samaki wadogo, mayai ya samaki kuepusha wale waliokuwa na tamaa ya kutaka samaki wote kwa siku moja kwa kutumia uvuvi haramu. Naiomba Wizara izidi kutoa elimu na wale wanaoendelee na hayo wachukuliwe hatua kali kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni na mimi naunga mkono hoja hii mia kwa mia na Bajeti ipite.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa awali ya yote naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu kwa Waziri, ndugu yangu Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo pamoja na watendaji wa Wizara kwa ujumla, Wizara hii ni ngumu sana hasa ukizingatia kuwa ina vyanzo vingi sana vya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; kwanza, maeneo ya Geita yana mapori ya asili kwa kuwa kumekuwa na matatizo ya ardhi na wengi sana tumeshajua uzuri wa utunzaji wa mazingira, ningeomba maeneo kama haya yaanzishwe au uanzishwe mradi wa ufugaji nyuki kwa kuwashirikisha wananchi wenye kipato cha chini. Itakumbukwa miaka ya 1960 zao la asali na nta lilikuwa linaliingizia Taifa letu fedha nyingi kutoka nje hivyo kwa mantiki hiyo tuwe na kanda ya kuzalisha zao la nyuki, kwa mfano Wilaya ya Geita, Kahama, Biharamlo, Cheto na Bukombe kuwa na kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hakuna ulinzi wa mali inayotokana na maziwa yetu na bahari kuu kwa kuwa ulinzi katika Ziwa Victoria ni wa kusuasua kiasi ambacho hata mipaka haijulikani hadi wananchi wa nchi za jirani wanaingia nchini na kuishi katika visiwa ndani ya Ziwa bila bughudha yoyote hasa ikizingatiwa kuwa huko visiwani hakuna maafisa uhamiaji wala polisi hawafiki huko. Matokeo yaliyopo huko ni kila mtu anakuwa na Serikali yake na kusababisha wahalifu wengi kutoka ndani na nje ya Tanzania kujificha kwenye visiwa hivyo na kuweza kurahisisha kuendeleza kazi zao za unyang'anyi wa injini, nyavu na samaki kwa wavuvi wadogo wadogo bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa hili kununua vyombo vya doria ili kulinda vyombo vya doria katika mipaka yetu na kuzuia wahamiaji haramu ambao

wanachafua sifa ya nchi yetu. Pia Ziwa ni sawa na hifadhi, ina maana kuwa uvunaji ukiwa mkubwa kuliko uzalishaji, kuliko mazalia ya samaki mtakuta baada ya miaka kadhaa hatutakuwa na samaki kabisa. Kwa maana hiyo naiomba Serikali itoe leseni kwa kuvuna kwa vipindi maalumu au wawe na vifalu vya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nasema naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ningependa niunge mkono hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Maliasilia na Utalii Mheshimiwa Profesa Maghembe, kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya Wizara hii kwa ufanisi mkubwa. Pia ningependa nimpongeze Naibu Waziri wake Mheshimiwa Zabein Mhita, kwanza ameonyesha uwezo mkubwa katika kipindi kifupi alichokuwepo katika Wizara hii. Pia ningependa niwapongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa Bajeti nzuri iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi inayo rasiliamali kubwa ya wanyamapori na katika Wilaya ya Nanyumbu kuna hifadhi ya uwindaji ya Lukwika ambayo katika maeneo mengi hifadhi hii hupakana na vijiji. Wananchi walio kando kando ya hifadhi hii huwa wanafanya shughuli zao za uzalishaji mali na hasa kilimo na mazao ya chakula na biashara. Mara nyingi juhudi hizi za wananchi zimekuwa zikikatishwa na wanyama waharibifu hasa tembo. Tembo hawa ambao tunadhani wamezaliana kwa wingi katika hifadhi hii ya Lukwika kwa mfano wamekula na kuharibu mazao mengi ya chakula na biashara katika vijiji kama Chimika, Mpombe, Bulusa, Chipukuta, Mpwahiya, Nanyumbu, Yumesule, Masugulu na vijiji vingi vinginevyo hivyo kuleta uhaba mkubwa wa chakula mwaka huu 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara hii kufanya juhudi za makusudi kuongeza ulinzi katika hifadhi hii kwa kupeleka maafisa wanyamapori kwa lengo la kuongeza doria na kuhakikisha kuwa tembo hawa hawavuki na kwenda maeneo ya wananchi. Hapa Serikali inaombwa kuwasaidia wananchi walioathirika na uharibifu huo kwa kuwapatia chakula cha msaada hasa katika Kata za Napacho, Chipuputa na Masuguru kwa kumaliza namuomba Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita, atimize ahadi yake ya kutembelea Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya misitu, Wilaya ya Nanyumbu imebahatika sana kuwa na misitu mikubwa mizuri na ya asili. Kumekuwepo na uvunaji wa kutisha wa mbao na magogo hasa miaka miwili iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya hii ina miti mingi aina ya mpingo ambayo kukomaa kwake kunachukua miaka mingi, naiomba Wizara ichukue hatua za makusudi

kuiokoa mipingo katika Wilaya hii kwani imekuwa ikivunwa kwa kasi kubwa na kuathiri hata mipingo midogo baada ya wavunaji kumaliza ile mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii, mikoa ya Kusini ina sehemu za vivutio kwa utalii. Pwani na fukwe za mikoa ya Mtwara na Lindi ni mizuri sana kwa utalii. Ujenzi wa Daraja la Umoja na barabara ya Masasi - Mangaka itakayojengwa hivi karibuni ni kichocheo kwa watalii. Hata hivyo tunaiomba Serikali kuchochea uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi wawekeze katika utalii katika mikoa ya Kusini na kuongeza kuitangaza Lukwika ambayo ni msitu wa uwindaji na Mto Ruvuma ambao pia ni mzuri kwa utalii katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya uvuvi, Wilaya ya Nanyumbu ina bahati ya kuwa na mto mkubwa wa Ruvuma ambao uko mpakani mwa nchi yetu ya Msumbuji. Lakini kwa baadhi ya maeneo ambayo Wizara hii ya Maliasili na Utalii inawakataza wananchi wasifanye shughuli za uvuvi katika mto huo hivyo kuwanyima wananchi kupata kitoweo na kufanya shughuli za biashara. Naiomba Serikali itoe tamko la kuwaruhusu wananchi kufanya shughuli za uvuvi katika Mto Ruvuma kwa wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuiunga mkono hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri mnayofanya. Aidha, napenda kuchangia machache katika kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbao zinazotoka sehemu za Nyanda za Juu Kusini *(soft wood)* ni muhimu sana katika suala zima la ujenzi wa nyumba hasa hasa za wanyonge na kwa hali ilivyo bei ni kubwa na huenda ikawa kubwa zaidi. Kutokana na umhimu huo naiomba Wizara ijitahidi kudhibiti bei ili bidhaa hii wananchi waweze kuinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwindaji wa kitalii, ningependa Mheshimiwa Waziri anieleze mimi Mbunge kuhusu ugavi wa vitalu hivi unamilikiwa vipi? Je, ni wageni tu wenye kumiliki au wananchi wa Tanzania pia wanamiliki na ni kwa kiasi gani?

Aidha, ningependa kuelewa jinsi vitalu hivi wanavyochangia siyo tu uchumi wa Taifa bali pia wamiliki wa vitalu wanavyochangia Halmashauri na Manispaa husika. Kwa kuwa hali halisi inaonyesha kuwa kuna meli za uvuvi katika mwambao wa Pemba Kaskazini ambazo hukaa muda mrefu kuvua pengine isivyohalali, je, Wizara hii inasaidiana vipi na Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mazingira ya Zanzibar ili kudhibiti uvuvi huu haramu na holela. Nashukuru na kila la heri.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu zilizosahaulika. Pamoja na vivutio kama milima, mabonde na mbuga za wanyama bado kuna vivutio vingi vilivyosahaulika. Mkoa wa Bagamoyo ni maskini lakini kama vivutio vilivyopo vitapewa umuhimu, pato la Mkoa litaongezeka. Bagamoyo imesheheni historia

ya watumwa, wavumbuzi kama vile *Livingstone,* Kanisa la kwanza, nyumba au mabaki ya nyumba za karne ya 14 hadi 17.

Kuhusu Bagamoyo iko karibu na Dar es Salaam na Arusha. Bagamoyo ina hoteli nzuri sana, je, ni lini Serikali itatoa kipaumbele kwa vivutio vya Bagamoyo kuweka *tour guide* wa kuelezea vivutio hivyo na lini nyumba za kale hizo zitakarabatiwa? Kuna kaburi la Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Yeye alikuwa kiongozi wa Kitaifa na Kimataifa, alipendwa na kuheshimiwa na watu wengi duniani. Ningependa kujua ni lini mazingira na miundombinu itaboreshwa kuruhusu watalii wanaotaka kuona kaburi la kiongozi huyo shupavu kufanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukatwa misitu ya asili ovyo, Mkoa wa Kagera ulikuwa na misitu ya asili mingi sana, mingi imetoweka kwa sababu ya miti kukatwa ovyo. Kinachochangia uvunaji holela ni vibali vinavyotolewa kutoka ngazi mbalimbali bila ya udhibiti wa kutosha. Naambiwa kuna misitu ya Serikali Kuu, kuna misitu ya Halmashauri za Wilaya na kuna misitu ya vijiji, viongozi wa vijiji wanashuhudia misitu inakatwa kwa kisingizio kuwa wamepata vibali Serikalini. Kwa vile hakuna *coordination* kati ya Serikali Kuu na Halmashauri (watoa vibali), watu wanatumia mwanya huu kuiba na kukata miti hii bila vibali. Ni lini sasa Serikali itatoa utata huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nawapongeza Wizara kwa mipango mizuri iliyo kwenye hotuba ya Waziri. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nawapongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa hotuba nzuri.

Kwa nini bei hizo za kuwinda tembo, chui na simba hazizidi hata dola 20. Tunaogopa nini wakati sisi Tanzania *we have the best lion in the world?* Nashauri mzipandishe japo zingekuwa dola 100. Kuna hisia kuwa baadhi ya watumishi hununua vibali hivyo kwa bei ya chini hizo dola moja na kuziuza tena kwa dola 100 kabla hajapandisha bei.

Kuhusu kuhifadhi mali kale, je, Wizara ina mpango gani wa kuangalia kivutio cha Tanga cha Mapango ya Amboni? Ni kwa kiasi gani Wizara inakarabati mazingira haya hasa baada ya yale wafuriko yaliyoharibu mandhari ya *Amboni Caves* kule Tanga hivi karibuni? Naomba ufafanuzi. Je, mna habari na eneo la pale Tanga chumvi chumvi penye maji yenye *sulphur* na yakiwa moto (vuguvugu) ambalo hutumiwa na wananchi kwa matibabu ya magonjwa ya ngozi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani anashughulikia Wizara au Manispaa kama ni Wizara kuna mpango gani wa kuboresha? *All the best.*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara hiyo kwa kutengeneza hotuba nzuri iliyojaa mambo ya kuleta maendeleo.

Naomba kumpongeza Katibu Mkuu Ndugu Blandina Nyoni, binafsi huyu mwanadada anafahamika kwa kuwa mchapakazi makini. Tunaimani kuwa Wizara itaongeze ufanisi katika utendaji wake.

Kuhusu misitu, tunaomba tusimamishe kwa dhati ufyekaji wa miti (magogo) ovyo hasa kutoka katika misitu ya Wilaya Rufiji. Ombi lingine ni kufanyike utafiti wa *scientific forest density* ya misitu yetu. Matokeo ya utafiti huo ndio yawe dira ya kuruhusu kiasi cha magogo yanaweza kuvunwa kwa mwaka. Aidha, utafiti huo utuwezeshe kuwa mwongozo wa *reforestation* ya sehemu iliyokwishafyekwa huko Rufiji, Kilwa na Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara sasa ilivalie njuga suala la kuitangaza Mbuga za Hifadhi ya Selous kule Rufiji, tunaomba mbuga hii itangazwa kwa dhati dunia nzima. Tuongeze ujenzi wa hoteli za kitalii katika Mbuga hizo na tunaomba Selous ing'are nayo ili tuongeze biashara ya utalii katika Wilaya ya Rufiji, Kilwa na Liwale. Kwa vile sasa bei ya vitalu vya uwindaji imeongezeka na kwa vile mahitaji ya maendeleo ya wanavijiji yanazidi kuongezeka, sasa mchango wa 25% inayolipwa kwa mwaka inabidi uongezeke ufike angao ufike 40% kwa mwaka kwa ajili ya kusukuma maendeleo katika vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mabwawa ya asili hasa katika Wilaya ya Rufiji na yamejaa samaki hapo zamani, wananchi walikuwa wanapewa kibali cha kuvua kwa muda maalumu vibali hivi vilikuwa vinahalalisha uvuvi katika mabwawa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Warufiji tunawaomba tena vibali vya kuvua katika mabwawa ya asili yaliyo katika Hifadhi ya Selous, Wilaya ya Rufiji virudishwe ili wananchi wapate fursa ya kuvua samaki kwa ajili ya chakula na biashara. Utaratibu huu utainua na kuongeza MKUKUTA wa wananchi wa Rufiji. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa jitihada anazozifanya katika kuzitangaza maliasili zetu duniani kote ikiwemo utalii, wanyama pori, uvuvi na kadhalika kwa kuiweka Tanzania kuwa ni nchi mojawapo yenye vivutio vya duniani. Kwa juhudi zake sasa hivi Tanzania tutaanza kutangazwa katika *CCN International.* Naomba viongozi na watendaji wakuu wamuunge mkono Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zake kubwa anazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza pia Naibu Waziri Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa juhudi zake na ukaribu wake na Kamati ya Maliasili na Utalii. Kero kubwa niliyokuwa nayo ni usafirishaji na uvunaji holela wa magogo kutoka Mkoa wa Lindi na Pwani, hii idara bado haimuungi mkono Waziri kwa vile bado mianya ni mikubwa na bado misitu inakatwa ovyo na kusafirishwa nchi nje bila kuionea huruma nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari bubu za bidhaa katika Mikoa ya Lindi na Pwani inabidi kufuatilia na kuweka ulinzi wa kutosha na doria katika bahari na maziwa yetu ili kuhakikisha kuwa mali yetu ya asili (magogo na mikoko) inalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kupitia Idara ya Uvuvi napenda kushauri kuwa imefika wakati idara hii ibadilike na kuwasaidia wavuvi wetu ambao ni maskini wa kutupwa, wanahitaji mafunzo na miongozo mbalimbali itakayowaondolea adha ya umaskini. Katika kuendeleza uvuvi wa bahari kwa kuanzisha viwanda kwa kusindika samaki itasaidia kuleta ajira kwa wananchi na pia itaitoa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa Lindi lakini cha kushangaza sijaona mikakati inayofanywa na *MACEMP* katika kuendeleza maendeleo ya uvuvi zaidi ya semina nyingi kuliko kulenga maendeleo ya uvuvi na kuingizia kipato. Napenda kutoa pongezi kwa Mkurugenzi wa wanyamapori kwa kuiona Liwale, ni misaada ambayo ameanzisha kuipelekea, kwa niaba ya wananchi wa Liwale wanatoa pongezi za dhati kwa misaada ikiwemo ya vijana watatu walemavu wa familia moja, ni juhudi anazozifanya kuwasaidia vijana hawa. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie upya ushuru wa magogo na mbao kwa sababu wananchi hawatamudu na wavunaji wadogo wadogo pia watatoweka na ile dhana ya maisha bora kwa kila Mtanzania itabaki kama ndoto. Ushuru uliopanda toka shilingi 70,000/= hadi shilingi 250,000/= na shilingi 60,000/= hadi shilingi 200,000/= kwa mita ni mkubwa mno ukilinganisha na ushuru wa msituni kabla ubao haujatoka nje ya msitu. Nina hakika kuwa mwananchi wa kawaida hawezi kununua ubao kwa shilingi 40/= hadi 50/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri na wataalam wake waliangalie suala hili la bei. Ushuru kwa wavunaji wa ndani na wanaohudumia wananchi wa kawaida usiongezwe kwa kiasi kikubwa bali kwa wale ambao wanapeleka nje ya nchi na yale makampuni makubwa yanayovuna mazao haya kwa kutumia mashine. Katika mradi wa Serikali usimamizi wa Bahari na Mazingira ya Pwani *(MACEMP),* je, ni kweli kuwa baadhi ya miamba ya Kilwa Kivinje, Masoko, Somanga na Songosongo inatakiwa kuwekwa hifadhi? Kama kweli majina ya miamba hiyo ni yapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ili wananchi wa Kilwa na Pwani wafahamu.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii, napongeza juhudi zinazofanywa kukuza utalii nchini, pamoja na juhudi hizi naomba kuzungumzia uendelezaji wa maeneo ya utalii Mkoani Iringa. Mkoa wa Iringa una maeneo mengi ya historia yakiwemo eneo la Lufulo, Kalenga na kadhalika. Lakini maeneo haya hayajapewa uzito unaostahili ikiwa ni pamoja na kuweka vivutio kwa wananchi. Lufulo inahitaji kujengwa mnara badala ya

kutegemea ule uliopo na Wajerumani, pembeni mwake ujengwe mnara wa kuwakumbuka Watanzania waliokufa katika vita katika eneo hilo. Makumbusho ya Kalenga yatangazwe ili watalii waje hivyo eneo linahitaji pia kuimarishwa ikiwa ni pamoja na majengo na wafanyakazi kupata motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya utalii itolewe kwa wananchi wanaozunguka maeneo haya na wahamasishwe na kupewa miradi midogo midogo kuendeleza utengenezaji wa vifaa vya asili ambavyo uuzaji wake utawasaidia kuinua kipato chao hasa wanawake na vijana. Napongeza kazi nzuri inayofanywa na *TANAPA* hasa katika utekelezaji wa miradi ya ujirani mwema. Naomba wasaidie maeneo ya jirani na *National Parks* mitaji kuendeleza miradi ya kiuchumi hasa kwa vikundi vya wanawake Wilaya ya Kilolo, Makete na Wilaya ya Iringa Vijijini ili kuweza kupata kipato na kuweza kulinda maliasili katika hifadhi zinazowazunguka kama Udzungwa, Ruaha na Kitulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kiwanja cha ndege ya Nduli, tunaomba Serikali itusaidie kuhamasisha wawekezaji kutumia uwanja wa ndege wa Nduli kwa kufanya safari angalau mara mbili kwa wiki, hii itasaidia kuleta watalii na wawekezaji wengine Mkoani. Kuhusu ujenzi wa hoteli za kitalii Mkoani Iringa, Serikali itusaidie kuhamasisha wawekezaji kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja hii.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa heshima naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara wote kwa hotuba nzuri iliyojaa utaalamu na mpango mzuri ya kuleta mafanikio ya kiuchumi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachangia sekta zifuatazo, kwanza ni sekta ya uvuvi, katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu ni dhahiri kwamba sasa tutumie kwa bidii uvuvi wa bahari yetu kuu na maziwa yetu makuu kwa vile vyombo vyetu vya uvuvi ni kidogo na havina uwezo wa kiuchumi. Bahari yetu kuu basi Serikali itafute wawekezaji ili tupate meli ya uvuvi ya kisasa yeenye zana za utaalamu wa kisasa na utayarishaji wa minofu ta samaki na kuweza kusafirisha.

Pili ni sekta ya utalii. Utalii ni sehemu ya kunyanyua uchumi wetu kwani Tanzania ina utajiri mkubwa kwa vivutio vya utalii. Tuna mali kale nzuri, tuna fukwe safi kabisa, tuna makumbusho ya mambo ya kihistoria mazuri kabisa ukitilia maanani visiwa vya Unguja na Pemba ambayo umejaa vivutio vya kihistoria pamoja na viungo mbalimbali yaani *(spices Islands).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu sekta ya misitu na nyuki ni eneo lingine kuu la kuleta fedha na kuongeza uchumi wetu katika Taifa ni sehemu ya misitu. Umefika wakati sasa kuvuna vizuri magogo yetu bila ya kuathiri mazingira. Aidha, kuimarisha vizuri mradi wa nyuki ambapo mavuno ya asali inahitajika sana nchi za Arabuni ambapo fedha nyingi za uuzaji wa asali zitapatikana. Aidha, ulinzi mkali uwepo katika uwindaji

haramu na kufuatilia kwa vizuri wale wawindaji wanyamapori waliokubaliwa na kudhibitiwa vizuri fedha za kigeni zinazopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kuwe na uangalizi mzuri kwa waharibifu wa mazingira na wale wanaochoma moto ovyo na kusababisha uharibifu mkubwa wa mapori yetu na hata kupoteza viumbe hai vya porini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo mdogo sasa naomba kwa heshima zote kuunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi na kuwasilisha hotuba nzuri sana yenye kulenga mapinduzi makubwa ya kuboresha sekta ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo na maono ya sasa ya Wizara hii mwaka 2007/2008 imelenga kuielekeza Tanzania katika kuwa na uchumi kiongozi utakaotokana na sekta ya maliasili na utalii. Tunawatakia Watanzania wote hasa wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi katika uvunaji wa maliasili na utalii kutoa ushirikiano hasa kuwa na uwazi katika bei halisi za mazao ya misitu nje ya nchi ili kuweka uwiano kati ya bei za manunuzi toka Tanzania na bei za mauzo nje ya nchi ili washiriki yaani Taifa na wafanyabiashara wanufaike kwa usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kutoa ushauri, mapendekezo katika ufafanuzi katika maeneo yafuatayo, kwanza, naomba ufafanuzi juu ya vibali vya kukata miti hasa mivule iliyopo ndani ya mashamba miliki ya wananchi. Tunaomba ufafanuzi kama bado ni halali kutolewa na Maafisa Misitu wa Mikoa na Wilaya kukata mivule iliyopo ndani ya mashamba miliki ya wananchi bila wenye mashamba hayo kushirikishwa. Vitendo vya aina hii vimeendelea katika Wilaya ya Muheza, wenye vibali kihasibu mazao ya wakulima na kuacha matawi ovyo katika mashamba bila fidia yoyote kwa mwenye shamba wala Serikali za vijiji. Nini mwongozo wa kisheria juu ya hili?

Pili kuhusu ushirikishwaji wa vikundi na wazalendo katika uvunaji wa miti ya Mitiki misitu wa Lunguza (Muheza), naipongeza Wizara kwa kutoa fursa kwa vikundi mbalimbali zaidi ya 40 katika uvunaji wa miti ya Mitiki katika msitu wa Lunguza - Muheza. Hata hivyo kumekuwa na matatizo ya utendaji ambapo baadhi ya vikundi vimepewa leseni bila kutakiwa kuwa na leseni za biashara, Hati za malipo ya kodi *(TIN)* wakati vikundi vingine kutakiwa kufanya hivyo.

Hata hivyo bado fursa ipo kwa utekelezaji wa masharti hayo. Pamoja na hayo natoa ushauri ufuatao, viwanda vidogo vidogo vya mbao vilivyopo Muheza na sehemu jirani katika mikoa mingine viruhusiwe kupata fursa ya kushiriki uvunaji kwa kiwango cha mahitaji yao. Hii itasaidia kufanya bei za fenicha zisipande sana na kuwa ghali.

Pia iundwe Kamati maalumu ya muda ya kusimamia utoaji wa vibali na leseni kwa vikundi vya wananchi katika Wilaya na Mkoa unaohusika na uvunaji. Kamati hii

iwe Mkoani ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa kushirikiana na *DED,* Mbunge au Diwani, mwakilishi wa Serikali za vijiji vinavyozunguka eneo la msitu na meneja wa msitu na Maafisa Misitu Wilaya au Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali za vijiji zipewe kipaumbele licha ya kutolewa leseni kwa vikundi mbalimbali vinavyozunguka maeneo ya msitu wa Lunguza mpango huo haukulenga kusaidia Serikali za vijiji kuchangia ujenzi wa miradi ya kijamii, sana sana imesaidia watu binafsi wachache walioweza kutumia majina ya vikundi kujiwezesha. Hata hivyo mzunguko wa faida walizopata zimeboresha hali zao katika vijiji vyao.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa malalamiko hayo, napendekeza Serikali za vijiji vifuatavyo vilivyozunguka msitu wa Lunguza - Muheza vipewe leseni maalumu za uwakala za muda, ili ziweze kushiriki uvunaji na uwakala wa uuzaji, ili kuziwesesha kupata fedha kwa utekelezaji wa miradi maalumu ya kijamii kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ya Kijiji cha Kisiwani kuwezesha mradi maalumu wa kuendeleza ujenzi wa shule yao mpya ya msingi inayoendelea.

(ii) Serikali ya Kijiji cha Mashewa kuwezesha Serikali ya kijiji kujenga maabara ili kuboresha zahanati yao ya kisasa ambayo imekamilishwa, pia ujenzi wa nyumba ya daktari.

(iii) Serikali ya Kijiji cha Kiwanda kusaidia ujenzi wa shule mpya ya sekondari ili Kata yao ya Nkumba iwe na shule ya pili ya sekondari kutokana na ukubwa wa kata hiyo. Wananchi wako tayari kwa utekelezaji.

(iv) Serikali ya Kijiji cha Bombani kuwezesha Serikali ya kijiji kuendelea na ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu shule ya msingi Bombani.

(v) Serikali ya Kijiji cha Kimbo kuwezesha kuendeleza ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu katika shule ya msingi Kimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri avitazame kwa jicho la huruma vijiji na Serikali zao ili kusaidia michango ya miradi ya jamii niliyoitaja. Mheshimiwa Mbunge, Madiwani wa maeneo husika na viongozi wa Serikali za vijiji hivyo wanaahidi kutoa msaada wa usimamizi. Naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa asubuhi hii. Ni kweli usiopingika kwamba kama mipango iliyoainishwa katika hotuba yake itasimamiwa vizuri, tutaona mapinduzi ya hali ya juu katika eneo la maliasili na utalii. Ninatamka bila wasiwasi wowote ule kwamba ninaunga mkono hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukumbushia ombi la muda mrefu la wananchi wa Kijiji cha Mese ambacho ni jirani na msitu wa asili ili wasaidiwe na Wizara hii kuingiza umeme katika kijiji hicho. Tunashukuru kuona kwamba Wizara ina nia ya kusaidia jambo hili ili wananchi wasiingilie eneo hilo kwa ajili ya nishati ya kuni, mkaa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi viongozi wa wananchi tunaahidi kwamba tutaendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira na wameanza kutoelewa. Ninaamini Wizara ikitusaidia kupeleka umeme kijiji cha Mese tutakuwa tumeondokana kabisa na tatizo la uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia tena kusema kwamba ninaunga mkono hotuba hii.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na viongozi wote wa Wizara na naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Wizara ina mpango gani wa kuendeleza mashamba makubwa ya miti ya Serikali, Taasisi, watu binafsi na wanavijiji katika Wilaya ya Lushoto hasa Tarafa ya Mlola na kote nchini ili mashamba ya miti yawe na mazao mbadala ya biashara. Katika maeneo yenye ukame.

Pili, kuna utata kuhusu matumizi ya *Chain-Saw* katika kuvuna miti na kupasua mbao. Ni ipi kauli sahihi ya Serikali kuhusu teknolojia za kisasa katika sekta ya misitu?

Tatu, kuhusu rasilimali za mambo ya kale na mali kale, je ni vituo vipi vimetambuliwa kwa lengo la kuviendeleza Wilayani Lushoto Wilaya ambayo ina historia ndefu ya utawala wa Wajerumani na Ufalme wa Wakilindi?

Nne, kwa nini Wilaya ya Lushoto haimo katika mpango wa kufufua zao la nyuki wakati ina ekolojia nzuri ya zao hilo?

Tano, ni aina zipi za samaki zinazofaa kufugwa Wilayani Lushoto na kuna mpango gani wa kuwapatia wananchi ushauri wa kitaalamu na mbegu za samaki hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Mtwara ni lini itaingizwa kwenye Mradi wa *MACEMP?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri anitolee ufafanuzi wananchi wa Mtwara Vijijini walioko kwenye eneo la Hifadhi ya Ruvula

wanawezeshwa vipi ili waweze kuvua mbali na eneo la Hifadhi kwani kufanya hivyo wanahitaji zana bora zaidi ambazo hawana uwezo nazo.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Kwanza kabisa, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuendeleza utalii Tanzania. Naomba Wizara itambue kuwepo kwa vivutio vya utalii katika Jimbo la Nkenge kama vile Mapango ya Mugana yenye kumbukumbu ya mambo ya kale, msitu wa Minziro, wenye vivutio vya aina mbalimbali vya miti na vipepeo wasiopatikana kwingine duniani.

Vile vile katika Kata ya Minziro kuna kambi ya zamani ya Wajerumani ambayo ikiboreshwa inaweza kuvutia watalii. Aidha, mabaki ya Kanisa ya Kyaka iliyobomolewa wakati wa vita vya Kagera na kumbukumbu nyingine za vita ni vivutio tosha kwa watalii wa ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mkoa wa Kagera unaweza kuwa Kitovu cha Utamaduni wa Kitalii *(Cultural Tourism)* kama mikakati ya makusudi itawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri kwa kupandisha bei na hivyo kuongeza mapato ya Serikali. Hata hivyo, nyongeza ya mapato iliyotangazwa katika hotuba yake haiendani na kitabu cha I *(Revenue Estimate).* Mwaka 2007/2008 amepanga kukusanya shilingi 15,601,745,000 katika Idara ya Misitu na Nyuki tu. Maelezo aliyotoa katika hotuba yake Idara hii itaingiza jumla ya shilingi 4,500,000,000. Rekebisha takwimu zako ili Waziri wa Fedha aingize katika *Finance Bill.*

Pili, ameongelea *revenue measure only*, vipi udhibiti *(control measures)?* Hili ndiyo eneo lenye tatizo. Hapa wageni wanaibia sana Serikali (hasa Chinese) kwa bei zile zile za zamani, ukiweza kudhibiti utaingiza fedha maradufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto zifuatazo; kwanza hakuna vipimo, mwekezaji anapata leseni ya daraja tatu, anavuna daraja la kwanza, wageni wanakwenda kuvuna porini. Unasema nini kuhusu *control?* Wageni wasivune wala wasi-*export* wafanye *processing.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Idara ya Wanyamapori iwe *agency* na itoke Wizarani ili isimamie vema. Hili linawezekana *soon*, ndani ya *Finance Bill*. *Please take this my father*, *it will work*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kuhusu UWAMKU waliomba kuvuna magogo ya *Teak,* waliomba *126,000 cubic meter* huko Ruhunguze. Wamepewa *300 cubic meters*

tu. *Celman Company* mkawapa *26,000 cubic meter,* hebu nieleze hili, mnaweza namna gani kumpa mgeni mmoja 26,000 na Watanzania katika kikundi *300 cubic meter* tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, katika hotuba yako Ziwa Tanganyika hukuliingiza kabisa. Vipi kuhusu *Beach Management Units (BMU)* kama Ziwa Victoria? Hebu Waziri anieleze mipango iliyopo kwa uvuvi katika Ziwa Tanganyika katika vijiji vya Kakilanyobo, Kigalye, Mtanga, Mwamgongo, Bugamba, Kiziba, Zashe na Kagunga. Kuna mpango wowote wa maendeleo ya uvuvi Ziwa Tanganyika? Vipi mpango wa *Lake Tanganyika Biodiversity programme?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma haipati mapato yoyote kutokea *Gombe National Park*, achana na madarasa na kadhalika, *revenue* katika *council* na saba, programu ya hoteli kupitia *ADB* na *CRDB* ni nzuri sana na hongera sana.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Tunduru imezungukwa na Hifadhi za Taifa. Hali hii inasababisha wananchi wa Jimbo hili kupata usumbufu mkubwa na wanyama wakali (simba) na wanyama wanaoharibu mazao (tembo).

Pili, Mheshimiwa Waziri tarehe 20 Aprili, 2007 nilikuandikia kukuomba utuongezee askari angalau 10 , bunduki na risasi ili kuongeza nguvu za kuwadhibiti wanyama hao. Kwa masikitiko makubwa hadi leo hatujapokea hata askari mmoja. Mazao ya wakulima wanyonge yanaliwa na tembo na sasa tembo wanashambulia zao la korosho, zao la pekee la biashara. Wananchi hawana chakula kwa masikitiko wanyonge hawa watakosa fedha za kununua chakula kwa vile zao la korosho linaangamizwa na hao tembo.

Tatu, Mheshimiwa Waziri, kwa kushindwa kwako kupeleka askari wa nyongeza Tunduru, kumepelekea tarehe 18 Mei, 2007 askari Wanyamapori aitwaye Sadik Zuberi Kiwaya kuuawa na tembo. Askari huyo alishambuliwa na tembo kwa vile alikuwa peke yake na wasaidizi raia wasio na silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni ushauri. Moja, naishauri Serikali ijenge uzio wa umeme wa jua *(solar power fenced)* kama walivyofanya nchi jirani ya Msumbiji ili kuwazuia tembo wasiingie maeneo ya wananchi. Pili, Serikali ianzishe mashamba ya mazao kandokando ya hifadhi ili yawe malisho kwa wanyamapori, tatu, Serikali itoe ruksa kwa wananchi waweze kujilinda wenyewe kwa kadri wawezavyo na nne, aidha, Serikali itoe msisitizo kwa makandarasi ujenzi kutumia zaidi mirunda ya chuma badala ya miti wanapofanya miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri, Mheshimiwa Zubein Mhita, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja

na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii yenye mwelekeo thabiti wa kuboresha Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo kabla sijaanza kutoa mchango wangu napenda kutamka rasmi kuwa naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Mwenyezi Mungu awatie nguvu, uwezo na mshikamano ili waweze kutekeleza yote waliyoyaainisha kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunga mkono hoja, sasa napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu msitu wa Hifadhi za Rungwa, Kizigo na Mhesa Manyoni naishukuru Serikali kwa kutenga mapori ya akiba *(Game Reserve)* yaliyopo Wilaya ya Manyoni. Kwa kuwa Serikali ilikata mipaka mipya katika hifadhi hizi, naomba wananchi waelimishwe wahame wasiyatumie tena maeneo ya hifadhi kwa shughuli za kilimo, ufugaji na kilimo .

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu ni waelewa sana wala haina haja ya kutumia nguvu bali ni elimu tu. Nadhani itasaidia wananchi kutokuingilia maeneo haya na kusababisha mauaji yasiyokuwa na msingi. Ikumbukwe ndani ya miaka miwili wameuawa watu watatu na mifugo takribani hamsini. Vile vile ukataji wa mipaka bila ya kushirikisha jamii ni tatizo pia, ama mpaka wa pori urudi nyuma toka makazi kilometa tano kwa vijiji vyote vilivyo karibu na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapori ya Hifadhi ya Minyunge na Mgori, Singida Vijijini. Naendelea kuipongeza Serikali kuweka mipaka katika mapori yetu ya Hifadhi ambayo yanaviletea vijiji na Halmashauri faida kwa kupata asilimia 25 ya malipo kutoka kwa wawindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi kwa kuwa hifadhi ya pori la Minyuge imezungukwa na wafugaji wa kabila la Wasukuma, naiomba Serikali itoe elimu na sio nguvu kuwataka wafugaji hao kutoingilia maeneo hayo ya hifadhi kwa kuchungia mifugo, kukata mbao, kulima ili hifadhi hizi ziendelee kuvutia watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malipo ya Hifadhi asilimia 25, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa wawindaji wa kitalii kutoa asilimia 25 kwenye Halmashauri zenye hifadhi hizi. Naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza asilimia hii angalau iwe asilimia 40. Vile vile ruzuku hii itumwe kwenye vijiji husika moja kwa moja badala ya kupeleka kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvunaji wa wanyama, naishauri Serikali itoe maelekezo kwa wawindaji wa kitalii wawe wanavuna wanyama hasa wale ambao wamezidi kuwa wengi na kuleta athari kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia kwa watu waliouawa na wanyama, natambua wazi kuwa binadamu hafananishwi na kiasi chochote cha fedha anapokufa

na kufidiwa bali ikumbukwe kuwa marehemu alikuwa na mchango mkubwa kwa familia, hivyo anapouawa familia huathirika. Hivyo, fidia ikiongezeka itasaidia familia iliyokuwa inamtegemea katika uhai wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukataji wa magogo, naishauri Serikali kuwa iwe na tahadhari au kiwango cha ukataji wa magogo kwenye misitu iliyotengwa kwani ukataji ukienda holela misitu itaisha yote na kuleta ukame katika vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji wa nyuki, kwa kuwa Mkoa wa Singida ni mmojawapo ya Mikoa inayofuga nyuki wa aina mbalimbali. Naiomba Serikali kuimarisha vituo vya ufugaji ili waweze kutengeneza mizinga ya kisasa ya kutosha ili wananchi wafugaji wa nyuki waweze kutundika mizinga ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uhaba wa mizinga ya kisasa pia vituo hivyo vingeimarishwa kutengeneza asali mbichi za aina mbalimbali za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Soko la Asali, pamoja na juhudi za wananchi kuvuna asali bado soko la uhakika la asali halipo. Hivyo basi ni vyema Serikali ikasaidia upatikanaji wa soko la asali ili kuinua vipato vya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utoaji wa leseni za ukataji wa magogo, naiomba Serikali suala la utoaji wa leseni litazamwe upya ili sekta hii iweze kuzalisha pato hili pia wazalendo wapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho baada ya mchango wangu napenda kurudia tena kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nitumie nafasi hii kutoa salamu za rambirambi zangu kwa familia za marehemu wote waliopoteza maisha yao. Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi. Lakini pia nitumie nafasi hii kutoa rambirambi zangu za dhati kabisa kwa familia ya aliyekuwa Mbunge wa Viti Maluum, Vijana CCM Taifa, Mheshimiwa Amina Chifupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie tena nafasi hii kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri waliyoileta hapa Bungeni leo tarehe 25 Julai, 2007. Ni hotuba ambayo imeleta imani kwa wananchi wote na imegusa maeneo yote. Nawapongeza Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la misitu na nyuki. Je, vibali vinavyotolewa vinalingana na magogo yanayovunwa? Ni kweli kwamba kuna ukiukwaji mkubwa sana katika uvunaji wa magogo katika misitu yetu hasa misitu ya Magharibi mwa nchi yetu na misitu ya Kusini mwa Tanzania? Kwa nini Serikali isiweke mazingira mazuri yatakayowezesha kuendeleza uvunaji wa maliasili hususan misitu yetu. Kwa kufanya hivyo Pato la Taifa litaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara kwa kuangalia kupandisha bei ya ukataji wa magogo na kupeleka nje. Kwa nini hakutofautisha magogo kwa asilimia, magogo yanayopandwa ya mikaratusi na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isielekeze nguvu kusaidia utalii wa ndani? Nadhani sasa ni wakati muafaka, juhudi za Serikali zielekezwe kukuza utalii wa ndani sanjari na utalii wa nje kwa kuwa athari za utalii wa wageni kutoka nje ni kubwa sana panapotokea matatizo kama vile mashambulizi ya kigaidi yaliyotokea Septamba 11, 2001 katika Kituo cha Biashara cha Kimataifa *(World Trade Centre)* huko Marekani. Katika kipindi hicho cha mwaka 2001 na sote ni mashahidi kwamba mapato ya nchi yatokanayo na sekta ya utalii yalishuka kwa kiwango kikubwa kutokana na watalii wengi kuogopa kusafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa namna inavyojitahidi kulinda wanyamapori. Hivi kuna sheria inayolinda wanyamapori? Kama tunataka hifadhi zetu ziwe endelevu lazima kuwepo na sheria zinazowalinda wanyamapori *(sustainable).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, vibali vinavyotolewa vya uwindaji vinalingana na wanayama wanaowindwa? Wizara inadhibiti vipi wanayama wanaowindwa? Je, ikiwa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ina takriban eneo la kilomita za mraba 20,000 nazo zote zimezagaa wanyama na wanaowinda hawana tatizo kwa kuwa wanyama hawawabughudhi hata kidogo, kwa nini basi Wilaya hii isiongezewe asilimia kufikia 40%; na kwa kuwa watumishi katika Wizara hii hawana vitendea kazi, je, Wizara ina mpango gani wa kuwapa vitendea kazi? Je, Wizara inawasaidia namna gani familia za wafanyakazi waliouawa na majangili hususan katika Wilaya ya Simanjiro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Waziri Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu Ndugu Blandina Nyoni, pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa maandalizi mazuri sana ya hoja hii. Naunga mkono hoja ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutekeleza majukumu yake vizuri ya Wizara hii, nashauri baadhi ya maeneo yapewe kipaumbele. Moja kati ya maeneo ambayo yanaweza kuipaka matope Wizara hii ni masuala ya Wanyamapori ambayo kwa bahati mbaya sheria yake imechelewa ili kuona namna ya kuwa na muundo ambao utatoa usimamizi mzuri na kumwacha Waziri na wasaidizi wasiendelee kupakwa matope kwa kuwa wao ndiyo wanaosimamia kila kitu. Uwindaji wowote, nashauri usiwe moja kwa moja chini ya Idara bali kuwepo na wakala wa Serikali ambao watashughulikia mambo mengi. Katika hali hii, pia watumishi itabidi wapangwe upya ili kuondoa wale wote ambao wamedhihirisha kuwa na tabia mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Waziri akasaidia kulieleza Bunge hili juu ya uwiano wa vitalu vya kuwinda ambavyo vinamilikiwa na wananchi kulingana na

vitalu vinavyomilikiwa na wageni. Pia Waziri aeleze kwa nini wananchi wengi wanashindwa kukidhi masharti ya kupewa vitalu na matatizo yao katika kutekeleza makubaliano ya kisheria. Hili ni muhimu kwa sababu wengi wanaliomba, wanalalamika kuwa hawapewi maeneo bali wageni ndiyo wanapewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini ingefaa kwa sasa zianze kupewa uzito wake unaostahili ili watalii waanze kuelekea Kusini mwa nchi hii. Mbuga za wanyama za Selous, Katavi, Mikumi ikiwa ni pamoja na vivutio vingine vilivyopo katika maeneo ya Kusini mwa nchi hii. Aidha, Idara ya Misitu na Nyuki ianze kupewa uzito unaostahili. Nyuki na mazao yake katika Mkoa wa Rukwa ungeweza kuchangia sana kuanzisha tena Chuo cha Nyuki. Pongezi kwa kuanzisha tena Chuo cha Nyuki - Tabora. Huu ni mwanzo mzuri wa kuwasaidia wananchi wa Mkoa huo na Mikoa mingi inayotegemea zao la asali na nta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *TPA* imeanza kuimarisha Bandari za Ziwa Tanganyika; Bandari ya Kasanga, Kipili, Karema hadi Kigoma, tunaiomba Wizara kwa maandalizi ya wavuvi ili watumie fursa hiyo kuvua samaki kwa biashara na nchi jirani za *DRC;* Burundi/Rwanda na hata Zambia. Maandalizi ya kuwawezesha wavuvi iwe ndiyo dira ya kuwaingiza kwenye MKUKUTA. Ziwa Rukwa nalo lipewe uzito unaostahili katika uvuvi na hasa uvuvi wa mamba ambao wanakuwa na athari kwa watu na samaki waliomo ndani ya Ziwa hilo. *Copping* ya mamba hawa ifanywe kila mwaka ili wasiongezeke sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wana Rukwa tungemwomba Waziri aone namna ya kusaidia Wilaya ya Sumbawanga kuweza kuhifadhi maeneo muhimu sana kama Ngome ya Wajerumani iliyopo Kasanga *(Bismark Point)*. Pia uhifadhi wa Mlima Milanzi ambao ndiyo chimbuko la Wafipa, eneo ambalo linawavutia sana watalii ni lile lililo mpakani na Zambia. Hapa kuna maporomoko makubwa kuliko yote Afrika yanayojulikana kama *Kalambo Falls.* Tunaomba hayo yawekwe kwenye orodha ya kushughulikiwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine naunga mkono hoja hii kwa jinsi Mheshimiwa Waziri alivyowasilisha Bungeni.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, Mheshimiwa Waziri uliyoyafanya kwenye Wizara hii ni Mapinduzi makubwa katika sekta ya utalii nchini mwetu! Hakika tumechelewa sana, haya yalitakiwa yafanyike miaka mingi iliyopita. Hakika Mheshimiwa Waziri tunakutakia kila la kheri kwa kazi hii nzuri unayoifanya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Tanzania unaweza kukua kwa kasi zaidi iwapo sekta hii itakuwa katika mipango mkakati katika kutumia rasilimali hii ya utalii na maliasili!

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo muhimu ya kufanyika katika kuendeleza sekta hii, kwanza *to map* nchi yetu ili kutambua kila eneo letu lenye maeneo ya utalii wa aina yoyote ile ili tupange matumizi yake!

Pili, miundombinu ni muhimu sana ili kuendeleza utalii wetu, tatu, mipango ifanywe kwa kuendeleza misitu yetu! Uvunaji wetu wa misitu uendane na upandaji wa miti na nne, Ziwa Tanganyika ni Ziwa refu kwa kina! Naomba Waziri aniambie nchi yetu inafanikiwaje na kuwepo Ziwa hilo? Hapa Tanzania Mheshimiwa Waziri naona hujaongea chochote kuhusu Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uvuvi ukizingatia Ziwa lile lina aina 378 wa samaki nadhani ni muhimu kuwa na mipango ya kufaidika na maliasili hii yetu! Utalii katika Ziwa lile kwa kuwa na michezo ya Marina *(Sports in the lake)?* Uvuvi uwekewe mipango endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa viwango vipya vya utalii katika misitu na uwindaji, kwanza viwango hivyo ni vidogo, natamani sana ungeongeza zaidi ya hapo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba niunge mkono hoja hii.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa
napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri.Kwa namna ya pekee nampongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kwa hotuba yake nzuri na iliyosomwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Naibu Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa jitihada zake pamoja na Katibu Mkuu Bibi Blandina Nyoni, pamoja na timu ya wataalamu wa Wizara hii. Bajeti ya Wizara hii imenisisimua hasa katika kufanya utafiti jinsi nchi nyingine zinavyofanya ikiwemo kodi mbalimbali na hivyo kuwa dira ya maboresho ya bidhaa na rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na wenzangu kuwa bei ya magogo ya ndani na nje ya nchi ziwe tofauti, kwani inaweza kukwamisha maisha ya Watanzania. Lakini napongeza kwa tahadhari zilizotolewa kuhusu wafanyabiashara na wawekezaji wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri je, ameshawahi kutembelea *Beach* za Ziwa Nyasa? Lini atakuja pamoja na wataalamu wake? Katika eneo la *Mbambabay* kuna visiwa vizuri sana na vingine ni vya kihistoria kwani wagonjwa wa ukoma walikuwa wanapelekwa huko wakae mpaka wafe. Mpaka sasa hata hatujui kama bado watu hao wanaishi au vipi. Je, Wizara ya Maliasili na Utalii ipo tayari kutoa Bajeti ya kufanya utafiti katika kisiwa hicho? Nani kashirikishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pwani ya Malawi imeendelezwa vizuri kabisa, nini kinazuia uendelezaji wa kitalii katika Pwani za Ziwa Nyasa? Hata kama ni kwa *small scale.* Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kama ana kiashiria chochote cha utalii cha Wizara yako katika Ziwa Nyasa ya Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba Wizara itupe mafunzo ya utalii kwa vijana watano wa kike na watano wa kiume kwa upande wa mafunzo ya utalii yatakayolingana na mazingira yetu ili kuweza kuibua biashara ya utalii katika Mkoa wetu kwani hali ya sasa inatulazimu kuanza na utalii mdogo mdogo. Kuhusu mfuko wa kuendeleza hoteli za utalii wa kati, taratibu za kupata mkopo huo wa Ufaransa ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho kabisa na kwa ujumla wake naomba kujua mikakati maalumu ya ku-*promote* utalii katika Mwambao wa Ziwa Nyasa, *Mbambabay*, Liuli na kadhalika kama walivyofanya wenzetu wa Malawi ili kuongeza kipato cha wananchi waishio huko. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa viongozi wa Wizara, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji walio chini yake kwa kuinua viwango vya maduhuli katika mbuga za wanyama na maeneo mengine yanayovutia watalii. Pia nazipongeza juhudi kubwa zinazofanywa za kuitangaza Tanzania na kujenga miundombinu na hoteli katika maeneo ya utalii

Mkoa wa Kilimanjaro hauna bahati ya kuwa na ardhi kubwa, mifugo mingi au madini. Baraka pekee ya asili kwa mkoa huo ni Mlima Kilimanjaro. Mlima huu unaongoza kwa kuliingizia Taifa letu fedha katika sekta ya utalii. Hakuna mbuga ya wanyama, siyo hata Serengeti inayoliingizia Taifa fedha nyingi namna hiyo. Mlima Kilimanjaro umeweza kuwa neema kwa Tanzania siyo tu kwa sababu ya kazi nzuri ya *Kilimanjaro National Park (KINAPA),* bali pia kutokana na mchango wa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro hasa wale wanaozunguka Mlima huu wa Majimbo ya Rombo, Vunjo, Moshi Vijijini, Moshi Manispaa, Hai na Siha.

Kwa niaba ya wananchi wa Moshi Vijijini, Mkoa wa Kilimanjaro, naiomba Wizara iweke utaratibu wa kuchangia katika Halmashauri zinazozunguka Mlima huo kama vile Migodi ya Madini inavyochangia katika Halmashauri migodi hiyo iliko au kama vile Mashirika au Kampuni za Uwindaji zinavyochangia maendeleo ya Halmashauri husika kwa kuzitengea Halmashauri hizi 25% ya mapato yote ya uwindaji. Halmashauri husika hapa ni nne ambazo ni Rombo, Moshi, Moshi Manispaa na Hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataja miti unaendelea katika mashamba binafsi kutokana na hali ya maisha kuwa ngumu. Kwa kuwa Wizara hii kwa namna fulani inaathiriwa kwani miti inapopungua katika mashamba wakataji huvamia maeneo ya asili kama msitu wa Mlima Kilimanjaro, napendekeza uwepo mkakati maalumu wa kuhimiza upandaji miti katika mashamba binafsi kwa kushirikiana na Halmashauri za Kilimanjaro kutengeneza vitalu vya miche ya miti na kuendesha mashindano ya upandaji miti katika taasisi mbalimbali hasa mashule. Wizara iwashirikishe Wabunge husika.

Katika Jimbo la Moshi Vijijini zipo njia mbili zilizokuwa zinapeleka watalii Mlima Kilimanmjaro nazo ni ile ya Kibosho-Umbwe na *Old Moshi,* Kikarara - Kidia ambazo sasa ama zimefungwa au hazitumiki ipasavyo, hivyo kuwafanya wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini kutokunufaika moja kwa moja na shughuli za utalii wa upandaji Mlima Kilimanjaro. Hali hii imepelekea hata barabara za maeneo haya kutopewa kipaumbele ambacho zinastahili endapo zingekuwa zinawapitisha watalii.

Naiomba Wizara izifungue njia hizi na kuziingiza rasmi katika muundo mzima wa njia za utalii wa upandaji Mlima Kilimanjaro na kuzipa barabara husika kipaumbele husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru kupata ufafanuzi wa hoja hizi au maombi haya ama leo au baadaye kwa maandishi. Nawasilisha.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe pongezi za dhati kwa Waziri Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita na Katibu Mkuu, Bibi Blandina Nyoni kwa hotuba, utendaji na uwajibikaji mzuri sana!

Kuhusu mapato yatokanayo na wanyamapori, licha ya Tanzania kuwa na wanyama wa kila aina na pengine wanyama wa pekee ambao hawapatikani nchi zingine za Afrika na duniani bado inachangia kidogo sana katika Pato la Taifa. Nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Maghembe, kwa kuthubutu kupandisha bei ya vitalu na wanyama wanaowindwa kwa muda mrefu, viwango vimekuwa havibadiliki na hata vinapobadilika ni kwa ongezeko dogo ikilinganishwa na sehemu zingineAfrika. Kupitia hotuba ya Waziri utasikitika kuona bei za kutupwa zilizokuwa zikitozwa mfano vitalu vyenye ukubwa wa kilometa za mraba 100 na 1000 kwa Botswana ni dola 150,000, Tanzania ni dola 10,000 na sasa ni dola 50,000.

Kuhusu wanyamapaori,simba kwa Botswana ni dola 18,000 , Afrika Kusini ni dola 20,000 – 25,000 na Tanzania ni dola 2,500 na sasa ni dola 12,000. Tembo ni dola 25,000 kwa Botswana, dola 25,000 kwa Afrika Kusini na Tanzania ni dola 5,000 na sasa ni dola 15,000! Kutokana na mabadiliko hayo pato litaongezeka kwa mwaka 2006/2007 na kuwa dola 12,000,000 na kwa mwaka 2007/2008 itakuwa 49,600,000. Hili ni ongezeko la zaidi ya 400% ni hatua kubwa sana kwa mara ya kwanza inahitaji pongezi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pato la Taifa litaongezeka na hivyo maisha bora kwa kila Mtanzania uliyoyaahidi yatapatikana, pato la Halmashauri zinazopata 25% ya mapato zilizo kando kando na hifadhi litaongezeka mfano Wilaya inayopata 32,000,000 sasa itapata shilingi 128,000,000. Pia kuweza kulinda maliasili zetu zisipotee bure. Kwa kuwa tumechelewa sana kupandisha viwango vya bei Waziri atakubaliana nami kuongeza bei hizi ili zilingane na sehemu zingine Afrika?

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa ruhusa ya kutoa mchango kwa maandishi. Nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu

Waziri, Katibu Mkuu kwa hotuba waliyoiandaa vizuri na imesomwa na Waziri vizuri sana, imenifanya niunge mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ningependa kuchangia baadhi ya maeneo ili kutoa picha ya Wizara kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Waziri ninafahamu kuwa anajua Misungwi inamiliki eneo fulani la Ziwa Victoria (mkondo) sehemu kubwa ni mazalia ya samaki ni kazi kubwa ya kufanya doria bila usafiri hivyo ni vyema pakawepo boti maana uzalishaji wa samaki unatokana na mazalia ya samaki katika mialo mbalimbali iliyoko Misungwi.

Kwa kuwa muda mrefu eneo la mkondo wa Ziwa Victoria Wilayani Misungwi hufungwa kwa ajili ya mazalia ya samaki si chini ya miezi sita watu wetu huwa wamezuiwa kuvua samaki je, Serikali/Wizara inasaidiaje wananchi wa maeneo hayo hasa wakati huu wa uchangiaji wa maendeleo zikiwemo shule, zahanati na kadhalika hasa watu wa maeneo husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikisaidia kuboresha mialo ya sehemu mbalimbali lakini mialo ya sehemu za mazalia iko katika hali mbaya je, Serikali kwa nini isisaidie kuboresha/kujenga mwalo mmoja ili iwe mfano kwa kuthaminiwa kwa walinzi wa mazalia ya samaki, hii itakuwa bora kwa walaji wa ndani wanunue samaki katika mazingira mazuri na safi kwa afya zao. Maana sasa wanaopeleka nje tu ndio wenye mialo mizuri hivyo ni vyema na walaji wa ndani wafaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu isikatwe kiholela, taratibu za sheria zifuatwe. Ombi langu, naiomba Serikali ifanye juu - chini juu ya nishati (umeme) hii itasaidia ukataji wa miti kwa matumizi ya kupikia na kadhalika. Ajira ziongezwe katika sekta hii na maslahi yao yaboreshwe.

Pia niipongeze Serikali kwa kuruhusu uvunaji wa miti katika mashamba yetu mfano msitu/shamba la Buhindi tunaiomba Serikali iendelee kuboresha mashamba yote ikiwepo kuwapa magari na vifaa vingine. Nawapongeza watendaji wa shamba la Buhindi kwa kufanyakazi vizuri na kwa kufuata sheria za nchi bila kuathiri zile za Halmashauri, mahusiano yao ni mazuri. Naiomba Serikali iwasaidie mahitaji yao. Mimi nikiwa Mbunge wa sehemu ya Mkoa wa Mwanza nitasaidiane nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri kwa kazi ngumu ya kuiongoza Wizara yenye maliasili nyingi za nchi hivyo Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na ile ya Fedha ziangalie Wizara hii maana ni chanzo cha mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuunga mkono na kuwaomba Wabunge wengine turuhusu pesa alizoomba tumpe akafanye kazi. Ahsante.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu katika Wizara hii, ningependa kuanzia eneo la uvuvi. Katika Bajeti ya mwaka jana nilichangia na kuuliza kuhusu kazi ya wakala wa *SUMATRA* kuna uhusiano

gani kati yake na wavuvi wa Ziwa Victora kwani anasumbua wavuvi ambao wako chini ya Wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu nililopewa Wizara hii itaongea na Wizara ya Miundombinu lakini mpaka leo sijapata jibu lolote au Miundombimu hawana jibu? Kwa hili Waziri wa Maliasili na Utalii alikiri kuwa Mbondo anasumbua. Kwa kuwa huamishwa mtu na Wizara hubaki pale pale basi naomba jibu, baada ya maongezi na Wizara ya Miundombinu ni kipi kilijibiwa na huyu mtu aliacha vitendo hivyo na kama bado ni nini kinafanyika katika wavuvi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hotuba ya Bajeti ya Wizara hii mwaka jana tuliambiwa msako wa nyavu haramu utafanyika duka hadi duka, godauni hadi godauni, naomba kujua msako huu katika Mkoa wa Mwanza ulifanyika lini na walikamata nyavu haramu ngapi na ni Wilaya gani ambayo iliongoza kwa nyavu haramu katika Mkoa wa Mwanza. Je, nyavu hizo zilienda wapi? Kama zoezi hili halijafanyika naomba sababu za kutofanyika. Kuhusu ada za mitumbwi ningependa kujua Wizara hii kwa nini inatoza kodi tofauti za mitumbwi katika eneo moja? Ni kigezo gani kinatumika naomba jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini katika msako wa Ziwani haufanyika na askari wa Maliasili na hufanywa na askari wa Usalama wa Raia. Hii inasababisha wavuvi hawa kupata dhima na hata kufikia kubambikizwa kesi kama hawajatoa rushwa. Kwa hili naomba jibu katika eneo la Kigoma Ujiji katika mahali alipoishi au kufikia Fred Willliamson kwa sasa watalii wamepungua sana, baada ya Babu ambaye (jina lake nimelisahau) alikuwa anatembeza wageni hao na kuwaeleza historia ya hapo na Fred Williamson, kuacha au kuachishwa kazi. Je, Wizara haioni kama kufanya hivyo na watalii hao kupungua kutarudisha nyuma mji wa Ujiji na ni kwa nini babu huyo hakuwa na mshahara kwa kazi yake aliyokuwa anaifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Wizara iangalie hasa pale ambapo inapiga marufuku kufanya kitu kimoja hapo ndipo tatizo linanzia. Mfano kupiga marufuku mkaa, tatizo limekuja ni kupanda bei kwa mkaa, sasa hivi tangu tatizo hili lianze yapata mwaka sasa. Bajeti ya mwaka jana nililiongelea kwa uchache mkaa ulitoka shilingi 11,500 hadi 30,000 kwa uchache shilingi 28,000 au 25,000, hii ni hatari sana. Tunaomba Wizara iangalie hilo kwani umeme haushikiki, mafuta bei juu na mkaa bei ghali, tunaiomba Serikali ichukue hatua hiyo haraka ili kauli wa maisha bora kwa kila Mtanzania yafike mahala pake. Ahsante.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuendeleza maliasili zetu na hasa kubadilisha mfumo ambao kwa muda mrefu sasa amekuwa anasema vibaya kwenye sehemu ya sekta kama vile upande wa misitu na wanyamapori. Nina imani kubwa Mheshimiwa Waziri na wanaomsaidia watayaweka vizuri hayo maeneo yanayosemwa vibaya kwa faida na maendeleo ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi karibuni amezungumzia kwa undani kuhusu kupandisha gharama za ukataji wa miti na leo hii ametoa. Kwa wale wafanyabiashara wanaosafirisha nje mimi sina tatizo kwanza ilitakiwa mpandishe mara kumi zaidi. Tatizo

langu ni kwa wananchi ambao hutumia mbao toka kwenye mashamba yetu ya Mufindi, *West Kilimanjaro,* Rombo, Rubya na kadhalika mbao hizi hutumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Kwa vile sasa hivi Serikali yetu inahimiza wananchi wajenge nyumba bora za kisasa naomba Serikali iwafikirie wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Maghembe ameingia Wizara hii pia amekuta bei za wanyamapori, vitalu na kadhalika ziko chini sana. Nakuomba sana bei hizi zipande zaidi ya hapa alipofikia maana yangu aongeza tena bei na asiyekubaliana naye asiwinde ili sisi tuendelee kuhifadhi wanyamapori wetu kwa matumizi ya vizazi vijavyo na nafahamu watakuja tu kuwinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumefika wakati wa kutenganisha shughuli za uwindaji wa kitalii kutoka Idara ya Wanyamapori, Kitengo hiki kiwe na Bodi yake ambayo itatambulika kisheria na isimamie *Hunting Blocks* na uwindaji wa kitalii, uamuzi huu utapunguza au kumaliza kabisa malalamiko yaliyopo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika letu la Utafiti *(TAWIRI)* ndilo Shirika linalofanya tafiti zote hapa nchini na matokeo yake hutumiwa na *TANAPA, NCAA (Ngorongoro)* Idara ya Wanyamapori na hata wenye *Hunting Blocks.* Huku nyuma ilikubalika kwamba *TANAPA,* Idara ya Wanyamapori na Ngorongoro walitakiwa kuichangia *TAWIRI* fedha za uendeshaji, mpaka sasa Shirika hilo liko kwenye hali mbaya kifedha, nataka nipate majibu kwa nini watajwa hapo juu hawalichangii Shirika hilo? Pia Mheshimiwa Waziri *Director General* wa *TAWIRI* mpaka sasa ana Kaimu, Wakurugenzi wote wa Kanda wanakaimu kwa nini? Nataka maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna imani Serikali imeshafahamu ya kwamba kuna matatizo makubwa ya uongozi upande wa Idara ya Wanyamapori na Misitu. Bado nina imani kubwa kwamba sasa baada ya Serikali kutumia njia zake mbalimbali imeshafahamu matatizo yako wapi na sasa tunaomba hatua zichukuliwe kwa wahusika kwa faida ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maliasili Wilayani haziendi vizuri kutokana na uhaba wa fedha, vitendea kazi na kadhalika. Naomba Serikali na ifahamu ya kwamba uhifadhi unaanzia chini kwa hiyo, naomba uchukue hatua kuokoa hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Muswada wa Kurekebisha Sheria ya Wanyamapori utaletwa Bungeni? Kwa nini na nani anachelewesha kuleta sheria hiyo Bungeni. Naomba maelezo.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa mchango huu naanza kwa kueleza kuwa naunga hoja mkono. Hata hivyo ninayo haya ya kuangalia na kutanabahisha ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kiufanisi kwa lengo la kuleta tija na kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mgogoro usio wa lazima kati ya Hifadhi ya Mahale wa Kijiji cha Kalilani, kijiji cha Kalilani ambacho kinapakana na hifadhi ya

Mahale ni kijiji halali ambacho kimesajiliwa na kupatiwa hati ambayo mimi nikiwa Mbunge wa eneo hilo (Kigoma Kusini) nilikabidhiwa hati hiyo nami nikaikabidhi kwanza kwa uongozi wa Serikali mkoani na Wilayani Kigoma na hatimaye kuikabidhi kwa uongozi wa kijiji cha Kalilani. Wakati hati ilikabidhiwa kijijini, uongozi wa hifadhi ya Mahale uliwakilishwa na Bwana Seki aliyekuwa muhifadhi wakati huo mwaka 1992.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza na kusikitisha ni kwamba uongozi wa hifadhi kuwapa tafrani wakazi wa Kalilani kwa madai kuwa Kalilani ni kambi ya uvuvi na sio kijiji. Hapa ndio ulipo mwanzo wa tatizo. Uongozi umekuwa unawabughuzi wavuvi toka Kalilani. Napenda Wizara itambue kuwa kama Kalilani sio kijiji iweje hao hifadhi wawe wanabadili mipaka na kudai kuwa Kalilani imeingia katika himaya ya hifadhi uongozi wa Tarafa, Mkoa na Wilaya unalitambua Kalilani kuwa ni kijiji na ndio maana ipo Serikali halali kama katika vijiji vingine vyote nchini. Wizara itoe maelekezo ya wavuvi kutonyang'nywa zana zao za uvuvi za mavuno wanaovuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo, mwaka jana Waziri aliyekutangulia alitembelea hifadhi hiyo. Kwanza hakuna amepangiwa kukutana na uongozi wa kijiji. Uongozi ulinusa ziara hiyo ambayo hata Mbunge alipigwa chenga hivyo akajipeleka kuonana na Mheshimiwa Waziri. Jambo la kushangaza kwanza Waziri huyo aliruhusu hadhi ya Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini idhalilishwe kwa uongozi wa hifadhi ulinikejeli Mbunge eti si lolote kwa sababu tu naunga mkono kuwepo kwa kijiji cha Kalilani. Lakini cha kushangaza zaidi Waziri huyo aliacha anaagiza mipaka ya Kijiji irekebishwe na wataalamu toka Wizarani ilikwenda. Kijiji hakikutoa ushirikiano kwa sababu hapakuwa na sababu ya kufanya hivyo kwani kijiji hakikupewa hati na Wizara ya Maliasili na Utalii. Nitaomba Waziri anijulishe ni kwa nini madhila haya yanafanywa na Wizara na hakuna hatua zinazochukuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya uvuvi, Ziwa Tanganyika linao utajiri mkubwa wa viumbe hai wakiwemo samaki na dagaa. Hivi Wizara imechukua hatua zipi za kusaidia wavuvi wadogo ili nao wakue na siku moja wawe wavuvi wakubwa? Kwa nini Wizara isishawishi waliowekeza Ziwa Victoria wakawekeza Ziwa Tanganyika? Ieleweke kuwa hata hao Sangara wanatoa jina miji ya Bukoba, Mwanza na Mara asili yake ni Ziwa Tanganyika. Kwa nini Kigoma na Kasanga kusiwakwaze katika zao hili? Ieleweke wazi pia kuwa hakuna dagaa watamu na wenye virutubisho kama wale watokao Ziwa Tanganyika. Ni kwa nini hadi sasa hakuna azma ya makusudi ya kutangaza zao hili ili wavuvi wafaidike, tunao *peasant fishermen.* Naiomba Wizara inielimishe na namna gani watasaidia kuwezesha wavuvi hawa kupata zana za kisasa ili wavune maliasili katika Ziwa Tanganyika?

Kuhusu kituo cha Utalii *(Livingstone )* Ujiji, Mjini Ujiji kuna Kituo cha Utalii ambapo walikutana Henry Martin Stanley na Dr. David Livingstone. Tunashukuru kinajengwa kisasa. Lakini naiomba Wizara ichukue ushauri wa Mhe. Rais alioutoa hivi karibuni alipotembelea Kigoma. Aliagiza ijengwe hoteli ya kitalii jirani na kituo hicho cha *Livingstone.* Aidha, Mheshimiwa Rais aliagiza njia ya kutoka Ujiji hadi Bagamoyo kupitia maeneo muhimu kama Kongwa isimamiwe na kuwapo njia ya kupita kwa punda na farasi na sio magari ianzishwe ili watalii waweze kupita humo. Pia Mheshimiwa Rais

alishauri njia hii iweke zoezi la kudumu la kila mwaka kwa lengo la kutangaza utalii wa eneo hilo. Nashauri Wizara ihakikishe inatafuta wawekezaji watakaoshughulikia utalii wa kupitia njia ya watumwa.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara hii na taasisi zake kwa hotuba nzuri na utendaji mahiri na makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za uboreshaji na ukuzaji utalii pamoja na uboreshaji na uhifadhi wa misitu, wanyamapori na mazao ya bahari zimefanyika kwa jitihada kubwa na zinazostahili pongezi nyingine. Hata hivyo bado jitihada kubwa zaidi zinahitajika dhidi ya ujangili, uvunaji mbaya wa misitu na mazao ya baharini. Mafunzo maalumu na hatua thabiti za ulinzi na taaluma stahiki ziwekewe mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mkinga na Mkoa wa Tanga kwa ujumla una nafasi nzuri sana ya kuchangia zaidi katika Pato la Taifa kwa kuzingatia maliasili nyingi zilizonazo Wilaya ya Mkinga. Wilaya hiyo ina mwambao mrefu wa Bahari ya Hindi ambao una samaki wengi na migodi mingi ya chumvi, mwambao huo una nafasi nzuri ya kuendeleza utalii. Nafasi ya kuboresha utalii katika Wilaya ya Mkinga inaongezwa na kupandishwa hadhi Pori la Mkomazi/Umba kuwa Mbuga ya Wanyama ya Taifa. Hali hii ikizingatiwa na kuwepo Hifadhi za Taifa za Milima ya Usambara Mashariki pamoja na Wilaya ya Mkinga kuwa katikati ya maeneo ya Kitalu ya Tanga, Amani, Mombasa, Pemba na Zanzibar inakuwa katika nafasi nzuri ya kuyaweka katika Utalii wa Pwani *(Coastal Tourism)* na utalii wa milimani na kwenye mbuga za Taifa.

Naiomba Serikali itazame uendelezaji wa utalii Wilayani Mkinga kwa mtazamo mpya na ari mpya kwa kuzingatia haya na pia kwa kuzingatia kwamba uendelezaji wa *Northern (Tanga corridor)* utaibua maendeleo makubwa kwa Wilaya ya Mkinga na maeneo yanayoizunguka. Ni dhahiri hali hiyo itajitangaza sana nafasi ya kukuza utalii Wilayani humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi nzuri ya kukuza na kuendeleza uvuvi Wilayani Mkinga inadumazwa na mapungufu mengi yaliyopo. Kuna upungufu mkubwa wa huduma ya ugani, kuna upungufu mkubwa wa utaalamu wa uvuvi wa kisasa na pia kuna upungufu mkubwa wa vifaa vya uvuvi wa kisasa na ugumu wa kupata mikopo kwa ajili ya kununulia vifaa vya kisasa. Pia ukosefu wa mashine za doria na ulinzi wa kutosha unaleta athari mbili, moja wavuvi wakubwa wa nchi za kigeni hupata fursa ya kuvuna samaki wengi, bila manufaa yoyote, kwetu. Pili, hali hii inatoa mwanya mkubwa kwa wahalifu kuendelea na uvuvi gharamu uliopigwa marufuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi nzuri ya kufaidika na mazao na misitu inakabiliwa na changamoto nyingi. Kwanza pamoja na jitihada kubwa za kupanda miti na kupiga marufuku uvunaji wa misitu, bado wananchi wanakwenda kinyume cha hapa bado kampeni kubwa inahitajika kuwaelimisha wananchi kuhusu misitu ni mali na kwamba zipo ajira nyingine bora zaidi kuliko kuchoma mikaa, kukata kuni na miti kwa

ajili ya ujenzi. Pili, elimu kubwa zaidi na huduma kubwa zaidi za ugani zinahitajika ili wananchi waweze kufaidika na kuboresha na kuendeleza ufugaji wa nyuki wa uzalishaji mkubwa na bora wa asali na nta. Hali kadhalika mipango thabiti ikifanyika uzalishaji wa gundi na ubani bora unaweza ukaongezeka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja naitakia Wizara mafanikio mema.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja! Nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri kwa kukubali kukiendeleza Chuo cha Nyuki Tabora kama alivyosema kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wafugaji wa zao la asali wapewe mikopo ya mizinga ya kisasa ili waendane na wakati. Katika Ukurasa wa 21 aya ya 35, naomba Wizara ifikirie kuiongeza Wilaya ya Sikonge ambayo inatoa asali kwa wingi.

Kuhusu uvuvi, Tabora kuna maeneo ya bwawa ambayo kuna samaki ambao hutumika kama kitoweo kwenye maeneo ya Mkoa wetu. Pia kuna vikundi vidogo vidogo kama vile Urambo, Sikonge, Uyui ambavyo vinaendesha uvunaji wa zao la samaki. Naomba wapewe mikopo na nyavu za kisasa ili waweze kuondokana na umaskini. Pia Bwawa la Igombe lipewe samaki wakubwa au mbegu ya kulingana na eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hifadhi za misitu, Serikali au Wizara iangalie jinsi ya kusaidia kutoa fidia ya wananchi ndani ya hifadhi ambao wana hatimiliki ya ardhi ili waweze kuondoka maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nampongeza mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali idhamirie na itekeleze usimamiaji mzuri na bora zaidi wa rasilimali za Taifa kwa faida kubwa zaidi hali inayoonyesha kama vile tunadharau au tunatupa rasilimali zetu iachwe kabisa. Misitu yetu inakwisha, wanyama wetu wanakwisha, mito inatoweka na kadhalika huku vizazi vijavyo vinakosa raha ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa hatua za awali alizozieleza msoma hotuba/mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana; watendaji wake wawe macho, wasimwangushe nasi tukaumia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie upya mapato yatokanayo na mazao ya uvuvi hasa kwenye Ziwa letu la Victoria. Pia usalama wa wavuvi katika Ziwa letu hasa wavuvi wadogo waangaliwe kwa upya ili wawe salama wao na mali zao wanapovua. Upo uonevu mkubwa dhidi ya wavuvi wadogo na unyang'anyi wa mali zao hasa nyavu na *engine* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa kisayansi ni siri ya mafanikio kwa lile linalokusudiwa kufikiwa. Tumevisahau vituo vyetu vya utafiti hasa *TAFIRI*. *TAFIRI* inapewa chini ya nusu ya Bajeti yake, eti ifanye kazi nzuri! *TAFIRI* inao watafiti wengi mahiri ambao wanalipwa vizuri sana lakini hawapewi fedha za kufanyia utafiti.

Mhehimiwa Mwenyekiti, katika mambo mazito yenye fadia kubwa kwa Watazania, wafadhili hawavutiwi kutuunga mkono kwa dhati. Wafadhili nao wana vipaumbele vyao dhidi ya vile vya kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iipatie fungu *TAFIRI* kwa sababu samaki wanatoa mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa. Ni kwa nini basi isipate fungu lake ikawezeshwa kufanya kazi nzuri ambayo itachangia zaidi Pato la Taifa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya utafiti Kyela na Kigoma havipewi pesa za kufanya utafiti hali inayopunguza kasi ya kazi ya utafiti katika Maziwa ya Nyasa na Tanganyika. Naishauri Serikali itenge pesa na izipeleke Kyela na Kigoma, huko hata miradi ya wafadhili haipo. Tuwatumie vizuri wataalamu wetu maana sasa hawana kazi ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kujenga Kituo cha Dar es Salaam cha *TAFIRI* Makao Makuu, hadi sasa ni sehemu tu imejengwa. Naishauri Serikali ione sasa uwezekano wa kutoa pesa za kujenga *TAFIRI* Makao Makuu Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi utaratibu/mpango wa kuanzisha mabwawa ya ufugaji wa samaki umefikia wapi? Nashauri katika kasi ya maisha bora kwa kila Mtanzania, ajira zinaweza kupatikana kupitia ufugaji wa samaki na lishe kuongezeka kwa afya bora na kadhalika kwa ufugaji samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha!

**MHE DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Wilaya ya Karatu inazungukwa na Hifadhi za Taifa za Ngorongoro *(Conservation Area)* kwa upande wa Kaskazini/Kaskazini Magharibi na Hifadhi ya Manyara *(TANAPA)* kwa upande wa Mashariki/Mashariki Kusini; na kwa kuwa kila mwaka wananchi wa Wilaya ya Karatu hasa vijiji vya Makhromba, Mang'ola Juu, Tloma, Ayalabe, Rhotia, Slhathamo, Kambi ya Simba na *Upper Kitete* (Maeneo ya *NCAA)* na vijiji vya Kilimanjaro, Chemchem, Endallah, Getamwele na Buger *(TANAPA)*. Wanyama hasa tembo na mbogo wanatoka kwenye hifadhi na kushambulia mazao ya wananchi na pamoja na hali ngumu ya uchumi na hasa ukame unaokumba Wilaya ya

Karatu katika miaka ya hivi karibuni na hivyo hata kidogo wanachopata wananchi humalizwa kabisa na wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango au mkakati gani endelevu licha ya vikao vya ujirani mwema kuweka mipango maalumu vipindi vya mazao kuweka askari/makambi ya kudumu katika maeneo yote yanakopita wanyama hao kwenda mashamba hayo (inasemekana njia hizo hazibadiliki) kuliko hali ya sasa ambapo wananchi wanahangaika kutoa taarifa na mara zote askari hawafiki kwa wakati?

Je, pamoja na mahusiano mazuri yaliyopo kati ya uongozi wa hifadhi hizo na viongozi wa Wilaya, lakini askari wanaoenda kwenye maeneo huwa na kauli mbovu, huwanyanyasa wananchi na hata kujiingiza katika mambo yasiyowahusu ikiwa ni pamoja na kujiingiza kwenye kusaka pombe haramu ya gongo (kama ilivyotokea Buger) au kwenda kufanya upekuzi majumbani na kuwatisha wananchi kwa lengo la kuwabambikizia kesi au hata kuwakamata majumbani kwa kudai waliingia msituni mambo yanayoleta uhasama baina yao na wananchi kama ilivyotokea mgogoro mkubwa kati yao na hifadhi katika vijiji vya Buger na Kansay? Serikali inachukua hatua gani kwanza kukemea vitendo hivi vya askari hao wanaodhalilisha na kuchafua sura nzuri ya hifadhi yetu na askari wake wengi wazuri wanaofanya kazi katika mazingira magumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa kauli gani sasa kuhusu pendekezo langu la mwaka jana kuhusu kuundwa kwa mfumo maalumu wa fidia kwa mazao ya wananchi yanayoharibiwa na wanyama hao wakati au pale wanapowadhuru au kuwaua binadamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kauli ya Waziri kuzuia biashara ya magogo nje ya nchi *(export),* vyombo vya habari vimendelea kutoa taarifa kuwa agizo hilo la Waziri halijazaa matunda hasa kwa makampuni ya Kichina. Waziri anasemaje kuhusu taarifa hizo na kama ni kweli, kwa nini agizo hilo halikutekelezwa na Waziri ataeleza vipi Bunge hili tatizo la msingi ni nini na iwapo tatizo ni sheria, lini atawasilisha marekebisho ya sheria ili kumpa meno zaidi?

Pamoja na majibu ya Waziri ndani ya Bunge hili, taarifa zilizopo ni kuwa katika kutoa leseni ya vitalu katika maeneo ya Yayeda Chini - Wilaya ya Mbulu, maeneo mahsusi kwa ajili ya kabila la Wahadzabe, kabila lililoko hatarini kutoweka; ni kuwa viongozi wa kabla hilo hawakushirikishwa kabisa katika maamuzi hayo ambayo kimsingi yataathiri maisha yao na chakula chao. Je, Waziri yuko tayari kusimamisha zoezi hilo hadi hapo atakapofanya uchunguzi wa kina kuhusu madhara na hata ikiwa lazima kupima uwiano wa manufaa ya vitalu hivyo dhidi ya ya madhara kwa kabila hilo?

Kwa vile wawekezaji hao wameomba pia kupewa vibali vya kuwinda/kupiga picha maeneo ya Matala, Dumbechand, Qanded na Endamagharg, Wilaya ya Karatu ambayo pia hukaliwa na Wahadzabe na Wabarbaig na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu haijatoa kibali na wala haifikirii kutoa kibali hicho, lakini taarifa zilizoko ni kuwa wawekezaji hao wamepewa vibali toka Taifa. Waziri anatoa kauli gani kuhusu taarifa hiyo?

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upanuzi wa Mbunga za akiba za Mhesi na Chaya umezua malalamiko mengi sana miongoni mwa wananchi wanaoishi pembezoni/karibu na mbuga hizo kwamba ukataji wa maeneo yaliyokuwa wazi *(open areas)* haukuwashirikisha wananchi katika vijiji vyao. Halmashauri haikuwapa nafasi ya kushiriki kutoa maoni yao na matokeo yake ni kwamba walipoteza huduma muhimu kama mabwawa na mashamba na pia maeneo muhimu ya malisho ya mifugo yao. Maeneo kama Doroto, Damweru, Ipande na Muhanga, walijikuta katika matatizo haya, walishirikishwa kwa taarifa tu baada ya mamuzi kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusogezwa kwa mipaka kumeleta athari za wanyama wakali na wanyama waharibifu wa mazao. Watu wameuwawa na wanyama, simba, tembo, fisi na mashamba yao kuharibiwa na kusababisha njaa *(artificial famine),* tembo kwa makundi wamekula mazao ya mashamba, mifugo kwa makundi imeuwaua na kuliwa na simba, wananchi wamepoteza mizinga yao kutokana na kukatwa kwa mipaka ya vijiji vingi katika kuunda *Game Reserves.* Wananchi wanahisi kwamba Serikali yao inajali zaidi mapato ya wanyamapori kuliko maisha ya wananchi. Wanashindwa kuelewa kama watu wapo kwa ajili ya wanyama au wanyama wapo kwa ajili ya watu na maendeleo yao. Ulinzi wa maisha ya watu na mali zao upewe kipaumbele na si suala la uchangiaji wa maendeleo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa wa askari wa wanyamapori, hufanya doria pale tu uharibifu unapokuwa umefanywa na wanyama kama simba na tembo. Askari hawa hawana usafiri na vitendea kazi na posho, wengi hawana ari ya kufanya kazi kwa sababu hawana nyenzo za kazi na hata risasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvunaji wa wanyamapori haufanywi kwa ufanisi unaolenga kuwalinda wanadamu na pia kuwahifadhi wanyamapori. Wanyamapori wanaongezeka sana, wanazagaa ovyo hata kwenye maeneo ya makazi ya watu. Askari wanapoitwa huwatishia tu wanyama ili warejee maeneo ya *reserve,* wanyama wamejenga tabia ya kutoogopa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo, Halmashauri ziagizwe kukaa tena na wananchi wa vijiji husika wa-*review* mipaka ya mbuga za akiba na vijiji vyao ili wapate maeneo ya kulisha mifugo, mabwawa na mashamba. Fidia kamili itolewe kwa familia ya anayeuawa na wanyamapori na kifuta jasho. Fidia kamili itolewe kwa mashamba yanayoharibiwa. Fidia kamili itolewe kwa kila mfugo unaouawa na wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *crash progrmme* ya *recruitment* ya askari wanyamapori ifanywe kupunguza upungufu mkubwa wa askari na vitendea kazi vinunuliwe. Tunaomba gari na pikipiki kumi kutokana na eneo la kilometa 16,000 za Rungwa, Mhesi na Kizigo. Pia Wizara ifanye uvunaji wa makusudi kupunguza idadi ya wanyama.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara hii kwa maamuzi yake mazito na mazuri. Napenda kuipongeza Serikali kwa kuongeza tozo katika sekta ya uwindaji na ningependekeza pia hata tozo ya kuingilia kwenye Mbuga zetu za Wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutofautiana na Wizara kuhusu kupandisha bei ya mbao laini *(soft wood)*. Mimi nikiwa mwakilishi wa wananchi wa Wilaya ya Mufindi inayotoa zaidi ya asilimia 60 ya mbao hizo, tunaona kuwa tumezibwa pumzi kwa bei hii mpya pine na *soft wood* nyingine. Kuhusu *hard wood* na magogo yote yanayouzwa nje kwani biashara hii haina fadia kwa wananchi.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara hii kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni, Serikali ilipiga marufuku wananchi kuvuna mbao ambazo zimekuwa zikitumika kwa ujenzi wa nyumba za watu binafsi pamoja na kuendeleza miradi ya Serikali na Halmashauri. Hali hii imesababisha miradi mingi kukwama na hasa katika Halmashauri yangu ya Kibondo kwa sababu wale ambao wamekuwa wakivuna mbao na kuuza walipigwa marufuku na kutokuendelea na uvunaji wa mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kibondo imezungukwa na pori pande zote, hivyo naishauri Serikali iruhusu wananchi kuvuna mbao ili kuendeleza miradi na pia kuwapa ajira wananchi wanaoishi kwa kutegemea ufundi wa kutumia mbao kama vile mafundi seremala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkaa, wananchi wa Wilaya ya Kibondo wamejikuta pia wanakumbwa na tatizo la kukosa kuni na pia mkaa kwa shughuli ama matumizi ya kupikia. Kila wanapojaribu kwenda kuvuna bidhaa hizo porini hukamatwa na maafisa wa misitu na kupelekwa mahakamani. Kwa kuwa hakuna njia nyingine mbadala ya bidhaa hiyo na kwa matumizi hayo, naomba Serikali kulegeza sharti hilo ili kuwarahisishia maisha wananchi. Kwa wale wanaotumia mbinu za kupata bidhaa hiyo, huiuza kwa bei ya juu wakati kipato cha mwananchi wa kawaida ni cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu warina asali, katika Wilaya ya Kibondo ina warina asali wengi. Tatizo kubwa lililopo ni asali hiyo kutokupata soko mbali na ushirika uliopo unaoitwa *UKI.* Naomba umoja huu ambao kazi yake ni kurina asali na kuuza ili waweze kuwa na makusanyo makubwa ya asali na kusafirisha nje ya nchi ama mahali popote penye soko kwa sababu tatizo la soko kwa zao hilo na kwa wananchi wa Kibondo hakuna. Baada ya kujibiwa haya, naunga mkono hoja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Zabein Mhita pamoja na watendaji wake wote wa Wizara ambayo nimeifanyia kazi kwa miaka saba.

Aidha, nichukue fursa hii kumpongeza Mkurugenzi wa Wanyamapori Bwana Severe pamoja na ofisi (Idara) yake kwa msaada, ushauri na mshikamano mkubwa wanaotupa Wilaya ya Kilindi. Pongezi maalumu zimfikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Mheshinmiwa Waziri ana taarifa kuwa kuna mbuga ya wanyama katika Wilaya ya Kilindi iitwayo Kitwai katika kata za Saunyi na Mkindi? Mbuga hii ni *hunting block* moja inayomilikiwa na *Masai land.* Mkurugenzi wa wanyamapori na ofisi yake wanazo taarifa za mbuga hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 4 (sera na sheria), nanukuu; "Jukumu kubwa la sekta ya wanyamapori wamaendelea kuwepo katika mazingira yao na wananchi wanashiriki katika kuwahifadhi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbuga hii wawindaji wanaingia na kutoka wawezavyo, hakuna geti wala posti ya kudhibiti. Je, Wizara haiwezi kutusaidia kujenga posti ili kuwe na udhibiti endelevu? Je, Wizara yako haiwezi kuwaelimisha wananchi wanaozunguka mbuga hiyo kuhusu uhifadhi wa wanyamapori? Je, fedha zitapatikana kwa mwaka huu 2007/2008?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *game scout* ambao wamekuwa wakijitolea, je, Mheshimiwa Waziri kwa nini wasiajiriwe ili kuongeza nguvu kazi kwani wamejitolea kwa muda mrefu? Niombe Wizara itupatie *experienced ranger* ambaye atawafundisha *(on job training),* huyu agharamiwe na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyuki, katika ukurasa wa 27 (sahihisho dogo); Kijiji cha Mswaki kipo Wilaya ya Kilindi kabisa siyo mpakani. Naishukuru sana Wizara kwa kutuwezesha wana-Kilindi, lakini naomba sasa tutafutiwe masoko ya kuuza asali na wawekezaji wa kuwekeza kwenye *packing* ya asali hiyo. Hii ni muhimu sana ili lengo lenyewe lionekane na kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii/wanyamapori, hivi mkataba wa Loliondo wameshindwa kuupitia upya? Lipi linalomshinda Mheshimiwa Waziri na ofisi yake! Wanaelewa yanayoendelea huko? *Please show your ability to take action!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Wanyamapori, ni vipi kile kilichotokea Forodhani, Tandale, lini kitajengwa katika kiwanja chake kilichopatikana karibu na eneo la Karimjee?

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza watumishi wote wa Wizara hii muhimu. Wizara hii ni moja ya Wizara nzito zenye malalamiko mengi kwa watu wasioijua kwa undani. Kwa watu wanaofahamu lazima watapogeza shughuli zifuatazo:-

Kwanza wanyamapori, napongeza Wizara kwa kuongeza bei ya wanyamapori kama ilivyotangazwa na Mheshimiwa Waziri kwenye Bajeti yake. Ni muhimu Wizara iwe macho sana kwani bei inapongezeka ndipo uwindaji haramu utaongezeka kwa wawindaji kukwepa kodi. Hata askari wa wanyamapori watakaoongoza wawindaji nao waangaliwe ili wasirubuniwe na wawindaji hao. Kutokana na ada kupanda na kwa kuwa Serikali inatoa asilimia 25 kwa vijiji vinavyopakana na vitalu vya uwindaji ada hiyo iongezeke kwa maeneo hayo ili wananchi nao waone manufaa ya wanyamapori.

Pili ni kuhusu usalama wa watalii. Usalama wa watalii ni muhimu sana kwani uvamizi ukiendelea watalii wanaweza wasije kabisa na kusababisha kukosekana kwa mapato. Usalama huu inafaa kuhusishwa wananchi ili washirikishwe kuwataja majangili kwani wanaweza kuwa sehemu muhimu ya ulinzi.

Kuhusu wawindaji wenye vitalu vya uwandaji waelezwe washiriki kwa hali na mali kulinda maeneo yao na kusaidia wakati matukio ya ujambazi yanapotokea isiwe tu wanajitokeza kwenye vitalu vyao.

Mheshimiwa Waziri Kamati imefanya ziara nyingi kwenye maeneo mbalimbali kuna baadhi ya matatizo ambayo yanafaa yaboreshwe. Kwenye eneo la Ngorongoro inafaa kubuni njia sahihi ya magari kuingia ndani ya kreta kwani magari yamezidi na kuharibu mazingira ya eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuandaa na kuanzisha kreta ya Embakai ili kupunguza mafuriko ya magari ndani ya kreta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi kwenye *PWPF* kwa kuwa kuhifadhi wanyamapori ni muhimu sana katika kuwezesha kulinda rasilimali ya wanyamapori katika mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo ya wazi. Ili ulinzi uimarike ni afadhali watumishi waongezwe katika maeneo yenye upungufu pamoja na kuongeza vifaa muhimu vya ulinzi.

Mwisho, naomba Serikali ifanye jitihada za kuelimisha jamii kuhusu kulinda wanyamapori pamoja na kuwasaidia kuanzishwa kwa *WMA* ili nao washirikishwe katika matumizi endelevu ya wanyamapori nao wapewe mgao wa mapato ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mweyekiti, ombi, kwa kuwa Tanzania ina Chuo maarufu cha Mweka, inafaa sasa chuo hicho kiwe Chuo Kikuu cha Wanyamapri ili kupunguza kukosekana nafasi ya masomo na kupunguza wanafunzi kwenda Afrika Kusini au Ujerumani kutafuta elimu ya Chuo Kikuu kwani kushindwe hili. Naomba sana. Mheshimiwa Waziri naomba majibu kwenye majumuisho yako.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Hata hivyo, ningependa nimuulize Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii maswali yafutayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la muda mrefu katika Wilaya ya Kasulu na hasa Kasulu Mashariki inayopakana na Pori la Hifadhi ya Moyowosi na misitu mingi tu ya hifadhi katika eneo hilo. Tatizo kubwa ni kwamba mipaka ya hifadhi imesogelea sana maeneo ya makazi ya wananchi katika vijiji 16 vya Jimbo langu. Tatizo hili liliongezeka sana baada ya oparesheni vijiji iliyofanyika mwaka 1974 bila kuzingatia maeneo ya hifadhi (mipaka) . Wananchi wao hawana makosa walipelekwa pale na Serikali. Vipo vijiji sasa vya Kagera, Nkanda, Mvinza, Zeze, Asante Nyerere, Mvugwe, Makere,

Kwaga, Kigembe na kadhalika vipo ndani au karibu sana na mpaka wa hifadhi. Mipaka hii ya hifadhi iliwekwa na utawala wa kikoloni mwaka 1954 wakati huo idadi ya wakazi/wananchi walikuwa wachache tena wachache sana. Maeneo mengine hayakuwa na watu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Wizara itamaliza tatizo hili kwa kupitia upya mipaka hii ya hifadhi zetu? Sisi Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu tumeshaanza mchakato huu. Ni matumaini yangu Wizara yako inazo taarifa hizi na hivyo kuomba ushirikiano wa karibu. Misitu mingi na mapori yetu ya akiba *(Forest Reserve)* yaliyopo Wilaya ya Kasulu yameathirika sana na kuwepo kwa wakimbizi (kukata miti ovyo) bahati nzuri sasa wakimbizi wameondoka, ni mkakati gani wa Wizara kurejesha misitu yote katika uasilia wake? Nashauri moja ya mikakati iwe kuimarisha Idara ya Misitu ya Wilaya kwa kunipatia gari la doria na mafunzo ya maafisa wake. Waliopo ujuzi wao unatia shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya *Commonity Forestry* ni nzuri sana inapewaje msukumu wa Wizara yako mama? Vitalu vijijini viko wapi? Mabwana misitu wako wapi? Dhana hii ndiyo msingi wa kukendeleza sekta hii ya misitu.

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naipongeza sana Wizara kwa marekebisho ya bei na ada za uwindaji kwani sasa nchi itapata fedha kulingana na uvunaji wa maliasili inayovuna.

Kuhusu utunzwaji wa fukwe za bahari ya Hindi siyo endelevu na kwamba ni chafu kiasi cha kukatisha tamaa hali ya kuwa wenzetu nchi jirani hunufaika sana na fukwe. Nashauri kiwepo chombo kitakachokuwa kinahudumia fukwe na kuweka vivutio kama vile boti za usafiri ndogo kwenda visiwa vya karibu na kuridi ili kujiingizia mapato. Fukwe ni rasilimali kubwa, nashauri tuzifanyie utafiti ili zituletee faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvunaji wa mikoko. Kumekuwepo na uvunaji wa miti hiyo ya asili bila kuwashirikisha wanakijiji/vijiji husika, mifano ni mingi. Hali hii imewafanya wananchi wa maeneo husika kuvuna kwa wizi na hivyo kuinyima Serikali mapato makubwa. Baada ya kukemea na kuwaadhibu wanaokamatwa nashauri elimu ya makusudi itolewe kwa wanavijiji husika ili waelewe nini umuhimu wa mikoko na faida zake kwa nchi yetu. Aidha, zitumike mbinu shirikishi katika kulinda rasilimali hizo. Pamoja na ushauri huo naomba pia asilimia fulani ibakie kwa vijiji ambavyo rasilimali hizo hutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri kila palipo na hifadhi ya misitu au wanyama, wananchi wasiruhusiwe kuishi kwani hujenga shule, zahanati na kusababisha kuwa makazi yao ya kudumu jambo ambalo huleta matatizo makubwa kwa watumishi na pia ni hatari katika maeneo hayo.

Naomba kuwepo na timu kazi ili kuelimisha umma na kwamba Halmashauri ziombwe kutotoa vibali vya ujenzi katika maeneo hayo mfano Saadani, Kiteto, Selous, Rombo na kadhalika.

Pia naomba kuchangia kuhusu mradi wa uvuvi. Nimeleta mapendekezo ya namna ya kuwasaidia wavuvi wasivue kwa kutumia zana duni za hatari. Sijajibiwa. Vijana wangewezwa kutumiwa kwa kupitia mradi wa *MACEMPT* lakini wapi? Hivi tatizo ni nini? Fedha tunaelezwa ipo utekelezaji unakwama wapi? Hapa nazungumzia uvuvi wa Bahari ya Hindi hasa Tanga, Lindi, Mtwara, Dar es Salaam na Pwani. Naomba tu tuwasaidie vijana wainue uchumi na kuboresha maisha yao. Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia heri na naunga mkono hoja hii.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi kubwa waliyoifanya wakati wa kuandaa Bajeti hii.

Naanza kuchaingia maeneo yafuatayo; Idara ya Misitu na Nyuki. Naipongeza Wizara kwa kuongeza mapato ambayo ni makubwa sana, naishauri Serikali iweke mkakati mahususi hasa kufuatilia utendaji kazi wa maafisa misitu wa Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika pori la Kigosi/Myowosi uvunaji wa misitu ni mkubwa sana, nafikiri kwa kuwa watendaji hawa wamekaa muda mrefu yanahitajika mabadiliko. Kwa kuwa, wapo watendaji ambao si waaminifu mfano kati ya tarehe 06 Aprili hadi 09 Aprili, 2007 watumishi wa Idara ya Misitu walienda kijiji cha Mjimwema kilichopo Bukombe muda wa saa nane, wakapiga risasi ng’ombe wanaokadiriwa kuwa kumi, uharibifu wa baiskeli na mengine mengi wakiwatuhumu kwamba wako ndani ya hifadhi. Naiomba Serikali iwaeleza wananchi wa Bukombe na kijiji cha Mjimwema hawa watumishi wa Serikali inawachukulia hatua gani ?

Aidha, naipongeza Serikali kwa kuanzisha mradi kabambe wa ufugaji wa nyuki ikiwemo Bukombe. Naiomba Serikali kupitia Bunge lako Tukufu iwaeleze wananchi wa Bukombe hasa wafugaji wa nyuki ni lini vibali vya kuingia pori la Kigosi /Myowosi kuvuna mazao yao vitatolewa Bukombe badala ya kwenda Kahama?

Mheshimiwa Mwenyekiit, Idara ya Wanyamapori, najua Serikali inafanya kazi kubwa sana, nawapongeza kwa kuamua kupandisha viwango vya uwindaji ili kuongeza mapato ya Taifa. Ni ukweli usiopingika nchi yetu ni nchi yenye rasilimali nyingi ni tajiri sana, fungeni mkanda, kaza kamba, Taifa liondokane na umaskini.

Mheshimiwa mwenyekiti, kuhusu Idara ya Utalii napenda kuishauri Serikali ili kuongeza hoteli kwa ajili ya watalii, Serikali ifanye mazungumzo na mashirika yasiyo ya Kiserikali wawekeze kujenga hoteli kwenye hifadhi zetu, mfano *PPF* na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanini Mashirika hayo yatasaidia mzunguko wa hela kubaki ndani ya nchi na kukuza uchumi kwa Watanzania. Pia naishauri Serikali ikusanye mapato ya maliasili na utalii kupitia *TRA,* vinginevyo utaratibu mpya wenye mfumo mzuri kama *TRA* uandaliwe na Wizara ili mapato yasipotee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Serikali iangalie kwa makini ongezeko katika mkaa na maliasili ambayo mwananchi wa kawaida anatumia. Pia Serikali iangalie ongezeko la mapato ambalo ni zaidi ya 100% kama kweli litafanyakazi vizuri. Hata kwenye Kamati lilizungumzwa hili kwa kulinganisha na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusije tukafika sehemu Watanzania wakaumia vinginevyo naipongeza Wizara endapo hatutaumiza Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo naomba kusema naunga mkono hoja ila Serikali/Wizara itekeleze vizuri.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo kutengwa kwa ajili ya watu wanaoishi kandokando ya hifadhi ili watu hao wapate mahali pa kupata mahitaji kama kuni, majani ya kuezeka, nguzo za kujengea, malisho na mashamba, naomba kufahamu kiasi cha fedha kinachotolewa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kila mwaka kutoka Hifadhi ya Burigi, kiasi kinachotolewa na Hifadhi ya Burugi kwa vijiji vinavyopakana na hifadhi hiyo na mpango wa wananchi wanaoishi karibu na mbuga za wanayama kuwa wanapewa nyama inayotokana na wanyama ili nao waone kuwa wanyama ni mali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mali iliyohusika na ujangili huchukuliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, je, mali inayokamatwa na hifadhi ya Burigi imeiingizia Taifa kiasi gani cha fedha? Je, Serikali hadi leo imetumia kiasi gani cha fedha kwa ajili ya fidia kwa mazao ya wananchi yanayoharibiwa na wanyamapori kama tembo?

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote waliohusika kutayarisha hotuba hii yenye matarajio mema katika sekta hii muhimu. Pamoja na pongezi hizo, lakini kuna mapungufu makubwa ambayo wanaomba Mheshimiwa Waziri na timu nzima ihakikishe inakarabati maeneo ambayo yanaleta fedheha kwa uongozi mzima ambao hauna hatia.

Kwanza maofisa misitu wa Wilaya ambao hawajawahi kusikia kasi mpya wapumzike wawape nafasi vijana wazalendo ambao wana ari ya kazi, Wizara itunge Sheria ambayo itawabana wenye malori ambayo yatapatikana yamebeba mbao au magogo bila kulipa ushuru yataifishwe, hii itasaidia kuzuia njia za magendo na pia mapato ya Serikali yataongezeka maradufu, mtandao unaohujumu maliasili za magogo na nyinginezo, kuanzia Wizarani, Halmashauri na hata watendaji wa kata wajulikane maana wanaupaka matope viongozi waadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiit, kuhusu maeneo ya utalii katika Mkoa wa Dar es Salaam kama Jengo la Makumbusho ya Taifa, Nyumba ya Sanaa ya Mwalimu Nyerere, Kijiji cha Makumbusho Kijitonyama, fukwe za bahari katika maeneo ya Kigamboni zijengwe hoteli zenye hadhi ya kuanzia nyota tatu hadi tano na Wizara itangaze Kigamboni kuwa ni eneo la kitalii kwa kuwakaribisha wawekezaji kujenga majengo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bodi ya utalii ipewe uwezo wa kuchapisha vijarida ili visambazwe sehemu mbalimbali duniani na hasa katika mashirika ya ndege kama *Emirates Airlines, British Airways* na kadhalika. Vijarida vipatikane kila ofisi ya Balozi. Bodi hii ya utalii ifanye ziara maalumu ya mafunzo katika nchi ya Singapore, waende wakaone ile *zoo* ambayo inapata watalii 800,000 kwa mwezi ambayo ina wanyama toka *East Africa* na duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji la China *(CCTV 9)* litangaze maliasili zetu kuliko ilivyo sasa ni Zambia ndiyo wanatoa matangazo. Pia viwanja vya ndege vya nchi kubwa kama *Beijing Airport* (China) Marekani, *Singapore Airport* na kadhalika kwa kushirikiana na bodi ya utalii zitafute uwezekano wa kuweka matangazo katika viwanja vyao kwa lengo la kuitangaza Tanzania na maliasili zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kuwapongeza Waziri Naibu Waziri na Katibu Mkuu mpya. Naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mmwenyekiti, kwanza ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Pili, ninaupongeza uongozi wa Wizara kwa kufanya kazi nzuri. Mwenyewe Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusudi langu ni ombi. Vikundi vya uvuvi walioacha uvuaji haramu wasaidiwe zana mbadala ili wasirudie tena. Wavuvi hao tayari wameshajiunga katika vikundi kwa Lindi na Mtwara.

Kuhusu boti, nimeambiwa boti ya ulinzi kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu imetengwa sina neno ahsante. Kuhusu utalii Kusini upo pia, napo kuangaliwe kwa jicho la huruma kuna mambo mengi yafutayo kwa tahadhali ili yaangaliwe na msitufikirie utalii uje Tendanguru Mipingo/ Lindi Vijijini ambako alitolewa *dinnossor* (aina ya mjusi) ambaye yupo Ujerumani wanakuja kila mwaka Wajerumani kumtafuta mjusi mwingine kwani inasemekana kuwa yupo mwingine baba yao aliyechukuliwa ni mama na mtoto tu. Eneo hilo hutembelewa na *Archaelogists* na *Historical Scientists* wa nje.

Pili, Lindi ni ya tatu katika Tanzania kwa msitu mkubwa, pori la Miombo ikiwa ni ya kwanza ni Tabora milioni 5.3, hali ya pili ni Rukwa milioni 4.9 na ya tatu ni Lindi milioni 4.3 na pia kuna *mangrove Forest* 26,500. Kuna *White Beach* Lindi Mjini, Kilwa, Mchinga, *Mitema Beach* ambayo ipo katika ramani ya dunia ya wajiolojia. Pia kuna *Hippo Kingdom* kisiwa kikubwa Kilwa takribani Bokoe 500 na zaidi wanaosema na watu, kuna *Ruins of Kilwa* ya Waarabu, makaburi 40 ya watu walizikwa siku moja baada ya kufa siku moja kwa ajili ya ugomvi wa familia (Masharifu), maeneo ya *Vasco Dagama* katika karne ya 16 hadi karne ya 21, pia kuna *Selous Game Reserve* ambayo kuna aina zote za wanayama wakiwemo twiga, tembo, simba, swala na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Haita 800 za uwindaji maalumu, kuna boma ya Wajerumani Liwale ambayo ndani yake kuna maonyesho mengi moja wapo ni alama ya vichwa vya ma-*chief* wa Liwale, walioongoza vita dhidi ya Wajerumani *(Ngindo*

*Chiefs),* kuna *Arabic Ruins* ya Kilwa Kivinje, Kilwa Kisiwani na Songo Mnara ambayo ni kivutio kikubwa kwa jamii mbalimbali nchini. Kuna vijiji au miji wa karne ya 14 hadi 19 ambayo ilikuwa chini ya Masultani 14 katika miaka ya 1956 ya utawala wao na pia kuna Mapango, kuna pango kubwa Tanzania liitwalo *Nang'oma Caves* ambalo liliutumika wakati wa vita vya Wajerumani wananchi wa Kilwa, Wamatumbi wakijificha wananchi wa Kilwa Wamatumbi wakijificha wakati wa vita vya Majimaji. Pango ambalo kuna mapango 20 ndani yake zaidi kuna njia moja ya kuingilia ndani na 4 za kutokea nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mengi lakini kwa leo yanatosha. Hizo ni tosha kwa utalii. Ombi tu na sisi Lindi tufikiriwe utalii Kusini. Ahsante sana.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe kwa kuanza kazi ya Wizara hii kwa umakini na kwa jitihada kubwa. Aidha, nawapongeza pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita na Katibu Mkuu wa Wizara hii Bibi Blandina Nyoni pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii.

Naanza kuchangia kuhusu kwanza kabisa msitu wa Vikindu uliopo kilometa chache toka Jiji la Dar es Salaam kuelekea Mkuranga, Mkoa wa Pwani. Msitu wa Vikindu umeelezewa ni msitu pekee duniani wenye vinyonga vyenye pembe tatu. Nimewahi kabla kuzungumzia jambo hili kwa bahati mbaya msitu huu umeanza kuisha kabisa. Wenyeji wamekata miti yote mingi na kuacha miti michache karibu na barabara, msitu huu katika miaka ya 1981 na kuendelea bado ulikuwa na simba. Kwa masikitiko makubwa vinyonga hawa wa pembe tatu wanatoweka. Ningefurahi iwapo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ataliangalia kwa karibu jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya mambo ya kale, kwanza kabisa kuhusu uhifadhi wa barabara zilizotumika kwa biashara ya utumwa wakibeba biashara ya ndovu, nafurahi kuona Wizara hii inathamini eneo hili la urithi wa kale. Naomba sana tena sana katika eneo la Chuo cha Chimwaga Dodoma, ipo barabara iliyotumika wakati wa utumwa sehemu ambayo watumwa walipopitia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali sana Wizara hii bila kuchelewa ishirikiane na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)* ili kuonyeshwe sehemu hiyo kabla haijapotea hasa wakati huu wa ujenzi wa Chuo Kikuu hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba iliyopo Magomeni, Dar es Salaam ambapo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliishi. Napongeza kwanza Wizara iliwahi kukarabati nyumba hii. Kutokana na umaarufu wa Baba wa Taifa na juhudi zake za kuleta Uhuru wa nchi yetu na kukomboa nchi nyingine za jirani ni muhimu basi nyumba hii ya Magomeni ihifadhiwe kama *Museum* ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuitengenezea mandhari nzuri, ni vyema kuweka ndani baadhi ya vifaa alivyotumia yeye na familia yake zikiwemo picha mbalimbali za familia na za harakati ya Uhuru pamoja na zawadi mbalimbali alizozipata toka sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu lingine kwa Waziri ni kutaka kujua kama katika sekta hii watu binafsi wenye vifaa vya zamani mbalimbali kama wanaweza kuhifadhi vifaa hivyo katika maeneo yao na kuwezesha watalii na wananchi kuvitembelea vifaa hivyo. Aidha, wanaruhusiwa kupeleka vifaa hivyo katika jumba la kuhifadhi mambo ya kale, *museum* ya Baresse.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bonde la Olduvai, karibu na barabara ya kutoka Arusha kuelekea Mwanza. Eneo hili la Bonde la Olduvai halijatangazwa vizuri na halionekani vizuri toka hata barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Oldupai ni mmea unaoota katika maeneo makavu yasiyo na mvua za kutosha na unahimili sana ukavu. Wakati wa ukoloni, wakoloni walishindwa kutamka Oldupai wakatamka Olduvai, naomba sasa Wizara hii ijitahidi sana kurudisha heshima ya jina hili nchini na nje ya nchi na kuwa Oldupai.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge huyo ndiye Dr. James M. Wanyacha, anaweza kuamua kumwalika mtu yeyote na wakati wowote akiwa ndani. Waheshimiwa Wabunge huyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho jioni hii ya leo kwa kuzungumza na sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri na yeye aweze kuchangia hoja kwa dakika kumi na tano na baadaye tutampa nafasi Mheshimiwa Waziri kwa dakika arobaini na tano ndipo tuingie kwenye hatua inayofuata. Mheshimiwa Naibu Waziri karibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, naomba tu nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kisha nichangie hoja iliyo mbele yetu kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah wa Mafia na Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji Mbunge wa Kilwa walikuwa wanahoji kuhusu mradi wa *MANSEP*. Shabaha kubwa ya Mradi wa *MANSEP* ni kuimarisha mfumo wa usimamizi wa rasilimali zilizopo baharini na Pwani kwa kushirikisha Serikali jamii, sekta binafsi na wadau wengine ili kuboresha maisha ya wananchi. Mradi wa *MANSEP* utatekelezwa katika Wilaya zote 14 za Pwani ya Bara na katika Visiwa vya Unguja na Pemba kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unayo maeneo manne ya utekelezaji kama ifuatavyo; eneo la kwanza linahusiana na usimamizi madhubuti wa ukanda wa uchumi wa bahari. Eneo la pili linahusika na kuweka usimamizi madhubuti wa mazingira ya bahari na ya Pwani. Eneo la tatu linahusika na mfuko wa maendeleo ya jamii za Pwani na ni katika eneo hili ndipo ambapo mfuko unawezesha jamii za Pwani kuibua, kutekeleza na kusimamia miradi midogo midogo ya kuboresha maisha ya jamii husika na hivyo kuwezesha kuwepo kwa mfumo wa *Ecologies* ambao ni endelevu. Eneo hili lina kazi kubwa mbili zifuatazo: Moja, utoaji wa fedha kwa ajili ya kuwezesha uendesha miradi midogo midogo na kuwapa uwezo wanajamii ili wawe na uwezo wa kuibua, kusimamia na kufuatilia miradi yao. Eneo la nne, ni huduma kwa utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ambazo tayari mradi huu umekwisha kufanya ni: Kwanza, mikutano ya kuelimisha wananchi kuhusu kuibua na kuendesha miradi, imefanyika kwa wananchi 12,700. Jumla ya shilingi 476, 508,382/= zimepelekwa katika Wilaya tatu za majaribio kwa ajili ya kuwezesha Halmashauri husika kutekeleza na kufuatilia utekelezaji wa kazi mbalimbali za mradi. Pia jumla ya shilingi 69,484,870/= za mfuko wa vijiji vya Pwani tayari zimekwisha tolewa kufadhili miradi ya vikundi vya wavuvi katika Wilaya ya Mafya.

Vikundi 19 vya mfano vimehamasisha kuanzisha vikundi vya kulinda rasilimali. Jumla ya vikundi 33 vyenye jumla ya wanavijiji 339 katika vijiji 9 Wilaya ya Kilwa wamefahamishwa jinsi ya kuendesha miradi midogo midogo na wamepatiwa vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 84.

Mabwawa ya samaki matatu yameanzishwa katika Wilaya ya Kilwa na vifaranga 13,000 vimepandikizwa na kikundi kimoja kimeshavuna kilo 1800 zenye thamani ya shilingi mililioni mbili. Wilaya zote tatu zimepelekewa vifaa vya ofisi kama kompyuta na *printers* pamoja na thamani.

Boti sita ikiwa na maana kwamba mbili kila Wilaya na pikipiki 14 ikiwa na maana sita kila Wilaya zinasubiri kusambazwa hivi karibuni katika Wilaya hizo husika. Pia ununuzi wa magari matatu moja kwa kila Wilaya umekwisha pitishwa na zabuni ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kwa kifupi sababu ambazo zimefanya mradi wa *MAMSEP* kuchelewa. Moja, matakwa ya mradi huu ni kuwa na wananchi wanaotakiwa kuibua miradi wenyewe, kwa hiyo, kulikuwa na haja ya kuhusisha wanavijiji na kujenga uwezo ili kuzuia udanganyifu na kuhakikisha kuwa manufaa ya mradi yanawafikia walengwa. Mlolongo wa uchambuzi wa miradi iliyoibuliwa na wananchi ilikuwa inachukua muda mrefu, mlolongo huo sasa umepunguzwa na hivyo kuchukua muda mfupi kuliko ule uliokuwa unatumiwa hapo mwanzoni. *TASAF* ambao ni watekelezaji wa mradi hawakuwa na uwezo wa kutosha hapo mwanzo, sasa Wizara imeongeza watalaamu wa uvuvi ili kuongeza kasi ya utekelezaji unaotarajiwa.

Vilevile uchache wa watumishi katika mradi wa upande wa Wizara ambayo ina dhamana kwa mradi wa upande wa *TASAF* katika ngazi ya Wilaya, watumishi wa *TASAF* wameeleweshwa kuhusu mfuko wa vijiji vya Pwani ambao unatumika kwa ajili ya miradi mdogo midogo kwa watumishi kwa utaratibu wa *TASAF*. Vile vile utekelezaji wa mradi katika ngazi ya vijiji unahitaji wananchi wawe na vikundi, ukosefu wa vikundi katika vijiji ulisababisha ucheleweshaji wa kutekeleza malengo ya mradi. Muda ulihitajika kuhamasisha wananchi kuunda vikundi na kuwaelewesha jinsi ya kuibua na kuendesha miradi, hii ilihitaji muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uzoefu ambao tumeupata pamoja na washirika wetu kwa maana ya *TASAF* na Benki ya Dunia, mpango huu utaenezwa katika Wilaya zote zinazopakana na Bahari ya Hindi kutoka Tanga mpaka Mtwara. Kwa

hiyo, naomba niwatoe wasiwasi Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah na Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji kwamba sasa mradi utakwenda kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dunstan Daniel Mkapa ameongelea kuhusu suala la Tembo kuwa kero kwa wananchi katika Wilaya ya Nanyumbu na ameeleza kwamba Tembo hao wanatokea kwenye Pori la Akiba la Lukwika Lumisule. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu itachukua hatua za kupambana na hawa tembo waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *DED* wa Nanyumbu anashauriwa kuajiri Askari Wanyamapori kufikia_ idadi itakayowezesha kupunguza tatizo hilo, lakini vilevile utaratibu uliopo kwa hivi sasa utatumika ambapo Afisa Wanyama Pori anapaswa kutoa taarifa kwa Mkurugenzi Idara ya Wanyamapori ili msaada utolewe mara moja kutoka katika vikundi vya kuzuia ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti yeye alikuwa anashauri kwamba Sheria ya Wanyamapori iwasilishwe Bungeni kuondoa matope wanayopakwa Viongozi na Watendaji kutokana na Sheria ambayo ipo sasa kupitwa na wakati. Sera ya Wanyamapori imekwisha pitishwa na Serikali baada ya hatua hii, Sheria itawasilishwa Bungeni mwaka huu wa fedha baada ya kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga naye pia alikuwa amezungumzia suala la Tembo waharibifu. Yeye amesema katika Jimbo lake watu ambao wameathiriwa na Tembo kwa maana ya kuharibiwa mazao yao na kuuawa hawajalipwa kifuta machozi.

Ninaomba nimshauri Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga kwamba utaratibu utumike na taarifa zitolewa kwa Afisa Maliasili wa Wilaya ili naye afikishe taarifa hizo Wizarani ili wale wanaostahili kulipwa waweze kulipwa.

Kama nilivyokwisha eleza wakati nikijibu swali hapa Bungeni kuhusiana na Wanyama waharibifu vilevile tulieleza kwamba Serikali imeamua tangu Julai, 2007 kuongeza kifuta machozi ambacho kilikuwa 50,000/= na kuwa 200,000/= na vilevile kulipa shilingi 100,000/= kwa shamba lililoharibiwa na wanyamapori ambalo lina ukubwa wa zaidi ya ekari moja linalipwa shilingi 100,000/=.

Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo alieleza kwamba *GTZ* iliahidi kukarabati boma kwa shilingi milioni 8 lakini tangu watoke halijashughulikiwa na Wizara iliahidi kwamba ingeweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukiri kwamba ni kweli Wizara iliahidi kwamba ingetoa shilingi milioni 8 kukarabati boma hilo lakini naomba nimwahidi Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo kwamba pesa hizo zipo na zitatolewa ili kukamilisha kazi ya ukarabati wa boma hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura yeye alikuwa na hoja ya kusema kwamba Serikali itoe ruhusa kwa wananchi waweze kujilinda dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Sheria ya kuhifadhi wanyamapori inatoa mwanya kwa wananchi kujilinda dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu lakini wanachopaswa kufanya ni pale ambapo wanyamapori hao wametishia maisha yao, ama wametishia kufanya uharibifu wa mali yao na baada ya kuwaua wanatakiwa kutoa taarifa katika Ofisi ya Wanyapori iliyokaribu na kuwasilisha nyara iliyotokana na wanyama hao. Kwa hiyo, haitawezekana kwamba wamuue mnyama halafu wabaki na nyara itakuwa ni makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda naomba niiishie hapo lakini naomba tena kwa mara nyingine niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi)*

**MWENYEKITIl:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kuunga mkono hoja na hasa kwa ukarimu wako katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Waziri ili na yeye aje kutoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa. Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe tafadhali karibu!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru sana kwa fursa hii ambayo umetupatia ili tuweze kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wenzetu wakati wa kujadili hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imechangiwa kwa kuongelewa hapa Bungeni na Wabunge 11, imechangiwa kwa maaandishi na Wabunge 81 na Wabunge wengine 29 walichangia hoja hii wakati wa hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na wakati wa kujadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa sababu hiyo, hoja nyingi zimetolewa wakati wa kujadili hoja hii na kwa hivi nitawaomba sana Waheshimiwa Wabunge kwamba tutajibu hoja nyingi inavyowezekana kutokana na muda uliopo lakini napenda niwahakikishie kwamba tunazithamini sana hoja ambazo zimetolewa na tutazitumia kwa kiasi kukubwa katika kuboresha utendaji wetu katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja zile ambazo kwa namna moja ama nyingine hatutaweza kuzijibu moja kwa moja hapa Bungeni basi tunaahidi tutazitolea majibu na tutawapatia Waheshimiwa Wabunge maelezo moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliochangia kwa kuongea hapa ndani leo ni: Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga ambaye ni Msemaji wa Kamati ya Maliasili na Mazingira., Mheshimiwa Ali Khamis Seif, nakushukuru sana kwa hotuba yako.

Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji Mbunge wa Kilwa Kusini, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mbunge wa Mchinga, Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo Mbunge wa Liwale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga Viti Maalum, Mheshimiwa James Daudi Lembeli , Mbunge wa Kahama, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah Mbunge

wa Mafia, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi.

Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha na Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Napenda niwashukuru sana kwa michango yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maaandishi ni: Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela na Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa Dr. Aisha Omar Kigoda , Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Mohammed Abdi Abdulaziz na Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis.

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mlingwa, Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri, Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu na Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Dr. Cyril August Chami, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid.

Pia Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibitili, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu, Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mheshimiwa Halima James Mdee na Mheshimiwa Eustace Osler Katagira.

Wengine ni Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, Mheshimiwa Dorah Herial Mushi. Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala na Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o. Nimeletewa taarifa hapa pia umepokelewa mchango wa maandishi kutoka kwa Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge 29 waliochangia hoja hii kupitia hoja za Mawaziri wenzangu ni: Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama – Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Mwantumu Bakar Mahiza, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mheshimiwa Dr. Cyril August Chami, Mheshimiwa Bahati A. Abeid, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Halima James Mdee na Mheshimiwa Bernadeta Mushashu. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa Bujibu Sakila, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Jacob Shibiliti na Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumai utanipatia fursa kidogo ili kufidia muda huu wa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia katika hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tutalizingatia hilo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nafurahi sana kwamba wachangiaji wengi waliunga mkono hoja, lakini kipekee kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa kuunga mkono hoja yetu kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya michango mingi ambayo imetolewa hapa juu ya biashara ya magogo, hakuna shaka kwamba kila Mheshimiwa Mbunge aliyezungumza aliona kwamba kasi ya kuvuna magogo hapa nchini ina athari kubwa kwenye mazingira yetu, inatuibia fedha nyingi sana za ndani na za kigeni na inapunguza kasi ya mapato ya wananchi wetu. Kwa hiyo, hatua ya kwanza hii tuliyoichukua ya kurekebisha bei ya magogo ni hatua muhimu ya kufanya watu ambao hawana nia hasa ya kukata magogo basi wasiendelee kukata magogo hayo.

Pili, magogo haya kwa miaka mingi hayajaangaliwa bei zake, yanauzwa kwa mazoea, msemaji mmoja wa wafanyabiashara hawa wa magogo na mwingine wa uwindaji wa utalii alipoona tumebadilisha bei akauliza nani amemfungua kipofu macho?

Kwa hiyo, hata wenyewe wanajua kwamba bei ya magogo ya dola 3.5 kwa *cubic metre* ya magogo ni bei ya kipofu sasa kipofu anaona tafadhalini eleweni. Bei ya magogo ya *pulp* katika dunia ncima na kiwanda chetu tunacho kimoja mimi nawapongeza sana wenye kwanda cha Mgogolo kwa sababu wamekigeuza kiwanda hicho kutoka kiwanda ambacho kinapewa ruzuku na Serikali.

Sasa kinatengeneza dola milioni tisa kila mwaka za karatasi iliyouzwa nje, ni muhimu sana. kinauza karatasi Mashariki ya Kati, kinauza Thailand, Malaysia, Ujerumani na kinauza Uingereza. *(Makofi)*

Sasa kule wanakouzia karatasi hizi bei ya magogo ya *pulp* ni 30 *cubic meters* kama ni *pine sparkler* kama ile inayouzwa *Sao Hill.* Hapa wananunua 3.5 *per cubic meter*, ndiyo tumerekebisha tukasema kwa sababu kiwanda chetu kina kasoro ya kuwa ndani ya nchi yaani kutoka Dar es Salaam Baharini wanaposafirishia mpaka Mgololo ni mbali. Basi tukarekebisha bei ya magogo haya ya kutengeneza *pulp* kutoka *dollar* 3.5 mpaka *dollar* 9 ili tuwaachie *dollar* 21 kufidia gharama za usafirishaji. Kwa hiyo, hakuna utata kwamba viwanda vya ndani vitaumia.

Pili, bei ya magogo ya kutoka kwenye miti laini *pine sparkler* hiyo inayotoka *Sao Hill* na *cypress*. Naomba nirudie tena kwamba Serikali inapokuza magogo haya, inakuza kwa uwekezaji wa riba ya asilimia 8 kwa miaka 25 mpaka 30. Miti hii ambayo imeanza *rotation* ya mwanzo kwa maana miti imetolewa nje imepanda katika mashamba yaliyopo kwa mara ya kwanza, mbegu zile tuliagiza kutoka nje kwa bei ya *dollar* 100 kwa kilo moja. Tumetoa *Honduras*, tumetoa *Costa Rica*, tumetoa *Belize, Dollar* 100 kwa kilo moja. Tukakuza miche. Bei ya mche mmoja ni shilingi 1,000, haiwezekani tulime shamba, tupande, tupalilie, tuondoa matawi, tupunguze miti midogo iliyo mingi ili tupate miti mizuri, tutumie shilingi 21,500 halafu turudi tuseme tunauza kwa shilingi 4,800, hii haiingi kwenye kichwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanaotuzunguka, Wakenya ndiyo maana wanapenda kuchukua mbao kutoka *Sao Hill* kwa sababu *cubic meter* moja ni *dollar* 3.5. Mwenendo, ni kuanza na tumeanza shughuli hii, tunayo rasilimali nyingi ya kutosha, tutaweza kuongeza mapato ya Serikali *in a very significant way* . Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunawaomba mtuunge mkono. *(Makofi)*

Tatu, katika eneo la miti migumu na miti ya asili hapa ndipo mazingira yanaharibiwa sana. Kama mazingira yataharibiwa yanahitaji kurudishwa. Utayarudisha na nini kama mtu anachukua magogo yako *class one logs* ni *dollar* 2,000 kwa *cubic meter* mpaka *dollar* 10,000. Mvule, Mkangazi, Mkuluti, Mninga hata miti ya kutengenezea vinyago inachukuliwa kwa shilingi 70,000, haiwezekani jamani! Hatuwezi kuuza mali za wananchi wa Tanzania kwa bei ya kutupa, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kabisa kwamba eti mbao zitapanda bei. Kwa sababu mbao zilikuwa zinauzwa bei ndogo sana, wakatokea wajasiriamali katikati hapa wanarusha magogo, wanakuja wanaandikiwa *permit* ya kununua magogo, wanakwenda wananunua *dollar* 3.5, wakitoka nje ya ofisi pale wanauza shilingi 150,000. Mbona mbao hazikupanda? Sisi tumepandisha kuanzia hiyo bei ya kutupa magogo, ya kukata kuyafikisha dola 21 ilingane tu na ile bei ya Serikali ya kukuza magogo hayo, bado hatujapata faida, bado tuna-*subsidize.* Kwa hiyo, jamani tuelewe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mimi naheshimu sana mawazo yote, lakini jamani una duka, unauza sukari, ukianza kuuza bei ya shangazi, bei ya Mariam, bei ya Mjomba, utaingia hasara na duka utalifunga. Tumesema tunataka kwenda kwa kasi, nafuu twende kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, magogo haya yamegawanywa katika *class* tano. *Class* ya kwanza ni kuni, akinamama wakienda kuchukua kuni kwa mzigo hakuna tatizo, haikubadilika bei. Hakuna mabadiliko katika kuni. *Class* ya nne ni yale magogo ambayo watu hawayatumii kwa sababu kuna magogo mazuri zaidi kwa bei ambayo ni poa kabisa. Kwa hiyo, yapo magogo kutoka kwenye misitu ya asili ya *cubic meter* moja, shilingi 80,000 kwa wale ambao hawataki kutumia mninga, wanatumia hayo. Yote yameelezwa vizuri katika *Government Notice.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wasome vizuri *Government Notice* kwa sababu *Class one* ni Mvule, Mkangazi na wenzake wa namna hiyo. *Class two* ni Kavasi, Mpoda, *Rosewood*, Mkuluti na miti ya namna hiyo. *Class three* ni mlingalinga na miti ya namna hiyo. *Class four* iko miti yake na mizuri tu. Kwa hiyo, hilo ninaliacha. Nimalizie tu kusema kwamba kama tungekuwa tunayauza magogo hayo vizuri tungekuwa na maeneo ya misitu ambayo tunakata miti, hatuwezi kupanda. Kwa mabadiliko hayo tutapanda miti maeneo yote ambayo yalishindikana kutokana na ukosefu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumshukuru mtani wangu Ali Khamis Seif, Waziri Kivuli wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Ameeleza kwa kirefu kweli kweli jinsi gani tungeweza kuongeza mapato kwenye Sekta ya Uvuvi. Lakini ningependa tu nieleze kwamba alisema nchini Namibia inakadiriwa kwamba wanapata kwa mwaka milioni *U$D* 152 wakati sisi tunapata chini ya *dollar* milioni 9. Ningependa nimshauri asome vizuri hotuba ile. Hayo ni maduhuli ya Serikali yaliyokusanywa, siyo mapato kutoka kwenye Sekta ya Uvuvi. Mwaka 2006/2007 jumla ya tani 341,550 za samaki walivuliwa nchi nzima na kutuletea mapato ya shilingi bilioni 285.7. Aidha, kiasi cha tani 50,350 kiliuzwa nchi za nje na kutupatia fedha za *dollar* za Kimerikani milioni 141.3 ambazo ni kama mara tatu ya mapato ya Namibia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tena kitu kingine ambacho tumekuwa tunazungumza sana kuhusu leseni kwamba leseni zetu ni *dollar* 18,000, ni kidogo. Hata mimi ningependa iwe kubwa. Lakini ningependa niwaeleze wenzangu kwamba tuelewe tofauti ya Bahari katika maeneo ya *template* na Bahari katika maeneo ya Ikweta kama kwetu. Katika maeneo ya Ikweta ukienda kwenye Msitu utakuta miti mingi, lakini yote

ni aina mbalimbali. Hakuna miti mingi ambayo inaota katika eneo moja lenyewe peke yake. Unakuta Mkuluti, mninga, na majani na vitu vingine vingi tu. Lakini hakuna kimoja ambacho kina wajumbe wengi wa kupiga kura kikamzidi mwenzake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vigumu sana kuanzisha kiwanda kwa ajili ya samaki wa aina moja kama ilivyo katika maeneo ya *template.* Katika maeneo ya *template* wale mliokwenda kule nadhani wote mmekwenda, mmekuta kwenye ardhi kuna miti mingi, lakini ni aina moja au mbili na baharini hivyo hivyo. Ikiwa ni *cold* ni *cold* pekee yake. Kwa hiyo, unaweza kuanzisha kiwanda kikubwa kabisa cha ku-*process cold* kutoka maji ya asili katika maeneo ya *template* na unaweza kuwakusanya wengi. Kwa sababu kile kitu kinaitwa a *puling of water.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiwa kama hapa Tanzania una *king fish*, una kibua, huwezi kuwa na *advantage* aliyonayo Mfaransa anayevua kwenye *North Sea*. Kwa hiyo, lazima tutofautishe. Hapa wanakuja kuvua samaki wanaozunguka kwenye Bahari kama Jodari. Hapa kwetu Jodari wanakuja kwenye mwezi Septemba mpaka Novemba, sasa wanazunguka kufuata chakula. Mwaka huu tumejiunga kwenye *confederation* ya *Indian Ocean Tune Commission* ili tuweze kupata takwimu zaidi kuhusu idadi na msimu wanapokuja kwa sababu mabadiliko ya Tabia nchi yameleta mabadiliko katika mzunguko wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wenzetu wanaotuzunguka leseni zao kama Msumbiji ni *dollar* 15,000 kwa mwaka, *Madagascar* ni *dollar* 11,000 kwa mwaka, *Seychelles* ni *dollar* 16,000 kwa mwaka na Kenya ni *dollar* 15,000 kwa mwaka. Mtani wangu amesema Somalia wanapata *dolla*r 100,000. Tatizo ni kwamba wale wahuni wa Somalia wakishakuta kuna meli huko wanakwenda wanazidai zikikataa wanazizamisha kwenye maji. Lakini wale ambao wanakwenda Somali *Land* upande ule mwingine wanalipa *dollar* 7,500 kwa mwaka. Kwa hiyo, naomba sana tuelewane hapa, hatuwezi ku-*charge* maembe, machungwa na mandazi bei moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imetolewa hoja kuhusu utalii na nadhani hoja hii ni nzuri kwamba *package tourism* ni mbaya sana inabakiza fedha Ulaya na inaleta fedha kidogo huku. Naomba jamani tuelewane tu kule Uingereza kuna Makampuni matatu tu ambayo yanahodhi karibu asilimia 67 ya utalii wa nchi zile, yale ndiyo yanakuwa na ushirikiano na makampuni yaliyopo kwetu hapa. Kwa hiyo, wao wanajua kwamba gharama zetu za utalii hapa ni kiasi gani na sisi hapa Tanzania hatutaki mtu aje na bangili, akishakuja na bangili anaingia kwenye hoteli anakula na bangili, anatoka anaingia kwenye baa anakunywa na bangili, anaingia kwenye *National Park* na bangili, haturuhusu hiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye mlango wa *National Park* unalipa *add dollars,* ukiingia kwenye hoteli yetu hapa Tanzania unalipa *add dollars*, kutegemeana na bei zetu. Tatizo sisi hatuna ubavu wa kuzifuata hizo *dollar* kule Uingereza na kushindana na wale wakubwa. Lakini kama tukiweka bei zetu vizuri sioni tatizo kwa wale kutulipa sisi na kulipia huduma zetu. Kwa mfano, kama huduma yetu, faida yetu ni *dollar* 10,000, yule Bwana akizungumza na mtu wa Ujerumani akampata *dollar* 15,000,

sisi kinatusumbua nini? Kwa sababu ndiyo biashara, yeye amezungumza naye vizuri. Siku moja mimi nilikwenda kwenye duka la *DHL* nikakuta bei imepanda kweli kweli. Lakini wameweka watu waliopo pale huwezi kusema hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kitu muhimu sana sisi Watanzania na wakala wote wa Utalii hapa nchini kwetu tunahimiza wapange bei zao vizuri ili waweze kulipwa vizuri. Najua kwamba hili suala la *package tourism* lina matatizo kule Visiwani. Lakini tutashirikiana na wenzetu tuone ni jinsi gani tutasaidiana ili kupunguza tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge na ningependa nijibu michango michache kati ya hiyo. Nina mtani wangu hapa Bungeni anaitwa Mheshimiwa Aloyce Kimaro. Sasa ameniona nimekaa hapa akaona Mpare amekaa hapa zamu yake kupigilia. Lakini alikuwa na masuala ya msingi. Suala la wale wabeba mizigo wanaowasaidia watalii kupanda Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aloyce Kimaro aliuliza tena swali hili kama swali la msingi ndani ya Bunge, tukajaribu kumjibu. Lakini mnajua utani wa mtu wa Vunjo na Mtu wa Mwanga unaendelea, usipoendelea mambo yanasimama. Niseme kwamba Mheshimiwa Aloyce Kimaro, yeye ndiyo Mwenyekiti wa *Association* ya wale wapanda Mlima. Kwa hiyo, mnajua katika mambo haya kuna mambo ambayo Serikali inaweza kukufanyia kwenye Jimbo lako, lakini kuna yale mambo ambayo wewe kama Mheshimiwa Mbunge unajitahidi unayafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulimshauri Mheshimiwa Aloyce Kimaro kuhakikisha kwamba suala la kazi na mapato linashughulikiwa vizuri, lishughulikiwa kisheria. Masuala ya kazi na malipo ya kazi yanashughulikiwa chini ya Sheria Namba 6 ya mwaka 2004, *Employment and Labour Relation Act,* na kwamba ingekuwa vizuri hiyo Jumuiya yao imwandikie Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ili atume mtaalamu awasaidie waweze kuwa na *Association* yao. Hii imekuwa kwa muda mrefu haiji. Kwa hiyo, juzi Jumatatu mtaalamu kutoka Wizarani ameombwa aende aonane na wale vijana ili mchakato wa kuanzisha Chama Huru cha Wafanyakazi cha hao wabeba mizigo kiweze kuanzishwa na wao waweze kuwa na nguvu ya majadiliano kuhusu maslahi yao na mazingira yao ya kazi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Aloyce Kimaro avute subira amsaidie huyo *Registrar* wa Vyama Huru vya Wafanyakazi ili aweze kuwaunganisha vijana wale, ama waunde Chama chao au wajiunge na Chama cha *CHODAW*, Chama kinachohusiana *na Domestic and Hotel Workers Union.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lekule Laizer aliuliza juu ya uwezekano wa Chuo cha Mweka kuwa Chuo Kikuu. Serikali ilikwishatamka kwamba kuanzia sasa Vyuo vyote nchini vinavyotoa wataalamu wa kati katika ngazi za Shahada na Stashahada havipandishwi hadhi kuwa Vyuo Vikuu. Kwa sababu kuna mahitaji makubwa sana ya wataalamu hao na wa katikati. Kwa hiyo, Wizara haiwezi kwenda kinyume na agizo hilo la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liliulizwa swali moja kuhusu Chuo Kikuu cha Utalii hapa Tanzania. Nilipokuwa nawasilisha hotuba yangu nililieleza kidogo. Kwanza, mwaka kesho tutakamilisha ujenzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii kitakachotoa Shahada na Stashahada za utalii na maeneo ya hoteli. Aidha, Chuo Kikuu cha Dunia cha Biashara, *World Trade University* kimeomba kwamba Chuo Kikuu cha Utalii cha Dunia kwa Bara la Afrika kijengwa Tanzania. Tunategemea kwamba Mheshimiwa Rais atakapokwenda kule kupewa Uenyekiti wa *Second World Tourism Marketing Summit* pia tutawekeana Mkataba juu ya ujenzi wa Chuo Kikuu hicho cha Dunia hapa Tanzania. Kwa hiyo, Chuo hicho kitakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa rai kwamba tuzungumzie kidogo juu ya vitalu vya uwindaji. Vitalu vya uwindaji katika *Game Reserves* kama *Selous*. Ndani ya *Selous* watu huwa wanaomba maeneo ya hekta moja mpaka hekta 5 wajenge *lodge* za kuwaweka watalii au wajenge *tented camps* za kuwaweka watalii. *Concession fee* ya hekta hizo tano au chini yake ni *dollar* 36,000 kwa mwaka. Sasa tunao wawindaji wana hekta 80,000 ndani ya *Selous,* hekta 5 ni *dollar* 36,000, hekta 80,000 ni *dollar* 10,000. Hivi hii biashara inaeleweka? Kule Afrika Kusini amesema Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, kitalu kimoja ni mpaka *dollar* 250,000, tumepandisha kidogo tu. Watu wanalalamika kuanzia *London* mpaka Dar es Salaam na kuanzia Dar es Salaam mpaka Dodoma kama Mungu ameamka. Jamani msione aibu marekebisho haya ni haki yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitalu vile ambavyo havina wingi wa wanyama sana tumesema vilivyokuwa vinatoa *dollar* 10,000 vifikie *dollar* 40,000. Lakini vitalu vingine hivi ni vikubwa kuliko Wilaya ya Mwanga. Mtu ana kitalu *square kilometre* 3,000 analipa *concession dollar* 10,000, hii inawezekana jamani? Haiwezakani! Haya mambo tulikuwa tunaimba zamani haiwezekani! Bei za wanyama, sisi katika Afrika na katika dunia ndiyo wenyewe *prestige hunting conditions* kwa maana ya kuwinda katika maeneo kama Adam na Hawa walivyoyaacha huku duniani. Unakuja unaingia pori lile lililonona kweli kweli kama wenzetu wa Kenya walivyosema. Hakuna mtu ameingia huko kufanya vurugu vurugu, tumelitunza vizuri. Unatafuta simba mpaka unatoa jasho, siku 21 unapewa mpaka unampata. Simba mzuri aliyezaliwa *naturally,* amezaliwa *naturally*. Tembo mzuri amezaliwa *naturally*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wanafikiria mbali zaidi, lakini mimi nafikiri kwenye ndovu huyo mkubwa. Nchini Malawi wanavuna ndovu kama 25 tu kwa mwaka, kwa sababu hawapo. Sisi ndiyo wenye *population* kubwa ya ndovu katika dunia nzima na wenye Tembo wengi kupita nchi yoyote dunia nzima. Kule Botswana kumpiga tembo ni *dollar* 25,000. Haya nisiende mbali sana. Hapa Tanzania wanataka kumpiga watu hao hao *dollar* 5,000, inawezekana hiyo jamani? Haipo na haiwezekani! Lile suala tulikuwa tunasema haiwezekani, haiwezekani! Simba, chui hawa wapo *Class one* kwenye *Cites* wanawindwa kwa nadra, kwa kibali maalumu cha dunia nzima. Kwa wenzetu wanauza kwa *dollar* 18,000 mpaka *dollar* 25,000, kwetu wanataka kuwachukua kwa *dollar* 2500, inawezekana? haiwezekani! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mewnyekiti, wanyama wengine hao tumeongeza kidogo kidogo sana. Sasa jamani nogwa inatoka wapi? Mimi nataka kusema wazi hapa kwamba Serikali ina dhamira kabisa ya kuhakikisha inapata mapato ya kutosha kutoka kwenye maliasili zake. Kuna makubaliano dhahiri kabisa umepewa kitalu lazima ulipie ada ya kitalu, ulipie ada ya kuwinda na ulipie ada zingine zote zile ambazo tumezipanga katika bajeti ziweze kuleta shilingi bilioni 33.355. Kama hulipi kitalu tutakichukua. Kwa hiyo, Serikali haitavumilia, mtu wanasema wataandamana, sijui watakwenda wapi, wataandamana kwenda wapi? Kama machungwa yanauzwa kwa bei ya juu kama huyawezi uyaache! *(Makofi)*

Watanzania tuko tayari kuvikusanya vitalu vyetu vyote na mwaka kesho tutaita *International Tender* ili tuuze mali yetu kwa soko la dunia. Kwa wale wote ambao hawataki, wapishe wakati ni huu. Sasa hivi tumewaweka maji jikoni kabla hayajachemka waondoke. Kwa hiyo, hii biashara ya watu kuzunguka zunguka hapa kwenye Bunge wanapiga soga haiwezekani. Watanzania wamekaa muda mrefu wa kutosha. Huko nyuma tumevutia watalii, tumevuta subira watu wameishatufahamu wanajua tulipo, wanajua mali tuliyonayo sasa tunauza kwa bei ya soko. Hakuna tena masuala ya kubembelezana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo mafupi. Kwanza nawaomba Waheshimiwa Wabunge, watuunge mkono kwa dhati katika Kamati ya Matumizi na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, waiunge mkono Serikali katika azma hii ya kuhakikisha tunapata mapato yote ya maliasili ambayo tunastahili. Nataka kuwahakikishia kwamba Serikali itadhibiti kwa nguvu sana na kusimamia bajeti hii kwa nguvu sana ili tuweze kupata mapato yote ambayo yapo katika makadirio yetu. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kifungu 1001–*Administration and General*... ...sh. 1,720,120,000/=

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante *Vote* 69, programu 10 *sub vote* l001, kifungu kidogo 250100 – Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nahitaji ufafanuzi kidogo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Wakati nachangia kwa maandishi nilizungumzia kuhusu eneo ambalo linaongezwa kwenye Hifadhi ya Ruaha. Sasa kabla ya hotuba hii ya leo, Wizara ilileta mapendekezo ya kuongeza hilo eneo ambalo *RCC* tulikaa na kukubaliana kuondoa vijiji 7 ambavyo vitaingia kwenye hifadhi. Lakini hivi karibuni imeonekana tena kuna kuongeza vijiji vingine 7, nilikuwa nahitaji ufafanuzi.

Lakini la pili, katika vijiji ambavyo tayari tulishawahamasisha na wamekubali na tathmini imefanywa, wananchi wamekuwa wakisubiri kujua ni lini zoezi hili litakamilika. Lakini leo kwenye hotuba Waziri anasema mwezi Novemba Azimio la kuridhia ongezeko la hifadhi litaletwa na sasa tangu mwaka jana Juni tathmini imefanywa na wananchi wamekuwa hawafanyi chochote wakisubiri kuhama. Sasa kama kuna kijiji kama Ikoga wameshakuwa tayari na wako langoni kabisa kwenye hifadhi hii ambayo tunaizungumza hapa. Je, Waziri atanipa maelezo ambayo wananchi wakisikia kwamba hawa ambao wako tayari kuhama waweze kuhama mapema? Kwa hiyo, nilikuwa nahitaji ufafanuzi wa hilo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo kwa swali alilouliza Mheshimiwa Estherin A. Kilasi, Mbunge wa Mbarali kama ifuatavyo: Kutokana na matatizo ya bajeti hatukuweza kuwawezesha wananchi waliokuwa tayari kuondoka kabla ya mwaka huu wa fedha. Lakini baada ya bajeti hii kupita tutakuwa tayari kushughulikia suala hili na wananchi walio tayari tutaweza kuwasaidia kuhama.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati nachangia kwa maandishi niliomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi kwamba licha ya kuzungukwa na hifadhi, sheria zinawakataza kabisa wananchi kuingia, kuwinda kiraia wala kuchungia kwenye eneo la hifadhi. Lakini wananchi hawa walikwisha nyang'anywa maeneo yao kwa sababu ya kuruhusu shughuli hizi za hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini sasa Serikali itatenga maeneo kwa ajili ya malisho kuwachimbia mabwawa hawa wananchi wanaoishi kandokando ya hifadhi? Katika jimbo langu vijiji vyenye shida kubwa sana na hali hii ni vile vilivyoko kandokando ya hifadhi ya Maswa *Game Reserve,* vijiji vya Semu, Nyanza, Mwanindwa, Buturi, Ming'ongwa, Mwasengela na Mwang'ongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika migodi kuna wachimbaji wadogo wadogo ambao haki zao zimekuwa kwa kweli zikishughulikiwa na Serikali kila siku. Je, ni lini sasa Serikali itawaangalia hao wananchi wanaoishi kando kando ya hifadhi ili iruhusu wawindaji wadogo wadogo watakaoweza kuwinda na kuwauzia wananchi wengine kwenye bucha za kawaida na ili kuondoa sasa adha ya wananchi hao wanaoishi kandokando na kuwatunza hao wanyamapori lakini hawaruhusiwi kabisa kula nyama ya porini? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya suala alilouliza Mheshimwa Luhaga Mpina, Mbunge wa Kisesa kama ifuatavyo: Sheria ya Wanyamapori iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu hairuhusu watu waingie kuwinda ndani ya hifadhi. Lakini kila Wilaya ambayo inazunguka maeneo kama *Maswa Game Reserve,* yanayo maeneo ambayo wawindaji wa kienyeji wanaweza kukata leseni kutoka kwenye Halmashauri yao ya Wilaya wakawinda katika maeneo hayo. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mpina aangalie kwamba ni kota gani ya uwindaji ambayo wanayo mwaka huu. Kota ya uwindaji katika kipindi hiki cha Julai mpaka Desemba imekwishatoka, aangalie kwamba katika Wilaya yake ni wanyama wangapi na aina gani

ambao wanaruhusiwa kuwinda na hao wananchi wanaotaka kuwinda waweze kukata leseni na kuwinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikulielewa suala hili la migodi kwa sababu kwa kweli mimi sielewi migodi vizuri.

**MWENYEKITI:** Nafikiri Mheshimiwa Mpina amekuelewa. Tunaendelea!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi nazungumzia kifungu ..!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe tafadhali. Waheshimiwa Wabunge kwa kanuni ninaomba niwaruhusu kuendelea kutoa hoja zenu bila kuanza kutaja tena kifungu ili tuweze kuendana na muda.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa ufafanuzi huo. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa *boldness* ambayo ameionyesha katika suala zima la magogo na vitalu na pia kupokea ushauri ambao Kambi ya Upinzani imekuwa ikiutoa toka bajeti hii imeanza kuhusiana na eneo hili. Kitendo cha Kiongozi wa Upinzani Bungeni kuunga mkono hotuba yako ni kuonyesha kwamba wewe ni mmoja wa Mawaziri wachache ambao mnasikiliza na mnatekeleza kile ambacho mmeambiwa.

Sasa nina vitu viwili ambavyo nilikuwa naomba ufafanuzi. Nadhani ni kimoja na kingine ni kidogo tu. Cha kwanza ni kwamba katika hotuba yako umeonyesha kuwa tutaweza kukusanya takribani shilingi bilioni 45 kutokana na upandishaji wa bidhaa za misitu, bei za magogo na kadhalika. Lakini hotuba yako kwa mujibu wa taratibu zetu za Kibunge ni maneno tu. Fedha imeonekana kwenye kitabu cha kwanza ambacho katika kitabu cha kwanza fedha inayoonekana kukusanywa na Wizara yako ni shilingi bilioni 15 tu pungufu bilioni 30.

Lakini vilevile katika hotuba yako umeonyesha kwamba tutakusanya shilingi bilioni 11 katika upande wa uwindaji *(hunting blocks)*. Lakini katika kitabu cha *revenue* inaonekana kwamba tunatarajia kukusanya shilingi bilioni 49.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba utoe maelezo kuweza ku-*clarify* hizi tofauti za *figure*. Najua kwamba mlikuwa na haraka baada ya kupata ushauri wetu hamkuweza kuangalia vitabu vyote kwa ujumla, nilikuwa naomba uweze ku-*clarify* hilo.

La pili, ambalo nilikuwa nataka unipatie maelezo nalo ni la kisera. Mheshimiwa Waziri ni kwamba tatizo tulilonalo sio upandaji wa bei, tatizo ni udhibiti wa utoroshaji wa bidhaa za misitu. Hii inatokana na Idara imekuwa ikiruhusu wageni na hasa watu kutoka China, Cambodia na kutoka Mashariki ya mbali kwenda kuvuna moja kwa moja kwenye misitu yetu kiasi kwamba wanakuwa wanadanganya idadi ya magogo ambayo wanayoyavuna. Sasa Waziri unaweza ukatoa kauli rasmi kwamba uvunaji *field* kule

utabaki ni wa Watanzania tu na wageni kazi yao itakuwa ni kununua kutoka kwa Watanzania. Ahsante!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kwa hoja yake aliyoileta kwa maandishi, muda haukuwepo wa kuweza kujibu hoja zote. Hoja hii pia ililetwa na Waheshimiwa Wabunge kadhaa. Ni kweli kwamba kuna kasoro kidogo kwenye kitabu hiki, lakini Waziri wa Fedha ataleta marekebisho na masahihisho yako katika ma-*book* haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kwa sehemu ya pili kwamba Serikali sasa imeunda kikosi kikubwa cha kushughulikia udhibiti wa kuhakikisha kwamba wale waliokuwa wamezoea kukata magogo bwelele na kupeleka siku zao zimekwisha. Kwa siku takriban siku kadhaa sasa kazi hiyo imekuwa ikiaendelea na inaonyesha mafanikio makubwa. Kwa hiyo, hakuna shaka kabisa juu ya uwezo wa Serikali kudhibiti na kusimamia ukataji katika misitu yetu ya asili ya vijiji na mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa kwenye hotuba kwamba tunawakaribisha watu waje kuwekeza viwanda sio kukata magogo na kupeleka makwao. Kama tukiruhusu watu kukata magogo na kupeleka kwao na bei zetu ni hizi ambazo mnasema tuwe na bei ya shangazi, Asia na Mwajuma haiwezekani tukavutia viwanda vikaja kwetu.

Nataka niseme kitu kingine kwamba katika dunia ya leo mazao yote ya maliasili ambayo yanaweza kuwa na athari kwenye mazingira wakati yakivunwa, huwezi kuuza bidhaa zako katika soko la wazi. Lazima ijulikane rasmi kabisa kwamba wewe unachukua bidhaa hizi kutokana na misitu iliyosimamiwa na umeuziwa katika utaratibu ambao baada ya kukata unakuwa na hifadhi endelevu.

Kwa hivi kama wajasiriamali wetu wataelewa hili na mimi kupitia Kiti chako Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa wito kwamba wajasiriamali Watanzania ambao wanauza magogo nje wanawajua hao watu walioko huko na wanajua wanafanya nayo nini wale hawawezi kuuza bidhaa zao hizo wanazotoa hapa katika soko la wazi. Kwa hiyo, kuanzia kukata mpaka kutengeneza mpaka kuuza lazima wafanye kwa bongo bongo hivi.

Tunatoa wito kwa Watanzania hao wanaofanya biashara ya magogo walete *Business Plans* za kuwa na viwanda vya kupasua mbao maana wengi ni wakubwa, wana viwanda vya kutengeneza fenicha, gunia na mazao mbalimbali ya miti ili tuongeze ajira, mapato na tukuze uchumi wa nchi yetu. Serikali iko tayari kuwasaidia waweze kupata *guarantee* kwa kuweka viwanda hivi kwa sababu tunajua umuhimu wa viwanda hivi.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nilitaka kujibu tu majibu ya nyongeza, ni kwamba wakati nikiwasilisha bajeti na katika mchanganuo wa bajeti ilionesha wazi wazi fedha zaidi ambazo zilitokana na Wizara ya Maliasili na Utalii

shilingi bilioni 33. Kwa maana hiyo ni kwamba utaratibu huu ulishafanywa na Serikali kabla ya mapendekezo haya ya upande wa Kambi ya Upinzani kama tulivyoeleza.

Pia wakati ambapo nitaleta *Finance Bill,* nitaeleza kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii itaongeza hizi kutokana na *GN* ambayo iliyokwishatolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa ufafanuzi na Waheshimiwa Wabunge. Ni kweli kabla hatujahitimisha shughuli za bajeti ni lazima tutampa nafasi tena Waziri wa Fedha ili aje mbele yetu na *Finance Bill* na nadhani tunaweza kupata maelezo ya ziada katika yale yote yanayotutatanisha.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nina mawili, lakini kwanza nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya na hasa ya kupandisha ada ya wanyama hawa tembo, simba, ingawa sikusikia kupandishwa kwa ada ya fisi. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, langu mimi katika mchango wangu wa maandishi, nilieleza kilio changu cha muda mrefu cha ndege anayeitwa Kasuku. Kwamba ukiacha *queleaquelea* ambao nilishazungumza wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ni ndege mmoja mwenye mdomo mwekundu hivi na ni miongoni mwa ndege ambao wanaathiri sana mazao ya wananchi kule kwenye jimbo langu Singida Kusini na hasa vijiji vya Ihombwe, Mlandala, Minyuhe, Mwaru na vinginevyo.

Kwamba kwa muda mrefu tuliambiwa Mashirika ya Kimataifa, kuna Shirika la Kimataifa linalohusika na ndege hawa walikuwa wamezuia kuvunwa na kusafirishwa kwenda nchi za nje. Kwa sababu huko nyuma walikuwa wanakamatwa, wanavunwa na kusafirishwa, kwa hiyo, pia ilikuwa inapunguza ule uwingi wao. Sasa muda wote ambao hawajavunwa wamekuwa wengi na wanafanya athari kubwa sana katika kilimo cha wananchi.

Sasa niliuliza kama je hiyo *ban* bado ipo kwa sababu Wizara ilisema huku nyuma bado wanashughulikia kuomba kibali ili kuruhusu wananchi wawavune. Hii itasaidia kuwapa vijana wetu ajira lakini vilevile wakishapelekwa huko nchi za nje pia tunaweza tukapata fedha hata ikiwezekana fedha kutoka nchi za kigeni. Sasa katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri pale sijasikia jambo hilo, ningeomba kupata maelezo kwa sababu wananchi wangu wanasubiri kwa hamu, anasema tutawavuna soko liko wapi? Naomba nijue soko ndani ya nchi, lakini kubwa zaidi soko nje ya nchi.

Pili, ameeleleza kiasi fulani Mheshimiwa Naibu Waziri habari ya wanyama wakali hawa ndovu na simba kwamba wanafanya madhara ya kilimo, lakini pia wananchi wanakufa kutokana na wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilieleza tatizo mojawapo tulilonalo ni kwamba Maafisa Wanyamapori kwa Halmashauri yetu ya Wilaya wako wawili tu na Wilaya ile ni kubwa mno, sitaki kurudia agenda nyingine.

Nilikuwa nafikiri kwamba na tulishauri hata kwenye Halmashauri kwamba tupewe kibali cha kuongeza Maafisa Wanyamapori ili walau tarafa tatu ambazo zina wanyama wakali walau ziwe na maafisa hawa Wanyamapori ili kusudi likitokea tatizo waweze kwenda haraka kutatua matatizo yale yaliyopo; je, katika maelezo ambayo walimjibu mwenzangu nichukulie kwamba kibali kimetolewa kwa Halmashauri ya Wilaya kuwaajiri Maafisa Wanyamapori zaidi ili kuendana na hali halisi ya matatizo tuliyonayo katika jimbo letu? Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilikuwa nataka nimhakikishie shemeji yangu Mheshimiwa Missanga kwamba yule mnyama anayeitwa korukutakoruta au fisi ameongezwa bei kutoka dola 500 kufika dola 1000. Kule Upare nasikia huwa wanatumika kama farasi, kwa hiyo, nadhani wale wanaotumia watawatoa sasa ili waweze kuwindwa.

Kuhusu suala la Kasuku hili ni la kuangalia kwa makini. Kwa hiyo, tutatuma timu ya wataalamu kule ishirikiane na wataalamu walioko kule tuangalie hawa Wanyamapori wanaleta athari gani katika eneo hilo na tunaweza kuchukua hatua gani tuweze kuondokana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni kweli kwamba wanyama hawa wana soko zuri huko nje na wataalamu wetu hawa wa kushika wanyama kwa ajili ya kuuza na wenyewe watafuatana na timu hiyo ili kuwashauri wananchi ambao wangependa kuwauza wanyama hao kama biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshauri kwamba Halmashauri za Wilaya ziangalie uwezekano wa kuajiri Maafisa Wanyamapori katika maeneo yao kutokana na mahitaji.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,suala la hawa vijana wanaopanda Mlima kwangu na kwa wale vijana ni suala zito sana. Mheshimiwa Waziri mtani wangu , Mchaga na Mpare, naomba tuweke utani pembeni tuzungumzie masuala ya maslahi ya hawa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Kilimanjaro National Park* ndiyo inayosimamia shughuli zote za kupanda Mlima wa Kilimanjaro. *Kilimanjaro National Park* ndiyo inayotoa leseni ya *guide* kwa anayepandisha mtalii mlimani. *Kilimanjaro National Park* ndiyo inayosimamia kwamba mtalii mmoja atalipa dola 550 kwa siku tano atafuatana na *guide* mmoja, atafutana na mpishi mmoja, atafuatana na *porters* wawili au zaidi, kila *porter* asibebe zaidi ya kilo 18. *Kilimanjaro National Park* ndiyo inasimamia na ndizo kazi zao za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa Mtalii yuko tayari kulipa Dola 20...!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kimaro naomba kuhusu utaratibu! Tukifikia katika hatua hiyo si hatua tena ya kuchangia hoja ni hatua ambayo unaeleza ni jambo gani ambalo unataka upatiwe ufafanuzi. Kwa sababu maelezo yalishafanyika, ama kwa maandishi au kwa kuzungumza. Kwa hiyo, ningeomba ili tuweze kuokoa muda na

Waheshimiwa Wabunge wengine wapate muda wa kupata ufafanuzi wa mahitaji yao basi niombe nikupeleke kwenye suala unalotaka kupatiwa ufafanuzi. Tafadhali naomba tufuate utaratibu.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kutumia zile dakika zangu 5 lakini sasa nitakatisha. Nimwombe Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi, inakuwaje vigumu kama *Kilimanjaro National Park* inasimamia shughuli zote hizo inashindwaje kusimamia hiyo mishahara ya *guides and porters* ambapo watalii wako tayari kulipa, wakilipa kwa *Tour Operators* hawafikishi kwa *guides* na *porters* wanabaki kuwa ombaomba wanapokuwa huko Mlimani. Naomba ufafanuzi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nadhani nimetoa maelezo ya kutosha kuhusu suala hili. Nadhani ingekuwa vizuri niseme tu kama Mheshimiwa Kimaro hili suala ni kweli linamsibu sana na angependa apate jawabu ambalo ni rahisi, suala hili ni la kisheria. Kwamba mashamba ya kazi yanashughulikiwa na Sheria ya Kazi. Masuala ya Kazi, saa za kazi, huduma za mtu anayekufanyia kazi na kadhalika yanashughulikiwa na sheria ya kazi. Hili ni suala Mbunge analiweza, na yeye ndiye Mbunge wa Vunjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale vijana wako Vunjo, yeye ndiye Mwenyekiti wao, wasaidie vijana hawa waweze kuwa na chama chao huru cha wafanyakazi ili waweze kuingia katika majadiliano ya hali yao ya kazi, hicho ndicho tulichosema. Tumesema tumemtuma ofisa wa *Labour*.

Nimemwomba Mheshimiwa Waziri amekubali kutuma ofisa wa *labour* kuwasaidia wale vijana ili waweze kuunda chama chao cha wafanyakazi. *Association* ile ya kuandikisha kule Wizara ya Mambo ya Ndani haitoshi, kile sio chama cha wafanyakazi. Hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kila siku Serikali inatoa leseni watu wawe na maduka, wawe na viwanda, wawe na mashirika mbalimbali. Hivi Serikali inakwenda itoe mishahara ya wafanyakazi au Mashirika? Mimi sioni ni kitu gani kigumu ambacho Mheshimiwa Kimaro anashindwa kukitekeleza.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri wa Maliasili na Utalii kwa majibu thabiti kabisa. Ningetaka niongeze kidogo tu kwa Mheshimiwa Kimaro kwamba maelezo aliyopewa na Mheshimiwa Waziri hapa ni maelezo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale vijana wanapunjwa kwa sababu hawana umoja na siku zote kama hamna umoja mnakuwa dhaifu. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Kwa hiyo, Wizara yangu kwa sababu yule Msajili wa hivyo vyama yuko ofisini kwangu, tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge Kimaro katika muda mfupi sana ujao.

Tunaahidi kwamba watasajiliwa, na kwa sababu Bodi za Kisekta zinazoangalia mishahara sasa hivi ziko kazini,  vijana hao wakishapata chama chao watakutana na ile Bodi ya mishahara ya sekta ili masuala yao yarekebishwe.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake na majibu yake mazuri. Lakini imenibidi nizungumze kwa sababu nimehamasika na kupata imani kwamba sasa hata wananchi wa Ruvuma hususan Mbinga na kule Nyasa watafaidika. Swali langu la msingi au ufafanuzi ninaouhitaji ni kwamba Mbinga katika maeneo ya Mpepo na mwambao wa Ziwa Nyasa kuna Simba na Chui ambao wanawala watu ambao kumbe wangetuingizia hizo fedha ambazo sasa hivi tunazitafuta. Je, naomba ufafanuzi ni jinsi gani tutaanza sasa kufanya utalii wa sehemu zile uweze kuwa *active*?

Lakini  la pili, katika Ziwa Nyasa wale wavuvi wamepigwa marufuku kuvua katika maeneo ya jirani, inabidi wakavue kule kati kabisa na pia wanaambiwa watumie nyavu ambazo ni za *size* kubwa. Lakini kuna samaki aina ya vitui kwa kweli hawakui miaka nenda rudi wako vilevile wadogo wadogo. Sasa Mheshimiwa Waziri atawasaidia vipi wavuvi wale ili waweze kwenda kuvua kwenye maji marefu badala ya kutumia hii mitumbwi ya kawaida? Naomba ufafanuzi ahsante sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri wananchi wa vijiji ambavyo vina wanyama hao, simba na chui waanzishe *Wildlife Management Areas (WMA)* ili wao wenyewe waweze kuwauza hao wanyama kwa *quota* ambayo watapatiwa wakishirikiana na Idara ya Wanyamapori. Wizara yangu itawasaidia katika kuanzisha *Wildlife Management Areas* hizi na baada ya kufikia hatua mwafaka mtapewa *certificate* ya matumizi ya wanyama hao na kupewa *quota*  kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri alikwenda katika Wilaya ya Mbinga na katika Wilaya ya Ludewa na kuendesha mafunzo ya uvuvi katika ukanda wa Ziwa Nyasa kwa kutumia ndoano na mishipi. Kwa hivi namshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri yake kuendeleza uvuvi huu ambao una tija zaidi ya ule wanaotumia kwa hivi sasa.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi naomba ufafanuzi kulingana na mchango wangu nilioutoa kwa maandishi lakini pamoja na kutoa mchango wangu kwa maandishi kwa mara kadhaa nimewahi kuuliza maswali na nimewahi pengine hata kuwasiliana na Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri mwenyewe kuhusiana na hili suala ambalo nitalizungumza.

Suala la kwanza linahusiana na pori tengefu la Msai lililopo Kata ya Mtoa.   Hili ni pori ambalo ni la asili na lina miti maarufu  inayojulikana kwa jina la mpingo. Mpingo unachukua takriban miaka 70 hadi 100 mpaka uje uvunwe. Lakini kwa  kwa kipindi fulani pori hili linaingiliwa na wavamizi wanakuja wanavuna holela bila utaratibu wowote na hakuna uangalizi wowote na tatizo kubwa linasababishwa na Maafisa Misitu wa pale waliopo, pengine wanashirikiana na wale wavunaji haramu na kufanya uhalifu huo. Sasa naomba ufafanuzi kwamba Wizara inaliangaliaje hilo pori kwamba tuliache lipotee hivi hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili nimewahi kuuliza swali na nimewahi kuzungumza na kuandika barua kuhusiana na Ziwa Kitangiri. Tangu alipokuwa Waziri Mheshimiwa Meghji wa Wizara hii , aliwahi kwenda Kitangiri na alipokwenda huko wananchi wa pale na wananchi wa maeneo mengine ya Iramba, Jimboni kwangu tunategemea sana shughuli zinazotokana na uvuvi wa samaki pale Kitangiri.

Lakini hatuna ulinzi wowote unaotolewa kwa ajili ya lile Ziwa. Watu wanavua kwa makokoro, kwa kupiga chochote na kila kinachowezekana. Wakati ule niliomba na wananchi waliwahi kuomba boti. Sasa naomba katika mchango wangu nilioutoa je, katika Bajeti ya mwaka huu Wizara imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa hiyo boti wakati tayari Mheshimiwa Meghji alishawahi kutoa ahadi kwa ajili ya boti hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Killimbah, masuala ya boti ni masuala ya *development,* kwa hiyo, hayo yanatakiwa kuulizwa kwenye *Development Budget,* na hapa sasa hivi ni masuala ya kisera. Kwa hiyo, nitaomba Mheshimiwa Waziri ajibu lile swali la kwanza la kuhusu namna gani mtatoa ulinzi kwenye pori la huko Singida.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Juma Killimbah kwa kufuatilia mambo ya maliasili yaliyoko katika Wilaya yake. Tunamshukuru sana na nataka nimhakikishie kwamba Wizara yangu itafuatilia kwa karibu suala hilo na kuchukua hatua stahili.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kupata ufafanuzi katika suala linalofuata. Kwanza kabla ya ufafanuzi nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Wizara nzima kwa Bajeti nzuri na hotuba nzuri na hatua nzuri zilizochukuliwa na kwamba naziunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Ufafanuzi ninaouomba ni kwamba katika mchango wangu wa maandishi pamoja na mambo mengine niliyoomba kufahamishwa au kutekelezewa na Serikali ni pamoja na kwamba utalii wetu umejikita sana katika eneo la Kaskazini ya nchi na Pwani. Ukizungumza utalii wa Tanzania ni Arusha, Serengeti na Pwani basi. Pwani kwa maana ya Zanzibar na Ukanda wetu wa mashariki. Lakini nchi hii imejaliwa, ina sehemu nyingi sana ambazo zinaweza kuwa ni maeneo ya utalii. Tukizifikia sehemu hizo hesabu za mchango wa Sekta ya Utalii itakuwa kubwa sana. Sasa ufafanuzi ninaouomba ni kwamba kuna maeneo, kwa mfano, Mbuga ya Katavi Rukwa, Mpembampazi eneo la Ulyakhulu, Gombe Kigoma; haya ni maeneo yaliyopo magharibi ya nchi. Sera inasema nini juu ya kuchanganya utalii wa kaskazini na utalii wa magharibi na sehemu nyingine ya nchi ili kuongeza mapato ya Sekta ya Utalii? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunamshukuru sana Mheshimiwa Siraji Juma Kaboyonga kwa pongezi zake. Ninakubaliana naye kwamba wakati umefika kwa Serikali kuweka juhudi zaidi katika kupanua utalii uelekee magharibi ya nchi, kusini mwa na nyanda za juu kusini. Tunavyo vivutio katika maeneo ya Magharibi ambavyo havipo duniani humu kama Hifadhi ya

Katavi. Hakuna kitu unachoweza kujisikia ukiwa Katavi kama ukiwa pale. *Animal experience* ya Katavi haiko duniani, ni Katavi peke yake. Kwa hiyo, tumechukua hatua kwanza kwa wale wawekezaji ambao wana mvuto mkubwa kuwekeza. Tunaanza kuwawekea *condition* kidogo kwamba ukiwekeza hapa uwekeze na Ruaha, uwekeze na Katavi, uwekeze na Mahale na wengi wanakubali. Mahale kuna *chimpanzee* wengi kuliko eneo lolote duniani, pale kwenye *beach* ya *Lake Tanganyika.* Kwa hiyo, hivi sasa kuna timu inakwenda kule kuangalia uwezekano wa kujenga *lodge* yenye nyota saba na kupanda yaani kwa ajili ya wakuu wa nchi katika Hifadhi ya Katavi na Hifadhi ya Mahale.

Mwaka 2009 tumekubali sisi Tanzania na tumeombwa kuwa nchi ya kwanza duniani kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Waafrika walioondoka Afrika wakaenda kwa njia mbalimbali kuishi nchi za nje. Na tumesema njia ya Kati hii ya utumwa na usafirishaji wa vipusa itakuwa ndiyo *centre* ya Mkutano huo na watakuja viongozi wa waafrika kutoka duniani kote katika hatua kubwa ya ku-*promote* utalii katika eneo la Kigoma, Mkoa wa Rukwa, Tabora na Mkoa wa Dodoma na kwenda mpaka Bagamoyo na Mji Mkongwe Zanzibar.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuwa katika Kitabu chake cha Bajeti, Mheshimiwa Waziri ameeleza maeneo mbalimbali ambayo yataongeza mapato, jambo ambalo Kambi yetu kwa muda mrefu imekuwa ikisisitiza na ndiyo maana leo tunamuunga mkono mia kwa mia kabla ya wewe mwenyewe hujatuuliza. Na kwa kuwa ipo haja ya kuleta mabadaliko makubwa katika sekta ya uvuvi je, Mheshimiwa Waziri atakubali kaunzisha *fish ports* katika bandari zetu kwa mfano Mtwara, Dar es Salaam na Zanziba kwa meli zinazovua Bahari Kuu na vilevile atakuwa tayari kutoza mrabaha kwa meli hizo ambazo zinavua kama tulivyopendekeza katika Hotuba yetu?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukutokea tu tukaanza kuja hapa, tukaanza kutangaza mabadiliko ya bei ya maliasili. Mtakumbuka kwamba *GN* hizi ni sehemu ya majedwali katika Hotuba ya Waziri wa Fedha. Hili ni suala tumelijadili kwa muda mrefu, tumejaribu kueleza hapa ndani ya Bunge na kama mnakubaliana na sisi ni vizuri. Lakini tusitoke hapa kama vile tulikuwa tumepanda *kihongwe* aliyekuwa anaendeshwa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaingia kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii aliyenitangulia alikuwa ameshaanza kutengeneza *proposals* kwa ajili ya kuanzisha *fishing ports* katika Pwani yetu ya Tanzania. Shughuli hii tutaendelea nayo. Sisi sote hapa kazi yetu ni kuendeleza nchi yetu na ndiyo maana siasa za Tanzania ni tofauti sana na siasa za nchi nyingine.

Kwamba sisi ndani ya Bunge na hata nje ya Bunge ni makomredi. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwamba nchi haitasimama, tutaendeleza Sekta ya Uvuvi na tutahakikisha kwamba meli ambazo zinavua katika Bahari Kuu zinakuja kwenye Bandari zetu, zinakunywa maji, zinakunywa mafuta, zinaajiri watu kutoka katika nchi yetu na tunaweza kudhibiti kwa karibu zaidi kazi wanayofanya.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia mchana, mbali ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa ujasiri wake katika suala la *fees,* nilizungumzia pia umuhimu wa kujenga utalii endelevu hapa nchini kwa maana ya kwamba tutengeneze mazingira bora kwa watalii kutoka nje lakini pia utalii wa ndani. Sasa naomba ufafanuzi ni hatua gani Serikali itachukua kuhakikisha kwamba mazingira yatakayovutia utalii wa ndani katika maeneo ya hifadhi zitachukuliwa.

Lakini niligusia suala la Mawakala wa Utalii wazalendo hasa pale Arusha ambao hivi sasa wanapata shida ya kupata malazi kwa watalii au wateja wao kutoka nje ya nchi katika mahoteli yaliyoko hifadhi ya taifa. Nilikuwa naomba ufafanuzi kwa sababu ni muhimu pia kukawa na hoteli za kawaida katika maeneo ya hifadhi ya taifa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kama anavyosema Mheshimiwa Lembeli, Mbunge wa Kahama kwamba ni muhimu tunavyotangaza utalii nje, tujenge utashi wa wananchi wa Tanzania kwenda kuona vivutio vya kupumzika ndani ya nchi yetu. Kule kwenye vivutio vyetu tumeweka gharama za kuingia mle kwa makusudi kabisa ziwe chini sana.

Kwa mfano wakati mgeni anaingia Serengeti au Ngorongoro kwa kulipa dola 60 kwa siku moja, Mtanzania anaingia kwa kulipa shilingi 1,500. Hiki ni kitu muhimu sana cha kuweza kuwapa utashi Watanzania waende kuangalia. Wanafunzi wa Tanzania wanaingia bure katika hifadhi zetu za Taifa. Hiyo ni hatua moja.

Lakini hatua ya pili nilitangaza hapa wakati nikisoma Bajeti kwamba Shirika la Kifaransa hili la *AFD* ambalo linatusaidia kujenga chuo cha utalii hapa nchini pia limekubali kwamba wakati watalii wanaongezeka hapa nchini wangependa kushirikiana na Mabenki ya nchini kwetu kuwa na mfuko ambao watu wenye hoteli ndogo ndogo hizi waweze kukopa kwa mikopo ya miaka minne mpaka sita wapandishe hadhi ya hoteli zao zifike nyota mbili ili na watanzania wakienda kule wakae kwenye hoteli zao.

Hivi sasa kuna Watanzania ambao watagawiwa viwanja kule ndani ya Serengeti ili kupunguza *monopoly* ya wageni. Kuna wawekezaji wa *Kempski* wanajenga kule na kuna wawekezaji wengine wataendelea kujenga ili kuondoa *monopoly* na kuhakikisha kwamba wasafirishaji wa utalii wazalendo wanaweza kupata nafasi za kulala kwa ajili ya wageni wao. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. Kwanza natangaza kuungana na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa hatua ambazo amechukua ili kuongeza mapato ya Wizara hii. Na pia atakumbuka Katibu Mkuu au Afisa Mhasibu wa Fungu hili, sisi kama Kamati ya *PAC* tulisisitiza sana ubunifu wa katika njia hii na hili ni vizuri tumeona limefanyika. Kwa hiyo, hongera sana Mheshimiwa Waziri.

Ninalotaka kuuliza hapa ni kwamba wakati nachangia kwenye Wizara ya Fedha juu ya Mapato, nilizungumzia pia dhana ya mapato ya Halmashauri kutokana na

rasilimali za misitu ambayo ni pamoja na kutopunguziwa mapato wenyeji kwa mazao yao kuliwa na wanyama pori.

Sasa ninachoomba ni kitu kidogo tu kwamba Mheshimiwa Waziri atusaidie sisi Waheshimiwa Wabunge ambao tunapakana na Hifadhi hizi kama kule kwangu ambako kuna kijiji cha Longalombogo, Lumwa na sehemu nyingine na Magharibi pia kuna zingine, namna ya kudai fidia kwa ajili ya watu wetu na pia namna ya kudai mapato yanayotokana na vitalu pamoja na hoteli kama vile *Sopper Lodge* kule kwetu kwa ajili ya Halmashauri. Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru, Kaka yangu, Mheshimiwa John Cheyo kwa pongezi zake. Suala la vitalu vilivyoko kwenye maeneo ya Wilaya limewekwa wazi. Kila wawindaji wanapokwenda kwenye vitalu hivi wanakwenda na Afisa Wanyamapori anayeteuliwa na Afisa Wanyamapori wa Wilaya ama Afisa Maliasili wa Wilaya waende naye katika kazi hii ya kuwinda. Na yeye ndiye atakayehakiki vitu vyote vilivyofanywa kule, kama ni watalii wangapi wamekuja, mabingwa wangapi wamekuja, wanyama aina gani wameuawa, *trophy* ngapi zimetoka huko na thamani yake na zile zinalipwa kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo inaziwasilisha Hazina na kadhalika. Hazina inatoa asilimia 25 ya fedha hizo ziende kwenye Wilaya kule Wilaya zilipo, huo ndiyo utaratibu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijapata jibu juu ya mapato ya Hoteli!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua mapato ya Hoteli yanasaidiaje hizo Halmashauri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya Maliasili kama misitu ina-*access* ambayo ni asilimia tano ya ule mrabaha na wanyamapori ni asilimia 25, sina uhakika kama hoteli zinalipa. Kwenye *Hotel levy* ni *levy* ya Serikali, kwa hiyo, haya ya mazao ya maliasili ndiyo asilimia zake, asilimia tano kwa magogo, asilimia 25 kwa wanyama waliowindwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo una nafasi pia ya kumwona Mheshimiwa Waziri hata baada ya shughuli hizi akaendelea kukusaidia kupata ufafanuzi zaidi. Mheshimiwa Shah atafuatiwa na Mheshimiwa Lwanji.

**MHE. ABDULKARIM ISMAIL SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante mimi namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu maelezo kuhusu *MACEMP* niliyokuwa nayo ni marefu na muda umekwisha.

Je, ninaweza kumwomba Mheshimiwa Waziri kupitia kwako akubali yeye na watendaji wake upande wa Idara ya uvuvi na vitengo vyake vyote vinavyoshughulikia masuala ya baharini tuweze kuja kukaa na Kamati ya Maliasili na Mazingira kwa pamoja ili tuweze kupata maelezo zaidi ya kuufahamu mradi huu wa *MACEMP*, mradi wa RUMAKI, mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Japan ambao Mheshimiwa Dialo alitupa

shilingi milioni 900 pale Kilwa lakini hazijulikani kama zimefanya kazi. Maelezo hatupati ili tuokoe muda na wengine waweze kupata muda wa kuchangia, ni hayo tu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Abdukalima Shah kwa maombi yake, ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Maziringira.

Tumepata kutoa Semina juu ya *MACEMP,* tutatoa tena Semina kama inahitajika na mimi mwenyewe nimekwenda Mafia, nimetembelea wavuvi kule na nipo tayari kurudi tena tuendelee kushirikiana katika kuhakikisha kwamba mradi wa *MACEMP* unaendelea vizuri. Kuanzia mwaka huu utaenda katika Wilaya zote za pwani ya Bahari ya Hindi.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi pia naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ila inapokuja na sera nzuri za kuboresha mapato katika sekta hii ya utalii basi ingelikuja pia na sera nzuri ya kuhakikisha kwamba maisha ya watu na mali zao yanakuwa salama. Nasema hivyo kwa sababu tuna tatizo kwamba simba wamekuwa ni hatari sana na maisha ya watu yanapotea na katika ukurasa wa sita wa Hotuba yake nimeona mikakati waliyoifanya kujaribu kuwaokoa watu wanaoliwa na mamba lakini sijaona mikakati inayofanywa kuwaokoa watu wanaoliwa na simba kila siku.

Kwa kweli hata juzi tulikuwa na ziara ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri alishuhudia watu waliojeruhiwa na simba. Sasa naomba ufafanuzi kwamba mikakati ipi imefanywa ili kuhakikisha kwamba eneo hilo watu wanaishi kwa usalama.

Pili, tuna sera kwamba wakulima kama shamba limeharibiwa kuna shilingi 100,000 zinatolewa kwa hekta na pia hicho kifuta jasho kwa huyo anayeliwa na simba. Lakini kuna mifugo inaliwa kila siku. Sasa wafugaji wanawekwa wapi? Maana yake juzi hapa katika ziara.....!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lwanji, Waheshimiwa Wabunge naomba tuelewane kitu kimoja. Nadhani tunashindwa kuelewa matumizi ya Kamati. Matumizi ya Kamati si kuanza kutoa hotuba na kuelezea mambo yanayokuhusu ndani ya Jimbo lako.

Kwa kuwa umeshayachangia na Mheshimiwa Waziri alishayapata, unatakiwa kwenda moja kwa moja katika suala unalohitaji kupatiwa ufafanuzi, na nirudie kusema kwamba Kanuni zinamkataza Waziri na Mbunge yeyote kurudia yaliyokwisha kusemwa. Masuala ya fidia yamejibiwa tayari hapa ndani. Simba akijeruhi shamba, sijui shamba likijeruhiwa na nani. Ufafanuzi umekwishatolewa.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tujali namna ya kutumia Kanuni ndani ya kujenga hoja ndani ya Kamati yetu. Kwa hiyo, nakushauri Mheshimiwa Lwanji wakati majibu yakitolewa kama ulikuwa haupo nitakuomba umfuate Mheshimiwa Waziri kwa muda wako. Haya yote unayoyazungumza yameshatolewa ufafanuzi ndani ya Bunge.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu waliompongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Lakini pamoja na kumpongeza sana ningependa kusema jambo moja au mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza linahusiana na upandishaji wa misitu, hususan misitu inayozalisha mbao laini. Ni kweli kwamba upandishaji huu umeleta fadhaa na kukata tamaa sana kwa wananchi wanaozalisha mbao zile.

Sasa kwa sababu Mufindi ni Wilaya inayozalisha sana mbao; je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuja kuongea na wananchi wale ili angalau waweze kujua ni kitu gani hasa Serikali imefanya na watatakiwa kulipa kwa kila mti shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kweli kwamba wako wazalishaji wakubwa sana wanaotumia misitu ya *SAO HILL* na walikuja hapa juzi wakitaka kuonana na Waziri Maghembe na walionana naye, lakini inaonekana hawakuridhika na majibu yale, wakawa wanapanga kwenda kumwona Waziri Mkuu.

Jambo hili ni kubwa na ni zito hasa kwa wadau wa mbao. Hapo mwanzo, nakumbuka Mheshimiwa Meghji alikuja kuongea na wafanyakazi na wazalishaji wa mbao katika maeneo hayo lakini safari hii bei hii imepandishwa tu bila kuwahusisha wadau. Kwa hiyo, ninaomba suala la kuwahusisha wadau liangaliwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, labda ujibu lile la kuombwa kwenda huko Mufindi kwa ajili ya kuzungumza na wananchi. Lakini suala la wadau wengine kuja, kutoridhishwa na majibu ya Waziri na kuomba wajibiwe na Waziri Mkuu, naamini Waziri ndio Serikali, anamwakilisha Waziri Mkuu. Sasa sijui majibu hayo ya ziada ni ya kutoka wapi!

Mimi nafikiri ujibu hilo la kwanza, hilo la pili, nadhani lifuate misingi mingine inayotakiwa. Lakini ninachoamini Waziri Mkuu ndiye Waziri wa Maliasili ndani ya Wizara hiyo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na pia namshukurru Mheshimiwa Benito Malangalila kwa swali lake zuri. Niko tayari kwenda Mufindi na Mheshimiwa Malangalila alishakuja Mwanga, tukaenda tukawahutubia wananchi, na mimi nitakwenda kwake twende tukawahutubie wananchi. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni Na.81(6) inanipa mwongozo na inaniruhusu kusema yafuatayo ili tuweze kumalizia hoja hii ndani ya Bunge.

“Endapo Spika (kwa sasa Spika ni mimi Mwenyekiti) ataona kuwa muda uliotengwa kwa ajili ya kujadili bajeti ya Wizara inayohusika umekaribia kwisha, atafunga mjadala ili aweze kumpatia mtoa hoja nafasi ya kujibu ndani ya muda uliosalia, halikadhalika, wakati Bunge liko katika Kamati ya Matumizi, isipokuwa kama itatolewa hoja ya kuongeza muda wa kikao cha Kamati hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 21(4) ya Kanuni hizi za Bunge, zikibaki dakika kumi tu kabla ya muda wa Kuahirisha Bunge kwa siku hiyo na Kamati bado haijamaliza kufikiria mafungu yote yanayohusika, Mwenyekiti atafunga mazungumzo yoyote yaliyoruhusiwa katika aya ya (b) na (c) za Kanuni hii na papo hapo atawahoji kuhusu mafungu yaliyosalia kama yapo”.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tukubaliane na mimi, sasa tunaelekea kubakiwa na dakika kumi, mpaka nitakapokaa tutakuwa tumebakiwa na dakika kumi ili tuweze kuahirisha shughuli za leo.

Kwa maana hiyo, nitaomba tuingie sasa kwenye *guillotine* ili tuweze kuendana na utaratibu na Kanuni za Bunge, tufanikiwe kuyapitisha mafungu kabla muda haujatutupa mkono. *(Makofi)*

Kifungu1002 -*Finance and Accounts* ... ... ... .....Sh.641,256,000/=
Kifungu1002 -*Finance and Accounts* ... ... ... ... ...Sh.641,256,000/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning*.. ... ... ... ... .Sh.325,728,000/=
Kifungu 1004 - *Information*, *Communication & Education*.. ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh.25,187,000/=
Kifungu 1005 -*Internal Audit* .. ... ... ... ... ... ... ... ...Sh.61,511,000/=
Kifungu 1006 - *Procurement Unit*.. ... ... ... ... ... ...Sh.141,174,000/=
Kifungu 1007 – *Legal Unit* ... ... .. ... ... ... ... ... ... ...Sh. 28,668,000/=
Kifungu 2001 – *Wildlife* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ..Sh. 6,950,135,000/=
Kifungu 3001 – *Forestry and Beekeeping*... ... Sh.9,387,206,000/=
Kifungu3002 - *Fisheries* ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh.5,918,164,000/=
Kifungu 4001 – *Tourism* .. ... ... ... ... ... .. ... ... ... Sh.4,540,735,000/=
Kifungu 4002 – *Antiquities Unit* ... ... .... ... ... ...Sh.1,077,740,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kifungu 1001- *Administration and General*.....Sh. 200,000,000/=
Kifungu 2001 – *Wildlife*………………………...Sh.2,657,594,000/=
Kifungu3001– *Forestry and Beekeeping*…….Sh.5,993,300,000/=
Kifungu 3002 – *Fisheries*…………………… Sh.9,200,000,000/=

Kifungu 4001 – *Tourism*……………………… .Sh.4,345,106,000/=
Kifungu 4002 – *Antiquities Unit*………………Sh.2,280,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri, ninaomba nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aweze kutoa maelezo machache.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Niliomba nafasi wakati ule kabla hatujamaliza Kamati ya Matumizi ili kuweka sawa mambo ambayo yamesemwa humu ndani. Wenzetu wa Upinzani toka asubuhi wamekuwa wakisema kwamba hizi tunazotekeleza ni sera zao. Sisi kama wana-CCM hatuna tatizo la kusikiliza wenzetu, hatuna tatizo kabisa. Lakini kwa kweli kwa sera tunajitosheleza! Tunajitosheleza na ndio maana Watanzania walitupima, wakatuamini, wakatupa kura kwa wingi kiasi hiki kuja humu Bungeni. Sasa wenzetu wa Upinzani wanapoanza kusema "mmeiga hiki, mmesikiliza hiki", nataka niwaonyeshe kwenye Ilani; huwa ni hodari wa kusoma Ilani, nashangaa leo kwa nini hawakusoma Ilani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya CCM inasema hivi, "Serikali chini ya CCM itachukua hatua zifuatazo: Kuendelea kuelekeza nguvu zake katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza, kudumisha na kuvuna maliasili kwa manufaa ya taifa letu". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine moja imesema, "Kuandaa mikakati ya kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya utalii" na nyingine "Serikali kujihusisha kwa ukamilifu katika kutangaza fursa za utalii zilizomo nchini na kuongeza bajeti ya kutangaza utalii ifanane na zile za nchi jirani". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kurudia tena, Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru sana kwa maoni yenu, lakini sera tunazo, tulikuwa tunatekeleza sera zetu. Na mimi napenda kumpongeza sana Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kutekeleza vizuri Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

*(Bunge lilirudia)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imepitia makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makisio ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nichukue nafasi hii sasa nitangaze rasmi kwamba Bunge la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeyakubali na kuyapitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008, kwa ujumla na kwa kwa kauli moja.

Mheshimiwa Waziri, ninachukua nafasi hii nikutakie kila la heri wewe, Naibu wako, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara katika kusimamia mpango huu na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kupitia katika Wizara yako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli nichukue nafasi nyingine kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, ameonyesha ujasiri wa ajabu na wa namna yake kabisa! Wengi waliochangia wamekiri Wizara hii ni nyeti na kwa kweli ina majukumu mazito, na nadhani tunaweza kufikiria mwakani kuipa hata siku mbili za kuweza kuifikiria bajeti hii. Lakini kwa kweli Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana, ujasiri uliouonyesha hapa mbele yetu ninaamini ndivyo utakavyofanya katika kusimamia haya tuliyoyapitisha leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumpongeza Waziri na Timu yake na kuwatakia kila la heri, ninayo matangazo machache:-

Tangazo la kwanza, ninaomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge mtambue vazi rasmi la Mheshimiwa Missanga leo, amevaa koti jekundu na tai nyekundu na ameonekana katika mwonekano mzuri sana ingawa yeye ni shabiki wa Yanga. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili, nimeletewa hapa na Ofisi yetu ya Bunge niwaambie kwamba pamoja na shughuli nzito ambayo tunaifanya wiki hii na tunaelekea mwishoni mwa wiki, kuanzia Ijumaa - Jumamosi, wenzetu wa *CELTEL* tutakuwa nao hapa Bungeni, watakuja kufanya *presentation* ya *products* zao. Halafu Jumamosi Jioni tutakuwa na shughuli maalumu ya kupima yale waliyotuonyesha katika maonyesho yao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutakuwa na hafla ya kutosha. Na nimeombwa niseme tu kwamba Mama Khadija Kopa atakuwepo, Nasma Khamis Kadogoo atakuwepo, Banana Zoro

atakuwepo, Hafsa Kazinja atakuwepo, na nimeambiwa kwamba *DJ* atakuwa *Too Short*, na mimi huyu mtu ni mpya kabisa kwangu hata simfahamu. Nadhani itakuwa ni nafasi nzuri ya kuona hayo mambo baada ya kazi nzito ya wiki hii ambayo tunaendelea nayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niseme tu kwamba ninawashukuru sana kwa ushirikiano mlionipa katika kupitia bajeti na ratiba nzima ya shughuli za Bunge katika siku hii ya leo.

Basi niseme tu nawatakia sasa jioni njema na nitamke kwamba ninaahirisha shughuli za Bunge za siku hii ya leo na tukutane tena kesho saa tatu asubuhi ndani ya ukumbi wa Bunge.

*(Saa 11.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 26 Julai, 2007 saa tatu asubuhi)*